Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 09 Julai, 2009**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:-**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. MAIDA HAMADI ABDALLAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. MGENI JADI KADIKA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia na Watoto kwa mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika kipindi cha maswali kilichopita, niliwahi kumuuliza Waziri Mkuu juu ya kuvunjwa kwa Katiba ya Muungano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Uchaguzi ambayo inataka Wabunge, Rais wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania wachaguliwe kwa muujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande wa Zanzibar, Tume ya Uchaguzi ya Muungano imewapa *agents* Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na kwa hiyo wanatumia Sheria ya Zanzibar kuwapata wapiga kura na wagombea kwa Sheria ya Zanzibar kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kinyume ya Sheria ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa zoezi linalofanywa la uandikishaji hivi sasa mpaka tarehe ya leo wananchi wa Tanzania wasiopungua 2001 wameshakoseshwa haki ya kujiandikisha. Waziri Mkuu aliniomba nimpelekee uthibitisho, nimempelekea uthibitisho na mpaka leo hatujapata majibu na hali hiyo ya kuandikisha watu bila kupata idhini, haijatekelezwa. Je, Waziri Mkuu unasema nini juu ya haki ya raia ambao wangetakiwa kuandikishwa chini ya Sheria ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na mpaka leo hawajaandikishwa?

**MHE. WAZIRI MKUU:** Mheshimwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Hamad Rashid, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Zanzibar inayo Serikali na kwa mujibu wa Katiba yetu ya nchi. Serikali ile ya Zanzibar inayo Mamlaka fulani yanayotawala maeneo fulani fulani. Sasa Sheria namba 11 ya Mwaka 1984, ndiyo inayotawala uchaguzi ndani ya Zanzibar. Na Sheria ile imefanyiwa marekebisho mbalimbali mpaka mwaka 2004; katika marekebisho yale, kipengele kimojawapo kilichoingizwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi ni hilo la mpiga kura anaye taka kujiandikisha au kupiga kura upande wa Serikali ya mapinduzi Zanzibar ni lazima awe ni mkazi mwenye hati maalum ambayo inatambulika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Sheria ile vilevile imeruhusu, kwamba kwa wale ambao ni wakazi wa kawaida katika majimbo ya Uchaguzi, wanachohitaji pale kwa mujibu wa Sheria ile, ni kuwa ameishi pale kwa miezi, angalau takribani miezi 36. Kwa hiyo ni mkazi, yupo pale, anajulikana yupo pale, siku zote anafahamika.

Kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba, jambo hili linaweza likaonekana kama pengine kuna ukiukaji wa Katiba na Uvunjaji wa Sheria, lakini mimi nataka niseme kama liko tatizo, ni vizuri Baraza la Wawakilishi likachughulikia kwanza hiyo Sheria yenyewe; yafanyikishe mabadiliko pale ili kuweza sasa kupata ufumbuzi wa tatizo hili kwa ujumla wake.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vinginevyo kujaribu kuona kwamba Serikali ya Muungano tunaweza tukasema hiyo Sheria haifai, labda sasa twende Mahakamani pengine ndio

tunaweza tukapata jibu ambalo ni sahihi zaidi. Lakini kwa sasa kilichofanyika kipo pale kwa mujibu wa taratibu na ni halali kabisa.( *Makofi*)

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika**,** Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zote hakuna hata kipengele kimoja waliokiuka sharti hili, kwamba ni sharti la msingi. Sharti la msingi ni Mtanzania ambaye amezaliwa Tanzania na anayo *registration* ya uzaliwa wake.

Mheshimiwa Spika**,** vitambulisho vinavyotolewa hivi sasa anavyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu; kwanza havijulikani idadi yake, pili hivi sasa ninavyokuambia ukikitaka kipande hiki kukipata, uende kwa shehe na shehe anakuambia hana fomu.

Kwa hiyo utaratibu mzima ni kinyume cha Sheria. Swali langu, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je tuna Sheria mbili kwa Uchaguzi wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nirudie nilichosema. Zanzibar hamuwezi kukataa kwamba wanazo Sheria zinazosimamia shughuli fulani fulani. Hilo ni jambo linalokubalika na linaeleweka, ndio maana nimekusihi sana nikasema kwa hili kwa sababu liko pale kwa mujibu wa Sheria namba 11 ya Mwaka 1984, basi Baraza la Wawakilishi ndilo mngetakiwa mlisihi lifanye marekebisho haya, ili yaweze kuwiana na dhana ambayo mnadhani itatuweka katika mazingira mazuri. Maana ukiniuliza mimi, nitasema, aah! Bahati nzuri Baraza la Wawakilishi lina uwakilishi mkubwa tu wa *CUF* na Vyama Vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni dhahiri jambo hili lilikubaliwa na sehemu zote kwa ujumla. Waliona katika mazingira ya Zanzibar, jambo hilo ni la muhimu. Kwa hiyo, mimi nadhani jambo hili lingerejeshwa pale, lakini kama bado Mheshimiwa Hamad anaona ni jambo haliwezekani; vema bado tuna mfumo mzuri tu wa kwenda Mahakamani, ku-*challenge* au kuhoji uhalali wa ile Sheria, ili tuweze kupata jambo ambalo linaweza likafikia mahali tukasema huwo ndio uamuzi sahihi. Lakini kutegemea kwamba hata Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nasema hata Bunge lako kwamba tunaweza tukasema hata Sheria hile haifai, sidhani kama tutakuwa tunafanya kitu sahihi. (*Makofi*)

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru sana Serikali, kwa kusikia kilio na ushauri na maombi ya wadau wa pamba katika kufidia hasara za wafanyabiashara, pamoja na kuongeza bei ya mkulima. Naipongeza sana Serikali, Serikali yetu ni sikivu na naamini kwamba wakulima wa pamba wataongeza uzalishaji msimu ujao. Baada ya pongezi hizo, napenda nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali kama ifuatavyo:-

Ukanda wa Ziwa Victoria, ukianzia Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Mwanza mpaka Mkoa wa Mara, kuna miji midogomidogo kama Izigo, Muleba, Geita, Misungwi, Nyanguge, Magu, Lamadi na Bunda. Imekuwa na matatizo ya maji kwa muda mrefu sana. Wananchi wanahangaika usiku na mchana na wengine wanaliwa na mamba. Nauli za Serikali halioni kwamba wananchi wa maeneo hayo wanasikitika kwamba Serikali haiwatendei haki wakati maji wanayaona yako karibu? Ni lini Serikali itawapatia maji ya uhakika muda wote wananchi wa maeneo hayo, wakiwemo wananchi wa Magu?

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu rafiki yangu Dr. Limbu, kama ifuatavyo:-

Kwanza tukubali kwamba tatizo la maji bado ni kubwa. Kubwa tu na ndio maana unaona jitihada ni kubwa sana za Serikali kujaribu kutoa huduma hiyo kwa Watanzania. Matarajio yangu ni kwamba mpango wa maji ambao Mheshimiwa Waziri wa Maji aliueleza, unaona unaendelea kutoa matunda siku zinavyokwenda. Kwa hiyo, tutajitahidi, tutaendelea kufanya juhudi kubwa, lakini nataka tu niseme kwamba Mheshimiwa Limbu, unajua tatizo lile lipo kwa maeneo hayo, lakini angalau hawa Ziwa liko karibu, kwa maana kwamba maji yako karibu na wao wenyewe. Ni suala tu la teknolojia gani itumike kutoa maji yale na kuwapatia unafuu ya kuyapata.

Mheshimiwa Spika, lakini fikiria maeneo kama Dodoma, maeneo kama Singida, fikiria maeneo yote ya *hinterland*, ambayo hata maziwa hatuna. Unaona tatizo ni kubwa zaidi. Kwa hiyo mi nadhani ukubali tu kwamba Serikali itaendeleza juhudi zake kwa dhati, kuhakikisha kwamba tunafikia kiwango cha asilimia 65 kwa ajili ya maeneo ya vijijini na lengo ni kufikia kiasi cha asilimia 90 kwa ajili ya maeneo ya mijini. *Inshallahah,* Mwenyezi Mungu atatufikisha hapo na nadhani na watu wako watafarijika.

**MHE. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 25 Juni, 2009, wakati ukijibu swali la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani linalohusiana na Uchaguzi usio kuwa huru na wa haki. Pamoja na mambo mengine, ulijibu kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani itachukua tahadhari na kuwahakikishia kwamba usalama unatunzwa na shwari inapatikana.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa uandikishaji unaendelea na Pemba si shwari tena. Na moja katika sababu ni kwamba Jeshi la Wananchi, pamoja na polisi limepelekwa kule na silaha. Kiasi kwamba imekuwa ni tatizo.

Je, kupeleka Jeshi kubwa kama hilo, ni kusababisha uandikishaji ulio huru au ni kusababisha na kuwatisha wananchi ili wasiweze kujiandikisha na hatimaye kutoweza kupiga kura wakati kura ni *process*?

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Spika, nilidhani Mheshimwa Mnyaa anataka kuishukuru Serikali kwa kufanya kazi hiyo. Sasa kumbe kibao kimetugeukia. Sasa kama unasema hali si shwari, *the solution* moja ni kuona kama mnaweza mkapeleka vyombo pale viweze kudhibiti hiyo hali, ili waweze kufanya kazi iwe shwari zaidi.Mimi ndio

uwelewa wangu huo. Sasa sina hakika kwako hilo unaliona ni tatizo? Mimi nafikiri ndiyo njia rahisi kama una hofu, kukiwa na polisi wengi pale itasaidia sana na ikibidi hata Jeshi kama inaonekana kuna fujo za ziada zaidi.*( Kicheko na Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kabla halijapelekwa hilo Jeshi la polisi na Jeshi la wananchi, na kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani jana, kwamba askari mmoja kwa Tanzania Bara kwa raia 1300, kwa visiwani askari moja ni sawasawa na raia 30 tu na Pemba kulikuwa ni shwari, sasa kinachoshangaza. Je, Serikali inapeleka ujumbe gani kwa raia wa Tanzania na Mataifa kwa kupeleka Jeshi Pemba wakati kulikuwa na amani likaachwa kupelekwa Jeshi Tarime na Rorya kunako machafuko? ( *Makofi*)

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Spika, inawezekana Mheshimwa Mnyaa ana jambo anataka kusema lakini nadhani anapata shida. Kwa hiyo na mimi nashindwa kujibu kwa namna ambayo nitakusaidia. Mimi nadhani tufanye subira. Kama kuwepo kwa polisi na Jeshi pale itaonekana kweli ndiyo inafanya maeneo yale yasiwe shwari, basi Serikali itakuwa tayari kuchukua hatua zozote zile zinazositahili ili kuhakikisha kwamba tunawaondoa ikibidi hata wote, eeh! Kama tatizo ni hilo au kuweka kiwango ambacho tunafikiri kinawiana. Lakini kama bado hali haijafikia hatua yeyote ambayo unasema inapunja amani na utulivu, mie nafikiri tupige moyo konde. Mi nadhani wako pale kwa nia nzuri tu.

**MHE. JUMA S. N'HUNGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, swali langu mimi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu litahusu kero ya mlundikano katika magereza yetu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nadhani unaelewa fika kwamba magereza yetu yana mlundikano mkubwa sana na wanaochangia kuwa na mlundikano mkubwa ni mahabusu. Mahabusu ni wengi sana. Shida inayotokea kuwa mahabusu hao kuwa wengi ni mbili. Moja kubambikiziwa kesi wananchi wasiokuwa na hatia, lakini la pili ni ucheleweshaji wa kusikilizwa kesi. Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi za kutatua tatizo hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analolieleza Mheshimiwa Nh'unga nadhani ni dhahiri kwamba magereza yetu karibu yote nchini hapa yana idadi kubwa sana ya wafungwa lakini pamoja na mahabusu. Baadhi ya sababu anazozitoa ni kweli kwamba wakati mwingine ni kucheleweshwa kwa kesi au aina ya kesi zenyewe zinazohusika pengine ni zile ambazo hazihitaji dhamana kama mauaji. Lakini ninachoweza kusema tu kwamba ndio maana Serikali imejitahidi sana kujaribu kuweka taratibu za aina mbalimbali ikiwemo zile Kamati za kuharakisha usikilizaji wa kesi. Lakini vile vile hata *Parole* tuliyokuja tukaianzisha baadaye lengo lake ni hilo hilo kujaribu kuhakikisha kwamba zile kesi ndogo ndogo ambazo si lazima ziende kule ziweze kushughulikiwa kwa taratibu ambazo ni tofauti kidogo.

Kwa hiyo, hata haya Mabaraza tuliyokuja kuyaanzisha baadaye ya vijiji na Kata nayo yanalenga kujaribu kupunguza kwa kiasi kikubwa mlundikano katika magereza yetu. Kwa hiyo, ni jambo linajulikana na Serikali na tunaendelea kufanya juhudi kubwa

naamini kadri muda unavyokwenda pengine huenda tukachukua hatua za kuongeza sehemu nyingine ya magereza kama ikibidi. Kwa sababu tatizo ni kwamba idadi ya watu inaongezeka na kwa hiyo, makosa vile vile yanaongezeka, na kwa hiyo, lazima tuwe na mpango vile vile wa kuongeza maeneo haya kwa ajili ya kuhifadhi wafungwa pamoja na mahabusu. Kwa hiyo, tutajitahidi kujaribu kuona namna ya kupunguza kasi hiyo. (*Makofi*)

**MHE. JUMA S. N'HUNGA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yake mazuri. Amejibu hali halisi. Lakini ninachopenda kujua wale wanaobambikiziwa kesi kwa makusudi ambao wamo kwenye magereza hivi sasa kama mahabusu juhudi gani za Serikali za kuhakikisha hivi sasa kwamba hilo tatizo linatoka na wale wanaobambikizia kesi wanachukuliwa hatua gani?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, wakati mwingine si rahisi sana kujua ni kesi ipi imebambikizwa na kesi ipi ni ya kweli. Lakini ninachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Juma Nh'unga tu ni kwamba Serikali inajitahidi sana kupitia vyombo vyake kujaribu kupitia majalada haya ya polisi kila inapowezekana, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inafanya hiyo kazi, lakini hata Mahakimu wanafanya hiyo kazi. Kila wanapofanya ukaguzi wakati mwingine wanatoa amri za papo kwa papo ili zile kesi ndogo ndogo ambazo zinaonekana hazina msingi ziweze kufutwa au kuondolewa kabisa katika mfumo wa Mahakama.

Kwa hiyo, ndiyo maana nasema tukubali tu kwamba tatizo ni pana zaidi kuliko suala la ubambikaji kesi peke yake, maana tukianza kushughulika hilo maana yake ni kwamba tutakuwa tunawaasa Watanzania hasa polisi na hasa Watanzania wenyewe tunaotoa malalamiko tusitoe malalamiko ambayo hayana msingi kwa maana ya kumkomoa mtu. Na kama ni vyombo vya dola tutimize wajibu wetu kwa kuzingatia maadili ya kazi zetu. Tukiyachanganya yote kwa pamoja tunaweza tukapunguza kasi kubwa sana ya mlundikano katika magereza yetu. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. KABWE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu suala la uwekezaji, tarehe 24 Julai, 2008 katika Mkutano wa 12 nilikuuliza swali kuhusiana na majadiliano yaliyokuwa yanafanyika kati ya Serikali yetu na Serikali ya Canada kuhusu *Foreign Investment Protection Agreements* na katika majibu yako naomba kunukuu kutoka kwenye *Hansard*, pamoja na mambo mengine ulisema: *"Mimi sijaona na sijapata nafasi pengine ya kuzungumza na Mheshimiwa Waziri Membe. Kwa hiyo, labda nitende haki kwa kusema hebu nipe muda basi na mimi nilitazame."* Mwaka sasa umepita, ulipata muda kulitazama suala hili na unaliambia nini Taifa kuhusu suala hilo? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe unangoja mpaka mwaka upite bwana ndiyo unaniuliza tena? Ungenikaba koo siku zile za mwanzoni mwanzoni pengine nimeshatoa suluhu ya jambo hilo.

Lakini labda niseme tu ningekuwa kwamba mimi nililifanyia kazi,nikapewa maelezo. Lakini sasa mwaka mzima umeshapita na nilidhani na wewe umesahau kumbe bado unakumbuka. Lakini niseme tu kwamba kwa maelezo niliyopewa mikataba ya aina

hiyo si Canada tu, tunayo Mikataba kati yetu na Uingereza, Mikataba na Canada na lengo lake kwa ujumla wake ni zuri. Isipokuwa tu pale ambapo pengine tumekosa kuwa waangalifu sana. Kwa sababu kinachozungumzwa pale ni kwamba ni namna tu ya kuwavutia na kuwatia moyo wawekezaji wanapokuja kuwekeza basi wawe na uhakika kwamba katika kufanya shughuli hiyo watakuwa na mahusiano ambayo yatawezesha kufanya shughuli zao vizuri ndio hasa lengo la ile Mikataba ambayo tumekuwa tukiiweka kati ya nchi za nje fulani fulani na sisi hapa Serikalini.

Kwa hiyo, mimi nadhani nia si mbaya. Lakini kama pengine una jambo mahsusi kwa Canada ambalo unaona pengine Serikali ni lazima ilifanyie kazi na ungependa pengine tutoe ufumbuzi wa jambo fulani, lakini kwa maelezo niliyopewa mikataba ile ni ya jumla na lengo lake, linapaswa kuwa la namna hiyo.

**MHE. KABWE Z. KABWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa nilinayo ni kwamba *round* ya mwisho ya mazungumzo kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Canada ilifanyika kati ya tarehe 15 mpaka tarehe 18 Septemba, 2008. Katika moja ya vitu ambavyo Serikali ya Tanzania ime-*offer* kwa Serikali ya Canada ni kulinda kabisa hata pale ambapo yanapotokea makosa ya dhahiri kwa mfano kama ilivyotokea katika tatizo la *North Mara* kulinda uwekezaji ule wa Canada na hasa hasa katika sekta ya madini kwa sababu ndiyo inapoongoza.

Je, iwapo mikataba hii inalinda makampuni ya Canada na wakati mwingine inakuwa juu ya Sheria zetu na kwa mfano tatizo lililotokea *North Mara* kwa wananchi kuweza kupata matatizo kutokana na kutumia maji ya sumu, Serikali inaweka tahadhari gani ili pale ambapo itakapofikia kwamba ni lazima Sheria zetu zichukue mkondo tuweze kuepuka hiyo mikataba? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mkataba ule ni wa jumla sana. Si mkataba ambao unatawala kila jambo linalohusiana na mikataba tunayoingia na nchi hiyo katika Taifa letu. Ndiyo maana hata unapokuja kuanza kushughulikia mkataba wa aina nyingine yoyote ni lazima ndani ya mkataba huo kuwepo na vifungu ambavyo vitasaidia kuweza kuwalinda Watanzania. Ule ni mkataba tu wa kutoa matumaini/faraja za namna fulani lakini si kwamba mkataba ambao utaongoza kila jambo.

Kwa hiyo, hata kesi ya *North Mara* ile maadamu tumeanza kupata maelezo kutoka *step* mbalimbali pale ambapo itahitajika hatua za dhati kuchukuliwa dhidi ya mwekezaji, zitachukuliwa tu bila kujali kwamba ule mkataba upo kwa sababu uko mkataba ambao unatawala mazingira ya pale kwenye mgodi na huo ndiyo tunatakiwa sisi tuuzingatie zaidi kuliko kitu kingine chochote?

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu utakumbuka kuwa mwaka jana ulikubali baada ya maombi yangu kuunda Tume ya kufanya uchunguzi juu ya mgogoro wa shamba la Sukanya kati ya wananchi wa Kitongoji cha Sukanya na mwekezaji wa Kampuni ya

*Thomson Safari* ya *Boston* Marekani. Nashukuru mchakato huo umeendelea lakini bado Mheshimiwa Waziri Mkuu hatujapata matokeo ya Tume hiyo. Lakini kana kwamba hiyo haitoshi wiki mbili zilizopita kuna operesheni katika eneo, katika Kitalu cha Uwindahi imefanyika cha Kampuni ya (*OBC), Ortello Business Coperation.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, lenga swali tafadhali.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu je, Serikali ina taarifa ya operesheni hiyo ambayo zaidi ya maboma 25 yamechomwa moto na mazao kuungulia ndani ya majumba hayo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Telele swali lake kama ifuatavyo: Kwanza nakubali kwamba tuliunda timu imekamilisha uchunguzi. Taarifa ililetwa ofisini kwangu na mimi kwa msingi wa ushirikishwaji wa jamii nikachukua taarifa ile nikairejesha kwenye Halmashauri yake ili iweze kujadiliwa na wahusika kwanza, ili yale yaliyopendekezwa yawe ni mambo vile vile ambayo inaonekana yamekubalika na Halmashauri husika. Baada ya pale nikashauri mapendekezo kutoka kwenye Halmashauri yaende sasa kwenye Kamati ya Mashauriano ya Mkoa *(RCC).*

Baada ya pale ndiyo Mkoa uturejeshee mapendekezo ambayo yatakuwa yamezingatia maslahi ya sehemu zote mbili. Tangu nimewapelekea sijapata mrejesho. Kwa hiyo, siwezi nikasema Mkoa umesema nini na Halmashauri imesema nini.

Lakini kuhusu hii sehemu ya pili ya operesheni anayosema imesababisha kuunguzwa nyumba nyingi pale kwenye eneo la kitalu lazima nikiri mimi sijapata hiyo taarifa lakini ni imani yangu pengine Wizara ya Kisekta inayo hiyo taarifa. Lakini kwa sababu umeniarifu na mimi nitachukua hatua za kufuatilia kuona kilitokea nini ili tuweze kuchukua hatua stahiki kurekebisha kasoro zozote zile. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kumwuliza swali moja Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeshafanya chaguzi tatu za vyama vingi hapa nchini. Karibu chaguzi zote tatu kumekuwa na malalamiko ama ndani ya nchi ama nje ya nchi ama kote kote kwa uchaguzi upande wa Zanzibar.

Sasa tunaelekea kwenye uchaguzi wa mara ya nne. Unatoa kauli gani kwamba uchaguzi ujao 2010 utakuwa huru na wa haki hasa upande wa Zanzibar?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi siyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, nataka kwanza lijulikane hilo. Kwa hiyo, kuna mambo naweza nikayasemea vizuri sana kwa niaba ya Serikali lakini mengine inabidi kuwa mwangalifu tu unapotaka kuyasema. Ukinitaka nitoe kauli kulithibitishia Taifa hili kwamba uchaguzi

wa mwaka kesho kabisa utakuwa hivi na hivi nitasema maana yake unanipa kazi mimi kubwa ambayo si ya kwangu.

Lakini nataka niseme kwamba suala la uchaguzi ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwa shwari, huru ni swala ambalo linawagusa Wazanzibar wote kwa ujumla wao. Bila kujali itikadi zao na wala kujali imani zao ni lazima wote washirikiane kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha wanajiwekea misingi mizuri ya kuheshimiana na kuweza kwa kweli kulumbana lakini bila kupigana. Wakidhamiria kwa dhati Wazanzibar wanaweza kabisa wakafanya uchaguzi ukawa mzuri na ukaisha vizuri sana.

Kwa hiyo, mimi nadhani ni suala la dhamira kwa pande zote mbili. Kwa hiyo, ninachoweza kusema kama Waziri Mkuu ni kutoa tu mwito kwa Wazanzibar kujaribu kukaa pamoja.

Kujaribu kuhakikisha yale maeneo yanayowaletea tofauti basi wayapunguze ikibidi wayaondoe ili kuweza kufanya uchaguzi uwe mzuri zaidi huko tunakokwenda. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu hayo. Lakini ili uchaguzi uwe huru na haki lazima taratibu zianze kufuatwa na zitekelezwe katika mikondo yote mitano ya uchaguzi kuanzia kuandikisha, kampeni, kupiga kura, kuhesabu kura na hatimaye matokeo. Hivi sasa tuko katika kipindi cha uandikishaji na tayari dosari kadhaa zimejitokeza katika uandikishaji.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na kusema kwamba wewe sio Rais wa Jamhuri ya Muungano, lakini ni Msimamizi wa Shughuli za Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar ni Serikali yenu. Huoni kwamba. *(Kicheko/Makofi)*

Nakusudia kwamba ni Serikali yenu kwamba iko chini ya Mamlaka yenu. Lahaula!

**SPIKA:** Mpeni nafasi Waheshimiwa

**MHE. ALI SAID SALIM:** Naomba mnipe nafasi, CCM mna matatizo jamani. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Utulivu, *order please*, utulivu tafadhali.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, naomba uwatoe nje wote wanaopiga kelele. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Spika, tayari hivi sasa kuanzia hatua ya awali ya uandikishaji Jimbo moja tu karibu vijana elfu moja na zaidi hawajaandikishwa na hakuna sababu ya msingi. Huoni kwamba tunaweka mazingira katika uchaguzi wa 2010? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimesema hivi suala hili ni lazima liangaliwe kwanza kutoka ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na nimesema kwa nini. Ni kwa sababu mnayo Sheria pale inayosimamia suala la Uchaguzi ndani ya Visiwa vya Zanzibar.

Sheria hiyo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi na ni Sheria hiyo hiyo iliyoweka hivyo unavyoviita vitambulisho vya ukaazi, likakubalika na Baraza hilo na imekuwa ikitumika pale kama ndiyo Sheria kamili.

Ndiyo maana nimesema kama liko tatizo turudi kwenye Baraza la Wawakilishi tukafanye marekebisho ili yaweze kuwiana na matarajio ya kile mnachokisema. Kwa sababu mimi nina hakika kama Baraza lilikaa likakubaliana lote kwa pamoja juu ya mfumo huo lazima kuna sababu zilizofanya wakafikia pale. *(Makofi)*

Ndiyo maana nasema dawa peke yake ni hiyo tu. Vinginevyo nimemwambia Mheshimiwa hapa nikasema lakini kama mnaona nalo hilo gumu twendeni tukatafute jambo kwa mfumo wa kawaida wa kwenda Mahakamani kujaribu kuweka hoja ili tuone Mahakama zitakavyoamua. Lakini ili mradi Sheria ile ipo kwa sasa, walahi ndugu Ali hakuna ujanja itabidi muendelee na hiyo hiyo Sheria. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Huo ndiyo mwisho wa Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Ahsante sasa hatua inayofuata Katibu tuendelee.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Swali la kwanza kwenye maswali ya kawaida linaelekezwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Anauliza Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba.

Na. 181

### Ujenzi wa Chuo cha *VETA* kwenye kila Wilaya nchini

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 ni pamoja na kujenga Chuo cha *VETA* kwenye kila Wilaya na kwa kuwa Wilaya ya Kwimba ilikuwa ni miongoni mwa Wilaya tano (5) za kwanza kujengewa chuo hicho kwa mujibu wa ahadi za Serikali kupitia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2008/2009.

(a) Je, maandalizi ya ujenzi wa chuo hicho katika Wilaya ya Kwimba yamefikia asilimia ngapi?

(b) Je, ujenzi huo katika Kijiji cha Kilyaboya ambako Wilaya imetenga eneo maalum kwa ajili ya ujenzi huo umepangwa kuanza na kukamilika lini?

(c) Kwa mujibu wa mpango kazi wa shughuli za ujenzi wa chuo hicho. Je, wanachuo wa kwanza wa kujiunga na chuo hicho wanapangiwa wajiunge mwaka gani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba, naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kwimba ni miongoni mwa Wilaya 28 zilizo katika awamu ya kwanza ya mpango wa ujenzi wa vyuo vya ufundi vya *VETA* Wilaya. Aidha, mpango huo ni kwa ajili ya Wilaya ambazo hazina chuo chochote cha ufundi cha Serikali au binafsi.

Baada ya kutoa maelezo hayo, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:- (a) Mheshimiwa Spika, maandalizi ya awali yamefanywa kwa Wilaya zote 28 zilizopo katika mpango huu. Kwanza ni uchambuzi stadi umefanyika kwa Wilaya zote ikiwemo Wilaya hiyo ya Kwimba, maandalizi ya michoro ya vyuo, andiko la mradi limeandaliwa na kuwasilishwa kwa wafadhili kwa ajili ya kuombea fedha.

(b)Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika kijiji cha Kilyaboya utaanza mara baada ya kukamilika taratibu za maandalizi ikiwa ni pamoja na kupata fedha kutoka kwa wafadhili. Kwa sasa kazi ya upimaji wa eneo la chuo imeishakamilika na michoro imepelekwa Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kuthibitishwa.

(c)Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tuko katika maandalizi ya ujenzi wa vyuo 28 vya *VETA* Wilaya, si rahisi kwa sasa kusema ni lini wanachuo wa kwanza watajiunga na chuo na kuanza masomo.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana hasa kwa kuendelea kuiweka Kwimba katika Awamu ya Kwanza na ujenzi wa chuo hicho katika Kijiji cha Kilyaboya. Nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ahadi hii ilitolewa mwaka jana takriban mwaka nzima kufikia leo. Taarifa tulioipata sasa hivi ni kwamba andiko la mradi huo ndiyo limekamilika na ndiyo limepelekwa kwa Wafadhili kwenda kuomba fedha. Naomba kujua wakati ahadi hii inatolewa mwaka jana ilijijenga katika misingi ipi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, ahadi iliyotolewa na Serikali ilikuwa ni ya kweli, kwanza niseme hivyo. Kwa sababu ilikuwa katika misingi ya kujenga hivi vyuo kwa ajili ya ufundi stadi katika maeneo mbalimbali Wilayani katika nchi yetu. Kwa hiyo, tulifahamu kwamba baada ya kutoa ahadi lazima tutafute fedha na kabla hatujapata fedha lazima tuandike andiko ili tulipeleke kwa wafadhili waliangalie wakubali watuletee hizo fedha na mambo yote haya sasa yameishakamilika na tunashukuru Wilaya nyingi zimeishatoa viwanja lakini pia ni lazima Wizara irudi tena kuthibitisha kwamba hivyo viwanja kweli vimetolewa. Kwa hiyo, yote haya ni maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivi na ninaomba tuvute subira vyuo hivi vitajengwa.

Na. 182

**Utafutaji Mafuta na Gesi katika Mambo ya Muungano**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa mjibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, mafuta na gesi asili yapo katika orodha ya Mambo ya Muungano tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000; na kwa kuwa nchi imekuwa ikichimba gesi ya *Mnazi Bay* na *Songo Songo:-*

(a) Je tangu gesi hiyo ilipoanza kuchimbwa hadi leo ni kiasi gani cha faida kimepatikana?

(b) Je, Zanzibar imepatiwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mafuta ghafi na gesi asili yaliingizwa katika orodha ya Muungano tangu mwaka 1968. Kwenye majibu yetu tumesema 1965 ni 1968, baada ya kuifanyia marekebisho madogo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1965 na sio mwaka 2000 kama ilivyoelezwa kwenye swali.

Mheshimiwa Spika, gesi asilia iligunguliwa katika maeneo ya Kisiwa cha Songo Songo Mkoani Lindi mwaka 1974 na *Mnazi Bay* Mkoani Mtwara mwaka 1982 na kampuni ya *AGIP* ya Italia.

Gesi asilia *Songo Songo* ilianza kuzalishwa mwezi Julai, 2004 kwa ajili ya kuzalisha umeme na kuendesha mitambo katika Kiwanda kama kiwanda cha Saruji cha

*Wazo Hill, Dar es Salaam* na gesi ya Mnazi ilianza kutumika kuzalisha umeme kwa ajili ya mji wa Mtwara na Lindi mwezi Desemba, 2006.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2009, gesi asili yenye thamani ya dola za Marekani 149.7 milioni ilizalishwa toka *Songo Songo* na *Mnazi Bay*.

Japokuwa hadi sasa gesi iliyozalishwa haijaweza kurudisha gharama za uwekezaji, nchi yetu imenufaika kwa kiasi kikubwa tangu kuanza kwa matumizi ya gesi asilia. Mapato ya Serikali yaliyopatikana kutokana na uzalishaji wa gesi asili nchini tangu mwaka 2005/2006 mpaka mwaka 2008/09 (Aprili, 2009), ni Sh. 50.8 bilioni. Hii ni mbali na faida za kiuchumi na kijamii zilizopatikana kutokana na uzalishaji wa gesi hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapa Bungeni tarehe 15 Julai, 2008 kuwa mapato yote yatokanayo na gesi hupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ambao unagharamia kazi za Serikali ya Muungano.

Pia kama ilivyoelezwa hapa Bungeni wakati tukijibu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge tarehe 27 Januari, 2009 mwaka huu na wakati tukiwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu tarehe 08 Julai, mwaka 2008 Serikali mbili ndani ya Muungano zimemwajiri Mshauri Mwelekezi kampuni ya *AUPEC* kutoka Uingereza ili pamoja na mambo mengine azishauri Serikali hizi namna ya kugawana gharama na mapato yatokanayo na shughuli za utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mshauri amewasilisha ripoti yake ya mwisho Serikalini (SMT na SMZ) tarehe 23 Juni, mwaka huu, Wizara husika za Serikali hizi zinayafanyia kazi mapendekezo ya Mshauri ili kuangalia namna bora ya kuyatekeleza. Hivyo, mpaka sasa mgao wa gharama na mapato yatokanayo na mafuta na gesi haujaafikiwa.

Aidha, kwa kuwa suala hjili pia limejadiliwa na kupokewa taarifa kwenye vikao vya Muungano, ni imani yangu kwamba muafaka wa namna bora ya kugawana gharama na mapato ya rasilimali hii ya gesi asili katika Jamhuri ya Muungano itafikiwa ndani ya muda mfupi, kwa kuwa hatua mbalimbali muhimu zimeshakamilika.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mara nyingi Mheshimiwa huwa unanisahausahau. Inaonekana kuanzia sasa hivi hili jina ulikariri, Vuai Abdallah Khamis. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sawasawa.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nimpongeze sana kwa kujibu suala langu na hata

hivyo ameonyesha nia nzuri sana au Serikali imeonyesha nia nzuri ya jambo hili kulipatia ufafanuzi haraka. Lakini kwa muda mrefu wananchi wa Tanzania hasa kule Zanzibar wanalitaka lipatiwe ufafanuzi haraka. Sasa je pamoja na jibu lako zuri hilo unasemaje kuhusu hili?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, wanasubiri kwa hamu na wanataka jibu haraka.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, jambo hili liko kwenye vikao vya viongozi wawili wakuu, Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano chini ya Uwenyekiti wa Makamu wa Rais. Hili jambo ni kweli limechukua muda mrefu.

Lakini tulifikia hatua tukasema kwa sababu ya mambo yenyewe yalivyo ya mafuta na *complications* zilizokuwepo, tumeajiri Kampuni kwa ridhaa ya Serikali zote mbili, Kampuni ambayo tunatarajia ya kufanya masuala kama hayo hasa kwa sababu huko Uingereza kwenyewe kule Scotland Kaskazini hilo jambo lilishafanyiwa kazi na ilikuwa ni jambo lilikuwa linasumbuasumbua wakati huo.

Mheshimiwa Spika, wataalam walikutana wa pande zote mbili Aprili, 2009 Zanzibar wakapata taarifa ya awali, wakaifanyia maboresho, akapewa Mshauri Mwelekezi ameifanyia kazi tumepewa tarehe 23 mwezi huu na ni imani yangu kwamba sasa hivi Wizara hizi mbili kwa kuwa sote tumeipokea kila mmoja anaifanyia kazi na kwa sasa hivi tumefikia hatua nzuri, taratibu zimekwenda vizuri na ratiba inakwenda vizuri. Ni imani yangu kwamba tutafikia muafaka hivi karibuni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Itakuwa ni 23 mwezi uliopita wa Juni, 2009. Wawili, Mheshimiwa Zitto mafupi tu. Hapana, hapana. Anza Mheshimiwa Zitto. *(Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Kwanza mwaka 1968 hapakuwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa ni Katiba ya muda. Kwa hiyo, suala hilo kuingizwa kwenye mambo ya Muungano mwaka wa 1968 nayo pia inaleta mashaka.

Lakini swali langu linakuja kwamba jana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetangaza kuliondoa suala la mafuta na gesi kwenye masuala ya Muungano. Serikali inatoa Kauli gani katika suala hili kwa sababu huko ni kutangaza mgogoro wa Katiba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zitto Zubeir Kabwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Julai, 1968 Mzee Rashid Mfaume Kawawa alisimama hapa kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Akatoa hoja ya kuleta mafuta kama suala la Muungano ili kubadilisha *Interim Constitution* ya Tanzania ya mwaka 1965 na

Mheshimiwa Spika, *Hansard* iko hapa Mzee Kawawa alihimiza kwamba hilo ni jambo ambalo lilikuwa limeridhiwa na pande zote mbili, kwa kuwa Baba wa Taifa alikuwa amekwenda kwenye Baraza la Mapinduzi alikuwa amezungumza nao, Makamu wa Kwanza wa Rais alikuwa amekuja huku.

Kwa hiyo, ni jambo ambalo lilifanyiwa mazungumzo kwa kina na yakakubaliwa na pande zote mbili na yakaja kuwekwa kama msingi wa Katiba humu ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, mimi kama yeye nimeisikia kauli ya Mheshimiwa Mansour kwenye Redio na Magazeti. Lakini ni imani yangu kwamba kwa kuwa mambo haya yana utaratibu wake, utaratibu ambao unastahili ni ule ambao labda sisi tutapokea barua ambayo inatoa hoja hiyo. Na kwa kuwa labda hoja ilikuwa imezungumzia kufanya marekebisho ya Katiba ili mafuta lisiwe jambo la Muungano. Bado jambo hilo bado linatakiwa kuja kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano kama lilivyofanywa mwaka 1968. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naamini hiyo ilikuwa ni Kauli ya Waziri lakini hayakuwa maamuzi ya Bunge. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mwongozo wa Spika. Kanuni ya 68. Mheshimiwa Zitto Kabwe hapa ametamka matamshi mazito mawili yanayopotosha ukweli. Kwanza amesema kwamba mwaka wa 1968 hakukuwa na Katiba kwamba kulikuwa na uwazi. Jambo ambalo sio kweli. Mwaka wa 1968 kulikuwa na Katiba ya Muda ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, hakukuwa na uwazi. Kulikuwa na Katiba na mambo yote yaliyotendeka katika Bunge wakati ule yalikuwa yametendeka kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, upotoshaji wa pili, anasema kwamba sasa kuna jambo limenyofolewa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Ninavyofahamu Katiba ya Jamhuri ya Muungano bado iko *intact* hakuna jambo lililoondolewa mpaka leo. Kwa hiyo, pengine tungepata mwongozo wako Mheshimiwa Spika, ili aondoe Mheshimiwa Mbunge matamshi haya ambayo kwa kweli yanapotosha taifa na dunia kwa ujumla. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kuhusu nchi kutokuwa na Katiba hilo si kweli ni dhahiri kabisa. Hakuna wakati wowote nchi yetu ilikuwa haina Katiba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hilo amepotoka, na si lazima nimtake yeye mwenyewe afute. Inatosha mimi nikisema kwamba yeye amekosea, ndiyo amekosea. *(Makofi)*

Pili, pia amekosea, huwezi kunyofoa kitu chochote hata kama ndivyo unapenda mtu yoyote katika Tanzania hata nje, ni upuuzi. Lakini hakuna Mtanzania anayeweza hata akipayuka basi sisi tumeondoa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano hawezi, tunaoondoa ni sisi Bunge huku basi, humu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Zitto uwe mwangalifu na kauli zako maana yake leo kauli zote mbili zimekuwa sifuri. Nakusamehe kwa sababu mwaka 1968 wewe ulikuwa wala hujazaliwa. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Utoto. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea, Waheshimiwa Wabunge, sasa hakuna nyongeza tena hapo. Tunakwenda Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Basil Mramba.

Na. 183

**Matumizi ya Maji ya Ziwa Challa – Rombo**

**MHE. BASIL P. MRAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali za Kenya na Tanzania zimekuwa zikijadili kwa muda mrefu sana namna ya kugawana maji ya Ziwa Challa Wilayani Rombo:-

(a) Je, ni nini matokeo ya majadiliano hayo?
(b) Je, Serikali ina mpango gani kuhusu matumizi ya maji hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali za Kenya na Tanzania tangu mwaka 1994, zimekuwa na majadiliano ya kitaalam juu ya matumizi na usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji katika Ziwa Challa. Mwaka 2004, majadiliano hayo, yalihusisha pia rasilimali za maji ya Ziwa Jipe na Mto Umba katika Wilaya za Rombo, Same, Mwanga, Lushoto, Muheza na Mkinga. Mwezi Juni, 2006 Programu ya Pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Ziwa Challa, Ziwa Jipe na Mto Umba ilizinduliwa mjini Moshi. Lengo kuu la Programu hii ni kutengeneza mazingira mazuri kwa nchi hizi mbili ili ziweze kuandaa mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kutumia rasilimali hizi kwa njia ya usawa na endelevu na kubaini miradi itakayotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza lengo hili, Programu imependekeza muundo unaoitaka kila nchui kuunda Kamati ya Kitaifa na Kamati ya Pamoja ya nchi zote mbili chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Serikali imeunda Kamati ya Kitaifa ya kuratibu utekelezaji wa Programu hii chini ya uratibu wa Ofisi ya Maji Bonde la Mto Pangani.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sera ya Maji ya mwaka 2002, usimamizi na upangaji wa matumizi ya rasilimali za maji ya kimataifa unatakiwa kuwa wa ushirikiano na nchi shiriki unaozingatia misingi ya usawa na haki na kwa uwiano unaofaa. Hivi sasa maji ya Ziwa Challa yanatumiwa na hoteli mbili za kitalii, moja ikiwa Tanzania na nyingine Kenya. Usimamizi na matumizi ya maji ya Ziwa Challa kwa sasa unakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na takwimu za kutosha za kihaidrolojia na baionuai kuhusu rasilimali za maji katika ziwa hilo.

Ili maji ya Ziwa Challa yaweze kutumiwa na wananchi wa Rombo, utafiti wa kina utafanyika katika Ziwa Challa, chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji, ili kufahamu mizania ya maji ya Ziwa Challa na kuandaa mipango ya maji hayo kwa wananchi wa Rombo.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na uhaba wa rasilimali za maji kwa matumizi mbalimbali katika Wilaya ya Rombo, Wizara yangu, katika mwaka wa 2008/2009, iliandaa zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi atakayefanya tathmini ya kina juu ya wingi, ubora na mahitaji ya maji kwa matumizi ya sekta mbalimbali katika eneo la Mlima Kilimanjaro, Ziwa Challa na Ziwa Jipe.

Aidha, mpango wa pamoja na matumizi ya rasilimali za maji katika Bonde la Pangani utaandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Mpango huu utatoa dira ya matumizi ya rasilimali za maji katika Bonde la Mto Pangani likiwemo Ziwa Challa.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake zuri. Nina maswali mawili madogo. Kwanza je, ni kweli kwamba upande wa Kenya tayari wanatumia maji haya kwa umwagiliaji kwenye Halmashauri ya Taita Taveta? Na kama ndivyo hivyo Serikali yetu inachukua hatua gani kwa mujibu wa jibu lake?

Je, kwa kuwa maji ya mto Challa yanatokana na mtiririko wa mito kutoka ardhini upande wa Tanzania na kwa kuwa kuwa mito mingi ya aina hiyo inajitokeza siyo tu kwenye Ziwa bali pia kwenye eneo la Kenya, lakini maji ni ya Tanzania. Kule wanayatumia kunywa na kumwagilia. Je, mazungumzo hayo yatabaini pia matumizi ya maji hayo yanayotokea Rombo kwenda Kenya lakini Rombo wasiyapate?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikiri kwamba sina hakika kama upande wa Kenya wanayatumia maji hayo. Nataka nimhakikishie kwamba tutaendelea kutazama jambo hili kwa njia za ushirikiano kwa sababu tayari tumeshaanzisha ushirikiano kati ya Tanzania na Kenya kuangalia matumizi ya maji ambayo ni maji shirikishi.

Lakini nataka niseme kwamba kama wenzetu wa Kenya wanayatumia basi mazungumzo ambayo yanaendelea sasa yataweka mfumo thabiti ambao utahakikisha kwamba maji yanatumika kwa misingi ambayo tutakuwa tumekubaliana.

Ndiyo maana tumeunda Kamati au ni kama Kamisheni ambayo itakuwa inasimamia matumizi shirikishi na siyo ya hili Ziwa tu ni pamoja na yale maziwa mengine kama nilivyosema Ziwa Jipe, na Mto Umba. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba tutaangalia kama kweli Kenya wanatumia maji hayo na wanatumia kwa misingi gani.

Swali la pili, kuhusu maji yanayotumika kule. Kwa ujumla niseme tu Mheshimiwa Mramba kwamba haidrolojia ya Ziwa Challa ambalo ni aina ya mfumo wa *creater* haijajulikana sawasawa na ndiyo maana tumeweka Mtaalam kwa ajili ya kuangalia haidrolojia na mfumo mzima unaoingiza maji katika Ziwa lile.

Hadi sasa mimi ninavyojua ni kwamba mfumo wa kuingiza unajulikana lakini mfumo wa kutoa maji nje ya ziwa haujulikani.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba tutafanya utafiti huu kwa kushirikiana na Kenya na matokeo ya ushirikiano tutaweka bayana kusudi matumizi yawe na manufaa kwa nchi zote mbili.

Na. 184

**Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kutekelezwa**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa mikoa ya Singida, Dodoma, Tabora na Shinyanga inaweza kuondolewa kabisa tatizo la maji kwa kutumia vizuri maji ya Ziwa Victoria na kwa kuwa, mradi endelevu wa maji ya Ziwa Victoria utawezesha mikoa hii kupata maji kwa matumizi ya binadamu, mifugo na umwagiliaji:-

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, ni lazima mradi huu utekelezwe?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Samuel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, napenda kutoa maelezo mafupi tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa kutumia Ziwa Victoria kama chanzo cha maji kwa mikoa kame kama ya Shinyanga, Tabora, Singida na Dodoma ni wa muda mrefu, hasa tangu kabla ya uhuru.

Tangu wakati huo hapakufanyika uamuzi wa kuutekeleza hadi mwaka wa fedha wa 2004/2005 wakati ambapo Serikali ya Awamu ya Tatu iliamua kutenga fedha za ndani kuanza kutekeleza mradi mkubwa wa maji kwenda katika miji ya Shinyanga na Kahama. Ujenzi wa mradi huu, unaopitia vijiji 54 vilivyopo katika Wilaya za Misungwi, Kwimba, Shinyanga Vijijini na Kahama, umekamilika na ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30/5/2009. Kwa sasa, mradi una uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za ujazo 80,000 kwa siku.

Kiasi hiki kinaweza kutosha mahitaji ya maji kwa watu 450,000 pamoja na mifugo yao kwa sasa. Aidha, ifikapo mwaka 2016 mradi utaongezewa uwezo wa kuzalisha hadi mita za ujazo 120,000 kwa siku, kiasi ambacho kitatosha mahitaji ya maji kwa watu 1,000,000 pamoja na mifugo, viwanda na migodi iliyo jirani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ipo kwenye mchakato wa kusanifu mtandao wa usambazaji maji kwenye vijiji vyote vilivyopangwa kuhudumiwa na mradi. Lengo ni kuhakikisha kuwa mradi huu unawanufaisha wananchi wengi zaidi katika maeneo husika, kama ilivyokusudiwa na wanavijiji wasitembee umbali urefu kufuata maji kwenye vituo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Samuel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika maelezo yangu ya utangulizi, Serikali imedhamiria kutumia maji ya Ziwa Victoria kadri inavyowezekana katika jitihada zake za kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la maji katika mikoa kame aliyotaja Mheshimiwa Mbunge. Ushahidi wa dhamira hii ni utekelezazji wa mradi mkubwa na wa kihistoria wa kupeleka maji katika miji ya Shinyanga na Kahama.

Lengo la Serikali ni kuendelea kujenga na kukuza uchumi wake ili hatimaye kujenga mradi mkubwa zaidi kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye mikoa ya Tabora, Singida na Dodoma ili uweze kutekelezwa kulingana na uwezo wa Serikali kiuchumi hapo baadaye. Hivi sasa, Wizara yangu imejielekeza zaidi kwenye upanuzi wa mtandao wa usambazaji maji kwenye maeneo yote yanayopitiwa na mradi katika awamu ya kwanza ili uweze kunufaisha wananchi wengi zaidi ya walio umbali wa zaidi ya kilomita tano.

Baada ya kukamilisha usambazaji wa maji katika vijiji vilivyoainishwa Serikali itaangalia uwezekano wa kupanua mradi. *(Makofi)*

Kutekeleza mradi mkubwa wa maji kwenda katika miji ya Shinyanga na Kahama. Ujenzi wa mradi huu unaopitia vijiji 54, vilivyopo katika Wilaya za Misungwi, Kwimba, Shinyanga Vijijini na Kahama, umekamilika na ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 30 Mei,

2009. Kwa sasa mradi una uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha meta za ujazo elfu 80 kwa siku.

Kiasi hiki kinaweza kutosha mahitaji ya maji kwa watu 450,000 pamoja na mifugo yao. Aidha ifikapo mwaka 2016, mradi utaongezewa uwezo wa kuzalisha hadi meta za ujazo 120,000 kwa siku, kiasi ambacho kitatosha mahitaji ya maji kwa watu milioni moja pamoja na mifugo, viwanda na migodi iliyo jirani.

Wizara yangu ipo kwenye mchakato wa wa kusanifu mtandao wa usambazaji maji kwenye vijiji vyote vilivyopangwa kuhudumiwa na mradi. Lengo ni kuhakikisha kuwa mradi huu unawanufaisha wananchi wengi zaidi katika maeneo husika, kama ilivyokusudiwa ili wanavijiji wasitembee umbali mrefu kufuata maji kwenye vituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kwa ufupi kujibu swali la Mheshimiwa Nyalandu, kama ifuatavyo: Kama nilivyosema katika maelezo yangu ya utangulizi, Serikali imepanga kutumia maji ya Ziwa Viktoria, kadiri inavyowezekana katika jitihada zake za kupata ufumbuzi wa kudumu katika mikoa kame aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Ushahidi wa dhamira hii ni utekelezaji wa mradi mkubwa na wa kihistoria wa kupeleka maji katika miji ya Shinyanga na Kahama. Lengo la Serikali ni kuendelea kujenga na kukuza uchumi wake ili hatimaye kujenga mradi mkubwa zaidi kutoka Ziwa Viktoria, kwenda kwenye mikoa ya Tabora, Singida na Dodoma, ili uweze kutekelezwa kulingana na uwezo wa Serikali kiuchumi hapo baadaye. Hivi sasa Wizara yangu imejilekeza zaidi kwenye upanuzi wa mtandao wa usambazaji wa maji kwenye maeneo yote yanayopitiwa na mradi katika awamu ya kwanza, ili uweze kunufaisha wananchi wengi zaidi walio umbali wa zaidi ya kilometa tano. Baada ya kukamilisha usambazaji wa maji katika vijiji vilivyoainishwa, Serikali itaangalia uwezekano wa kuupanua mradi. *(Makofi).*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya Waziri, inaonesha dhahiri kabisa huu mradi wa kutoka Ziwa Viktoria ili ufike katika Mikoa ya Kati ikiwemo Singida, itakuwa ni muda mrefu sana. Na kwa kuwa, pale Singida sisi tuna karibu maziwa matatu ambayo ni madogomadogo; tunalo Kindai na tunalo Singidani na pia lipo Kitangiri, lakini yote haya yanatoa maji chumvi. Je, kwa kutumia teknolojhia ambayo sasa hivi naamini kwamba inaweza ikageuza yale maji ya chumvi na yakawa maji ya kawaida yakatumika kwa binadamu. Wizara inasemaje kuweza kufanya hiyo teknolojia ili wananchi wa Singida wapate maji kwa kutumia maziwa hayo yaliyopo Singida? *(Makofi).*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Killimbah, kama ifuatavyo. Kwanza ninashukuru kwamba yeye mwenyewe ametambua kwamba maziwa matatu yale likiwemo ziwa Singidani, yana chumvi. Teknolojia ya kutoa chumvi katika maji mpaka maji yaweze kutumika kwa

binadamu na mifugo ni teknolojia  ambayo kwa kweli inahitaji pesa nyingi. Kwa sasa mimi ningesema Mheshimiwa Killimbah, uwe na subira. Singida ina maji mengi chini ya ardhi na tumejaribu kwa muda mrefu sana, hata sasa ukitizama ushahidi unajionesha kabisa kwenye visima ambavyo vina maji yale yanayovutwa kwa kutumia *wind mills.* Ni kwamba kuna maji mengi, hebu tuanze kwanza na haya maji ambayo ni ya baridi tuliyonayo, ambayo tunaweza tukayapata kwa gharama rahisi kabla hatujaingiza teknolojia hii ya kuchuja chumvi ambayo ni ghali. Tutakapofika hapo na tukilazimika kufanya hivyo, basi tutafanya hivyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Kanuni? Naam, Mheshimiwa Hamad Rashid, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68.

**SPIKA:** Naam, Mheshimiwa Hamad Rashid, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Zitto, anauliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, inaelekea kama maneno yake hayakusikika vizuri na ndipo Mheshimiwa *Chief Whip* akatoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zitto, la kwanza alilolifanya alisahihisha Waziri alipokuwa anajibu kwenye maandishi, alisema kwamba Mzee Kawawa alikuja aka-*quote* Katiba ya kudumu; Mheshimiwa Zitto, akasahihisha kwamba mwaka 1968 hakukuwa na Katiba ya Kudumu, kulikuwa na *Interim Constitution*, hilo la kwanza alifanya. La pili, akasema kwamba amem-*quote* Waziri wa Maji na Nishati wa Zanzibar, akisema kwamba jambo hili linatolewa katika Muungano. Je, Serikali inasema nini? Hayo ndio maneno niliyoyasikia mimi. Sasa kwa sababu kuna utata wa hii taarifa, ningeomba Mwongozo wako kwamba je, hatuwezi tukapata *Hansard*, tukapata *exactly* maneno yaliyosemwa ili tukaweka rekodi sahihi kwasababu naona kama Mheshimiwa Zitto, hakutendewa haki katika hili. Ahsante sana. *(Makofi).*

**SPIKA:** Ni haki ya kila Mbunge, anapodai kupatiwa *Hansard.* Nitaagiza Katibu, *hansard* ipatikane halafu tutaona namna ya kulimaliza. Sio kubwa sana ni tafsiri tu, Katiba ya Kudumu au Katiba ya Mpito au ya Muda na hilo jingine; yote tutaona kwenye *hansard.* Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, leo ninafurahi sana tuna Wageni Mashuhuri, nao ni kutoka Jamhuri ya Ireland na kiongozi wa msafara huo ni Waziri wa Nchi Masuala ya Maendeleo, *Minister of State for Development Cooperation,* Mheshimiwa Peter *Power, PD. Honourable Peter Power, could you please raise so that you can be recognised by the house.* Yule pale, *thank you. Accompanied by His Excellence the Ambassador of Ireland to Tanzania, His Excellence Ann Barrington,* yule pale.

*Others are Deputy Director General, Irish Aid, Mr. Michael Gafey* na *Director of Program Countries Irish Aid, Mr. Damian Col, thank you.* Na *Minister* ana ujumbe mrefu tu wa watu wengi kidogo, *accompanied by a Delegation from Ireland and Embassy in Tanzania. Your Excellencies we appreciate your being here, Ireland is a very well known supporter of programs for poverty reduction in our country and it's a great pleasure to welcome you here into Parliament. Thank you. I hope you have a very pleasany stay here and go back home with pleasant memories of Tanzania. Thank you. (Makofi).*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, ana mgeni anaitwa bwaba Singo Sempambo, anaishi Marekani lakini amekuja Tanzania ili kujua ni vipi anaweza kuitangaza Tanzania kule Marekani. Bwana Sempambo, tafadhali, aah haa! Ahsante, tunashukuru sana kwa mtanzania mwenye uzalendo wa kutaka kuitangaza nchi yetu kule nje, tunakushukuru sana.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, ambao ni Watumishi Waandamizi kutoka Ofisi yake, wakiongozwa na Ndugu Mariam Mwafisi, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Ahsante sana, Wakurugenzi naomba wasimame, sikupewa majina, labda wapo tayari kwenye gallery. Wageni wa Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto; kwanza ni Profesa Estomihi Nkya, mume wake. Naomba usimame, yule pale. Ahsante sana karibu sana tunashukuru kukuona hapa. *(Makofi)*

Bibi Bernadeta Ndunguru, Mwenyekiti Bodi ya Shirika la *ADAT*. Ndugu Bernadeta? Ahsante sana. Bibi Rose Mokoyola, Eliakim Simpasa, Makamu Mwenyekiti, Bodi ya Uratibu wa *NGOS*. Mheshimiwa Simpasa, yupo wapi? Ahh, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu Mheshimiwa Simpasa, ni Mbunge katika Bunge Bunge lililopita Bunge la Nane na ni maarufu sana kwa jinsi alivyotetea Haki na Heshima ya Bunge letu, tunamshukuru sana. *(Makofi).*

Wapo wageni wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrance Masha, nao ni Ndugu Buhilo, Mwakilishi wa *UNHCR* Tanzania. *The UNHCR Representative to Tanzania, please?* Ametoka eeh, pamoja na Profesa Rutinwa na James Tremon, wote wanatoka shirika hilo la *UNHCR*. Nadhani wametoka kwa hivi sasa.

Mgesni wa Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa, aah, ni Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mwenyekiti wa Taifa wa *CHADEMA*. Ahsante sana Mheshimiwa Freeman, karibu sana. Pole na mambo ya Biharamulo, lakini ndio siasa ilivyo. Ila chonde chonde

usiseme kuna umwagaji damu ni uchaguzi tu. Karibu sana, ni heshima kubwa kukuona hapa. *(Makofi/Kicheko).*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, ambao ni viongozi wa *CCM* wa Kata, Matawi na Shina. Ndugu Shida Ibrahim, wale pale, ahsante sana. Ahsante Viongozi Ndugu Shida Sefu Mkina, Ndugu Joram Sinyanya, Ndugu Nuru Kambuzi, Ndugu Michael Mchala, na kadhalika. Leo wageni ni wengi kidogo. Wageni wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke, ambao ni Wachungaji kutoka Kasulu Kigoma. Wakiongozwa na Mchungaji Justine Mkuyu, naomba wale wachungaji kutoka Kasulu. Hawapo naona. Wageni wa Mheshimiwa Hubert Mtangi, ni Mheshimiwa Mama Justina Mtangi, ambaye ni mke wa Mheshimiwa Mbunge wa Muheza; naomba asimame tafadhali. Alah, hawa ni kesho eeh? Nashukuru lakini Mheshimiwa Mtangi, machungwa jana nilipata. Imekuwa ni kawaida Waheshimiwa, wanapokuja wageni wa Mheshimiwa Mtangi kutoka Muheza, wananiletea kiroba hivi cha Machungwa, ni mazuri sana. *(Makofi/Makofi).*

Wageni wa Mheshimiwa Ernest Mabina, wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani mwanamke, Mheshimiwa Suzana Mashala, Diwani wa Kata ya Mtakuja. Wale pale Madiwani, ahsante sana na mfanyabiashara anaitwa Suleiman Sitta, inawezekana ni Ndugu yangu huyu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Shellukindo, sijui Shellukindo yupi lakini basi watakuwa wageni wa Mheshimiwa William na Mheshimiwa Beatrice. Bwana Nassoro Mfinanga na Bwana Khalifa Makame. Ahsante sana karibuni. Wageni 12 wa Mheshimiwa Dunstan Mkapa, wakiongozwa na Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Nanyumbu Bwana Nassoro Kamda. Naomba wale wa Nanyumbu tafadhali msimame, wale pale. Ahsanteni sana. Wageni wa Mheshimiwa Aloyce Kimaro, ni Katibu wake wa Mbunge, ambaye ni Mheshimiwa Diwani wa Kilema Kaskazini, Exuper Mosha, ahsante sana, ooh, wapo wengi Katibu wa Vijana, Makatibu na Wenyeviti wa *CCM* wa Kata za Vunjo. Ahsante, karibuni sana kutoka Vunjo, ahante sana. *(Makofi/Kicheko).*

Wageni wa Mheshimiwa Damas Nakei, ambao ni walimu wa shule ya Sekondari ya Wasichana ya Madunga Wilayani Babati, wakiongozwa na Sista Anita. Wale Masista kutoka Babati? Wale pale, ahsante sana. Alaah! Sio Masista wote looh! Wengine walimu wanaume pia, ahsante sana. Wameandika vibaya hapa. Mgeni wa Mheshimiwa Gaudensia Kabaka, ambaye ni mdogo wake anaitwa Modesta Sagara. Ahsante yule pale, ahsante sana. Na wanafunzi kutoka Kituo cha Mafunzo, Chamwino cha *FPCT;* wale wa Chamwino? Naambiwa wale pale, ahsante sana karibuni sana. *(Makofi).*

Waheshimiwa, naomba nimalizie na wageni wa Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, kama ifutavyo:- Kwanza naomba Wenyeviti wote wa Kata zetu 12 wa *CCM,* Urambo Mashariki naomba msimame. Ahsante sana. Makatibu wa *CCM,* Kata zote tena za Urambo Mashariki, ahsante sana. Sasa mnaguna, si ndiyo wakati wenyewe huu? Naomba pia Viongozi wa Muungano wa Wajasiriamali wa Kata ya Urambo Mjini, wakiongozwa na Chape Saidi, Mwenyekiti, Haruna Kategile, Habiba Mpamanga, wale pale. Tumeitikia wito wa kuwa na *SACCOS*

za kutosha na vikoba. Kwa hiyo wale ndio Wajasiriamali ninaowalea wale. Na mwisho ni Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Mbunge. *(Makofi/Kicheko).*

Sasa kwa wale kina George Simbachawene, mngesikiliza, wale vijana. Kama huna Kamati ya kukushauri, unda haraka, hii ndio Kamati yangu ya Ushauri, sifanyi ziara yoyote bila kukutana na hawa kwanza. Wanaongozwa na Ndugu Salum Hussein, ambaye ndio Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Ushauri. Salum Hussein pia, ndiye Imam wa Msikiti wa Urambo Mashariki.

Yupo Katibu wangu Bwana Paul Shija, wengine mukae kwanza lazima niwatambulishe vizuri; Katibu wa Mbunge, Bwana Paul Shija na ndio Katibu wa Kamati ya Ushauri. Aah yupo huku, amewaachia wazee, kijana ana heshima sana huyu. Wajumbe wengine ni Bwana Peter Sitta, ambaye pia ndio Mwenyekiti wa Serikali, Urambo Kati. Ndugu Omari Kalukanya, ahsante sana.

Ndugu Suedi Fundikira, Mzee Kalmati Mbavumbili, mzee ana busara sana huyu. Ndugu Mohamedi Weli, ni Mtunza Hazina wa hiyo Kamati, mana yake nayo ina gharama zake sio hivihivi tu. Halafu na mdogo wetu wa mwisho Bwana Paul Sitta. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko).*

Sasa msafara huu unaongozwa na watu wazito wafuatao, kwanza ni Ndugu Robert Mwijage, Katibu Msaidizi wa *CCM* wilaya ya Urambo, hapana huyo ni Mwijage wa *CCM,* yule pale ndio kiongozi wa *CCM* na anayemsaidia ni Ndugu Martha Susu, Mwenyekiti wa *UWT* Wilaya ya Urambo. Ahsante sana ahsante. Samahani imechukua muda, lakini jamani ndio jukwaa langu na mie hili. Kwa hiyo sasa ni matangazo mengine. *(Makofi?Kicheko).*

Aah! Mheshimiwa Waziri, Kepteni John Chiligati, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, anao wageni wafuatao ambao ni Makada, kutoka Biharamulo Magharibi. Komredi Swabi Razo, yule pale. Komredi Mihewa, Mzee Ernest Mzungu na Ndugu Mayalla. Mimi nilidhani mmekuja na yule mshindi lakini sasa basi, tutasubiri tumwone siku nyingine. *(Makofi).*

Haya, matangazo ya kazi sasa, Alhaji Mohamedi Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, anaomba Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati ya Miundombinu, mkutane leo saa 7.00 mchana Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, naomba wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi, *Steering Committee* ya Bunge, tukutane ukumbi wa Spika, saa 7.30 kuna ajenga muhimu za kuzingatia.

Naona huo ndio mwisho wa matangazo, sasa namwomba Katibu atusomee hatua inayofuata. Katibu tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010
### Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, na baada ya kuizingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uamuzi wake wa kufanya mapinduzi ya kilimo nchini, ambao unatupa matumaini makubwa ya kuinua na kuendeleza uchumi wetu. Utekelezaji ulioanza wa kuelekeza raslimali nyingi za Serikali katika kugharamia pembejeo za kilimo kama matrekta, mbolea na madawa, ni uthibitisho tosha wa utekelezaji wa dhamira yake. Aidha uamuzi wake wa kuzielekeza katika kuendeleza kilimo, fedha zilizorudishwa katika akaunti ya *EPA* ni faraja kwa wananchi wa Tanzania katika mchakato wa kuelekea maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii vilevile kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa juhudi zake kubwa za kuimarisha Muungano na kuhamasisha utekelezaji wa Sera mbalimbali za nchi yetu. Natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuunga mkono kwa vitendo uamuzi wa Mheshimiwa Rais wa kuleta mapinduzi ya kilimo nchini kwa kuziagiza halmashauri zote kununua matrekta kwa ajili ya kuboresha kilimo. Ni matumaini yetu kuwa kilimo kitaboreshwa, kushamiri na malengo ya dira ya maendeleo 2025 yatafikiwa.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe mwenyewe kwa kuonesha uhodari katika kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge kwa ufanisi. Aidha, nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika, Anna Makinda na Waheshimiwa Wenyeviti kwa kukusaidia kuliongoza Bunge vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa dhati Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.) kwa hotuba yake ambayo imekuwa dira ya mjadala wetu hapa Bungeni. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mustafa Haid Mkulo (Mb), Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba yake iliyofafanua mwelekeo wa uchumi wa nchi yetu na bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe mwenyewe kwa kuonesha uhodari katika kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge kwa ufanisi. Aidha nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika, Anna Makinda Mbunge, na Waheshimiwa Wenyeviti kwa kukusaidia kuliongoza Bunge vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kwa namna ya pekee kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Haroub Said Masoud (Mb.) kwa kuchambua na kujadili bajeti ya Wizara yangu. Ushauri na maelekezo ya Kamati hiyo yameiwezesha Wizara kukamilisha bajeti yake katika muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge Charles Nyanguru Mwera wa Tarime, Mchungaji Lackson Mwanjale wa Mbeya Vijijini na Lolesia Bukwimba wa Busanda na Ndugu Oscar Rwegasira Mkasa (Mb) Mteule wa Biharamulo Magharibi kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko natoa salaam za rambirambi kwa familia za Marehemu Chacha Zakayo Wangwe aliyekuwa Mbunge wa Tarime, Marehemu Richard Said Nyaulawa aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na Marehemu Kabuzi Faustine Rwilomba aliyekuwa Mbunge wa Busanda. Michango yao katika Bunge lako Tukufu itakumbukwa daima. Aidha natoa salaam za rambirambi kwa familia zilizopoteza ndugu zao katika milipuko ya mabomu Mbagala, jijini Dar es Salaam. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya Mwaka 2005 na Utekelezaji Wake Hadi Juni, 2009. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 imeelekeza Sekta ya Maendeleo ya Jamii itekeleze maeneo muhimu 14. Maeneo hayo na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

(i)Mheshimiwa Spika, Elimu na Mafunzo. Ilani imeelekeza kuimarisha Mipango ya Elimu ya Watu Wazima yenye manufaa pamoja na mafunzo ya fani mbalimbali za stadi za kazi na maisha mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hilo Wizara imeendesha mafunzo ya stadi mbalimbali za kazi na maisha zikiwemo stadi za uashi, useremala, ushonaji, mapishi, ufundi magari, kilimo cha mboga, ufugaji na kujikinga na janga la UKIMWI katika Vyuo 53 vya Maendeleo ya Wananchi. Jumla ya wananchi 97,736 wakiwemo wanawake 44,962 na wanaume 52,774 wamepata mafunzo hayo ndani na nje ya vyuo (Jedwali Na. 1). Mafunzo hayo yamewawezesha washiriki kujiajiri na kuajiriwa, na hivyo kuwapunguzia umaskini wa kipato.

(ii)Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu. Katika kuendeleza Elimu ya Juu, Ilani inaelekeza kuwezesha asilimia 12.5 ya wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Sita kupata nafasi ya kuendelea na masomo katika vyuo vikuu, taasisi za teknolojia na taasisi zingine za elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hili, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada katika Vyuo 9 vya Maendeleo ya Jamii vya Tengeru, Buhare, Rungemba, Missungwi, Monduli, Uyole, Ruaha, Mlale na Mabughai. Jumla ya wanachuo 2120 wakiwemo wanawake 1495 na wanaume 625 wamepata mafunzo hayo (Jedwali Na. 2a na 2b). Wahitimu wa mafunzo hayo huajiriwa na Halmashauri na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kupewa majukumu ya kuhamasisha jamii katika kubaini matatizo yao na kubuni mbinu na mikakati itakayowawezesha kuyatatua ili kujiletea maendeleo.

(iii)Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mazingira. Ilani vile vile inaelekeza jamii kuongeza juhudi za kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira na kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu hifadhi ya mazingira. Aidha, Ilani inaelekeza kuendeleza Kampeni ya Upandaji Miti ambayo imekuwa ikifanywa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira kwa wananchi kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Jumla ya miti 33,236 imepandwa katika Vyuo mbalimbali vya Maendeleo ya Wananchi ili kutoa elimu kwa vitendo. Wizara kupitia Vyuo vilivyoko katika Bonde la Mto Ruaha ilifanya kazi ya kuhifadhi mazingira kwa kupanda jumla ya miche 7,862 katika Vyuo vya Uyole, Ruaha, Ilula Ulembwe na Rungemba. Vilevile Kamati za Maji na Mazingira katika maeneo yanayozunguka Chuo cha Rungemba zilipatiwa mafunzo ya hifadhi ya mazingira na kuandaa mipango ya utekelezaji.

(iv)Mheshimiwa Spika, *UKIMWI*. Katika kuimarisha vita dhidi ya *UKIMWI*, Ilani inaelekeza kuongeza jitihada za kufikisha elimu kuhusu ugonjwa wa *UKIMWI* kwa wananchi mitaani na vijijini.Katika kutekeleza agizo, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo kwa wananchi wanaojiunga na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na wale walio jirani na Vyuo hivyo ili kuongeza uelewa wao katika masuala ya UKIMWI. Jumla ya wananchi 97,736 wakiwemo wanawake 44,962 na wanaume 52,774 wamepata mafunzo hayo.

(v)Mheshimiwa Spika, Nafasi na Fursa kwa Wanawake. Ilani imeelekeza kuongeza nafasi na fursa za wanawake katika ngazi za uteuzi za Utawala, Uongozi na Menejimenti ndani ya Serikali na Taasisi zake kufikia asilimia 50 ifikapo 2010.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hilo, Wizara imeandaa rasimu ya Mkakati wa Kuwezesha Tanzania Kuongeza Ushiriki wa Wanawake katika Ngazi Mbalimbali za Uongozi wa Kisiasa, Kiutendaji na Nafasi za Maamuzi. Rasimu hiyo tayari imekwishawasilishwa kwenye Sekretariati ya Baraza la Mawaziri kwa maamuzi. Aidha, Mheshimiwa Rais amefanya uteuzi wa wanawake wengi katika ngazi za kisiasa na kiutendaji wakiwemo Mawaziri, Wabunge, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, na Majaji. Natumia fursa hii kwa niaba ya Wizara kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada hizo za kuongeza wanawake katika ngazi za juu za uongozi.

(vi)Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Mikopo ya Wanawake. Ilani imeelekeza kuimarisha Mifuko ya Mikopo ili wanawake waweze kufaidika zaidi. katika kutekeleza maelekezo haya, Wizara yangu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, *WDF*, imeendelea kutoa mikopo kwa wanawake kupitia Halmashauri mbalimbali. Kati ya mwaka 2006 hadi 2009, jumla ya Halmashauri 88 zimepatiwa kiasi cha shilingi milioni 708,800,000 (Jedwali Na. 4). Aidha, Maafisa Maendeleo ya Jamii 265 kutoka ngazi ya Kata, Halmashauri na Mkoa walipatiwa mafunzo kuhusu kuhamasisha wanawake kujiunga na SACCOS na vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali kwa kuzingatia Sheria ya Ushirika ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Wanawake, Ilani inaelekeza kukamilisha taratibu na hatimaye kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo haya, Wizara yangu iliendelea na mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania. Hatua zilizofikiwa ni pamoja na:- Kupatikana kwa ofisi ya Benki katika jengo la Posta ya zamani Mtaa wa Mkwepu Dar es Salaam; Kulifanyia matengenezo jengo ili liwe katika hali ya kibenki; Kutafuta mtaji wa kuanzisha benki; Uuzaji wa hisa na utaratibu wa kupata watumishi.

Mheshimiwa Spika, Ilani imeelekeza kuendeleza vita dhidi ya utumikishwaji wa watoto.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara imetoa mafunzo kwa wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 36 na kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii 120 katika mikoa 18 ya Tanzania Bara kuhusu haki za mtoto za uhai, ulinzi, maendeleo, ushiriki na kutobaguliwa (Jedwali Na. 5). Washiriki wa mafunzo hayo wanaelimisha jamii kuhusu haki za mtoto katika maeneo yao ya kazi. Aidha Wizara imeendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu madhara ya utumikishwaji wa watoto kupitia vyombo vya habari, mabango na maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, Siku ya Familia Duniani pamoja na Siku ya Kupambana na Ajira mbaya ya Watoto Duniani.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM inaelekeza kuhakikisha kuwa Mikataba ya Haki za Mtoto iliyoridhiwa inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara yangu imedurusu Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 1996 ili kuelekeza namna ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika upatikanaji wa haki za mtoto. Aidha, Wizara yangu imeratibu na kuwezesha kuundwa kwa Mabaraza ya Watoto. Hadi hivi sasa Mabaraza hayo yameanzishwa katika mikoa yote 21 ya Tanzania Bara na katika Wilaya 48.

Uanzishwaji wa Mabaraza haya ni utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki za Mtoto. Mabaraza ya Watoto ni njia mojawapo ya ushirikishwaji wa Watoto katika kutoa mawazo yao kuhusu haki zao na wajibu wao katika ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM inaelekeza kupunguza vifo vya watoto wachanga na walio na umri chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hilo Wizara yangu imeendelea kuratibu utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa inayohusu haki na ustawi wa mtoto. Hii ni pamoja na kuwezesha kufanyika kwa mkutano wa nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto uliofanyika Arusha mwezi Februari 2008. Maazimio ya mkutano huu yaliagiza kila nchi mwanachama kuandaa Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM inaelekeza kutokomeza mila zenye kuleta madhara kwa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hili, Wizara imetoa mafunzo kwa wasimamizi wa sheria 190, wakiwemo Polisi 80, Askari Magereza 80 na Mahakimu 30, yanayohusu kuzuia na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake. Wizara pia inaendelea na kampeni ya Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake iliyozinduliwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 24 Mei, 2008. Aidha, uhamasishaji wa wananchi kuhusu kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake unaendelea kupitia vyombo vya Habari na kupitia gari maalumu lililotolewa na Shirika la Hanns Seidel Foundation litakalotumika katika kampeni kwa kuanzia Kanda ya Ziwa. Vilevile Kamati ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto imeshaundwa na inatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni. Lengo la kamati hii ni kuratibu utekelezaji wa kampeni wa kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake, watoto na mauaji ya vikongwe na albino.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, imeelekeza Vyama halali visivyo vya Kiserikali kupewa nafasi ya kuendesha shughuli zao kama ilivyokusudiwa na sheria.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo haya, Wizara yangu imeyapa Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* 3,263 hati za kutambulika kisheria (Jedwali Na. 6). Miongoni mwa haya 2,588 yalipatiwa vyeti vya usajili na 675 vyeti vya ukubalifu. Aidha jumla ya nakala 2,500 za Sera ya Taifa ya NGOs na nakala 400 za Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002 zimegawiwa kwa wadau mbalimbali.

Mashirika 391 yamewasilisha taarifa za mwaka zinazoainisha mapato na matumizi yao yaliyokaguliwa na Wakaguzi wa Hesabu wanaotambulika kisheria. Taarifa hizi zimechakatwa na kuingizwa kwenye Benki ya Takwimu kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 imeelekeza Kuimarisha na Kupanua Mfumo mpya wa mawasiliano unaotumia teknolojia ya kompyuta.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo haya, Wizara yangu imeimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Umma kwa kukipatia vitendea kazi kama vile kompyuta, printa, kamera na '*tape recorders*'. Aidha watumishi wawili wamepatiwa mafunzo ya mawasiliano ya uandaaji wa vipindi vya redio na televisheni.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2005 imeelekeza kuendelea kutoa mafunzo na mikakati ya utekelezaji wa mpango wa utawala.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo hayo Wizara yangu imetoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi ili kuwaongezea uelewa na kuwapa stadi na maarifa ya kutekeleza majukumu yao. Wizara imepeleka jumla ya watumishi 354 kwenye mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi kama inavyofafanuliwa.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya sekta ya maendeleo ya jamii na changamoto zilizopo, hali halisi ya sekta ya Maendeleo ya Jamii inajitokeza katika maeneo sita ya utekelezaji ambayo ni; ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo, mafunzo ya stadi za kazi na maisha, usawa wa jinsia, maendeleo ya mtoto, uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na watumishi wenye taaluma ya maendeleo ya jamii. Mafanikio na changamoto katika maeneo hayo ni kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo umekuwa ukiongezeka. Hali hii inaonekana katika upanuzi wa huduma za elimu katika ujenzi wa shule za msingi na za sekondari; ujenzi wa zahanati na barabara za vijijini na katika kamati mbalimbali za maendeleo kwenye ngazi ya mtaa, kijiji na kata. Juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Nne katika kuhamasisha wananchi kushiriki ndiyo iliyowezesha kufikia hatua ya sasa. Changamoto kubwa ni uwezo mdogo wa wananchi kifedha na uhaba wa wataalam wa Maendeleo ya Jamii wanaohamasisha wananchi kujiletea maendeleo mbalimbali. Serikali inaendelea kubaini fursa mbalimbali za kiuchumi ambazo wananchi wanazitumia katika kukuza kipato chao. Aidha, Wizara yangu imeongeza idadi ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii kutoka 4 hadi 9 kwa lengo la kuondoa upungufu uliopo wa wataalam 1421 katika ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya stadi za kazi na maisha yanaendelea kutolewa katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika fani za kilimo, ufugaji, useremala, ujenzi, ushonaji, uchongaji wa vinyago, uchoraji na upishi. Mafunzo hayo yanawezesha wananchi kujiajiri na kuajiriwa hivyo kupunguza umasikini. Changamoto inayovikabili vyuo hivi ni uchakavu wa majengo na miundombinu na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Wizara yangu inaendelea na juhudi za kukarabati majengo na miundombinu ya vyuo kila mwaka kulingana na uwezo wa kifedha. Wizara yangu itafanya ukarabati mkubwa katika vyuo vitano vya Maendeleo ya Wananchi vya Mwanhala, Nandembo, Same, Sofi na Msaginya. Aidha, ukamilishaji wa ukarabati wa vyuo vingine vya Maendeleo ya Wananchi 15 utaendelea. Vyuo hivyo ni Masasi, Nzega, Kiwanda, Urambo, Mtawanya, Bigwa, Malampaka, Kibondo, Kisangwa, Handeni, Karumo, Mwamva, Rubondo, Arnaoutoglu na Kibaha. Halikadhalika, Wizara

itakamilisha ukarabati wa vyuo vitano vya Maendeleo ya Jamii vya Uyole, Monduli, Mlale, Mabughai na Ruaha.

Mheshimiwa Spika, sekta ya Maendeleo ya Jamii ina jukumu la kuleta usawa wa jinsia ili kuharakisha maendeleo ya jamii. Kundi la wanawake ni kubwa (51%) katika jamii lakini mchango wao hautambuliki ipasavyo. Hiyo husababishwa na kuwepo kwa mfumo dume ambao hautoi fursa sawa kati ya wanawake na wanaume kushiriki katika masuala mbalimbali ya maendeleo. Ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi wa kisiasa na utendaji ni mdogo sana ikilinganishwa na wanaume. Hali duni ya ushiriki wa wanawake unaonekana kuanzia ngazi ya familia mpaka ngazi ya Taifa. Changamoto kubwa katika kufanikisha suala la usawa jinsia ni ufunyu wa rasilimali watu na fedha za kuhamasisha jamii kuachana na mila na desturi zisizofaa. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau inaendelea kuhamasisha jamii kuachana na mila na desturi zisizofaa. Aidha Wizara yangu inaendelea kutekeleza mikataba ya Kimataifa na Kikanda inayosisitiza usawa wa jinsia.

Mheshimiwa Spika, watoto ni Taifa la leo na kesho na ni nguvu kazi inayotegemewa kwa ajili ya maendeleo ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla. Ili maendeleo ya watoto yaweze kufikiwa wanahitaji kupewa haki zao za msingi za kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kutobaguliwa, maendeleo, kushiriki na kushirikishwa katika masuala mbalimbali ya maendeleo yao wenyewe na taifa. Haki hizo kwa sasa hazipatikani kwa baadhi ya watoto vijijini na mijini.

Kuna changamoto nyingi zinazotukabili kuhusu watoto ikiwemo kuongezeka kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, wakiwemo yatima na waoishi mitaani, wanaofanyiwa ukatili na wanaoatharika kutokana na mila na desturi. Wizara yangu inaendelea kukabiliana na changamoto hizi kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali katika kutekeleza Mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda inayolinda Haki za Mtoto.

Mheshimiwa Spika, Usajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali unaendelea vizuri. Hata hivyo, uratibu wa kazi zinazofanywa na NGOs haufanyiki kwa kasi iliyokusudiwa. Changamoto iliyopo ni uwezo mdogo wa kukidhi mahitaji ya vifaa na nyenzo za uratibu wa mashirika hayo. Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la NGOs imeendelea kuweka mazingira mazuri ya ushirikiano miongoni mwa wadau, uwazi, na uwajibikaji katika sekta ya NGO, kwa kuandaa na kutekeleza Kanuni za Maadili ya NGOs za mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, watumishi wenye taaluma ya Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana katika kuhamasisha shughuli mbalimbali za maendeleo katika Halmashauri zetu hapa nchini. Maafisa hawa ni chachu na nguvu ya kusukuma maendeleo ya wananchi katika sehemu zao hasa katika ngazi ya kata. Changamoto iliyopo ni kata nyingi hazina wataalam wa Maendeleo ya Jamii. Hadi sasa ni asilimia 43 tu ya watumishi wa kada ya Maendeleo ya Jamii ndiyo iliyopo katika ngazi ya kata.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2008/2009 na malengo ya mwaka 2009/2010, katika kusimamia na kutekeleza majukumu yake Wizara inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na

Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Malengo ya Milenia (MDGs), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 pamoja na Sera za Wizara ambazo ni:

- Sera ya Maendeleo ya Jamii 1996;
- Sera ya Maendeleo ya Mtoto toleo la Pili 2008;
- Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia 2000; na
- Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2001.

Mheshimiwa Spika, katika mambo muhimu yatakayoshughulikiwa na Wizara yangu kwa mwaka 2009/2010 maeneo mawili yafuatayo yamepewa kipaumbele:

- Utekelezaji wa Mikataba, Matamko na Maazimio ya Kimataifa, Kikanda kuhusu maendeleo ya Wanawake, Usawa wa Kijinsia na Ustawi wa Mtoto.
- Ukarabati wa Majengo na Miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

Maeneo haya kwa pamoja yametengewa asilimia 77.3 ya bajeti yote ya Wizara.

heshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara unafanyika kupitia Idara na Vitengo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya jamii, li kuongeza ajira, Wizara yangu inalo jukumu la kutoa ujuzi na stadi mbalimbali za maisha kwa wananchi. Kwa kutekeleza hili, katika mwaka 2008/2009 jumla ya Shilingi 1,405,470,900/- zilitumika kutoa mafunzo vyuoni. Wananchi 29,557 walipatiwa mafunzo kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 53 nchini (Jedwali Na. 8). Kati yao, wanawake walikuwa 14,410 na wanaume walikuwa 15,147. Aidha, wakufunzi 41 walijengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo kuhusu mfumo wa ukusanyaji taarifa na mawasiliano kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu nchini *(ESDP).*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2008/2009, Wizara iliahidi kukarabati majengo na miundombinu kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Vyuo vya Kilosa, Mtawanya, Urambo, Kiwanda na Ifakara vilipatiwa fedha za ukarabati mkubwa. Vyuo vya Chala, Chilala, Karumo na Sofi viliwekewa mitambo ya umeme unaotokana na nguvu za jua ambapo Vyuo vya Malya, Buhangija, Malampaka, Chisalu, Nzega, Msingi, Sengerema, Bigwa, Msinga na Rubondo vilipatiwa fedha kwa ajili ya ukarabati mdogo (Jedwali Na. 9). Jumla ya Shilingi 2,455,777,000/- zimetolewa kwa ukarabati huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uboreshaji wa majengo na miundombinu unaoendelea katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Wizara katika mwaka 2009/2010 inatarajia kuongeza udahili kufikia wananchi 31,000 katika fani mbali mbali. Aidha,

ukarabati mkubwa na mdogo utaendelea kufanyika katika mwaka 2009/2010 ambapo Vyuo vya Mwanhala, Same, Nandembo, Sofi na Msaginya vitafanyiwa ukarabati mkubwa na vyuo vya Masasi, Bigwa, Nzega na Rubondo watapatiwa fedha za kukamilisha ukarabati ulioanza mwaka 2008/2009.

Vyuo vya Ilula, Handeni, Karumo, Kibaha, Msingi, Tango na Tarime vitapatiwa fedha za ukarabati mdogo. Vyuo vya Ifakara, Kilosa, Kiwanda na Urambo vitapatiwa fedha za kununulia samani ambapo Vyuo vya Bariadi, Munguri na Mwanhala vitawekewa mitambo ya kutoa umeme unaotokana na nguvu za jua. Vile vile tutakamilisha ukarabati katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Mlale, Uyole, Mabughai, Ruaha na Monduli.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008/2009 Wizara yangu ilidahili na kuendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii kwa wanachuo 1236 katika ngazi nne: Shahada 122, Stashahada ya Juu 378, Stashahada 340 na Cheti 396 (Jedwali Na. 2a na 2b). Aidha wataalamu 204 walihitimu katika ngazi ya Stashahada ya Juu na 414 katika ngazi ya cheti. Jumla ya Shilingi 514,637,500/- zilitolewa kugharamia mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii ni muhimu katika kuhamasisha na kuelimisha wananchi ili kushiriki katika mchakato wa kujiletea maendeleo. Katika jitihada za kuongeza idadi ya wataalam hao, Wizara kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 itaendelea kuboresha mazingira katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na kutoa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii kwa wanachuo 846 ngazi ya cheti, wanachuo 946 ngazi ya Stashahada na wanachuo 254 ngazi ya Shahada.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija na kuwapunguzia mzigo wa kazi wananchi hususan wanawake, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2008/09 imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi na kuvihimiza Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kuendeleza na kusambaza teknolojia sahihi katika jamii zinazovizunguka. Aidha, Wizara imeandaa Andiko la Mradi litakalotumiwa kuwaomba wadau mbalimbali kusaidia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/10 Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo ya rejea kuhusu uandishi wa miradi shirikishi, uhamasishaji na uhimizaji wa matumizi ya teknolojia sahihi ili kuwapunguzia wananchi na hasa wanawake mzigo wa kazi na kuongeza tija ya uzalishaji mali vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia azma ya Serikali ya kuimarisha kilimo, Wizara yangu imeandaa mpango wa kusambaza na kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi nchini kupitia mafunzo yanayotolewa katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Aina ya teknolojia zitakazosambazwa ni zile zitakazo saidia kuongeza tija na ufanisi na kupunguza mzigo wa kazi hususan kwa wanawake. Katika mwaka 2009/2010 Wizara inategemea kusambaza teknolojia za Wanyama Kazi, Trekta 23 za Kusukumwa kwa Mikono, Majiko Sanifu, Mikokoteni, na Umeme wa Kuzalishwa na Mashine za Kusaga, kama inavyooneshwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha utendaji katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Wizara yangu kwa mwaka 2008/09 ilitumia Shilingi 133,000,000/- kuendesha Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Sekta uliohudhuriwa na wajumbe 275. Wajumbe walijadili na kupitisha maazimio yaliyolenga kuimarisha utendaji wao na uboreshaji wa mazingira yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha na kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu yetu, Wizara yangu kwa mwaka 2009/2010 itaendesha Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii kwa lengo la kubadilishana mawazo na kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia jitihada za Taifa za kupambana na janga la UKIMWI, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2008/09 imedurusu Mkakati wa Kijamii wa Kuwakinga Wanawake na Watoto dhidi ya Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa lengo la kuuboresha na kuutumia kulingana na matakwa ya sasa ya jamii.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya jinsia, katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara yangu inaendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (WDF) kwa kushirikiana na Halmashauri. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara imeendelea kupeleka fedha kwenye Halmashauri kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (WDF) ili kuwakopesha wanawake wajasiriamali kwenye maeneo yao. Jumla ya shilingi milioni mia moja ishirini na nne (124,000,000/=) zimepelekwa kwenye Halmashauri 18 zilizokamilisha marejesho ya mikopo (Jedwali Na.11). Wizara kwa kipindi cha 2009/2010 itaendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake kupitia Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Wizara yangu kwa kushirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF) ilichangia jumla ya shilingi 10,000,000/= ili kuwezesha mafunzo ya biashara na ujasiriamali kwa wanawake 250. Wanawake hao walitoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara, ambao baada ya mafunzo hayo walishiriki Maonesho ya 33 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam. Kwa mwaka 2009/2010 Wizara yangu itatoa mafunzo, kusimamia na kuratibu shughuli za wanawake wajasiriamali 300 watakaoshiriki Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake Tanzania imekamilisha hatua za msingi za uanzishwaji ikiwa ni kupata mtaji wa bilioni 2.9 ambao umewezesha kupata leseni. Bodi ya Benki imeundwa na idadi ya wafanyakazi walioajiriwa ni 17 kama wanavyohitajika. Benki hii tayari imekwishakaguliwa na kupewa kibali cha kuanza shughuli zake. Hivi sasa maandalizi ya mwisho yanakamilishwa kabla ya ufunguzi rasmi mwezi Julai. Aidha, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2009/2010 itahamasisha jamii na taasisi mbalimbali kununua hisa za benki ya Wanawake ili kuendelea kuiimarisha. Lengo likiwa ni kutoa huduma imara za kibenki na mafunzo ya ujasiriamali hususan kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2008/2009 Wizara yangu kupitia shirika la ‘Artisan Development Agency of Tanzania (ADAT)’ imetoa mafunzo ya ujasiriamali

kwa wanawake wajane 40 wanaoishi na virusi vya UKIMWI kutoka mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2009/2010, itatoa mafunzo kwa wanawake kama hao 50 kutoka mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, Wizara katika kipindi cha 2009/2010 itaanzisha kituo kimoja cha biashara cha wanawake mkoani Dar es Salaam ili kuongeza fursa kwa wanawake wajasiriamali kupata masoko ya bidhaa wanazozalisha. Lengo ni kuanzisha vituo vya biashara katika mikoa 9 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo ya uchambuzi wa masuala ya jinsia katika mipango, programu na bajeti za sekta mbalimbali. Jumla ya Shilingi 135,440,000/- zilitumika kutoa mafunzo kwa washiriki 175 kutoka katika makundi yafuatayo.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mahesabu ya Serikali za Mitaa 45; Makatibu Wakuu 25 wa Wizara zote, Wakurugenzi wa Idara za Mipango 43 na Waratibu wa Dawati la Jinsia 66. Aidha, Rasimu ya Mwongozo wa kuboresha utendaji wa Dawati la Jinsia umeandaliwa. Katika kipindi cha 2009/2010 Wizara itaendesha kikao cha Makatibu Wakuu ili kutathimini utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa katika mafunzo yaliyofanyika 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na juhudi za kutokomeza ukatili wa kijinsia hususan wanawake, watoto na albino. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Wizara ilitumia Shilingi 15,453,400/- kwa ajili ya kutafsiri na kutoa nakala elfu sita (6,000) za Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake katika lugha nyepesi. Mkataba huo umesambazwa kwa wadau mbalimbali. Serikali pia imeunda Kikundi Kazi cha kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia nchini ambacho kina wajumbe 15 kutoka Wizara na wadau mbalimbali wanaojishughulisha na masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Spika, Kampeni ya kataa ukatili dhidi ya wanawake, watoto na albino inaendelea kufanyika kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru ambazo zinaendelea nchini kote. Kaulimbiu ya mbio za Mwenge mwaka huu imebeba ujumbe wa "Pinga Ukatili wa Kijinsia, Wanawake, Watoto na Albino." Aidha vijarida vyenye ujumbe maalum kuhusu Kampeni ya Kataa Ukatili vinaendelea kusambazwa kwa jamii kupitia mbio hizo za Mwenge. Wizara pia imepata gari la sinema kutoka Hanns Seidel Foundation kwa ajili ya kufanya kampeni za kuhamasisha na kutoa elimu ya utokomezaji wa ukatili dhidi ya wanawake, watoto na albino.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na albino kupitia kampeni ya Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake na kuendelea kuhamasisha jamii katika mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara.Uhamasishaji huu utafanywa kupitia vyombo vya habari na gari la sinema ambalo tayari tumeshapatiwa na shirika la *Hanns Seidel Foundation.*

Mheshimiwa Spika, Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka 2008/2009 yameendelea kuadhimishwa kimkoa. Aidha kwa mwaka 2009/2010 maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yatafanyika ngazi ya Kitaifa. Maadhimisho hayo yatafanyika sambamba na kutoa taarifa ya awali ya utekelezaji wa maazimio ya miaka 15 ya utekelezaji wa Ulingo wa Beijing.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka 2009/2010 itaendelea kuratibu, kushiriki na kuiwakilisha Tanzania katika mikutano ya Kimataifa na Kikanda ili kutathmini utekelezaji wa maamuzi yanayotolewa kuhusu maendeleo ya wanawake na jinsia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2008/2009 Wizara imekamilisha kuandaa rasimu ya Mkakati wa Kuwezesha Tanzania Kuongeza Ushiriki wa Wanawake Katika Ngazi Mbalimbali za Uongozi wa Kisiasa, Kiutendaji na Nafasi za Maamuzi. Aidha, Wizara yangu katika kipindi hicho iliendelea kuhamasisha jamii kupitia vyombo vya habari ili kujenga uelewa kuhusu dhana ya ushiriki sawa katika ngazi za maamuzi na uongozi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2009/2010 itaendelea kuhamasisha jamii na viongozi katika ngazi mbalimbali ili kujenga uelewa kuhusu dhana ya ushiriki sawa katika ngazi za kiutendaji, maamuzi na uongozi. Wizara pia itatoa mafunzo kwa wanawake 40 ili kuwajengea uwezo wakugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya mtoto, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2008/2009 kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na wadau wengine wa masuala ya watoto imeandaa rasimu ya Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto. Lengo la Sera hiyo ni kuhakikisha kuwa watoto wenye umri wa miaka 0-8 wanapatiwa haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara yangu itakamilisha Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, ambayo hivi sasa inapata maoni ya wadau kabla ya kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi. Aidha, Mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo utaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara yangu ilipanga kuhamasisha jamii kuhusu Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia. Jumla ya Shilingi 4,890,000/- zimetumika kuhamasisha jamii. Uhamasishaji huo ulifanyika kupitia viongozi wa Wizara katika vipindi vya radio na televisheni ambapo walizungumzia masuala mbalimbali yanayohusu familia, yakiwemo ukeketaji, mauaji ya vikongwe na Albino ikiwa ni njia moja wapo ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi. Aidha, Wizara ilitumia maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani (15 Mei, 2009 mkoani Shinyanga kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa familia na kuzindua rasmi Kitini cha Jamii kuhusu Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu itaendelea kuhamasisha jamii kuhusu tatizo la watoto wanaoishi mitaani, na kusambaza Kitini cha Jamii cha Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia. Lengo ni kuelimisha jamii kuhusu uwiano uliopo kati ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inajukumu la kuratibu uandaaji wa taarifa za nchi kuhusu utekelezaji wa Mikataba mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda ya Haki na Ustawi wa Mtoto. Katika mwaka wa 2008/2009 Wizara yangu iliratibu ushiriki wa serikali yetu katika kutetea taarifa za utekelezaji wa Itifaki za nyongeza za Mkataba wa Haki za Mtoto *(Convention on the Rights of the Child – CRC)* katika kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto, huko Geneva – Uswiss mwezi Septemba, 2008. Itifaki hizo ni Uhusishaji wa Watoto katika Migogoro ya Kivita (*Optional Protocol to the CRC in the Involvement of Children in Armed Conflict),* pamoja na Uuzaji wa Watoto, Ukahaba wa Watoto na Upigaji Picha za Udhalilishaji Watoto *(Optional Protocol on the Sale of Children, Child Prostitution and Child Pornography).*

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa mwaka 2008/2009 iliendelea kuratibu maadhimisho ya Siku ya Mtoto Afrika ambayo yalifanyika kimkoa. Kauli mbiu yake ilikuwa ni "Jamii Iwajibike: Isitelekeze Watoto".

Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Wizara yangu itaendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya Kimataifa. Hii ni pamoja na Mkataba wa Haki za Mtoto (CRC), na Itifaki zake za nyongeza pamoja na Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Watoto. Aidha, itaendelea kuratibu maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani na Siku ya Mtoto wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto wa mitaani limeshughulikiwa kwa kuandaa Rasimu ya Mpango Mkakati wa Kudhibiti Tatizo la Watoto wa Mitaani katika mwaka wa fedha 2008/2009. Lengo la Mkakati huo ni kubaini chanzo kinachosababisha watoto kuishi mitaani na kutafutia ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kukusanya taarifa za watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi ili kuwa na taarifa kamili za kufanyia kazi. Aidha, Wizara itakamilisha uandaaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ambao utayapa kipaumbele masuala yote yanayohusu haki na ustawi wa mtoto.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa ufuatiliaji wa haki za mtoto, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na wadau wengine imeandaa mswada wa Sheria moja ya Mtoto *(Law of the Child Act)* ambayo itakamilika katika mwaka wa fedha 2009/2010. Aidha, Wizara italifanyia kazi suala la kuwa na Kamati/Tume ya Haki za Mtoto.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeratibu uundwaji wa Mabaraza 17 ya watoto katika ngazi ya Wilaya (Jedwali Na.12) kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009. Usajili wa Baraza la Taifa la Watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

haujafanyika kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya mwaka 2008/2009. Hii ni kutokana na mchakato wa kuandaa Sheria Moja ya Mtoto ambayo inaelekeza uundwaji wa mabaraza hayo. Muswada wa sheria hiyo utawasilishwa katika Bunge lako tukufu ili upitishwe kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliratibu maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani katika mwaka wa fedha 2008/2009. Kaulimbiu ilikuwa ni "Upendo, Amani na Mshikamano: Msingi wa Maendeleo ya Familia". Aidha, rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Familia ambayo ni mwongozo na dira katika masuala yanayohusu familia kama kitovu cha jamii na Taifa, imeandaliwa na iko katika ngazi za juu za maamuzi. Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo utaandaliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, mashirika yasiyo ya kiserikali, izara yangu kwa kipindi 2008/2009, imeendelea kuratibu shughuli za NGOs na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya *NGOs* ya mwaka 2001 na Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002. Aidha, imeimarisha ushirikiano na Wasajili Wasaidizi wa *NGOs* wa ngazi za wilaya na mikoa ili kuboresha usajili wa *NGOs* kwa kupunguza urasimu na kurahisisha ufuatiliaji wa shughuli za Mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara itaimarisha Bodi ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuijengea uwezo na kuipatia rasilimali za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Bodi itaratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kutoa uelewa kwa wadau wa Sekta hii kuhusu Sera ya Taifa ya NGOs ya mwaka 2001 na Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002. Bodi kupitia vikao vyake vya kisheria na ukaguzi wa shughuli za NGOs imepanga kuwafikia wadau wengi zaidi katika mikoa ya Mbeya, Mtwara, Rukwa na Mara. Aidha, sekta ya NGOs itaweza kujiendesha kwa uwazi na uwajibikaji kwa kuzingatia matumizi bora ya Kanuni za Maadili ya *NGOs (NGOs Code of Conduct).*

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha usajili wa NGOs, Wizara yangu katika mwaka 2008/2009 imezindua Tovuti ya Idara ya NGOs ambayo itatumika kusajili NGOs kwa njia ya mtandao. Taarifa zote kuhusu NGOs zitapatikana kwa anwani www.tnnc.go.tz. Tovuti hii itasaidia pia kuongeza uwazi, uwajibikaji na ushirikiano miongoni mwa wadau wa sekta hii. Aidha katika kuimarisha sekta ya NGOs nchini wadau wamehamasishwa na kuunda mitandao ya NGOs 24 kati ya hiyo 11 ni ya Kiwilaya, 4 ya Kimkoa na 9 ya Kitaifa. Mitandao hii tayari inafanya kazi katika Halmashauri na mikoa husika.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuboresha na kuhuisha Tovuti na Benki ya Takwimu na taarifa za NGOs katika kipindi cha mwaka 2009/2010. Taarifa mbalimbali za sekta hii zitaingizwa kwenye Tovuti hii ikiwa ni pamoja na NGOs zilizosajiliwa na kupata cheti cha ukubalifu, zilizowasilisha taarifa za mwaka, mchango wa NGOs katika sekta mbalimbali za maendeleo na taratibu mbalimbali za usajili na uratibu. Kupitia tovuti hii wadau watapata fursa yakutoa taarifa kwa msajili wa NGOs kuhusu utendaji kazi wa NGOs katika maeneo yao na hivyo kuongeza uwajibikaji zaidi kwa jamii wanayoihudumia.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la uratibu wa Mashirka Yasiyo ya Kiserikali, Wizara yangu imeiwezesha Bodi ya Taifa ya Uratibu wa NGOs kufanya vikao vinne katika mwaka fedha 2008/2009. Vikao hivi vilifanyika katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara na Singida. Bodi ilipata fursa ya kutembelea shughuli za NGOs 43 na kutoa ushauri kuhusu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya NGOs ya mwaka 2001 na Sheria ya NGOs Na. 24 ya 2002. Aidha Bodi ilifanya mikutano mitano na wadau wa Sekta ya NGOs iliyohudhuriwa na wajumbe 403 kutoka katika mikoa husika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la NGOs imewezesha kukamilika kwa Kanuni za Maadili ya NGOs na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali (Taarifa ya Kawaida Na. 363) ya tarehe 5 Desemba, 2008.

Kanuni hizi zimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ili kurahisisha matumizi yake kwa kuziwezesha NGOs kujitawala na kuongeza uwazi na uwajibikaji wa Sekta ya NGOs. Kanuni hizi zimesambazwa kwa wadau mbalimbali kuanzia mwezi Juni 2009.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uteuzi wa Maafisa Maendeleo ya Jamii kuwa Wasajili Wasaidizi wa NGOs, Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009 imekwisha wasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupatiwa ufumbuzi wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, sera na mipango, katika kipindi cha 2008/2009 maafisa 23 wa bajeti wa Wizara walipatiwa mafunzo rejea ya upangaji mipango na uandaaji wa bajeti. Aidha iliwapatia Maafisa wengine 10 mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa kuwawezesha maafisa hao kupanga Mipango mizuri na kutoa taarifa sahihi kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wananchi kupata taarifa mbalimbali zinazohusu wanawake, watoto, jinsia na maendeleo ya jamii, Wizara yangu imeandaa Mfumo wa Kompyuta wa ukusanyaji, uchambuzi, uhifadhi na usambazaji wa takwimu zilizochambuliwa kijinsia. Aidha, Wizara yangu imeendelea kuratibu, kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa miradi ya Maendeleo katika vyuo vya vyote vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka wa 2008/2009, imeendelea kujenga uwezo kwa watumishi 210 wa Makao Makuu ya Wizara na kutoka vyuoni kuhusu uingizwaji wa masuala ya UKIMWI katika mipango. Mafunzo yalikamilika kwa walengwa na yanaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2009/2010 itakamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Kuimarisha Takwimu za Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Mpango Mkakati huu utawezesha Wizara kukusanya takwimu za sekta ya Maendeleo ya Jamii zilizochambuliwa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Lengo ni kuhakikisha yanakuwepo matumizi mazuri ya fedha na miradi kukamilika kwa ubora na muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, utawala na utumishi, Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009 iliendelea kusimamia utendaji kazi kwa misingi ya haki, usawa, uadilifu, utawala bora na uwazi na kuweka mkazo katika kudhibiti vitendo vya rushwa, uzembe kazini pamoja na janga la UKIMWI mahala pa kazi. Masuala haya ni ya msingi katika kuiwezesha Wizara kuwa na watumishi waadilifu na wanaowajibika, wenye ari, moyo, na msimamo thabiti kuhusu utumishi wa umma na walio tayari kutoa huduma bora kwa umma wakati wote na yataendelea kusisitizwa katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2009/2010 itaendelea kupiga vita rushwa kwa kutoa elimu kuhusu Sheria Na. 11 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini ya mwaka 2004 kwa watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuwapatia mafunzo watumishi kwa kuzingatia Mpango wa Kuendeleza Rasilimali Watu kwa lengo la kuwaongezea ari na ufanisi wa kazi. Katika mwaka 2008/2009 kiasi cha Shilingi 400,000,000/- kilitumika kutoa mafunzo ya muda mfupi, kati na ya muda mrefu kwa watumishi 217 katika nyanja mbalimbali. Mafunzo haya ni pamoja na mafunzo ya Menejimenti kwa Wakuu wa Vyuo 62 vya Wizara, mafunzo ya Uongozi kwa watumishi 9, mafunzo ya taratibu za Manunuzi na Ugavi watumishi 25, mafunzo ya Utunzaji Kumbukumbu kwa watumishi 10 wa Masjala kutoka Makao Makuu ya Wizara, mafunzo ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali watumishi 35 na mafunzo ya muda mrefu kwenye vyuo mbalimbali nchini watumishi 76.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia katika mwaka wa fedha 2009/2010, itaendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wake 203 walioko makao makuu ya Wizara na vyuoni kwa lengo la kuwaongezea ari ya utendaji kazi, ufanisi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, watumishi 627 wamepandishwa vyeo kwa kipindi cha 2008/2009. Aidha, watumishi 75 wamedhibitishwa kazini na wengine 281 wameingizwa katika Masharti ya Kudumu na Pensheni. Hii imetokana na kukamilika kwa zoezi la kukusanya takwimu za kiutumishi na kuzihifadhi kwenye kompyuta kwa matumizi mbalimbali ya kiofisi. Wizara yangu kwa kipindi cha 2009/2010 itaendelea kuwapandisha vyeo watumishi wa kada mbalimbali kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ili kuwaongezea ari ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008/2009 Wizara yangu imeanza kutekeleza utaratibu wa kupima matokeo ya utendaji kazi kwa uwazi ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji wa watumishi kwa kujiwekea malengo yanayopimika. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa kila mtumishi anapangiwa kazi za kutosha kulingana na majukumu ya

Wizara na kufanya tathmini ya utendaji wake. Aidha, Wizara yangu ilitoa mafunzo ya *OPRAS (Open Performance Review Appraisal System)* kwa viongozi na maafisa wakuu 40 wa Makao Makuu ya Wizara ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Kuboresha Sekta ya Umma. Wizara kwa mwaka 2009/2010 itakamilisha kutoa mafunzo ya *OPRAS* kwa maafisa waandamizi wote wa Wizara ambao hawajapata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009 ilitumia Shilingi 1,200,800,000/- katika kuendelea na awamu ya nne ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara na kuwezesha upatikanaji wa vyumba 84 vya ofisi pamoja na Ukumbi wa Mikutano. Sambamba na shughuli hizo mitambo ya mawasiliano na nishati imeshanunuliwa na ipo katika hatua za mwisho za kukamilishwa kufungwa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara itakamilisha awamu ya nne ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara sambamba na uwekaji wa mazingira mazuri ya ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imekuwa ikisisitiza utoaji huduma kwa wananchi kwa kiwango cha juu kwa wakati. Katika kufanikisha azma hii, Wizara katika mwaka wa fedha 2008/2009 imeanza kutekeleza mkakati wa kuelimisha watumishi kuhusu utoaji huduma kwa wateja. Jumla ya watumishi 33 wa kada za Ukatibu Mahsusi na Wasaidizi wa Kumbukumbu wamepata mafunzo hayo mwezi Desemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009 imeimarisha kiutendaji Kitengo cha Habari na Mawasiliano ya Umma. Kupitia Kitengo hicho, hoja mbalimbali zilizohusu Wizara zilijibiwa na kutolewa katika vyombo vya habari, zikiwemo taarifa zilizohusu ukatili dhidi ya watoto wenye ulemavu wa ngozi (albino) na kufuatilia utekelezaji wake. Aidha Wizara iliandaa na kudhamini matangazo ya vipindi vya Jinsia na Familia vilivyorushwa kupitia TBC1. Kwa mwaka 2009/2010 tutaendeleza juhudi za kuelimisha jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari kuhusu majukumu yetu na utekelezaji wa sera mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu itaratibu kikao kimoja cha ushirikiano na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Zanzibar.
Aidha, Wizara itaendesha vikao viwili kwa wajumbe 38 wa Baraza la Wafanyakazi kwa lengo la kuwashirikisha wafanyakazi katika masuala muhimu yanayowahusu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, Wizara itaendeleza mafanikio yaliyopatikana ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na usawa wa kijinsia hapa nchini, ukatili dhidi ya wanawake, watoto na maalbino unatokomezwa. Vilevile haki za mtoto zinalindwa na wananchi wanapewa fursa za kujiendeleza kiuchumi kwa kupatiwa stadi mbalimbali kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, wanawake watapewa fursa za kujiendeleza kiuchumi ili waweze kuchangia pato la familia na Taifa kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya shughuli zao za ujasiriamali. Changamoto tuliyonayo ni kuweza kutoa elimu na kuhamasisha jamii kuachana na mila zenye kuleta

madhara zikiwemo mauaji ya vikongwe na albino na ukeketaji wa wanawake na wasichana, kutokueleweka kwa usawa wa kijinsia na ugawaji sawa wa rasilimali kati ya wanawake na wanaume. Ni imani yangu kwamba tukiunganisha juhudi zetu pamoja, Serikali na wadau wengine wa maendeleo tutaweza kushughulikia haya yote ili kufanikisha azma yetu ya kuleta maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, shukrani, namshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya (Mb.), kwa ushirikiano, ushauri na usaidizi mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii. Natoa shukrani za dhati kwa Bibi Mariam J. Mwaffisi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu wa ngazi zote, na waliopo kwenye taasisi zetu zote, kwa jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako tukufu. Bila ya mchango wao muhimu ingekuwa vigumu kupiga hatua katika majukumu tuliyonayo ya kuendeleza sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kupitia Bunge lako tukufu, kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao: Asasi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA), Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF), Mtandao wa Jinsia Tanzania *(TGNP)*, Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (FAWETA), Medical Women Association of Tanzania (MEWATA), White Ribon, Plan International, Mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali pamoja na wale wanaofanya kazi kwa maslahi ya jamii kwa namna moja au nyingine. (*Makofi*)

Napenda pia kuzishukuru Serikali za nchi rafiki ambazo kwa kupitia Mashirika yake zinaendelea kutusaidia. Nchi hizo ni pamoja na Marekani *(USAID)*, *Denmark (DANIDA)* na *Canada (CIDA).* Aidha, Mashirika ya Kimataifa ambayo ni: *UNICEF*, *UNDP*, *UNFPA*, *UNESCO*, Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Maendeleo ya Wanawake *(UNIFEM)*, pamoja na mashirika mengine ya ndani na nje nayo pia nayashukuru kwa misaada yake. Aidha, napenda kuwashukuru Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)*, *ILO*, Ubalozi wa Ireland na Ubalozi wa Uingereza kwa kuwa tayari kushirikiana nasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kutenga kiasi cha shilingi milioni 7.2 kwa kila Halmashauri kwa mwaka 2009/2010 kutoka shilingi milioni 3.6 hii ni ongezeko la asilimia mia za mwaka Jana 2008. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa fedha hizo zitaendelea kuwafikia walengwa ambao ni mafias maendeleo ya jamii walioko huko. Aidha, naishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuongeza Bajeti ya Wizara yangu kutoka shilingi bilioni 14, 665,870,000 za mwaka Jana hadi shilingi bilioni 21,694,583,000 kwa mwaka huu 2009/2010. (Makofi)

Ni matumaini yangu kuwa bajeti ya Wizara itaendelea kuongezwa mwaka hadi mwaka ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nishukuru familia yangu hususani wewe Mheshimiwa Samweli Sitta, mume wangu na watoto kwa misaada mbalimbali mnayonipa. Aidha pia nashukuru ndugu, jamaa, na marafiki ambao wote hawa hunipa moyo katika kutimiza majukumu yangu. Aidha nawashukuru wafanyakazi wote wa Tanzania bila wao nisingekuwa nimesimama mbele yako hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara mwaka 2009/2010, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2009/2010, sasa kwa exima na taadhima naliomba Bunge lako tukufu liidhinishe matumizi ya Shilingi 21,694,583,000/-. Kati ya hizo Shilingi 14,549,281,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi 8,698,645,000/- ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 5,850,636,000/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(other charges).* Aidha, Shilingi 7,145,302,000/- ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo Shilingi 5,223,977,000/- ni fedha za hapa nchini na Shilingi 1,921,325,000/- ni fedha za nje.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri nakupongeza zaidi kwa kuweza kuisoma hotuba ndani ya muda ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge ninao wageni wengi leo nadhani katika hatua hii mniruhusu naomba Mheshimiwa Naibu Spika, aweze kuja ili aendeleze shughuli za Wizara hii.

*(Hapa Mheshimiwa Naibu Spika Anne S. Makinda Alikalia Kiti)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge habari ya asubuhi, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Wizara hii au mwakilishi wake.

**MHE. MAIDA HAMADI ABDALLAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 na Kanuni ya 114 (11), nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilifanya kazi za kuchambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto tarehe 10 Juni, 2009, Mjini Dodoma. Katika kikao hicho Kamati ilipewa taarifa ya utekelezaji wa malengo yaliyomo katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 na pia bajeti ya Wizara kwa

mwaka 2009/2010. Maelezo hayo yalitolewa na Mhe. Magreath Sitta, Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Aidha alitoa ufafanuzi kuhusu dira, dhima, majukumu ya wizara na utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009. Vile vile Kamati ilielezwa kwa kina kuhusu utekelezaji wa mpango wa maendeleo, mapato na matumizi kwa mwaka 2008/2009, makadirio ya mapato na matumizi ya fedha pamoja na kazi zilizopangwa kufanywa na wizara kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Utekelezaji wa maoni na maagizo ya kamati kwa mwaka 2008/2009, Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Kamati yangu ilitoa maoni na maagizo katika maeneo mbalimbali na hasa yanayohusu.

- Kuongeza Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.
- Mikakati ya kuboresha Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Malya.
- Kufufua na kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi·Mikakati ya kurekebisha Sheria zinazohusu haki za Wanawake na Watoto.
- Teknolojia rahisi katika kuhamasisha Wanaume kufanya kazi ya kusaidia Wanawake.
- Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) kupelekwa katika *SACCOS* zinazotambulika.
- Uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Wanawake.
- Mkakati wa kufikia asilimia 50:50.
- Maendeleo ya mtoto nchini.
- Mikakati ya kuboresha utendaji kazi wa Taasisi zisizo za Kiserikali *(NGO's)* hapa nchini.
- Wizara kurekebisha Upungufu wote ili isiendelee kupata hati ya mashaka.

- Mikakati ya kupata fedha kwa ajili ya mafunzo kwa maafisa maendeleo wa Wilaya na Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, Wizara kwa kiasi kikubwa imefanyia kazi ushauri wa Kamati katika maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika itaendelea kushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009, katika Mwaka wa Fedha 2008/2009, Wizara iliidhinishiwa na Bunge matumizi ya shilingi 14,665,870,000. Kamati ilielezwa kwa undani kuhusu matumizi katika kutekeleza bajeti ya Mwaka 2008/2009. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na mafanikio yake ni kama ifuatavyo:-

- Wizara imetoa mafunzo rejea ya uandishi wa miradi shirikishi na matumizi ya teknolojia sahihi kwa jumla ya wataalam 147 wakiwemo maafisa maendeleo ya jamii na mafundi sanifu.

- Wizara kupitia Shirika la ‘*Artsan Development Argency of* Tanzania (ADAT)’imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake wajane 40 wanaoishi na virus vya UKIMWI kutoka mikoa ya Dar Es Salaam, Pwani na Zanzibar.

- Wizara iko kwenye mchakato wa kutafuta eneo Kinondoni jijini Dar es salaam la kujenga Kituo cha wanawake wafanyabiashara Tanzania.

- Rasimu ya Waraka wa Mkakati wa Kuwezesha Tanzania Kuongeza Ushiriki wa Wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi umekamilika na kuwasilishwa katika ngazi ya mwisho ya maamuzi.

- Serikali imeunda kikundi kazi cha kushughulikia masuala ya unyanyasaji wa kijinsia nchini ambacho kina wajumbe 15 kutoka wizara na wadau mbalimbali.

- Kufanya ukarabati wa vyuo vya maendeleo ya wananchi na mafunzo katika vyuo vya Rubondo, Kisangwa, Ngara, Malya, Gera, Njombe, Ulembwe, Katumba, Nzovwe, Ilula, Tarime na Musoma.

- Vyuo 53 vya Maendeleo ya Wananchi vilitoa mafunzo kwa washiriki 29,557 ikiwa ni wanawake 14,410 na wanaume 15,147. Aidha kulikuwa na mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.

- Mkutano Mkuu wa mwaka wa sekta ya maendeleo ya jamii ulifanyika Dodoma ambapo wajumbe mia mbili sabini na tano (275) kutoka makao makuu ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri zote Tanzania Bara, Zanzibar na Sekta zingine walihudhuria.

- Katika suala la ufuatiliaji wa Haki na ustawi wa Mtoto, Wizara imeanza mchakato wa kuandaa Sera ya malezi , Makuzi na Maendeleo ya mtoto na utekelezaji wake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo wizara, Idara na Taasisi za serikali.

- Katika uratibu wa Mashirika yasiyo ya kiserikali, wizara imeendelea na usajili wa NGOs na kutoa Cheti cha Ukubalifu. Katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Mei, 2009 jumla ya *NGOs* 737 zimesajiliwa ambapo 629 ni usajili na 108 zimepatiwa Vyeti vya Ukubalifu.

- Wizara imeendelea na zoezi la kuingiza taarifa za sekta za mashirika yasiyokuwa ya kiserikali *(NGOs)* katika Tovuti ya NGOs. Tovuti hii itasaidia kutoa fursa kwa wadau kupata taarifa za mashirika haya *(NGOs)* wakati wote. Pamoja na mafanikio haya, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti ya Wizara kwa mwaka 2008/2009. Changamoto hizo ni:-

- Uhaba wa vifaa/nyenzo za kufanyia kazi iliathiri sana utendaji kazi na utoaji wa huduma.

- Ucheleweshwaji wa utoaji wa fedha hasa za maendeleo kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi.

- Uhaba wa Ofisi hasa katika Mikoa na Wilaya.

- Uhaba wa Wafanyakazi na Bajeti ndogo inayotolewa kwa wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2009/2010, Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2009/2010 imeomba kiasi cha shilingi 21,694,583,000. Ongezeko la Bajeti ya Wizara kutoka shilingi bilioni14.66 ya mwaka wa fedha 2008/09 hadi shilingi bilioni 21.6 linatokana na juhudi za Wizara za kuainisha maeneo ya vipaumbele ambavyo vimeonekana kuwa ni muhimu. Maeneo hayo ni pamoja na yafuatayo:-

- Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ikiwa ni pamoja na Uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania. *(Makofi)*

· Ukarabati wa vyuo 5 kati ya Vyuo 58 vya Maendeleo ya Wananchi ambavyo vimekuwa kwenye hali mbaya kwa muda mrefu. (*Makofi*)

· Uimarishaji wa dawati la jinsia katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baada ya kupata taarifa na maelezo ya malengo na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Kamati ilijadili kwa undani masuala mbalimbali na kuipitisha bajeti ya Wizara hii. Kamati yangu inaunga mkono maombi ya wizara, hata hivyo Kamati inatoa maoni na ushauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa kamati, Kuongeza Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Kwa niaba ya Kamati napenda kuipongeza serikali kwa kutambua umuhimu wa shughuli zinazofanywa na Wizara hii katika kuleta maendeleo ya jamii na kuiongezea bajeti japo haijakidhi mahitaji. Wizara bado inahitaji kuongezewa bajeti zaidi ili kuweza kufikia lengo la kuihudumia jamii kwa ufanisi.

Aidha, kwa namna ya pekee tunaipongeza wizara kwa kuzingatia wito wa '*Kilimo Kwanza'* kwa mifano halisi kwa kuwa sasa inatarajia kutekeleza mpango wa kusambaza teknolojia sahihi kupitia mafunzo yatakayotolewa katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambayo yataendeshwa katika Kanda saba (7) za Kaskazini, Kusini, Magharibi, Mashariki, Kati, Kanda ya ziwa na Nyanda za juu Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu utatoa msukumo maalum katika shughuli za kilimo hususan katika mikoa sita inayozalisha chakula kwa wingi nchini yaani Iringa, Mbeya, Ruvuma, Kigoma, Rukwa na Morogoro. Teknolojia zitakazopewa kipaumbele ni pamoja na:

(a) Trekta la kusukumwa kwa mkono *(Power tiller)* ambapo teknolojia hii itasambazwa katika mikoa sita (6) inayozalisha chakula kwa wingi nchini ili iweze kuinua uzalishaji wa mazao.

(b) Kilimo cha wanyama kazi (Maksai) ambapo teknolojia hii itasambazwa katika maeneo yenye mifugo mingi ili wananchi wake wapate uelewa wa kutosha wa kutumia wanyama kazi katika kilimo ili kuwapunguzia mzigo wa kazi.

(c) Matumizi ya majiko sanifu ni teknolojia itakayosambazwa katika maeneo ambayo kuna tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira utokanao na ukosefu wa nishati. Maeneo yanayozalisha mpunga kwa wingi, pumba zake zitatumika kupikia kwa kutumia majiko haya.

(d) Matumizi ya mikokoteni yatazingatia maeneo yanayozalisha chakula na bidhaa mbalimbali kwa wingi ili kuwarahisishia wananchi kazi ya ubebaji wa mizigo.

(e) Usambazaji wa umeme kutumia mashine ya kusaga ambapo teknolojia hii itasambazwa katika vyuo vinne vya maendeleo ya wananchi (Bariadi, Mwanhala, Tango, na Munguri) na hii itasaidia jamii zinazozunguka vyuo hivyo kujifunza na kupata hamasa ya kutumia teknolojia hiyo. Teknolojia za kukausha mboga za majani na matunda pia zitasambazwa katika vyuo hivi.

Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya mpango huu wa kutoa mafunzo na kusambaza teknolojia sahihi ni kuvipatia vyuo teknolojia sahihi ili viweze kutumiwa katika kutoa mafunzo kwa wananchi, kuwapa wananchi fursa ya kuzielewa ,kuzinunua, kuzitumia  na kuongeza ufanisi wa uzalishaji mali katika vyuo ili viweze kujitegemea.

Aidha mafanikio ya utekelezaji wa mpango huu yatategemea upatikanaji wa fedha za maendeleo ambazo mara nyingi hazipatikani kwa muda muafaka. Kamati inaishauri serikali kupitia Hazina kutoa fungu hilo la fedha mapema ili mafunzo hayo yatolewe kabla ya mwezi Oktoba na kuwahi msimu wa kilimo katika maeneo ambayo teknolojia za kilimo zitasambazwa.

Mheshimiwa Spika, Ukarabati wa vyuo vya maendeleo ya Wananchi *(FDCs)* na Jamii *(CDTIs)*, Maeneo haya yanahitaji kuongezewa fedha ili ukarabati wa vyuo 19 uweze kufanyika na kuwa na mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kutimiza masharti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* na hatimaye kupata hati ya usajili yaani *Accreditation*.

Mheshimiwa Spika, Ukarabati na Ujenzi wa ofisi za Wizara na Nyumba za Viongozi (*Rest house*) Dodoma, kwa kuwa Wizara haina Ofisi ya kudumu Dodoma na kwa kuwa kukodisha Ofisi za makazi ya viongozi wa wizara ni gharama kubwa, Kamati inaishauri serikali kuingia Mkataba na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama vile *NSSF*,

*LAPF, PPF, GEPF, PSPF* na *NHIF* kujenga Ofisi na nyumba za viongozi wa Wizara (Rest House) kuliko kuendelea na hali iliyopo ya kukodisha majengo kwa ajili ya ofisi na makazi ya viongozi.

Mheshimiwa Spika, Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) kuwafikia wanawake wa vijijini, kwa muda mrefu fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake zilikuwa zinapelekwa katika halmashauri mbalimbali ili waweze kuzikopesha kwa vikundi vya wanawake, lakini utaratibu huo umekuwa na manufaa kidogo sana kwa kuwa wanawake wa vijijini hawanufaiki. Kamati inashauri Serikali ihimize uanzishwaji wa Mifuko ya kuweka naKukopa (SACCOS) vijijini ili wanawake wenye hali duni ambao ndio walengwa waweze kukopa na kujikwamua kimaisha kutokana na mfuko huo.

Mheshimiwa Spika**,** Uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania, kwa kuwa mchakato wa uanzishwaji wa benki ya wanawake Tanzania umekamilika, na kwa kuwa benki hii ina lengo la kuwasaidia wanawake kujikwamua kiuchumi, Kamati inaishauri serikali kupitia vyombo vyake vya uelimishaji kuwahamasisha wanawake wengi wanunue hisa za benki hiyo kwa wingi na wananchi wengine kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Mtoto nchini. Kwa kuwa malezi na makuzi ya mtoto ni muhimu sana katika kujenga tabia bora kwa vijana wa Taifa letu; utafiti wa kitaalam unaonyesha kwamba karibu asilimia 80 ya ubongo wa mtoto unakua katika umri kati ya miaka 0-5 na asilimia ishirini iliyobaki ni katika maisha yake yaliyobaki. Kwa kuwa sio Wizara moja tu inayoshughulika na maendeleo ya mtoto hapa nchini. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa itifaki za Kimataifa ambazo nchi yetu imeridhia zinaitaka nchi kuwa na sheria ya mtoto, hivyo basi zifanyike juhudi mahsusi katika Wizara hii na ofisi ya Mwanasheria Mkuu za kukamilisha Muswada wa Sheria ya Mtoto (The *Law of Child Act, 2009*) ili sheria itakayopitishwa itoe mwongozo mzuri wa jinsi ya kumpatia mtoto haki zake.

(b) Kwa kuwa Wizara huwa inaandaa Sera ya Mtoto lakini watekelezaji wa Sera hizo ni Wizara zingine kama (Elimu, Afya, TAMISEMI, Mambo ya Ndani, Sheria n.k.) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iweke mikakati ya ufuatiliaji wa utekelezaji wake. Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya Kuboresha Sekta ya Maendeleo ya Jamii nchini. Kwa kuwa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii walikuwa ni muhimu sana katika kuhamasisha maendeleo hasa Vijijini kwa sababu wao wanajua mila na desturi za sehemu wanazokaa. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iweke mikakati ya kutoa mafunzo kwa wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na Mikoa na kuwateua rasmi kuwa Wasajili Wasaidizi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs.) katika maeneo hayo.

(b) Serikali ione umuhimu wa kurudisha uteuzi wa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa na Wilaya kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto badala ya kuteuliwa na TAMISEMI. Wizara iweke mazingira mazuri ya

kufanya kazi mfano ofisi na vitendea kazi kwa watendaji hao kama *Printers* na compu*t*ers za kutunzia kumbukumbu.

(c) Serikali iweke mikakati ya kupata fedha kwa ajili ya kuendesha programu ya mafunzo kwa maafisa maendeleo wa Wilaya na Kata ambao ndio chachu ya maendeleo ya jamii kwenye ngazi za chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani. Kwa niaba ya Wanakamati wenzangu naomba kukushukuru wewe binafsi, kwanza kwa namna unavyoendesha Vikao vya Bunge kwa umahiri na busara na kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu, pia kumshukuru Spika na Wenyeviti wote wa Bunge ambao ndio msingi wa mafanikio ya Bunge katika shughuli zake za kuisimamia Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Margaret S. Sitta (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri Mhe. Dkt. Lucy Nkya, (Mb), Katibu Mkuu ndugu Mariam Mwafisi na Watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Haroub Said Masoud (Mb) Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wenzangu kwa michango yao katika kuboresha mijadala, Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kama ifuatavyo:-

Wajumbe wenyewe ni Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Fatma O. Ally, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Salim A. Khalfan, Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mheshimiwa Capt. John D. Komba na Mheshimiwa AlShaymaa John Kwegyir.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Mchungaji Dr.Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Mohamed A. Said, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, na Mheshimiwa Elietta N. Switi.

Mheshimiwa Spika, Aidha napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashillilah kwa kazi nzito anayofanya akisaidiwa na Makatibu wa Kamati Ndugu Elieka

Saanya, Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Brown Mwangoka katika kuihudumia Kamati hii ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa hii kwa wakati.(*Makofi*)

Nashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza, na naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, umesoma vizuri sana na sasa nitamuita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto Mheshimiwa Anna Maulida Komu.

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi nimepata nafasi hii ya kuchangia yangu machache kuhusu makadirio ya mapato ya Wizara hii muhimu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na. 99(7) Toleo la Mwaka 2007. Kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma, amani na upendo kwa kutujaalia kukutana kwetu leo hii tukiwa bukheri wa afya. Pamoja na hilo na kwa udhati wa moyo wangu napenda pia kuchukua muda huu kuwashukuru wanachama wote, na viongozi wa chama changu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Chama imara na thabiti Tanzania, kwa ushirikianao wa dhati walionao katika kujenga demokrasia makini nchini na kujizatiti katika kuleta changamoto ya demokrasia ya vyama vingi. Nami naendelea kuwaahidi uzi ni uleule, kama nilivyo ahidi nitaendelea kufanya kila lililo ndani ya uwezo wangu kutimiza majukumu niliyopewa na chama changu pamoja na Watanzania wote kwa ujumla. Hakuna kulala mpaka kieleweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika nitakuwa mchoyo wa fadhila na mwingi wa husda kama sitatoa shukrani zangu za dhati kwa kambi ya upinzani hapa bungeni, kambi makini na inayofanya kazi kwa ufanisi mkubwa. Naishukuru kwa kuendelea kuniamini na kunipa fursa hii ya kuiwakilisha katika Wizara hii nyeti, muhimu na tegemeo la watanzania wote kwa mara nyingine tena. Sanjari na hilo pia napenda kuwashukuru wabunge wote wa kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wanaonipa ndani na nje ya bunge. Bila kumsahau Naibu Waziri kivuli wizara hii, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika kwa msaada wake wa mawazo na hekima katika hotuba hii.

Kwa pamoja nasema nawashukuru sana na nawaombea kwa mwenyezi Mungu msife moyo, kwani ili kujenga Tanzania iliyo bora, imara na yenye maendeleo mchango wenu ni mkubwa sana na unastahili pongezi. Changamoto mnayoitoa inafanya kazi na matunda sasa watanzania wameanza kuyaona kwa vitendo na si hisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba nitoe maoni ya kambi ya Upinzani katika Wizara ya maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Wizara. Kama nilivyohoji mwaka jana juu ya mkanganyiko wa majumu ya Wizara hii, nasikitika kuwa kambi ya upinzani imelazimika kurudisha tena suala hii katika mjadala huu.

Hii inatokana na unyeti na umuhimu wa suala hili. Sote tunafahamu juu ya umuhimu wa wizara hii, katika kukuza jamii yenye mwamko, kujiamini, kujituma na kuwa na Utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii katika kujiletea maisha bora kwa kuzingatia Usawa wa kijinsia na haki za watoto. Hakika Wizara hii ni muhimu kwa watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, huwa inajiuliza Je ni kwanini Wizara hii mama inayobeba Wizara zote haipewi kipaumbele na serikali, ilhali ni muhimu sana kwa maendeleo ya watanzania? Inasikitisha kuona wizara nyeti kama hii inapangiwa bajeti Tshs. 14,549,281,000/= ndogo mara 3.8 kuliko hata bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Hili ni suala la kujiuliza ni kwanini? Leo kambi ya upinzani imepata jibu hilo. Baada ya kuchukua muda na kuchanganua kwa kina leo kambi itawaelimisha ni kwanini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkanganyiko wa majukumu ya wizara hii pamoja na wizara nyingine ndio sababu ya msingi kabisa. Nilipouliza juu ya majukumu ya wizara hii, mheshimiwa waziri alipokuwa akijumuisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2007/2008 alinijibu na ninaomba kunukuu….

"Mheshimiwa Naibu Spika, kama zilivyo Wizara nyingine, Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, ina jukumu la kuandaa sera ya sekta ya maendeleo ya jamii; sera ya jinsia na maendeleo ya wanawake; sera ya maendeleo ya mtoto; sera ya maendeleo ya familia; sera ya mashirika yasio ya kiserikali. Pia Wizara inalo jukumu la kuandaa mkakati. Programu, miongozo mbali mbali na kusimamia utekelezaji wa sheria ya NGOs na kuratibu utekelezaji wa sera hizo unaofanywa na wadau mbali mbali wakiwemo jamii zenyewe, serikali za mitaa na mashirika yasio ya kiserikali na hata Wizara nyingine. Aidha, Wizara ina jukumu la kusimamia na kuendesha vyuo vya maendeleo ya jamii na vyuo vya maendeleo ya wananchi" (Hansard: 5 Agosti, 2008; uk. 192)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ilidhihirika wazi kuwa jukumu kubwa la Wizara hii hasa kwa upande wa wanawake na watoto ni kuandaa mipango na sera. Hii ndio sababu hakuna majukumu ya moja kwa moja ya kuangalia ustawi wa tabaka hili la watanzania linakuwa chini ya Wizara nyingine kwa mfano Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Lakini cha kustaajabisha ni kwamba katika kila Wizara hizo pia kuna idara za sera na mipango. Kitu ambacho ndani ya Wizara hizo kuna mamlaka ya ufuatiliji wa utelekelezaji. Katika lugha ya kiingereza tunaweza diriki kusema kuwa Wizara hii ni "*toothless*" ambalo jukumu kubwa walionalo ni kufikiria. Huu ndio mkanganyiko na si wa kusadikika na ni wadhahiri. Hiyo ndiyo sababu ya msingi kwa wizara hii kutopewa kipaumbele. Kwa sababu majukumu ambayo wizara hii ilitegemewa kufanya hufanywa na wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo dira ya kambi ya upinzani kuwa ni kukosoa kukemea na kuelimisha, basi ni wazi kuwa hapa pana tatizo. Hata kama hii wizara ni mtambuka basi ichukue jukumu la kufuatilia. Ni vizuri kama mheshimiwa waziri ataliangalia tena suala hili kwa umakini wake. Hii itawapa nafasi watanzania kujua utofauti wa wizara hii na ile inayoshughulikiwa na ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inarejea kutoa wito kuwa ni vyema Wizara iweke wazi juu ya mkanganyiko huu wa majukumu ya Wizara. Na pindi hili likirekebika basi ufanisi na uwajibikaji utapatikana. Pia kwa mtazamo wetu inaonyesha kuwa wizara imetumbukia katika kile kinachoitwa "*activity trap*". Inakuwa *busy* na kazi lakini inasahau lengo kuu la shughuli ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Jamii. Maendeleo ya jamii ina tafsiri pana sana. Hii inajumuisha maendeleo kwa wananchi wote wa jinsia zote. Na mara nyingi, tumekuwa tukipima maendeleo hayo kwa kutumia pato la mwananchi kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kuwa pato halisi la taifa limekuwa kwa kiwango cha asilimia 7.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.1 mwaka 2007. Lakini pato la wastani la kila Mtanzania kwa kila siku sasa hivi ni shs. 628,259 mwaka 2008 ikilinganishwa na shs 548,388 mwaka 2007. Sawa ni ongezeko la asilimia 14.8 ambalo wengine wanasherekea. Hii ni fedheha, ni aibu kwa Serikali iliyoko madarakani. Kwani mbona hatupimi ukuaji wa ugumu wa maisha. Je shilingi 600, Mtanzania huyu anakula nini? Anaweza kusomesha mtoto wake au kununua pembejeo? Kambi ya upinzani inachukua nafasi hii kuungana na wananchi wote ambao wanaendelea kutaabika kutokana na adha za maisha magumu yanayo wakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jamii ya Watanzania imegawanyika sana, katika mwaka wa 2008, watoto walio na umri kati ya 0-15 ndio wanaochukua asilimia 44.4 ya watanzania wote. Wenye umri wa miaka 15-24 ni asilimia 19.8, 25-64 ni asilimia 32.4 na wenye umri wa kuanzia miaka 65 na kuendelea ni asilimia 3.4 tu. Nimeona ni busara kuonyecha huo mgawanyiko mwanzo kabla ya kuanza kuzungumzia tabaka la nguvu kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguvu kazi ya watanzania ni asilimia 19.8 ya wananchi wote, asilimia themanini ya matabaka mengine yote yanategemea tabaka hili. Na huyu huyu Mtanzania anayepata shilingi 600 kwa siku. Haya ndio maisha bora. Inatia fedheha sana. Kambi ya upinzani inaitaka Wizara hii kuchukulia suala hili kwa uzito

wake. Lengo ni kumkomboa mtanzania na sii kumkomoa. Hebu tuangalie mishahara ya watanzania, tuangalie tunawezaje kuwasaidia watanzania hawa wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni Wizara hii ndio inalo jukumu la kuendeleza maendelo ya jamii yetu, kambi ya upinzani inataka Serikali itueleze hii idara ya maendeleo ya jamii inafanya nini? Na mafanikio yake ni yepi na kama ina mapungufu ni yepi? Na je wizara ina mkakati gani ambao utasaidia kukuza maisha ya watanzania walio wengi wanaoishi katika maisha duni?

Mheshimiwa Naibu Spika, maafisa maendeleo wa jamii, Wizara ilitoa takwimu zinazoonyesha kuwa kati ya kata 2,579 nchini ni 39% tu ya kata hizo ndizo zenye maafisa hawa. Tukiachilia mbali ugumu wa kazi zao na ukubwa wa kata zao, mazingira magumu ya majumu yao. Kambi ya upinzani inaitaka wizara hii ituambie ni maafisa wangapi wameajiriwa kwa mwaka uliopita wa fedha? Na kama hakuna ni nini sababu ya msingi? Ilhali wanafunzi katika nyuo vyetu vya maendeleo wameendela kuongezeka kwa kasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la upungufu huu wizara inalifahamu, hivyo ni matarajio ya kambi ya upinzani kuwa sasa limefanyiwa kazi. Hapa tunategemea habari njema. Kambi ya upinzani inaitaka wizara kuainisha bayana ni kata zipi zilizofaidika kwa kupata maafisa hawa kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Jinsia. Kuhakikisha kuwa Tanzania ina ulingano wa kijinsia ni jukumu lingine muhimu kwa wizara hii. Lengo la kufikia 50%/50% katika uwasilishi wa kina mama na kina baba katika nyombo vya maamuzi hakika ni la muhimu sana. Hata hivyo mheshimiwa Waziri, ataarifu bunge lako tukufu kuwa wizara imeandaa mkakati ambao mwaka jana ulikuwa umeshafika katika hatua za majadiliano na wadau, kabla ya kupelekwa kwenye vyombo vya maamuzi. Kambi ya upinzani inaamini kuwa sasa jibu lipo tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuongelea usawa kwa maneno tu, katika kipindi cha miaka minne sasa serikali ya awamu ya nne imekuwa ikiweka kipaumbele sana katika kuwainua wakina mama. Usawa wa kijinsia ni kitu cha msingi kwa maendeleo ya wanachi wote kwa ujumla. Kambi ya upinzani inapenda kuihoji serikali juu ya mkakati huo. Kama umekwisha fika juu katika vyombo vya maamuzi jee imeamuliwaje. Kwa uhakika kabisa ni wanawake wengi sana wanapenda kujua hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanawake. Sote tunafahamu umuhimu wa mama katika familia za kitanzania. Mama ndio mlezi, mtafutaji na mlinzi wa watoto. Mama ndio dereva wa taifa hili. Lakini pia mama huyu wa kitanzania ana sifa ya unyonge, umasikini na unyanyaswaji. Pamoja na adha zote hizo, mama huyu haachi majukumu yake. Atembee au aanguke hubeba majukumu yake kichwani. Pamoja na umuhimu wa mama huyu kwa taifa hili sasa ni muathirika wa kwanza na magonjwa ya ukimwi. Ukiacha matatizo yote ya vifo vya akina mama, umbali wa hospitali leo maambikizi ya ukimwi kwa mwanamke wa kitanzania ni asilimia 6.6 ukilinganisha na asilimia 4.6 kwa

wanaume. Aidha, vyanzo vikubwa vya uambukizi kwa akina mama hawa imebakia katika mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani inasikitika kuona kuwa pamoja na matatizo yote hayo majukumu yake ya ulezi ni moja ya chanzo kikubwa cha uambukizi. Wagojwa wa Ukimwi sasa hivi wapo katika kila familia, na ni mama ndio anaeangalia wagonjwa hao. Je, tunamsaidia vipi huyu mama, ili aweze kujua mbinu za kujilinda wakati anatimiza jukumulake la ulezi. Roho ya mama ni roho ya imani, hawezi kuacha kumhudumia mgojwa. Basi kambi ya upinzani inatoa wito kupitia Wizara hii inahusika na wakina mama moja kwa moja utengeneze mkakati ambao utaweza kuinua uwezo wa kina mama juu ya kuelewa njia bora za kuhudumia wagonjwa hao kwa njia iliyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, taarifa za hali ya ukimwi nchini inaonyesha wazi kuwa, tabaka la wajane limeathirika sana na ugonjwa huu. Wanawake wajane ni wanyoge zaidi. Mila na desturi zetu zinawanyima haki zao za msingi. Mfumo wa maisha ni mgumu na kufiwa na mwenza wao kunawafanya washindwe kuendesha familia zao katika viwango vinavyo kubalika. Kwa kuzingati hili, kambi ya upinzani inaomba wizara hii kuunda mkakati ambao utawajali wanawake hawa wajane walio katika taabu. Sera nzuri tunazo tunachotaka ni utekelezaji. Hebu tuokoe maisha ya watanzania hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana kwa kupitia wizara hii tulizindua kampeni kabambe ya kukataa ukatili dhidi ya wanawake, watoto na maalbino. Hii ilikuwa ni jambo la msingi sana. Lakini kama zilivyo program nyingine za maendeleo lazima zifanyiwe tathmini, kama ni mara nne kwa mwaka, mara mbili kwa mwaka au mara moja kwa mwaka. Sasa tumetimiza mwaka je tathmini zinasemaje? Tunafanikiwa au la? Tumejipima vipi?

Ni changamoto gani zimejitokeza? Je kuna mkakati gani wa kufuata? Kambi ya upinzani inaomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake ilitarajiwa kuwa mkombozi wa kina mama kiuchumi. Mwaka jana wa fedha serikali ilitoa jumla ya shilingi milioni 2.1 kwa ajili ya kununulia leseni. Na mnamo mwezi wa tano mwaka huu hisa ziliuzwa. Lakini hisa hizi ziliuzwa wizarani. Sasa sijui asilimia 74 ya watanzania walioko vijijini walifikiwaje? Je hii benki ni mkombozi wa wanawake wa Dar es Salam peke yao? Hapa hapaja kaa sawa. Kambi ya upinzani inahitaji majibu ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, mheshimiwa waziri alinukuliwa na gazeti moja la habari akisema kuwa, benki imekwisha anza kazi na Serikali imeipatia mtaji wa bilioni 2.6 kati ya bilioni sita ilizo omba. Hizi pesa zilipitishwa lini? Kambi ya upinzani inataka majibu. Je katika uuzaji wa hisa benki imetengeneza mtaji ya shs ngapi. Wanawake wenye benki yao wanataka kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho ya mheshimiwa waziri ya mwaka jana aliliahidi bunge hili kuwa atakuja na sera ya Malezi na Makuzi na maendeleo ya mtoto, wenye umri wa miaka sifuri mpaka miaka minane. Ikiwa jukumu la serikali hii ni kutunga sera je sera hiyo iko wapi? Mwaka sasa? Je wizara inahitaji miaka mingapi ili iweze kutengeneza sera hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani ilihoji sana juu ya watoto wanaoranda mitaani. Mheshimiwa waziri alitufahamisha juu ya ugumu wa suala hili. Na ni kwa jinsi gani lilivyo gumu katika kuchukua hatua. Akatuahidi kuwa utafiti utafanyika kwa kushirikiana na *International Consortium of Street Children* ili kugundua chanzo cha watoto wa mitaani na wakati huohuo kupata mikakati ya jinsi ya kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda wote huo wa mwaka hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa juu ya watoto hawa, mwaka sasa. Je utafiti unasemaje? Ni hatua gani sasa zitachukuliwa? Kambi haiulizi tena juu ya mataizo ya watoto hawa, sasa tunataka kufahamu juu ya hatua ambazo serikali inataka kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua matatizo yanayomkabili mtoto wa kike wa kitanzania. Ukeketaji ni moja ya kero kubwa. Tafiti iliyofanywa na *DHS* inaonyesha kuwa kati ya mwaka 1996 hadi mwaka 2004/2005 ukeketaji umepungua kwa asilimia 3 tu. Idara husika inafanya kazi siku zote. Je imeshidwa? Kambi ya upinzani inahitaji taarifa. Haiwezekani kwa muda wa miaka takriban tisa ya kazi matokeo ni hayo. Je sasa tupo wapi? Takwimu zinasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya upinzani ilihoji sana juu ya sheria ya ndoa ya mwaka 1971. Upungufu wa dhahiri upo katika sheria hii. Na inakingana wazi na haki za watoto ambazo wizara hii inatetea. Kambi hairudii kukumbusha matatizo ya sheria hii. Kwani hilo lipo wazi. Mheshimiwa waziri aliliahidi bunge hili kuwa mwezi oktoba, 2008 kwa kushirikiana na wizara ya sheria na katiba marekebisho hayo yangefika bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba kuna sheria ilipitishwa kupiga vita utumikishwaji wa watoto hapa nchini hususan kazi ngumu zinazo hatarisha maisha yao, ikiwemo kazi ya ukahaba. Je ni watu wangapi tangu kupitishwa kwa sheria hii wameishatiwa hatiani? Hasa ukizingatia kwamba kazi ya ukahaba uambukiza magonjwa hatari ya Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hayo tu, suala la mimba mashuleni pia ni moja kati ya vitu tete katika nchi yetu. Waziri mhusika alitoa taarifa kwa mjadala wa nini kifanyike kwa wasichana hawa wanaofukuzwa shule? Kambi ya upinzani inatumai kuwa mjadala umekwisha sasa. Kwa sababu haiwezekani mjadala ukadumi kwa mwaka mzima. Sasa ni majibu tu. Nini suluhu ya watoto hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Katika suala la kufuta kodi mashirika haya ni jambo ambalo kambi ya upinzani kwa nafasi ya kipekee kabisa inaipongeza Serikali na Wabunge wote waliopiga vita suala hilo. Naishukuru Serikali kwa kuendelea kufuta kodi kwa mashirika haya kwa sababu mchango wake ni mkubwa

sana. Na kwa sehemu nyingine zinawafikia watanzania kirahisi kuliko hata hiyo Serikali waliyoiweka madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu nilitaka kujua kuhusu tovuti lakini nashukuru Waziri sasa hivi amenijulisha kwamba tovuti hiyo iko tayari na nimeweza kunakili namba hapa nitashukuru kama Mungu akinisaidia niweze kupitia tovuti hii mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani, inasuala dogo sana katika mashirika haya. Mheshimiwa waziri aliahidi bunge lako tukufu kuwa tovuti ambayo itatumika kuingiza takwimu na taarifa za *NGOs* zilizosajiliwa nchini ilikuwa katika nafasi ya mwisho. Hii tovuti ni ipi? Na jee imesha anza kazi yake? Kwa sababu tukiijua tovuti hiyo maswali ya tuna *NGOs* ngapi yatakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna M. Komu umesoma vizuri. Waheshimiwa Wabunge tunao wenzetu ambao hawajapata nafasi kabisa ya kuchangia wako watano.

Sasa nimejifunza kwamba kuna wakati mwingine tumeanza kuzungumza hivi wale wasiochangia wanaanza kule vinote tena. Inaposomwa hotuba ya Waziri kama unataka kuomba ndiyo unaomba na si baadaye, unakuwa unavuruga ratiba yetu.

Kwa hiyo na waliochangia mara moja wako saba kwa hiyo kwa mujibu wa muda tulionao tunaweza kupata kama watachangia muda wote waliopewa basi tunaweza kupata watu kumi tu watakaojadili Wizara hii.

Kwa hiyo naanza na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Basi P. Mramba, Mheshimiwa Nuru Bafadhil na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar kwa asubuhi hii anaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika Karibu!

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii asubuhi hii.

Kwanza sina budi kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuweza kusimama hapa leo kuchangia katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa kuwa wote ni wanawake inaonyesha dhahiri kuwa wanawake tunaweza na pia tunaweza kusimamia Wizara vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru Mwenyekiti wangu na Makamu Mwenyekiti wangu wa Kambi ya Upinzani kwa kuendesha kambi kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sasa hivi nataka kutoa mchango wangu katika hotuba hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara mtambuka, ni Wizara mama inayobeba Wizara zote au takribani hasa Wizara ya Katiba na Sheria, Elimu, Afya na Kilimo pamoja na Wizara nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi wanavyosikia jinsia wanahisi kuwa ni jinsia moja, lakini Wizara hii ni ya jinsia zote mbili akiwemo Mwanamke, Mwanamke na Watoto wote wanabebwa katika Wizara hii, tofauti na wengine wanavyosema kwamba hii ni Wizara ya akina mama tu, siyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mwanamke ni mtu mwenye majukumu makubwa, mwanamke ana majukumu yaliyomkabili, kwanza ni uzazi, malezi ya watoto, kumtunza mume, kutunza mazingira na pia ana majukumu ya kujenga taifa lake kwa kuleta maendeleo ili kujikwamua katika maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, unyanyasaji wa Wanawake. Mwanamke inapotokea bahati mbaya akafiwa na mume wake kuna unyanyasi mkubwa katika baadhi ya familia. Mwanamke huyo hujikuta yuko katika mtihani kwanza kwa kuachiwa watoto kuwalea, pengine anaweza kufukuzwa ndani ya nyumba na ndugu wa marehemu mume wake au kunyang’anywa mali zake alizochuma na mumewe au kunyimwa haki ya watoto wake wasiweze kurithi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Wanawake wa Kiislam wanaotaka Mahakama ya Kadhi ianzishwe ili migogoro yao isimamiwe na dini yao ya kiislam kwani mirathi ya waislam inatatuliwa na Kadhi ni chombo cha Sheria na kutokana na kitabu chao cha Qurani Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni muda mrefu mchakato wa kuanzisha Mahakama bado haujafikiwa, kila siku kesho au keshokutwa, sijui Serikali ina kigugumizi gani kwa sababu duniani nchi nyingi ziko na zinaendesha mambo yao vizuri bila kuleta migogoro mfano nchi kama Kenya inayo Mahakama ya Kadhi, Uganda, Zanzibar na kuna dini tofauti wala hakuna mgogoro wowote ndani ya chombo hicho. Ni kwa nini na sisi hatuwekewi ili kuondoa migogoro yetu? Serikali hii ni sikivu naomba isikilize kilio chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile haki za Wanawake tunazozikosa ndani ya uislam Surai itaraq inasema “Mwanamke anapoachwa ana haki kukaa ndani ya nyumba mpaka eda imalizike ndipo aende kwao“ hii pia ni kukosa usimamizi wa chombo chetu. Hilo naliomba Serikali isikilize tena kilio chetu kwa mara nyingine tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naja kwenye UKIMWI. UKIMWI ni jamba la taifa, UKIMWI unatumaliza haidhuru Serikali tunaisifu imepiga hatua ya kupunguza UKIMWI kutoka 7.0% mpaka kufikia 5.8% kwa hiyo Serikali imepiga hatua lakini bado tunataka elimu na elimu tunataka haswa ielekezwe vijiji kwa sababu vijiji watu wanaathirika zaidi kwani hawana chakula bora, hawana huduma yoyote kwa hiyo tunataka elimu zaidi ifike vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, waathirika wakubwa ni wanawake. Kwa sababu wanawake ndio wanaohudumia yatima, wanauguza wagonjwa na wanawake ndio wanaotafuta chakula ili kuwahudumia wagonjwa hawa. Kwa hiyo, bajeti iongezwe ili wanawake wapate kuhudumia vizuri wagonjwa hawa, ili kuwatafutia chakula bora waathirika, kuwapa huduma mbalimbali kwa sababu kama mnavyojua ugonjwa wa Ukimwi, *time* zote unataka sabuni ya kufulia nguo kwa sababu mgonjwa anaharisha, hasa ikiwa mwanamke huyu hana kitu, atamshughulikiaje mgonjwa huyu? Kwa hiyo, tunaomba bajeti iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vya akina mama vinatisha, zaidi vijijini, vijijini hakuna miundombinu mizuri ya afya, zahanati hazina dawa, hazina Madaktari wa kutosha, Manesi hakuna, barabara ni mbovu, kwa hivyo tunaomba Serikali isimamie vizuri vijijini kwa kupeleka miundombinu ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naja kwenye usafiri, *SUMATRA*. Kwa kweli, vyombo vinapata ajali kila siku, lakini vyombo hivi vinavyopata ajali inasikitisha sana watoto wanakosa haki zao ndani ya usafiri huu, sijui ni sawa nitakavyozungumza, kama si sawa nitawekwa sawa, lakini ninaona mimi si sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uko utaratibu wa mtoto wa siku moja mpaka miaka mitano, huyo hana tiketi, huo ni utaratibu mzuri na tunataka uendelee. Lakini mzazi anapokwenda kukata tiketi, kama ni Mama, kama ni Baba, anakata tiketi ya mtu mmoja tu, ama yake yeye, ama ya mume wake, lakini watoto hawamo ndani ya tiketi. Kwa hivyo, tunaiomba SUMATRA, iweke fomu maalum ya kuweza kuwaorodhesha watoto wale, pindipo chombo kikipata ajali, wawe na wao wanajulikana ndani ya hesabu ile kuwa nao wamo. Lakini ikiwa hawakuorodheshwa wanapotea bila kujulikana, chombo hicho chaweza kuzama, chombo hicho chaweza kikaungua kama treni au vyombo vingine vyovyote. Kwa hivyo, kama utaratibu huo upo, basi haufanyi kazi ipasavyo na kama haupo tunaomba uanze mara moja, ili watoto hawa, wapate haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake. Kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake, ni chachu ya maendeleo. Wanawake watapata kufanya mambo yao, kuna kupata mikopo ili kujikwamua kiuchumi katika maisha yao na vilevile zaidi itolewe elimu vijijini ili wanawake wahamasike, waweze kununua hisa na kupata faida na wao wenyewe kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maalbino kwa kweli uaji huu unasikitisha, wenzetu wanateketea. Maalbino ni binadamu kama binadamu wengine, kwa nini leo wawe wanachinjwa kama kuku au wazee kwa misingi ya imani potofu? Kwa hivyo,

tunaviomba vyombo vya ulinzi, vizidi kusimamia na kwa kushirikiana na raia ili kuwafichua wahalifu hao, kwa sababu sisi wenyewe tunawaelewa. Kama ni waganga wa kienyeji au ni watu wengine wanaoshughulika na biashara hii tunawaelewa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali izidishe ari kuondosha matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mchango wangu ni huo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahasante sana, sasa nitamwita Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, ajiandae na Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, pia ajiandae.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafas ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya na hasa kuniwezesha mimi kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla sijaanza, niwapongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Magaret Sitta, Naibu wake, Mheshimiwa Lucy Nkya, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara, kwa kutuandalia kwa kweli bajeti nzuri sana, hotuba ambayo imetupa utekelezaji wa mambo yaliyoelezwa kwa bajeti ya mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu katika hotuba hii, naomba pia nichukue fursa hii, kwa niaba yangu mwenyewe na kwa niaba ya wanawake Mkoa wa Manyara na pengine kwa niaba ya wanawake wote wa Tanzania, kuishukuru sana Serikali kwa ajili ya kutupa fursa mbalimbali za kutuendeleza wanawake wa Tanzania, kwa kutupa kipaumbele kabisa katika nyanja mbalimbali za kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita, nakumbuka niliuliza swali hapa Bungeni na Naibu Waziri alianisha takwimu kuonyesha jinsi ambavyo Serikali yetu imeishatuendeleza sana wanawake katika sekta mbalimbali, ikiwemo fursa katika uongozi na ngazi za maamuzi, hasa kwa upande wa Wabunge, Mawaziri, Ma-*RC*, Ma-*DC*, Wakurugenzi na kwa kweli wanawake tunaendelea kuona juhudi kubwa ambayo Serikali yetu inatupa sisi kama wanawake wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wetu kuanzia Awamu ya Kwanza, wameweka misingi mizuri sana ya kuendeleza wanawake. Awamu ya Kwanza, iliweka fursa sawa ya elimu na hiyo ni misingi mizuri sana ya kuwawezesha wanawake kupata elimu bila kujali jinsia. Awamu ya Tatu, kila mmoja atakubaliana nami kwamba, Rais wetu Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliweza kuweka misingi mizuri vilevile ambayo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Nne, inaweka utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, mtakuabaliana na mimi kwamba, hakuna mwanamke atakayeunga mkono, mtu yeyote anayembeza Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa juhudi yake kubwa ambayo sote tumeiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, juhudi zake za wazi tunaziona na sasa uwiano unakuja mbele yetu wa uwakilishi Bungeni na mambo mengi sana. Kwa hivyo, kwa ujumla wake, tunaishukuru sana Serikali yetu ya Tanzania kwa kutujali sisi wanawake kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuchangia maeneo machache katika hotuba hii. Wizara hii kwa kweli, ni Wizara nyeti kama alivyosema mwenzangu, lakini kwa bahati mbaya bado tunaendelea kuona kwamba, inatengewa bajeti ndogo. Mwaka juzi ilikuwa na shilingi bilioni 10, mwaka jana shilingi bilioni 14, mwaka huu angalau si haba, shilingi bilioni 21 na milioni 600 (Shs.21, 600,000,000).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ulinganisho kidogo tu, barabara ya Babati - Dodoma, baada ya kupigiwa kelele sana, imetengewa shilingi bilioni 45, hii hata siyo nusu ya bajeti hii na yenyewe inaenda kujenga madaraja, pengine hata sio madaraja mengi. Kwa hivyo, bado tunaomba kwa kweli hii bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii na hasa tukizingatia uainisho mkubwa sana ambao Mheshimiwa Waziri, ametueleza katika hotuba yake kwamba, kuna mambo mengi mazuri sana ambayo yanahitaji utekelezaji kwa mwaka wa 2009/2010, basi tunaomba Wizara ya Fedha na Uchumi, iendelee kuifikiria Wizara hii ili kuitengea bajeti ya kutosha na kwa kuzingatia umuhimu wake katika kuendeleza jamii.

**NAIBU SPIKA:** Mbona mfano haufanani? Mfano wa barabara na Wizara, mbona haifanani?

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa mfano huu kwamba, bajeti hii hata haijafikia nusu ya kujenga madaraja ya barabara fupi ya kilometa 260, kwa hivyo, bajeti hii ya shilingi bilioni 21 bado ninaiona ni ndogo kwa Wizara nzima, ndiyo maana yangu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia eneo la marekebisho ya sheria. Kuna tafiti nyingi sana zimefanyika nchi hii, zikifanywa na Taasisi za Serikali, NGOs na watu mbalimbali na ambazo zimeibua mapendekezo ya kubadilisha Sheria ambazo zinakandamiza wanawake na zinaendelea kunyanyasa wanawake. Pamoja na kauli zote zinazotolewa na watu mbalimbali na Serikali lakini kwa bahati mbaya, tafiti hizi hazifanyiwi kazi kwa sababu naona kwamba, haziwafikii wale walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, ina maana kwamba, pamoja na gharama zinazotumika katika kufanya tafiti hizi, hizo gharama zinakwenda bure kwa sababu hazifanyiwi kazi. Kwa hivyo, nadhani ni vizuri Wizara ikaratibu utekelezaji wa tafiti hizi kwa sababu kuna wanaharakati wengi wanaibua mawazo mengi mazuri, ambayo kama Wizara ingeweza kuyaratibu na kuyafanyia kazi, tungeweza kupiga hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ifanye uratibu wa Miswada ambayo inaweza ikaletwa hapa Bungeni. Tunapendekeza kwamba, pamoja na Miswada mingi ambayo imepita hapa Bungeni, ya kufanyiwa marekebisho na mingine ya kuibua sheria mpya, lakini hatujaiona ambayo inalenga kurekebisha Sheria ambazo zinabagua na kukandamiza wanawake. Tuletewe sasa ya aina ninayoipendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo nadhani ni wakati muafaka sasa, tuletewe Miswada hapa sasa, ili tuweze kuona ni Sheria zipi tunaweza tukazirekebisha na hatimaye basi isiwe tu kauli za Serikali kwamba, wanawake wasinyanyaswe, wanawake wasifanywe hivi, wasibakwe, wasifanywe hivi, lakini hakuna Sheria yenye meno ambayo inaweza sasa ikatumika kuhakikisha kwamba, matatizo haya na kelele hizi tunazozipiga, zifikie mwisho kwa kuwa, Sheria itachukua mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara licha ya kufanya haya marekebisho, iweze kufanya uratibu wa mambo mengine mazuri ambayo yanatoka katika tafiti zinazofanywa na wataalamu, ili tunaposhughulika na masuala ya kuendeleza wanawake, tuwe na vipimo ambavyo tunavipima mwisho wa mwaka wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Serikali kuwa, tuwe na mwelekeo wa kutoa *feedback.* Mara nyingi katika maelezo ya hotuba na taarifa nyinginezo hazina vipimo, nashukuru kwamba, hii hotuba imeweza kueleza namna ambayo tutaweza kuwa na vipimo vya kupima mwisho wa mwaka, kwamba, sasa Wizara ilisema hivi mwaka huu, lakini basi tunataka kuoanisha utekelezaji wa suala hili na bajeti iliyopangwa, ili tuone kunahitajika nyongeza ya asilimia ngapi, ili matatizo haya yaweze kurekebishika. Kwa hivyo tuweke hoja zetu kwa mwelekeo wa kuweza kufanya *feedback* mwisho wa utekelezaji au mwisho wa mwaka mmoja wa bajeti. Bila kuwa na vipimo hivyo, utekelezaji utakuwa ni mgumu kuweza kuhoji kwamba hata nyongeza tunayohitaji ya bajeti, tunahitaji nyongeza hiyo kwa ajili ya nini?. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kutoa mfano kwamba, kama tunaweza kutoa hoja ya kusema, Wizara inaendelea kushughulikia suala hili kwa mwaka huu na mwaka unaofuata tunaisoma hivyo hivyo kwamba, Wizara inaendelea kushughulikia hili na lile, tunaendelea kutoa mafunzo, tunaendelea kushughulikia masuala mbalimbali, kwa namna hiyo hatutakuwa na vipimo vya kuweza kuhoji mwisho wa mwaka kabla ya bajeti inayofuata. Tunaweza tukawa tumepotea njia na hatuwezi hata kutetea bajeti zinazoongezeka, ili kuweza kutekeleza mambo mengi ambayo tumepanga kwa mwaka husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nikasema tufike mahali tuoanishe kabisa kwa kusema kwamba, Sheria Namba Moja, Mbili, Tatu, zimerekebishwa na hali kadhalika tumeweza kujenga vyuo kadhaa. Nashukuru kwa kweli Mheshimiwa Waziri, ameeleza vizuri sana katika bajeti hii, nimemfuatilia kwa makini,lakini bado tunasisitiza kwamba, suala hili ni muhimu sana kuwa *realistic* katika kuandika hoja zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu vifo vya wanawake wakati wa uzazi. Katika nchi yetu, hili nalo ni tatizo kubwa sana. Katika kipindi kilichopita, nilikuwa nasikiliza ripoti ya *RCC* ya Mkoa wetu wa Manyara na nikashitushwa sana kuona kwamba, takwimu hizi za vifo vya wanawake wakati wa uzazi, zinazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka. Nadhani sio Manyara tu, hata kwa nchi nzima kwa sababu, tunasikia hata kwenye vyombo vya habari wanawake 24 wanakufa kila siku na kadhalika. Sasa pamoja na ongezeko hilo, kuna Taasisi nyingi zinatoa takwimu, wanasiasa wengi wanalielezea suala hili, kelele zinapigwa kwa kila upande, lakini bado takwimu hizo zinapanda, vifo vinaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba Wizara husika, kama ni Wizara hii, ama ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, basi tupate suluhisho la kudumu kuhusu tatizo hili. Hivi, kweli Wizara hizi mbili haziguswi na tatizo hilo? Kwa sababu tukisikia eneo fulani watu kadhaa wamekufa kutokana na njaa, Serikali inakimbia mahala pale na kutoa tamko kabisa kwamba, "Hafi Mtanzania kwa njaa", Serikali itatafuta chakula hata kutoka nje ya nchi na kadhalika. Kwa nini basi hata hili nalo, kwa sababu kifo ni kifo, Serikali isifike mahali ikasema na yenyewe hii tuiwekee kauli mbiu, kusema kwamba, 'Hafi Mwanamke Mtanzania kutokana na uzazi"? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tukizungumzia sana suala moja mwaka hadi mwaka, ifike mahali Wizara itafute suluhisho la kudumu, bado hili liko ndani ya uwezo. Matatizo haya yanatokana na masuala tunayoyaelewa, kama ni suala la vifaa na nyenzo katika zahanati, ni kwa nini Wizara ya Afya ikiratibiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, isipange bajeti mahususi kwa ajili ya kuweka vifaa katika eneo hilo, ili takwimu hizo angalau zipungue mwaka hadi mwaka, badala ya kuongezeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tatizo ni watumishi, nadhani pia ni wakati muafaka sasa kutafuta suluhisho la watumishi katika vituo vya afya. Ni vizuri basi kufikiria hata kuongeza mishahara, angalau kupanga tatizo hili liweze kukabiliwa kwa namna gani, ili takwimu hizo zipungue na hatimaye suala hili liweze kuwa historia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie pia kwa kifupi kuhusu mimba za wanafunzi wetu mashuleni. Hili nalo ni janga lingine, lakini tutashangaa kuona kwamba, pamoja na kupigiwa kelele sana mwaka hadi mwaka na takwimu kuongezeka, lakini tutashangaa kuona Wizara ya Elimu, haitakuwa imetenga bajeti mahususi, tutaiona itakapofikiwa, kuona kwamba, sababu ya matatizo haya, kama ni kujenga Hosteli katika Sekondari za Kata, ni kwa nini basi kusiwe na bajeti mahususi ili kukabiliana na janga hilo? Kama tatizo ni lingine lolote lile, basi kwa sababu hili ni Bunge la bajeti na kwa sababu sasa hivi tunazungumzia suala la bajeti, Wizara husika zitenge bajeti na sisi tuelezwe kabisa kwamba, mikakati madhubuti itakayowekwa ni katika kukabiliana na kujenga *hostels* ama kukabiliana kwa namna nyingine yoyote, ili nalo suala hili lifike mahala tuseme *enough is enough.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza haya, naomba kuunga mkono hoja, ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza niseme kwamba, mimi ni mshabiki wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ni moja kwamba, wanawake wakiendelea, nchi inaendelea na ya pili ni kwamba kwa sababu wanawake wako nyuma wakilinganishwa na wanaume, ni lazima hatua mahususi zichukuliwe ili wanawake waende kwa kasi zaidi, yaani ukichukua ule msemo wa Baba wa Taifa, "*the women must run as others walk"*, sisi lazima tuwawezeshe wanawake wakimbie wakati wanaume wakitembea.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia moja kubwa na rahisi kabisa ni elimu. Wanawake wote wapeni elimu, haya mengine yote yatafuata, wape elimu. Najua tumefanya kazi kubwa ya kuwaelimisha wanawake lakini kundi kubwa la wanawake liko vijijini na kuwaelimisha leo tumeishachelewa, watu wazima tumeshachelewa. Lakini sio kweli kwamba, tumechelewa kabisa, *it is not a hopeless situation*, wanawake wanaweza wakapewa elimu ya watu wazima, lakini sio ile ya *A, B, C,* elimu elimu dunia vijijini kwa wanawake wa kawaida, ambao sasa ni watu wazima lakini wanahitaji elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningesema elimu hiyo ingelenga kuwapatia wanawake wenyewe na jamii kwa ujumla, maisha bora ambayo iko kwenye Ilani. Haya maisha bora vijijini yatakwendaje? Maisha bora vijijini yatakwenda tukielimisha wanawake, nitaeleza kidogo baadaye, lakini ili kazi hii ifanyike vizuri, ni lazima Wizara hii ipewe fedha zaidi, zaidi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na msemaji aliyetangulia kwamba, shilingi bilioni 21 kwa Wizara nzima ya Wanawake wote na watoto wote wa nchi hii, ni ndogo. Wizara hii inahitaji fedha nyingi, nyingi, nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi mtu anaweza akaniuliza, wewe ulipokuwa huko kwenye fedha ulitoaje? Lakini nataka niwaambie mimi ni mtu wa kwanza kuongeza fedha za Wizara hii, wakati wa Mheshimiwa Rose Migiro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la wakati ule na hata leo ni kwamba, kwa taratibu zetu zilivyo ni lazima Wizara iende na programu zinazoeleweka ili zipate fedha na nchi hii *budgeting* yake inakwenda kwa programu. Kama tungechukua programu ya elimu, hii ya elimu tu tukaigawa, elimu hii tunayofahamu ya Wizara ya Elimu na elimu dunia hii ninayoizungumza, ni fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwani vijijini tunahitaji nini? Tunaposema mahali pameendelea, tunasema watu walioendelea wanaishi kwenye nyumba bora, wanakunywa maji safi na salama, wanapanda magari na baiskeli na pikipiki, wanavaa viatu, wanavaa nadhifu, wanakula chakula ambacho sio kingi tu, lakini bora, wanafuata kanuni za lishe, wana namna za kujikinga na magonjwa na kutibu magonjwa ya kileo, barabara zao za

vijijini hata kama ni za tope, zinapitika  na ni nyingi, watu wanapanda mabasi, watu wanapanda hata ndege. Ukiwa na vitu hivi unasema, eeh watu hawa wameendelea.

Mheshimiwa Spika, huku Tanzania hatuwezi kusema Watanzania tumeendelea, yaani Watanzania tuna maisha bora, tunasema tu kwamba, inawezekana. Maisha bora kwa wote, inawezekana vipi?  Nani tunaweza tukamwuliza wewe ni mhusika na eneo hili la maisha bora? Tuonyeshe! Yeye atakwambia ili nikuonyeshe nipe fedha ili nikuonyeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona kwamba, maisha bora hayatakuja bila Wizara hii kupewa fedha nyingi sana za kutekeleza programu za maisha bora. Maji safi salama, nyumba safi na bora, mapishi safi na bora, nchi hii ina vyakula vingi sana lakini, hatuli vizuri, unasikia kwashakoo, utapiamlo, vyakula vipo lakini hatujui kuvila.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kwenda kwa Waziri, haya mambo ninayoyasema hapa niliishazungumza na Waziri, siyo habari mpya sana kwake, lakini nilitaka ijulikane hivyo kwamba, kule kwangu tuna vyakula vingi sana, lakini watu wana njaa, *nutrition* ipo. Lini utakula ndizi, lini utakula mahindi, lini utakula mboga, je, ukiishamchinja kuku, kuku anakatwa vipande vingapi?  Wewe una watoto Kumi (10), kuku mmoja mlo wa leo mtakulaje? Kwingine wanasema mpe Baba, eeh badala ya kusema wape watoto, anasema mpe Baba, hapo si panahitaji elimu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vyakula vipo hatujui kula, nguo zipo kuvaa tatizo, kufua tatizo, kupasi tatizo. Bwana Maendeleo wapo, wafikeje huko? Bibi Maendeleo wapo, wafikije huko? Wanahitaji usafiri, wanahitaji bajeti. Kazi hii hatuwezi kusema ni ya Halmashauri, hapana, kwa sababu raia hawa ni wa Taifa, watu wote hawa, sisi sote ni Watanzania, fedha ambazo zingepewa Wizara hii hii kiasi itatoka kwenye Halmashauri, kiasi kikubwa zaidi itatoka Taifani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna tatizo hili la wajane, wanaongezeka. Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni Mbunge, sisi ni Wabunge, wajane hawa wanaishi maisha magumu sana, elimu duni, mali wameishanyang'anywa, urithi hamna, watoto ni wengi, nani awasaidie?  Hata ile elimu tu ya namna ya kujitetea hamna! Wapo watu wengine waume zao wakifa, wale wanawake wanafukuzwa na watoto wote. Nani atawatetea hawa wanawake? Hata Mwanasheria mmoja tu pale Wilayani anaweza akawatetea hawa, yuko wapi? Mwanasheria huyo ni wa nani?  Lazima awe Mwanasheria anayesimamiwa na Wizara hii, ili apewe namna ya kupambana huko vijijini wanakokaa. Wizara hii inahitaji kila Wilaya ingekuwa na Mwanasheria wa Serikali, wa kusaidia wanawake hawa wanaonyanyaswa, mirathi hasa ni tatizo kubwa kabisa, lakini hakuna! Wizara hii ni lazima ipewe fedha ili kusudi ile kazi inayofanywa kitaifa, ya utetezi, ifanywe pale kijijini, watu wa kwenda Mahakamani kuwatetea bila kudai gharama za Mawakili, wanawake wanapofukuzwa, wanapopewa talaka za ajabu ajabu, wanaume wanavyotelekeza wake zao, hamna, Wizara hii lazima ipewe fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani miaka ya 1950, wakoloni walikuwa na kitu kilichokuwa kinaitwa Idara ya Maendeleo, wakawa wanafundisha watu vitu mbalimbali

ngazi za Kata, ngazi za Tarafa miaka hiyo. Leo Wizara hii, inahitaji kurejesha dhana ile, lakini kwa kufanya vitu vipya vinavyoendana na wakati wa sasa. Bwana maendeleo anakuwa ni wa Kata na ana ratiba yake pale kwenye Kata, ya kutetea wanaoonewa, ya kutetea watoto, ya kutetea wajane, ya kushirikiana na vyombo vingine kufundisha ulaji mzuri wa chakula na kilimo safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ‘Kilimo Kwanza’, ni wanawake, nani atatetea hawa wanawake na kuwafundisha Kilimo Kwanza? Ni lazima aweko mtu wa Maendeleo ya Jamii akishirikiana na mtu wa Kilimo, ili kwa pamoja waweze kuunda vikundi, kama ni vikundi vya ushirika au vikundi vingine, waweze kuwapa teknolojia, waweze kulima na waweze kujifunza jinsi ya kula na kupika na mambo ya namna ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo hili sio la Serikali tu, ndio pale tunasema, hata madhehebu wana nafasi yao ya kuelimisha, ya kutumia hata fedha zao kidogo kusaidiana na Idara ya Maendeleo ya Jamii, kufanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesimama hapa kusema niliyomwambia Waziri, ni haya haya niliyomwambia kwamba, leta programu kubwa, dai fedha nyingi ikiwa ngumu leta hapa sisi Wabunge tusaidie kupiga kelele, sisi tunatoka huko, tunajua haya matatizo. Ili kweli tuweze kuwa na maisha bora, maisha bora ni vile mtu anavyoonekana, mazingira anamoishi, anavyopambana na magonjwa yake asiugue hovyo hovyo, ni mahitaji mbalimbali ambayo kwa pamoja tungeweza tukayamaliza; lakini yawe na msemaji na msemaji mkuu wa wanawake na watoto na baba lazima afaidike ndani, *of course,* ukiwasemea hao, ni Wizara hii. Lakini hatuwezi kuendelea kuifanya kama ni *a peripheral Ministry in budgetary terms,* hatuwezi kuiweka pembezoni kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Wizara mtambuka na ingepewa fedha nyingi sana ingefanya kazi za Wizara nyingine nyingi sana. Lakini haipewi fedha, nadhani hatuelewi, hakuna mtu wa Wizara ya Fedha aliyekuwepo hapa ananisikiliza, hatuelewi kwamba Wizara hii sasa ndiyo yenyewe na sisi Wabunge tuko tayari kupiga kelele kama Waziri akituambia hapa niko tayari lakini hawanielewi, aje hapa sisi tusaidie kupiga kelele na huko vijijini tusaidie kusimamia kazi za Maafisa wake walioko huko na wananchi tusaidiane kuhamasisha ili waelewe na wakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni uanzishaji wa *NGO’s*. Nashukuru nimesoma vizuri sana, kazi imeanza vizuri, lakini ninapenda ieleweke wazi kwamba kuna *NGO’s* ambazo ni *SACCOS,* zimetajwa hapa. *SACCOS* ukienda kule vijijini ni Ushirika, ni Wizara nyingine. Wizara ya Maendeleo ni vikundi ile nayo inatakiwa iwe na fedha nyingi sana za kusaidia kuanzisha vikundi hivi *non-SACCOS* maana *SACCOS* ni ushirika. Kwa hiyo, napendekeza kila Kata na kila Afisa Maendeleo awe na ratiba ya kuanzisha vikundi vyake pale alipo ili tuweze kujua kila mwaka vikundi gani vinafanya nini na wapi. Hali ilivyo ni kama hiari hiari hivi, hapana!

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, Wizara sasa ifanye Kampeni kubwa ya kuwaelimisha watu juu ya hizi *NGO’s* zinaandikishwaje? Ile Sheria ipo labda *publicity* ndiyo inayotakiwa ili kusudi watu wajue kumbe *NGO’s* inaweza ikaandikishwa pale

Wilayani na wengine Taifani, watu wengi hawajui bado wanakwenda kuandikisha *NGO's* Wizara ya Mambo ya Ndani ambapo Sheria yenyewe inasema unaweza ukaandikisha hata pale Wilayani, *NGO* ya kwako pale, ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana, mawazo mazuri yanaanza kuibuka, fedha hamna na mimi natoa rai kwa Wabunge wote tena hasa nyie wanawake mlio hapa hii ndiyo *constituency* yenu, pigeni kelele na mimi nitawaunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo na mimi naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana umesema vizuri sana, Wizara ije na programu pengine fedha zitapatikana.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama hapa nikiwa katika hali ya afya njema. Pia napenda kumshukuru Mwenyekiti wangu wa *CUF* Taifa, Katibu Mkuu *CUF* Taifa kwa kuniteua mimi kuwa ni Katibu wa Jumuiya ya Wanawake *CUF* Taifa. Pia napenda kulishukuru Baraza langu la uongozi kwa kuthibitisha uteuzi huo, bila ya kuwasahau wanachama ambao wananisaidia katika kutekeleza majukumu haya niliyopewa. Kwa hiyo, naahidi Chama changu kwamba nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kutekeleza kazi nzito niliyopewa na sitawaangusha. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kuhusu mwanamke. Kwa kweli mwanamke ni mtu ambaye anakabiliwa na matatizo mengi ambayo yanamfanya awe ni kama mtu dhalili. Katika Tanzania asilimia 51 ya Watanzania ni wanawake na utakuta katika familia mwanamke ndio muongozaji. Leo utakuta nyumba nyingine baba anamsusia mama na familia, anamwacha mama anahangaika na watoto hajui anafanya nini, baba yeye anaendelea na mambo yake mengine ambayo hayana msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mama huyo huyo ana matatizo makubwa sana yanayomkuta kipindi kile cha kujifungua. Mama anakwenda hospitali kujifungua, anapofika hospitali, sisi wenyewe akinamama pia hatuoneani huruma, utakuta mama anamwambia mkunga pale najisikia nataka kujifungua au pengine anapiga kelele, utakuta majibu anayopewa ni mabaya sana ukizingatia yule ni mwanamke mwenzie. Wakati wa kujifungua tunasema, mtu ni nusu ya kufa, chochote kinaweza kutokea pale. Unatakiwa kumfariji, kama ni mkunga mwanamke, mfariji mama mwenzio ajione anajifungua katika hali nzuri. Lakini mtu anaweza kufikia kumwambiamaneno mabaya, kwani nilikuwepo wakati mlipokuwa mmefunga milango, lugha ambazo sio nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine kinachowakuta akinama, utakuta wakati mwingine anapokuwa mjamzito anatakiwa aende hospitalini kwa ajili ya kuhudhuria kliniki. Sasa kuna sehemu nyingine wakati mama anapohudhuria kliniki, kuna wakati mwingine anaweza kuhudhuria, wakati mwingine ana matatizo yanayomkabili ya kifamilia anashindwa kuhudhuria, utakuta mama yule anapofika anapewa adhabu. Ebu fikiria mama ni mjamzito halafu anapewa adhabu pengine anaambiwa alete karai tatu za kokoto ili afidie siku ambayo yeye hakufika pale kliniki, huo ni unyanyasaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari hizo nimezikuta wakati nimekwenda Busanda katika kampeni katika Kata ya Katoro mama anabebeshwa karai tatu za kokoto au anabebeshwa karai tatu za mchanga, huu ni unyanyasaji bila ya kumfikiria mama ana matatizo gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru ile Kampuni ya Ulinzi ambayo imewasaidia baadhi ya kinamama kuwaajiri, imewapa ajira kinamama, lakini tatizo limejitokeza kinamama walioajiriwa katika zile Kampuni za Ulinzi, ndoa zao zinavunjika, zinavunjika vipi? Kinamama wale wanaoajiriwa katika Kampuni za Ulinzi wakati mwingine wanakuwa na lindo la usiku, kwa hiyo mama anapokwenda kwenye lindo la usiku kasheshe inaanzia hapo, kwanza mama yeye anakwenda kwenye lindo la usiku, kule anakwenda kulinda atakuwa yeye halali anazunguka kwa ajili ya lindo lakini baba naye nyumbani pia siku hiyo anakuwa ni mlinzi kwa sababu na yeye usingizi unamruka kutokana na kuwa na yeye anafikiria mama atakuwa sasa hivi yuko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake mama yule anaachika, anapewa talaka kwa sababu baba hamuamini yule mama. Wakati mwingine katika lindo hilo hilo ndio chanzo cha kufanya ngono zembe na chanzo cha kupatikana kwa ugonjwa wa UKIMWI. Kwa sababu mama anapokwenda kulinda kule anakutana na mlindaji mwanamume ambapo watakapoafikiana katika mazungumzo yao, matokeo yake UKIMWI unaingia hapo hapo. Kwa hiyo, hilo linawaathiri sana kinamama. Kwa hiyo, kupitia Wizara hii, naomba Wizara iwatetee kinamama kwa kupitia hao waajiri kinamama wawe wanapata lindo la mchana wasipewe lindo la usiku ili waweze kudumu katika ndoa zao na kuweza kuziangalia vizuri familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watoto wa mitaani. Kwa kweli watoto wa mitaani wameongezeka sana. Watoto wa mitaani wako wengi na watoto wa mitaani wamesababishwa na mambo kadhaa ikiwemo tatizo la UKIMWI. Kwa sababu kuna familia nyingine watoto wamefiwa na baba, mama hawana mlezi wa kuwalea, bibi hali yake sio nzuri, kwa hiyo watoto wanabidi watoroke katika vijiji vyao waende mijini wakajitafutie kazi ili waweze kuishi. Lakini utakuta watoto hawa hawa wanaofika mjini, matokeo yake wengine wanabahatika wanaajiriwa katika nyumba lakini kuna wengine wanajiingiza katika masuala mabaya, watoto wa kike wanajiingiza kwenye ukahaba, watoto wa kiume wanajiingiza katika masuala mazima ya uvutaji bhangi, unga na wengine mwisho ya yote wanakuwa ni vibaka. Kwa hiyo, tunaomba Wizara watoto wengi wanapojazana mijini watoto wale waainishwe na waweze kujulikana wanatoka wapi na warudishwe katika vijiji vyao na kila kijiji kiandae mkakati wa kuweza kuwashughulisha watoto wale ili wasitoke katika vijiji vyao na kuja mjini bila hivyo watapata matatizo mengi mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la mikopo kwa kinamama. Tunashukuru Wizara iko katika mkakati wa kuanzisha hiyo Benki ambayo itawasaidia kinamama. Lakini ninachoomba, Benki hiyo itakapoanzishwa basi angalau iwe na riba nafuu. Kwa sababu leo kuna hizo Taasisi nyingine zinazokopesha sijui kuna *SEDA, PRIDE* na kadhalika kuna kinamama wengine wanalala chini hawana vitanda, kuna kinamama wengine wanatia nguo zao ndani ya maboksi hawana makabati kwa sababu

wanaposhindwa kulipa fedha zile basi wahusika wa Taasisi ile inayokopesha fedha inakuja kuwanyang'anya kila kitu. Wanawake tayari wameshanyang'anywa makochi, vitanda, makabati, wanalala chini, wengine mpaka nguo zinachukuliwa, kwa hiyo, huo pia ni unyanyasaji wa aina nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye hiyo mikopo ya kinamama, ninachoomba wakati watakapopewa mikopo iwaangalie pia kinamama hususan kinamama wanaoishi vijijini isiwe ile mikopo ya ile methali inayosema kuwa, "Apewayo ndio aongezwayo". Kwa sababu utakuta mikopo hii, kama mikopo tuliyoambiwa ni ya Bilioni ya Jakaya, badala ya kupewa walalahoi imekwendapewa watu wengine ambao wana uwezo, wale walengwa ambao wangestahili kupewa hawakupata mikopo hiyo. Kwa hiyo, naiomba Wizara, kama Wizara ambayo inaongozwa na kinamama, tunaomba mikopo hiyo itakapotoka, iwasaidie sana hususan kinamama wa vijijini na pia iwatambue wale wote ambao hali zao ni duni kimaisha ili iweze kuwapa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachoomba, kabla ya mikopo hiyo haijatoka, kama mlivyokwishazungumza katika vitabu hivi ni kwamba ihakikishe elimu inatolewa, kwa sababu kinamama wengi wanapopata ile mikopo kitu cha kwanza mtu anakimbilia kwa sonara anakwenda kununua vipodozi, dhahabu, anakwenda kununua samaki mkubwa kitu ambacho sio lengo la mikopo ile. Kwa hiyo, tunaomba iwepo elimu ambayo itakayowawezesha kuitumia mikopo ile. Pia uwepo ukaguzi wa mara kwa mara wa miradi ile watakayokuwa wameiandikia michanganuo kwa ajili ya mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye masuala ya watoto yatima, kwa kweli watoto yatima wanaongezeka siku hadi siku kutokana na sababu nilizokwishazitaja ikiwemo gonjwa baya hili la UKIMWI. Lakini utakuta pia na sisi wanadamu ni watu vigeugeu au ni watu ambao si wa kweli. Sasa hivi kumeanzishwa vikundi kadhaa vya kuwahudumia watoto yatima, vinaomba misaada na tunashukuru Serikali, inawapa misaada lakini misaada ile haiwaendei walengwa ambao ndio watoto yatima, badala yake misaada ile watu wanajenga majumba mazuri, wananunua magari ya kifahari watoto yatima wanabaki wanahangaika mitaani na kupata matatizo ambayo matokeo yake utakuta watoto hao aidha wa kike wanaweza kuwa ni changudoa wa kiume wakawa vibaka au majambazi sugu ambao wanahatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachoomba wale wote ambao wanawalea watoto yatima, misaada mnayoipokea wahakikishe inawafikia walengwa kwa sababu mkumbuke kama kuna Mungu na siku ya mwisho mtakuja kuhukumiwa. Kwa sababu mtu yoyote anayelea, kwa Mwenyezi Mungu ana sehemu yake aliyowekewa. Sasa ikiwa wewe unaomba msaada kwa ajili ya mtoto yatima lakini mtoto yatima yule haumfikii ule msaada, unakwenda kujenga nyumba yako, unajitengenezea dunia yako, unasahau kama kesho Mwenyezi Mungu atakuja kukuuliza. Kwa hiyo, tunawaomba wale wote mnaowaangalia watoto yatima, hakikisheni tunawasaidia katika hali nzuri kwa sababu kila mtu anaye mtoto yatima au anao watoto yatima anaowalea katika familia yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachoomba, tuwatendee vizuri kwa sababu wale hawakuomba kwa Mwenyezi Mungu wawe yatima, ni mipango ya

Mwenyezi Mungu kuwafanya vile. Ukiwalea vizuri watoto wale katika ulimwengu huu hujui atakayekuja kukufaa ni yupi, pengine huyo mtoto yatima atakuja kukuenzi kuliko mtoto wako uliomzaa mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi msisitizo wangu mkubwa nadhani mnanisikia wale ndugu zangu wapenzi mnaowalea watoto yatima, hakikisheni kwamba mnawalea katika maadili mazuri, mnawapa vyakula vizuri, vyakula vile vizuri mnavyopewa kama msaada, mhakikishe vinawafikia wao na mara nyingi viongozi inapofika siku za sikukuu wanahakikisha wanawapelekea watoto vyakula vizuri, lakini wengine hawawapi watoto vyakula vile wanavitumia wao na wengine wanaviuza, nguo wanaziuza matokeo yake watoto wanakuwa dhalili na ukiwakuta katika luninga wanajieleza kwa kweli inasikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa wosia kwa wanaohusika na kulea watoto yatima.

Sasa anafuatia Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar. Kwanza kabisa tunakupa pole kwa msiba wa kaka yako, naamini mmemlaza pema huko nyumbani. Haya Karibu. Atafutiwa na Mheshimiwa Haroub Said Masoud na Mheshimiwa Suzan Lyimo atafikiwa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya mimi kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa katika hali ya uzima na Mwenyezi Mungu akatujalia tukawa tunavuta pumzi mpaka muda huu tukawa tuko na wenzetu kwa sababu wengi wameshatangulia, tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kusini Pemba na wananchi wote wa Tanzania hususan wanawake wa Mkoa Kusini Pemba, napenda kusimama hapa ili kuchangia hoja hii lakini kwanza ninamshukuru sana ama naishukuru Ofisi ya Mheshimiwa Spika, kwa ushirikiano mkubwa ambao mmenipatia pamoja na Wabunge wote, marafiki mbalimbali, toka kaka yangu alivyokuwa anaumwa mpaka akafariki hapa Dodoma *General Hospital*. Kwa hiyo, napenda sana kutoa shukrani hizo na hasa hasa Madaktari wa *General Hospital* na wafanyakazi wote wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuchangia hoja hii kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mama Sitta na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mama Nkya, kwa kazi nzuri ambayo mmetuletea hapa mezani leo ambayo inatupa hamasa sana akinamama wa Tanzania kwamba akinamama tunasonga mbele. Napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza Serikali yetu ya Chama chetu cha Mapinduzi ikiongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Serikali hii ambayo haina utata, Serikali ambayo inafanya kazi yake nzuri na kule Zanzibar

ikiongozwa na Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Abeid Amani Karume, kwa utekelezaji wake wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2005/2010, *over hundreds percent*, imetekelezwa. Hii ni kwamba Serikali yetu inajali wananchi wake na ni sehemu kubwa sana imetekeleza katika miradi mbalimbali ama katika sekta mbalimbali za jamii, za kisiasa, miundombinu, afya, elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashangaa wale wanaobeza jitihada hizi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar kusema kwamba Serikali haijafanya kitu chochote. Nawaonya na nawaambia kwamba wanyamaze kimya wao hawaelewi, watuachie sisi. CCM ni namba moja na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi itasonga mbele na imefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake na maendeleo, nani asiyejua katika ulimwengu huu kama mwanamke ndio nyenzo ya maisha ya binadamu. Kwa sababu mwanamke ndiyo anayekwenda *labour*, akajifungua, akabeba mimba miezi 9, 10, 11 au 12. Lakini kuna watu wanaotubeza sisi wanawake wakatuona sisi si chochote si lolote, mfumo dume. Samahani akinababa lakini kuna akinababa wengi ambao wanawabeza sana wanawake. Kwa hiyo naiomba Serikali itupe nguvu sana sisi wanawake kwa sababu tukiwezeshwa, tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama tunaweza kisiasa, kijamii, tunaweza kila kitu, kila kitu ni mwanamke. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali yetu kutupa nguvu, Mama Sitta mwanamke mwenzetu, Mama Nkya mwanamke mwenzetu, Naibu Spika ni mwanamke mwenzetu, kwa hiyo, tunaomba sana Serikali hii ituwezeshe ili tuweze kuendelea mbele. Ituwezeshe kiuchumi, kisiasa, kijamii kwa sababu tunajua kama mwanamke mmoja akielimishwa inaelimishwa jamii yote. Sisi wanawake ndio wafanyakazi wakubwa, ndio walezi wakubwa, ndio wafanyabiashara wakubwa katika nchi hii, lakini tunanyanyasikanyanyasika hivi, hatupewi nyenzo nyingi za kujiendeleza. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itupe nguvu zaidi ili tuwaonyeshe akinababa wa Tanzania kwamba sisi wanawake tunaweza, CCM oyee!!!!!

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhongere sana sisi wanawake hususan wanawake wa Chama cha Mapinduzi, lazima nikisifie Chama changu kwa sababu wanawake wa Chama cha Mapinduzi hata ukiangalia humu Bungeni ndio wengi tunaweza. Kwa hiyo, napenda kuomba sana Serikali ituwezeshe zaidi ili tuweze kuendelea. Kuna wanawake Madaktari, wengine wanaendesha mpaka ndege, wanaendesha meli, ni wanawake wengi ambao tuko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake Tanzania. Naipongeza sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na Wizara hii katika mchakato wa kuanzisha Benki hii ya Wanawake wa Tanzania. Wameona kwamba wanawake tumebadilika sana, Mabenki mengi mengi ya binafsi katika nchi yetu ya Tanzania tukienda kutafuta mikopo hatupewi na hata tukipewa mikopo inakuwa mikopo midogo na vile vile riba yake inakuwa kubwa sana. Lakini naamini kwamba Benki hii Mheshimiwa Waziri Sitta kama walivyosema wenzangu kwanza iwe na riba nafuu na vile vile itawawezesha wanawake isije ikawa kwamba eti ni Benki ya Wanawake lakini ikawa jina wanawake kumbe

inawahudumia zaidi wababa. Kwa hiyo, wanawake wapewe mikopo katika Benki hii, wawekeze katika Benki hii ili wanawake wa Tanzania tuweze kusonga mbele katika kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili dhidi ya wanawake, kila siku nikisimama hapa naitetea hoja hii. Kwa kweli akinamama Tanzania ni wastahamilivu, wana upendo sana, lakini akinamama sisi wa Kitanzania baadhi tunakwamishwa na ukabila, kuna mambo ya ukabila ambayo yanaingilia kwenye familia kama baba akifariki basi mama ananyanyaswa sana huenda mpaka akafukuzwa na watoto hajui anakokwenda. Hapatiwi mirathi yake kama mwenzangu pale alivyoongea. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, akinababa waelimishwe ili sisi akinamama watupe fursa kubwa katika jamii kama mtu mume wake akifariki kwanza asiende kuolewa na mwanamume wa familia hiyo, analazimishwa kwamba lazima aolewe. Sio vizuri kwa sababu huwezi kujua yule unayemlazimisha kuolewa ana matatizo gani. Kwa hiyo, hatutaki kurithiwa wanawake kiasi hicho. Akinamama tukatae kurithiwa na waume hao ambao hatuwaelewi. Tunaomba na tunapiga vita sana suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili dhidi ya watoto, watoto ni wetu. Zamani tulikuwa tunasema kwamba watoto ni wa jamii lakini sasa imekuwa kwamba watoto kama si wa jamii. Mtoto akifiwa na mama yake au mzazi wake au akipata matatizo jamii haimuoni, inamnyanyapaa. Mtoto akifiwa na mama yake na baba yake, kwa kule kwetu Zanzibar nashukuru kwamba jamii inalelewa na jamii hata mzazi akifariki basi watoto wanalelewa na jamii. Lakini kuna jamii nyingine watoto wananyanyapaliwa wakishafiwa na wazazi wao hawasomi tena, hawavai nguo, ni kunyanyaswa mara nenda kwa shangazi mara kwa mjomba, kwa nani mpaka sasa tunapata watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasababishwa sana na umaskini lakini pia nako kutokujua, unaweza ukawa maskini lakini ukampenda mtoto wako. Kwa sababu kuna watu wengine wana wazazi wao lakini kuna wazazi makatili, juzi juzi tumeona kwenye TV na redio watu wanawafanyia ukatili watoto, wanawachoma moto, wanawachoma visu, jamani akinamama mpo? Akinamama lazima tuwapende watoto. Kama si mtoto wako ni mtoto wa mwenzio, mtoto wa jirani yako ni mtoto wa mwenzio, kwa hiyo, watoto tusiwanyanyapae, tuwape upendo hasa pale wakiondokewa na wazazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vya wanawake wajawazito na watoto. Tunaishukuru sana Serikali yetu kwamba imepunguza kwa kiasi kikubwa vifo hivi kwa kujenga vituo mbalimbali mpaka vijijini, vifaa pia wahudumu wako lakini la kushangaza ni kwamba kuna sehemu nyingine wahudumu ama Manesi, juzi nilisema hapa Bungeni wanawanyanyasa wajawazito wanapokwenda kujifungua, mimi hata sijui kwa nini, hasa wakiwa wanawake. Hivi kwa nini mwanamke unamwonea choyo mwanamke mwenzio anayekwenda kujifungua, kwa nini humpi huduma inayostahili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ila kwa upande mwingine hasa kule kwetu Pemba, mimi nashukuru sana kuna *Doctor* mmoja anaitwa Dr. Sauda Kassim na *Doctor* mmoja anaitwa Dr. Sauda Subeti Madaktari wale ni wa kupigiwa mfano katika Tanzania hii. Wanafanya kazi usiku mchana na wenzao, lakini Madaktari ama Manesi wengine

wanadhalilisha sana watu wanaokwenda kujifungua mpaka mtu unamwuliza kwa nini umechukua mimba. Kaa vizuri hapo jifungue, kwani wewe ndio unayemfungua au ni Mwenyezi Mungu anayemfungua? Kwa hiyo, vifo havitopungua kama na wale wahudumu wa hospitali, Manesi kama na wao watakuwa na roho mbaya dhidi yetu sisi wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikundi vya ushirika. Napenda kuipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuanzisha Mfuko huu wa JK na AK yaani Mfuko wa Jakaya Kikwete na Amani Karume kwa kule Zanzibar. Fedha hizi nyingi sana zimepelekwa Wilayani, Mikoani lakini cha kushangaza fedha hizi hasa hasa wanawake haziwafikii. Wakienda kuomba ni *process* kubwa sana mwisho wanaambiwa wewe huna biashara, kwani huyu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alivyoleta hii fedha yake alisema wakapewe watu wenye maduka makubwa makubwa na ma-*super market*? Alisema kwamba wakakomboke wananchi maskini walioko vijijini. Lakini mtu akienda anaambiwa kama huna mradi mkubwa huwezi kupata hiyo fedha. Kwa hiyo, tunaomba sana, akinamama wameanzisha vikundi mbalimbali vya ushirika sehemu mbalimbali, tunaomba Serikali iwaone watu hawa hasa hasa wanawake wa kule vijijini kwa sababu ukimkomboa mwanamke wa vijijini ndio umeikomboa jamii kwa sababu kule wako wengi wanalima, wana biashara mbalimbali kule. Kwa hiyo, tunaomba sana fedha hizi za JK na AK ziwafikie akinamama wa vikundi vya ushirika waliopo katika nchi yetu ya Tanzania kwa sababu akinamama wanafanya kazi kubwa sana wanastahili kupongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake na uongozi. Naipongeza Serikali kutupa sisi wanawake hamasa katika nyanja mbalimbali za uongozi hasa wa kisiasa. Nawaomba akinamama wenzangu wawe *strong* katika kugombea sehemu mbalimbali. Kuna mambo haya ya Ubunge, kuna Uwakilishi, kuna Udiwani, kuna sekta mbalimbali za kugombea, ukiona tayari wakati wa kugombea umefika basi nakuomba chukua fomu gombea, wa kumpa mtu ni Mwenyezi Mungu, tutasaidiana ili tuweze kushinda tuingie pamoja hapa Bungeni ama kwenye Baraza la Wawakilishi, Mwenyezi atatujalia sote tuwe katika salama na tuweze kushinda hasa Chama cha Mapinduzi kiweze kushinda na zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi ama Albino. Imekuwa sasa ni nyimbo kwamba wananchi hawa ni wenzetu. Jamani tujue kama Mwenyezi Mungu yupo na Mwenyezi Mungu ana rehema na sisi binadamu tumeumbwa na Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ameumba binadamu kwa njia mbalimbali wengine weupe, wengine weusi wengine ndio hao hao waliokuwa rangi zao Albino na kila rangi ili tujuane. Usimuone mwenzako amekuwa Albino ukamnyanyapaa, ukamkata kichwa chake, ukamkata miguu yake, ukamtoa roho yake, wewe sio uliyemleta duniani, aliyemleta duniani ni Mwenyezi Mungu. Turudi kwa Mwenyezi Mungu wananchi wa Tanzania tusiwaue Albino, Albino ni ndugu zetu, ni wananchi wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Umesikika kwa kweli. Mheshimiwa Haroub Said Masoud na Mheshimiwa Suzan Lyimo nadhani hawa watatosha kwa asubuhi.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia. Nisingepata nafasi, ningesononeka sana sana. Kwanza, nianze kwa kuiunga mkono hoja hii iliyopo mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana sana, Mheshimiwa Waziri Sitta, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Nkya, Katibu Mkuu, Ndugu Mariam Mwafisi na viongozi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kutuletea hotuba ambayo ina matumaini makubwa.

Kwanza niseme tu kwamba leo asubuhi Mheshimiwa Spika alipoingia ndani hapa nikasema ama kweli leo Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Kwa sababu wale wapambe wake waliomfuata nyuma, wote ni akina mama. Kwa hiyo, akina mama wanaweza. Aliniacha hoi sana tena kwa baadaye alipoona safu ya kinamama haijakamilika, akakuita wewe ukae juu ya Kiti hicho ili nyote hapo muwe wanawake watupu. Sasa hii ni ishara njema kwa Wizara, ishara njema kwa *fifty fifty*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hapo tu, yeye ni miongoni mwa watu ambao zamani kama si miaka miwili, anaitaka *fifty-fitty* iwe. Kamati yangu hii ya Maendeleo ya Jamii, ina wajumbe 22, miongoni mwa wajumbe 22, 13 ni wanawake, wanaume ni tisa tu, huo ni ushahidi kamili. Ninaamini katika Kamati yangu wanaofanya kazi nzuri zaidi, ni hawa kinamama hata leo tunaona wanavyochangia hapa.

**NAIBU SPIKA:** Ambapo wewe ndio Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri mimi ndio Makamu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa punde hivi, Mheshimiwa Mramba amezungumza, nikasema kweli wakati umebadilika. Utakumbuka mwaka 1995, Bunge tulivyokuwa pale kwenye ukumbi wa Msekwa, mwanaume akizungumza suala la akinamama anazomewa, nakumbuka vizuri sana. Yaani mnavyozungumza suala la akina mama wawezeshwe mnazomewa; lakini leo Mheshimiwa Mramba kasema yeye ni mshabiki lakini sasa nasema, yeye nakubali ni mshabiki na amenivutia sana na ningekuwa na uwezo wa kumweka katika Kamati hii, basi ningemuomba Spika amweke katika Kamati yetu. Lakini sasa mshabiki namba *on*e sio yeye, mshabiki namba *one* ni mimi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa 13 niko katika Kamati hii kama Makamu Mwenyekiti, kwanza nilikuwa mshauri, baadaye nikawa Makamu Mwenyekiti, miaka 13 niko Wizara hizi hizi tatu, naziongoza. Sasa mimi ndio shabiki namba *one*. Mi naomba kweli wote wajifunze kama Mheshimiwa Mramba alivyokwishaelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Quran Tukufu, inazungumzia, sisemi kwa muujibu wa Quran, inasema kwamba binadamu yeyote anaposhukuru kwa wema aliofanyiwa, basi atawazidishieni kila la heri. Lakini utapokuwa unabeza maendeleo au chochote kile, Mwenyezi Mungu atakuadhibuni adhabu shadida, adhabu shadida ni adhabu kubwa sawa na moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni lazima niipongeze Serikali, bajeti iliyopita, Wizara hii ilitengewa shilingi bilioni 14.66 kwa mara ya kwanza, bajeti ya Wizara hii imechupa kweli kweli kutoka shilingi bilioni 14 mpaka shilingi bilioni 21.6. Tunaishukuru sana Serikali na hatuwezi kuisema wala hatuwezi kubeza maendeleo haya, ingawa bado fedha hazitoshi. Ninachokiomba kama, alivyosema Mheshimiwa Mramba, Wizara hii bado ina matatizo mengi sana. Tuna kila wajibu kuitetea na kama alivyosema akina mama wanadhalilika sana, miaka miwili iliyopita, tunapokutana na wajumbe wa Wizara, unaona kama watu wamechoka, wanadhalilika pale, kumbe kulikuwa na kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ile, viongozi waliwekwa kwenye mabao muda wa miaka nenda, miaka rudi; hawathibitishwi kazini kwao wala hawapandishwi vyeo. Kwa mara ya kwanza hivi karibuni tumeonyeshwa watu kadha ambao wamepandishwa vyeo, inafurahisha. Tulipokutana kwa mara ya mwisho, nyuso zao zina tabasamu, wanachapa kazi, hawachoki na hata hotuba yao safari hii imeongoza katika hotuba za Wizara tulizozisimamia sisi. Hasa hii inatia moyo, wafanyakazi wanapokuwa kazini, wanataka motisha na haki zao wapewe. Mama Sitta tunamshukuru sana, Mwenyezi Mungu akujalie uendele na moyo huo huo na *Inshaallah* uwanyanyue zaidi wafanyakazi wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana kuona Rasimu ya Waraka wa Mkakati wa Kuwezesha Ushiriki wa Wanawake Tanzania, kwamba ulishatayarishwa. Ni mategemeo yetu kwamba Serikali itafanya kila juhudi ili yote yaliyokuwepo katika waraka huo yatimizwe na kama inavyozungumzwa, mimi imani yangu, unavyomwezesha mwanamke umeiwezesha jamii. Lakini vile vile, hata tuangalie, tujiulize, haya matatizo mengi mengi haya ya kula rushwa, nadhani Wizarani kama wapo wanawake basi wawili watatu lakini sisi kina baba, eeh, tukipata nafasi kidogo tu, unaongeza ziro mbele. Kidogo tu ukikaa, unachota hichi. Mimi nasema kwamba tutafikia pale ambapo tunapataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mtoto, ni suala ambalo linasubiriwa kwa muda mrefu sana. Mchakato wake umechukua muda mrefu na imani yetu kwamba karibu itawasilishwa Serikalini ifikie pahala ambapo; kwa sababu tukitaka tusitake sote tulikuwa watoto, leo tuna mamvii haya tele, lakini kama hatukulelewa vizuri na Serikali zetu na wazee wetu na majirani zetu, tusingefikia hapa. Watoto wanahudhunisha sana kutokana na matatizo wanayoyapata. Huwezi kuamini wanatoka wapi watoto wale, sababu ni nini? Sababu ni sisi kina baba!

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wengi hawa, ni sisi tuna chupa chupa humu mitaani lakini mimi simo; kabisa simo, una chupa chupa, unataka nini wewe? Una wako nyumbani, unaenziwa, una tandikiwa kitanda, unapikiwa, unafanyiwa kila kitu, bado eti

ukitoka kidogo, pya, pya, pya, unaenda kufanya mengine yasiyo kuwa na maana. Mtoto akizaliwa, humtaki unamkimbia, sasa hii ni hatari, tulete Sheria hapa ambayo itambana hata yule anayefanya mapenzi nje ya ndoa ili kuwazuia watu wasifanye mapenzi nje ya ndoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika dini yetu ya Kiislamu, inakatazwa sana kuzini. Zinaa ni kwenda na mtu ambaye hujamuowa. Ya nini? Nini unalolifuata? Hayana maana hayo. Ebu, tuacha jamani, kina baba tuambizane sote.

**NAIBU SPIKA**: Ni dini zote bwana!

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo sijui kuna tatizo gani kuhusu hawa watoto wasichana wanaotiwa mimba mashuleni. Tumepiga kelele sana Wabunge hapa na tumesema ebu tufuateni mfano wa Zanzibar, Zanzibar watoto wakitiwa mimba, kwanza nitatoa sababu, lakini baadaye akishazaa anabadilishwa shule tu, anapelekwa shule nyingine, hawekwi shule ile ile. Hasa unamtesa mtoto ambaye mara nyingi wengine wamebakwa na Walimu wao, wamebakwa na kina sisi, wamebakwa na watu kadhaa wa kadha. Sasa mtoto kama yule unamtia hatiani kwa jambo ambalo hakulitaka? Lakini je, mtu huyo huyo akimpata mwanaume laghai, eeh, kuna wanaume laghai hapa, akikuambia neno hata kama moto unauona, akikumbia hii pepo basi utakubali kwamba hii ni pepo, anamlaghai, anakubali, anashika mimba siku ile ile moja, hasa tuwaonee huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, kupitia kwako, naomba ashirikiane na Waziri wa Elimu kulitatua tatizo hili, ili mwakani tukija hapa, mwezi kama huu, tatizo hili liwe limetatuka. Hivi karibuni walikuja watu wa upande wa Umasaini kule, wameleta orodha ya wanafunzi 14, hawajapokelewa shule, walitiwa mimba maskini kwa kubakwa, sasa sisi pahala petu pa kusema ni hapa, tunaomba sana na hili litatuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili dhidi ya wanawake. Mimi inaniuma sana. Wewe umeowa kwa hiari yako mwenyewe, kwa ridhaa yako mwenyewe kama n'gombe umetoa, kama sisi tunatoa dhahabu, maana sisi kwetu baba zetu wanatoa dhahabu tu; hatutoi n'gombe lakini kila siku mateke, kila siku vibao, mwanamke huyu hawi mtu isipokuwa usiku saa nne za usiku, ndio anakuwa mtu. Tena wakati huo anabembelezwa, asubuhi maji yeye ateke, kuni akachukue yeye, kufua nazi akafue yeye, kupika apike yeye, halafu tena jioni mateke.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wa kesi ambayo ilimtokea jirani yangu. Jirani yangu ni mlevi sana, jina lake Michael, kutwa yuko *bar* tu yeye. Sasa siku ya pili yake alikuwa anasafiri, lakini yuko *bar* kiasi saa nne za usiku, akakumbuka akampelekea *message* mkewe. Mke wangu, kesho asubuhi uniamshe saa kumi na moja alfajiri kwa sababu *reporting time* ni saa kumi na moja na nusu. Karudi kalala na yule mama kasoma kama Mheshimiwa Faida yule, mjanja. *Time* ile ile aliyoambiwa amuamshe akampelekea *message* mumewe, mume wangu amka wakati umewadia. Ilipofika saa mbili ndio anayanyuka, anamwambia mke wangu hukuniamsha, nimekuamsha mume wangu,

angalia *message*. Kwani wewe umeniletea nini? Si *message*? Hii nyumba yako hukai hapa, kampiga mateke mpaka kalazwa hospitali. Sasa huu ndio ukatili na udhalilishaji sana, nasema sipendelei.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napongeza tovuti ambayo imezinduliwa hapo jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho kabisa tunaomba sana Vyuo vya Maendeleo viongezewe pesa. Imani yangu, Serikali badala ya shilingi bilioni 21 safari hii wataweka shilingi bilioni 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nawashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na nawatakia kila la kheri. Naunga mkono hoja kwa mara ya pili, kwa asilimia mia kwa mia. Ni imani yangu jioni vifungu twende, twende. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naona mambo yamebadilika siku hizi tunasemewa kwa nguvu kabisa. Sasa Mheshimiwa Susan Lyimo, ndio atakuwa msemaji wetu kipindi hiki cha asubuhi.

**MHE SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya Wizara nyeti sana ya Maendeleo ya Wanawake, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapojaribu kuchambua bajeti za Wizara mbalimbali, pamoja na mambo mengine, tunaangalia pia hali ya uchumi, tunaangalia randama za Wizara, pamoja na ripoti ya *CAG*, lakini vile vile pamoja na Ilani ya Chama ambacho kinatawala. Ni wazi kwamba Wizara hii ni nyeti sana, hasa tunapoangalia idadi ya wanawake ambayo ni kubwa zaidi kuliko ile ya wanaume. Kwa hiyo, naamini kabisa kama ambavyo Dr. Aggrey alisema, ‘Ukimuelimisha mwanamke, umeielimisha jamii lakini ukimuelimisha mwanaume umemuelimisha mtu mmoja mmoja’.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile sasa hivi tuna usemi unaosema kwamba ‘ukimwezesha mwanamke anaweza’ na tena anaweza kwa ufanisi mkubwa na mifano iko wazi. Tumeona jinsi gani kina mama ambao wamepata madaraka sio tu hapa nchini lakini ulimwenguni kote wameweza kufanya kazi zao kwa ufanisi na hivyo watu wamezidi kuwa na imani na kina mama hasa katika kipindi tulichonacho. Ni wazi kabisa kwamba Taifa lolote linaloendelea, lazima linakuwa limewekeza kwa akina mama. Mimi nasema hatusemi wanawake na maendeleo, ila tunasema wanawake ni maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Wizara hii ni nyeti sana na Wizara mtambuka, lakini kwa kweli kwa miaka mingi mfululizo tumekuwa tunaona ni jinsi gani Wizara hii imekuwa ikipata fedha kidogo. Pamoja na ongezeko la asilimia 33 walilolipata kutoka shilingi bilioni 14 mpaka shilingi bilioni 21, bado Wizara hii nadhani kwa kweli ina fedha ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niweke ulinganifu kidogo tu, ukiangalia katika bajeti hii ni *simple mathemetics*, kwamba kwa shilingi bilioni 21 kwa bajeti nzima ya nchi ya trilioni 9.5, Wizara hii ina asilimia 0.2 ya bajeti nzima. Kwa hiyo, bado mimi nadhani kwa kweli Wizara hii ina changamoto nyingi na kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mramba na pia mimi mwenyewe niliwahi kusikia kwamba, tatizo kubwa ni kwamba Wizara haipeleki *programmes* kubwa kubwa au *programmes* ambazo zitapata fedha nyingi. Kwa hiyo, nadhani kwa changamoto hii basi, naamini Wizara ina *programmes* nyingi, kwa sababu ni Wizara mtambuka kwa maana hiyo ni wajibu wa Wizara hii, nadhani ina wataalam wa kutosha; wahakikishe kwamba wanapeleka *programes* kubwa ili waweze kupata fedha ambazo zitakidhi mahitaji ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie tu katika randama ya Wizara hii. Mimi kidogo imenishtua. Ukiangalia kwenye mapato wanayotegemea kuyapata kwa mwaka mzima ukiachilia fedha ambazo zitapatikana kutoka kwa VIU ya shilingi milioni 6,900,000 mapato mengine yote wanayotegemea kuyapata ni shilingi 4,000 tu kwa mwaka mzima. Kwa hiyo, napata wasiwasi kidogo, kwa mfano ukiangalia kwenye *property income* wanategemea kupata fedha shilingi 1,000 tu kutokana na *rent*. Sasa nashindwa kuelewa hizo nyumba ni za namna gani. Lakini vile vile ukiangalia kwenye *funds*, kwenye *miscellaneous receipts and recovery of public money*, unakuta zote ni shilingi 1,000. Kwa hiyo, naomba wakati Waziri atakapokuja kujumuisha, atuambie ni kwa nini watapata mapato kidogo namna hii katika Wizara nzima ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini labda niende kwenye hoja zangu, hoja ya kwanza niipongeze sana lililokuwa Baraza la Wanawake Tanzania kwa kuweza kushinda ile kesi na ninaamini sasa wanawake tutakuwa wamoja tukiachana na itikadi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kina mama tuna matatizo mengi na matatizo haya yametokana na historia yetu. Ni wazi akina mama tulikosa elimu na hii si kwa Tanzania tu; kwa nchi nyingi za Afrika na hata nyingine za Ulaya na zile ambazo zimeendelea kama Marekani. Utakuta akina mama hata wa Marekani miaka ya nyuma walikuwa hawaruhusiwi hata kupiga kura lakini jinsi ambavyo tunaendelea kupigania haki za akina mama, akina mama wengi tumepata fursa; lakini bado tunabakia pale pale kwamba kwa kweli ukiangalia asilimia kubwa ya Watanzania akina mama wengi hawajapata elimu na wale wachache waliobahatika kupata elimu basi walau, tunashukuru kwamba sasa hivi wameweza kuingia katika siasa na vyombo vingine vya maamuzi. Lakini ni wazi kwamba ukiangalia kwa *percentage*, watoto wa kike wanaoingia Darasa la Kwanza Tanzania ni wengi lakini jinsi ambavyo wanaendelea katika elimu zao za sekondari na hasa elimu za juu unakuta kwamba idadi ile inapungua *tremendously*. Kwa hiyo, hapa kuna tatizo la msingi na nadhani baadhi ya wenzangu wameshalizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumzie hasa hasa tunapoona *drop out* kubwa au mdondoko katika elimu, unakuta mara nyingi kwa watoto wa kike ni mimba, tunaziita mimba za utotoni au *early pregnancies*. Kwa *data* nilizonazo, kwa mfano kwa mwaka jana tu, kwa Mkoa mmoja kama Mkoa wa Mwanza kulikuwa na wanafunzi zaidi 7,600 ambao walipata ujauzito; lakini vile vile Mkoa kama wa Kilimanjaro ni 885, jambo ambalo siku za nyuma kwa Mkoa kama wa Kilimanjaro lilikuwa halipo. Kwa hiyo, rai

yangu kama ambavyo Mheshimiwa Masoud amesema, tunajua Zanzibar na Tanganyika ziliungana kwa hiyo tuna Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Kule Zanzibar wana *policy* inayoitwa *Spinster Policy*; kwamba watoto wa kike wanapopata ujauzito, wanaweza kurudi mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku Tanzania Bara nakumbuka nilikuwa kwenye Kamati hiyo ya kukusanya maoni na tumejaribu kupita Mikoa mbalimbali na hasa wadau wa elimu tukizingatia pia watu wanaohusika na masuala ya dini walihusishwa ambapo tulidhani watakuwa wagumu sana lakini hata wao wenyewe wameona umuhimu wa kumsomesha mtoto wa kike. Mimi naamini kabisa kwamba ule mzunguko wa umaskini yaani ile *vision circle* ya umaskini, kama mama hajasoma ni wazi kabisa hatoweza kumsomesha mtoto wake. Kwa hiyo tunafikiri ni muhimu sana kwa Serikali ya Tanzania kuhakikisha kwamba tunakuwa na *policy* ambayo itawawezesha watoto wa kike wanaopata ujauzito, waweze kurudi shuleni hata kama itakuwa ni shule tofauti; ili waweze kumaliza elimu yao ya msingi na baadaye waweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia fursa hii kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo imeweza kuainisha au kuweza kuongeza idadi ya akina mama viongozi na tumeona kwenye jedwali nadhani jedwali namba moja, jinsi ambavyo akina mama wameongezeka katika vyombo vya maamuzi, hasa kwenye suala la watendaji kwa watu wanaotoa maamuzi kama Wabunge, Majaji na wengine wengi hata Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni wazi kwamba suala la *fifty-fifty* liko katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini vile vile niseme kwamba suala la *fifty-fifty* limetokana na Azimio la Umoja wa Nchi za Afrika ambapo pia Serikali yetu imeliridhia, kwa maantiki hiyo, Serikali ya Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi waliweka katika Ilani tukiamini kwamba mwaka 2010 basi uwakilishi utakuwa *fifty-fifty*. Lakini wakati nauliza swali langu hapa Bungeni tarehe 1 mwezi wa saba, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, aliweza kunijibu na ni kweli ni wazi kwamba sasa suala la *fifty-fifty* halitawezekana lakini mimi naamini kabisa Wizara hii, ikiwa ndio Wizara msemaji wa wanawake, itakuwa na mipango mikakati ya kuhakikisha kwamba kina mama wanaojitokeza katika chaguzi hasa chaguzi zijazo za Serikali za mitaa, inawawezesha ili waweze si tu kushiriki lakini waweze kushinda kwa sababu mimi naamini kabisa kina mama wakiwezeshwa wanaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lililozungumziwa la jinsi ambavyo watoto wanadhalilishwa. Ni wazi kwamba sasa hivi tunaona idadi ya watoto wa mitaani inaongezeka kwa kasi, lakini najua kuna juhudi mabalimabali ambazo zinafanywa na watu binafsi pamoja na mashirika ya Kiserikali ikiwa ni pamoja na kuwaweka katika vituo. Lakini bado tatizo lipo na ninaamini kwamba watoto wale pamoja na kwamba tunawaita ni watoto wa mitaani, hakuna watoto wa mitaani kwa sababu watoto wote wamezaliwa na hivyo ni jukumu letu sote kuhakikisha kwamba tunaweza kusaidia ili janga hili la watoto tunaowaita wa mitaani lipungue ama liishe kabisa kwa sababu tunaamini watoto hawa baadaye ni watoto ambao watakuja kuwa viongozi wa baadaye, lakini vile vile watakuja kuwa ni wapiga kura wetu. Lakini vile vile tunaamini kwamba watoto hawa wakijengewa mazingira mazuri watakuwa na maadili kwa sababu najua

kabisa huko wanakoishi, vitendo wanavyovifanya sio vitendo vizuri na kwa maana hiyo; watakapoweza kuwekwa katika mazingira mazuri, watoto hawa wanaweza kuja kuwa watoto wazuri sana au watu wema sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tunazungumzia suala kwamba Wizara hii hasa imejikita katika suala ya wanawake, lakini mimi naamini kabisa tunahitaji nguvu za wanaume, waweze kuwashirikisha sana kina baba ili waweze kutusaidia. Mimi ninaamini kabisa akina mama kama akina mama, pekee yetu hatutaweza, kwa sababu tukiangalia mifumo ipo, hasa vijijini na hata mijini akina baba ndio wamekuwa sehemu kubwa ya kutafuta kipato akina mama wameshindwa. Kwa hiyo, naamini kama akina baba watashirikishwa, wakaelewa umuhimu wa akina mama, tutaweza kupiga hatua mbele na kuhakikisha kwamba kina mama wanashiriki katika shughuli zote za maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka kulichangia hasa ni suala zima katika bajeti hii. Nimejaribu kuangalia nikaona kwamba ni kweli Wizara imepewa fedha chache kama ambavyo nimesema, lakini naamini kama zitatumika kama ilivyopangwa, zinaweza zikafanya mambo mazuri. Lakini suala la Vyuo vya Maendeleo; kwa kweli vyuo hivi ni vya muhimu sana na vimekuwa vikitoa wataalam mbalimbali. Lakini vyuo hivi vipo katika hali mbaya sana na vinahitaji ukarabati na hata ukiangalia fedha walizopewa za maendeleo bado ni kidogo kuweza kufanya ukarabati katika vyuo vyao vyote vilivyoko nchi nzima. Kwa hiyo, naomba, nakumbuka mwaka jana watu walisema ni afadhali basi vyuo hivyo vikapelekwa Wizara ya Elimu, lakini mimi naamini kabisa bado Wizara hii kimsingi ina wajibu wa kuwa na vyuo vyao na kwa maana hiyo ni jukumu la Serikali au la Wizara hii kuona kwamba wanapeleka *programme* kubwa ili waweze kupata fedha nyingi za kuweza kukarabati na hata kujenga vyuo vingine kwa sababu kweli taaluma ya maendeleo ya jamii inaitajika sana katika jamii kama ya Tanzania ambayo inaendelea. Kwa sababu hata ukiangalia nchi za wenzetu zilizoendelea, wanatumia sana wataalamu wa maendeleo ya jamii kwa sababu bila jamii, hakuna watu na watu wote wako katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vyuo hivi au wataalam watakaopatikana kutoka katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, vitasaidia sana kuboresha hali ya maisha ya Watanzania na hivyo basi kuleta maendeleo katika sekta zote tukijua kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni Wizara mtambuka na kwa maana hiyo ipo katika maeneo yote kuanzia mazingira, afya, elimu na mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba kwa kweli kilio cha Wizara hii sisi kama Wabunge, tutaendelea kupiga kelele kuhakikisha kwamba Wizara hii inapata fedha nyingi za kutosha ili iweze kukamilisha majukumu ambayo sisi tunaamini kabisa kama Wizara hii inashughulikia. Mambo ya kina mama kwa mfano; sasa hivi kero kubwa sana ya akina mama ni suala zima la maji. Lakini tukiangalia katika Wizara hii, kwa kiasi gani itasaidia kutekeleza, kuhakikisha kwamba kina mama wanapata maji salama na safi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile tuangalie ni jinsi gani Wizara hii inaweza kusaidia kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la watoto wa mitaani. Lakini kimsingi niseme tu kwa kweli, Wizara hii ina majukumu mazito sana na ikiyafanya kwa ufanisi, naamini kabisa akina mama tutasonga mbele na kwa maana hiyo tutakuwa na maendeleo makubw, tutashika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalizie tu kwa kusema kwamba, pamoja na kwamba kina mama wengi tuko katika ngazi za maamuzi, lakini niseme tu bado kwa kweli tunahitaji ile *political will* aliyonayo Mheshimiwa Rais aendelee nayo ili akina mama wengi zaidi wapatikane. Mimi naamini baada ya miaka ya 1960, akina mama wengi sasa hivi wamesoma, tuna wanawake wengi ambao ni Maprofesa, Madaktari, kwa hiyo bado ninaamini kwamba kina mama wapo waliosoma ambao wanaweza kabisa kuchukua madaraka ya nchi hii katika maamuzi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu naipongeza sana Serikali, nampongeza Waziri na nategemea fedha basi *next time* watapata nyingi, asante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa kipindi cha asubuhi, naona tumeishia hapo. Lakini tukirudi mchana atapewa nafasi Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond na Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, hao watapewa nafasi mchana. Baada ya hapo, tutamuita mtoa hoja, tutamalizia kazi.

Nina matangazo machache, kwanza kabisa Kamati ya Uongozi wa Bunge, watakuwa na kikao saa saba na nusu katika ukumbi wa Spika.

Pili, wanachama wa Chama cha Wanawake wa Bunge, wanawake wa Bunge wote mnaelezwa kwamba *DVD* ya uhamasishaji zilizofanwya na *Hans Sedor Foundation,* mnajua mlikuwa- *interviewed* na vitu kama hivyo, ipo tayari. Kwa hiyo, mkachukue kwenye ofisi yetu, chumba namba 208, nadhani ni nzuri sana.

Halafu pia ofisi inatangaza kwamba kesho tarehe 10 Julai, 2009 baada ya kuahirisha kikao cha Bunge, kutakuwa na tafrija ya Wabunge katika viwanja vya Bunge itakayofadhiliwa na Kampuni ya simu ya Vodacom Limited. Aidha, kutakuwa na shughuli za huduma ya pesa, maonyesho ya mavazi kwa Wabunge na Bendi ya muziki, *King Kiki* La Capital, itatumbuiza.

Naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba mara baada ya kusitisha shughuli za leo, saa hizi, wenye magari pale wanaombwa kuhamisha magari yao ili wapambaji waendelee na shughuli zao za maandalizi kwa ajili ya kesho. Kwa hiyo, mkitoka hapa, mkichukua magari yenu, jioni mkirudi msipaki pale kusudi maandalizi ya kupamba yaendelee.

Pia nimeagizwa niwatangazieni kwamba katika viwanja vyetu vile vya maonyesho, nadhani wengi mmeona toka maonyesho yameanza, kuna ndugu pale wa kampuni inaitwa VUNJA BEI ILOGANZARA, hiki nadhani Kisukuma, wanauza

vyombo vya nyumbani kwa bei ya kuvunja. Vile vyombo vinawafaa sana kule kijijini mnakokwenda, mpitie pale, muone kabla hajafunga biashara yake. Kuna vyombo vya ndani, bei yake ni ya kuvunja, mnakaribishwa mkavione.

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo mengine nasitisha shughuli hizi mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.55 Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Kama Wizara ni ya Watoto, wakilia ni haki yao! Siku ya Wizara yao, wakilia ndio haki yao! *(Mheshimiwa Naibu Spika aliyasema hayo baada ya sauti ya mtoto kutoka gallery kusikika akilia). (Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tulipokuwa tunasitisha shughuli mchana, niliwataja wafuatao ndio watakaochangia saa hizi. Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika hoja hii. Kwanza, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake kwa kazi nzuri sana ambazo wamekuwa wakifanya. Moja ya kazi hizo ni uanzishwaji wa Benki ya Wanawake ambayo tunaambiwa imekamilika na wakati wowote kuanzia sasa itaanza kufanya majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakiri kwamba shilingi inayoingia mkononi mwa mwanamke inafika nyumbani. Kama Benki hii itafanya majukumu yake ipasavyo, basi shilingi itafika nyumbani kuhudumia jamii wakiwepo watoto chini ya uongozi wa baba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tumepata mafanikio makubwa sana katika kuleta usawa wa jinsia katika jamii yetu na kukemea vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake. Haya mambo yamekuwa yakiimarika kadri muda unavyokwenda na nataka niipongeze sana Wizara kwa kuongoza katika suala hili. Lakini nitahadharishe tu kwamba hii Benki ikishakamilika, basi ipewe uwezo wa kujitegemea kikamilifu na wala isiwe ni sehemu ya Wizara kwa sababu tunajua urasimu ulioko Serikalini unaweza kukwamisha masuala ya biashara kama haya yasiende ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kuomba kuchangia ni ili nizungumzie juu ya Idara moja muhimu sana ya Maendeleo ya Jamii. Hii Idara ndio chombo ambacho kwa kweli kina uwezo wa kuwasaidia wananchi kuandaa mipango yao na kutafuta rasilimali za kuitekeleza. Kwa bahati mbaya sana, kwa miaka mingi sana, hii Idara imekuwa ikidhoofishwa mwaka hadi mwaka, wakati mwingine bila kukusudia. Watumishi wa Idara hii nafikiri kutokana na mafunzo wanayopewa vyuoni, wana uwezo mzuri sana wa

kuwasiliana na jamii, wana uwezo mzuri sana wa kuiandaa jamii na kwa hiyo, mara nyingi sana wamechukuliwa na kupewa kazi nyingine ambazo ni tofauti na zile ambazo walikusudiwa wafanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba Wizara iangalie sana jinsi ya kuimarisha Idara hii ya Maendeleo ya Jamii. Kila Serikali ya Mtaa, kila Mkurugenzi anapaswa kwa kweli kutambua kwamba Idara ya Maendeleo ya Jamii ni chombo cha kumsadia kutekeleza masuala yanayohusiana na wananchi. Tunazungumzia mipango mingi mikubwa na mizuri ya kuondoa umaskini. Sasa hivi tunazungumzia kilimo kwanza, tunazungumzia mipango mingi, lakini hatuzungumziii tutaifikishaje mipango hii kwa wananchi. Maana tunaweza tukakaa hapa na makabrasha tunayaandika kiingereza, kwa hiyo na yenyewe hayawezi kufika kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna chombo kingine kinachoweza kufikisha dhana hizi kwa wananchi isipokuwa Idara ya Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri pamoja na Serikali za Mitaa watambue umuhimu wa chombo hiki na wahakikishe kwamba wanakitumia ili kuwa ni daraja kati ya utawala na wananchi na ili kiwe ni chombo cha kusaidia wananchi kuandaa mipango yao na kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali za CCM zimekuwa zikijitahidi sana kutafuta njia za kuweza kuwafikia wananchi na kuwaletea maendeleo, kupunguza umaskini na kuhakikisha kwamba kuna chakula mezani. Lakini, kila tulipofanya hivyo hatukukumbuka kwamba tuna chombo ambacho tungeweza tukakitumia na wakati mwingine pengine hatukukumbuka kwa sababu chombo chenyewe kilikuwa dhaifu mno. Katika Jimbo langu nimekutana na Afisa Maendeleo ya Jamii mmoja tu, Mbezi Luis, kwingine ninakotembea siwaoni. Ina maa kwamba Idara lina watumishi wachache sana ambao wako katika jamii sasa hivi. Ninaona katika hotuba ya Waziri kwamba Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vinaendelea kufundisha watalaam hawa, lakini kuna haja ya kuchukua hatua za haraka kuajiri na kuwapeleka kwenye Serikali za Mitaa, kuwapeleka kwenye vijiji ili wakatusaidie kufanya hii kazi muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mapesa tunayozungumzia, mabilioni ya JK, pesa tunazotoa katika Serikali za Mitaa, zilipaswa zipite kwa Idara hii ya Maendeleo ya Jamii ambao ndio wangebaini ni wapi ambapo zitatumika kikamilifu na kwa hiyo kuwezesha kupata manufaa yale tuliyokusudia. Kwa bahati mbaya sana, zinapokuja zile kazi zinazoihusu Idara hii, kwa kweli hatuzitoi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Wizara hii ina vyuo vya aina mbili; Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vile ambavyo vinafundisha watalaam na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ama *FDCs* ambavyo kusudio lake ni kuwafundisha wananchi wenyewe *directly*. Tumeona katika uzoefu tuliopata, mimi nimekuwa Wizara ya Kilimo, kwa hiyo nimeona uzoefu katika kilimo. Wananchi waliopelekwa vyuoni wakafundishwa, halafu wakapewa mahitaji ya kuweza kutekeleza kile walichofundishwa, wamefanya vizuri sana, wakulima wa mpunga ni mfano.

Sasa tuna Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi mimi nilikuwa najua viko 54, lakini naona kwenye hotuba vinazungumziwa 58. Kuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii nane. Tukitumia vyuo vyote hivi na tukatumia vyuo vilivyo katika Wizara za sekta mbali mbali kufundisha *directly*, tutafundisha idadi kubwa sana ya wananchi. Mimi nasema tulenge kufundisha wananchi *directly* badala ya kutumia hizi huduma za ugani ambazo wote tunajua kwamba haziwafikii wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Idara ya Maendeleo ya Jamii ihakikishe kwamba Vyuo vinakarabatiwa, vina walimu wa kutosha na wanaohitaji ni, *core* (ni walimu wa msingi) kwa sababu kila atakayepeleka kozi yake pale anapaswa apeleke na watu wa kufundisha kozi hiyo na kuhakikisha kwamba Wizara zote za kisekta zinatumia vyuo hivi kuanzia mwanzo wa mwaka mpaka mwisho wa mwaka na kuanzia tena mwaka na kuendelea, kwa sababu hivi ni vyuo ambavyo vingeweza kufundisha idadi kubwa sana ya wananchi kila mwaka.

Tukitumia vyuo hivi vya maendeleo ya wananchi na vyuo vya maendeleo ya jamii tutafundisha idai kubwa sana ya wananchi na tukishawafundisha, halafu tukawapa sasa misaada ya fedha zile zinazotolewa katika mifuko mbali, maendeleo yao yatakuwa ni ya haraka na upunguzaji wa umaskini utakuwa ni wa haraka pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo ambalo ni lazima vile vile tulitilie mkazo ni lile nililotangulia kusema kwamba tunahitaji kuwa na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wengi wa kutosha na katika jamii ili waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, katika Idara hii kuna Vikosi vya Ujenzi. Hawa ni mafundi wanaofundishwa katika Chuo kilichoko Misungwi. Mtakumbuka siku moja Mheshimiwa Shibiliti alikuwa anazungumzia juu ya Chuo kile, ukarabati wake na maendeleo yake na kadhalika. Hawa ni watalaam muhimu sana, hata tunapozungumzia kupeleka tekinolojia katika jamii, tunazungumzia watalaam hawa. Hawa ndio watalaam ambao wangeweza kutusaidia tunapojenga yale majengo ambayo wananchi wanajenga kwa nguvu zao wenyewe ya kujitolea katika shule za msingi, shule za sekondari, zahanati na barabara. Hawa wanafundishwa jinsi ya kutumia nguvu kazi kufanya kazi za ujenzi wa madaraja, ujenzi wa barabara na hizi shughuli nyingine. Lakini mmi kwa miaka mingi sana sijakutana na fundi hata mmoja wa Vikosi vya Ujenzi. Lakini nafikiri bado vipo maana vyuo bado vinaendelea kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vikosi hivi viimarishwe ili kila Wilaya iwe na Kikosi chake cha Ujenzi ambacho kitasaidia wananchi katika kubuni miradi yao na katika kuitekeleza. Hawa ndio walianzisha mpango hapa wa kutengeneza barabara kwa kutumia nguvu kazi, ikaonekana kama ni jambo geni kabisa. Lakini Idara ya Maendeleo ya Jamii imekuwa ikitumia njia hizi za kutengeneza barabara kwa miaka mingi sana. Hapa katikati tumedhoofu katika kufanya majukumu haya na ningeomba sana turudie kwa sababu wananchi wanahitaji utalaam wa vikosi hivi ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umaskini wa wananchi wetu unatokana na vitu vidogo vidogo sana ambavyo wakipata mtu wa kuwaelekeza, mtu wa kuwasaidia, wanawreza katika kipindi kifupi sana kuondokana na umaskini na kuishi maisha bora zaidi kama ambavyo tunaahidi katika Ilani yetu. Idara hii ndio Idara yenye uwezo wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kuwasiliana na Wizara nyingine zote kuhakikisha kwamba kuna *coordination* inayomsaidia huyu mwananchi ili aweze kupiga hatua kwa haraka zaidi na hili ndio jambo lingine na la mwisho ambalo nilitaka kulizungumzia kwamba moja ya kazi za Idara ya Maendeleo ya Jamii ni *coordination*, ni uratibu wa watu wote, wawe ni NGOs au ni Idara za Serikali ambao wanahusiana na mwananchi katika Mtaa ama katika Kijiji. Kwa hiyo, ndio wanapaswa kuratibu shughuli hizo na katika kuratibu, kubaini wananchi wanahitaji nini kwa maendeleo yao na kwenda kwa hawa walio na utalaam huo ili waje wakawasaidie wananchi katika njia hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wakurugenzi wetu wa Serikali za Mitaa wangetambua hilo, nina hakika Idara ambayo ingekuwa karibu nao sana ni hii Idara ya Maendeleo ya Jamii, lakini Idara ya Maendeleo ya Jamii iliyoimarishwa, maana kama katika Wilaya hakuna watalaam hawa wa Maendeleo ya Jamii, hizi kazi hata ukiwapa hazitafanyika. Kwa hiyo, tunaomba sana Wizara ihakikishe kwamba hii Idara inaimarishwa katika Serikali za Mitaa ili iwe ndio chombo cha kuchochea maendeleo ya wananchi. Nina hakika hii Idara ikiimarika vya kutosha na ikafanya kazi zake kwa utaratibu wa kuridhisha, tutaona mabadiliko makubwa sana katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kwa mara ya kwanza mtu ameeleza maendeleo ya jamii maana yake nini. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru tu kwa kunipatia nafasi hii ambayo ni nadra kwa kipindi hiki cha bajeti ambapo kwa kweli ukipata nafasi unasema ahsante Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napanda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii ambayo, labda niseme iliyo kweli kwamba mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati inayohusika na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii kumpongeza Mama huyu akiwa na Naibu Waziri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumza hivyo kwa sababu Wizara hii inatangazwa kwamba ni watoaji wa sera, sijui ni wanasiasa hawa akina mama, kwamba wenyewe ni kumwaga sera tu, halafu itekelezwe mahali fulani. Maana yake ni nini? Ni kama vile Chama kinatoa kitu, halafu Serikali yake ndiyo inatekeleza ambayo ni hali ngumu. Ni ngumu, ni ngumu! Halafu bajeti yake ni ya mwisho. Napenda kusema kwamba kwa kweli hawa wanawake mpaka kufikia hatua hii, wanastahili hongera na hongera za dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwingine ambaye ningelipenda nimpongeze kwa dhati kabisa ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa nchi yetu Tanzania - Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete. Ni kwa nini ninampongeza? Mimi leo kusimama hapa, asingekuwa yeye, nisingesimama hapa. Ninasema hivyo kwa sababu yeye ni mpiganaji mkubwa wa kutaka wanawake wasimame sehemu zote tangu Tawi, tangu Kata, Wilaya, Mkoa, mmh, naogopa kusema tungechukua nafasi yake. Lakini ninachotaka kusema, nimshukuru tu sana kwamba ni mpiga debe mkubwa wa wanawake waweze kushika hatamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaomwongelea Mkapa, wote ni wanaume hapa wanasimama pwa pwa pwa wanaongea. Hivi kuna mwanamke kasimama! Wanawake tupuge makofi. Ninasema hivyo kwa sababu, sisi leo hoja ya mwanamke atoke huko aliko na yeye aonekane. Tumesema kwamba mwanamke aonekane! Tukapokelewa, tulipokelewa na nani? Tufike mahali basi tuseme ahsante. Hata ahsante inatukosa, tunabaki kuamua kumsulubu mtu badala ya kusema ahsante! Hebu tujifunze kusema ahsante Watanzania! Badala ya kuongelea maendeleo ya majimbo yetu, tunataka maji, tunataka barabara, tunataka UKIMWI uishe, tunataka vituo vya afya, tunataka mambo yote ya maendeleo. Wenye kuongelea Marais wawekwe Mahakamani ni nchi zilizoendelea. Tanzania imefikia mahali hapo kweli! Tufike mahali basi, hebu tuongelee maendeleo badala ya kusulubu Marais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema tumetoka kwa Mkapa ana thelathini, hata sisi wanawake tuliomo humu tuko kwa ajili ya nani?. Kwanza wanawake ni wazazi, tunazaa mpaka Marais, mnataka....*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea sasa na hoja yangu ya bajeti. Bajeti ya Maendeleo ya Jamii ni finyu. Ni finyu kwa misingi ipi? Tunapoongelea Wizara hii tunajikuta tunaongelea jinsi zote mbili. Walio wengi wanadhani maendeleo ya jamii inamwongelea mwanamke, hapana! Tunaongelea pande zote na mtu unayemzaa katika jinsi, baba na mama anatokea na mtoto. Leo hii tunainyima bajeti kwa misingi ipi? Wenzangu wamezungumza mapema wakisema wazi kabisa jinsi gani tunavyoinyanyasa Wizara hii Maendeleo ya Jamii. Hivi jamii ni nani? Jamii, yaani ni upana wa binadamu alivyo katika maisha yake ili kupata maendeleo kuvusha kile ambacho kiko mbele yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambieni jamani ndugu zangu, tunapofika mahali tunaongelea bajeti hii, eti tumetoka 14 tumefika 21, eti ni bilioni tano zimeongezeka, tunapiga makofi, hivi kweli! Kwa jinsi gani bajeti hii inavyokuja, hebu tufike mahali mtujaribu basi, katika maendeleo ya jamii hebu tuwekeni na sisi, muweke *priorities* zenu tu; wekeni tu kipaumbele mnavyoweza mkaweka wekeni tu, ya kwanza, ya pili, hebu tuwekeni wa tatu kipindi kijacho mwone na sisi tutakavyotenda maajabu. Kwa sababu ninyi mnadhani kipaumbele ni elimu, mimi sikatai. Kilimo mpaka kimewekewa kaulimbiu inasema, “kilimo kwanza,” sikatai na mambo mengine sikatai. Hivi mkiweka maendeleo ya jamii hata ya nne, ya tano kuna unbaya gain? Hebu tuwekeni basi mwone kwa nini tunapiga kelele. Kwa nini bajeti ya Maendeleo ya Jamii haipewi kipaumbele?

Naomba bajeti ya Mandeleo ya Jamii iweze kupanda, mwone jinsi tutakavyotenda maajabu ndani ya bajeti hii. Tutoke tu mahali mnapotuzungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la watoto. Napenda niongelee suala la Muswada wa Watoto. Watoto jamani, kuna siku moja Mbunge mmoja aliongea suala la kupewa 100. Alipojibiwa akaambiwa kuna *White Paper* itazunguka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hewa, kupewa 100 nini?

**MHE. MARIA I. HEWA:** 100 Shilingi. *100 Tanzania shillings ya hundred!* 100 eeh, analipwa mwanamke Sh. 100/= akatunze mtoto uliyeshughulika wewe mwanaume! Sasa watoto hawa, unamtunza kwa Sh. 100/=, atatoka na elimu ya namna gani? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niinakubali kwa sababu imeingia na *issue* ya Mahakama ya Kadhi. Naomba mnisikilize. Ni ngumu kwa sababu imeingia hiyo, kwa sababu na watoto wa Kiislamu wako kule ambapo mtoto wa Kiislamu akizaliwa nje ya ndoa, hatari! Hathaminiwi kabisa. Basi, acha ikifika hapo, nasema acha nivumilie. Acha nivumilie kwa sababu yeye ndio kabisa anaonekana ni wa ajabu na kweli, lakini baba alishughulika. Lakini, ninashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri amesema Muswada huu ni wa mwaka huu 2009 mpaka 2010, nikifika hapo, ninakubali kwamba kabla sijatoka ndani ya Bunge hili Muswada huu utakuwa umeshaonekana. Hilo ndio mimi ninakubaliana naye, lakini vinginevyo kweli ningekataa pamoja na kwamba niko ndani ya Kamati ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Margaret, anafanya kazi ya ziada kwa kweli. Nasema ni mama shupavu kwa kweli, ni shupavu sana. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Unamaanisha Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Ndiyo!

**NAIBU SPIKA:** Kwa nini hukusema?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Basi, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Akisema yeye, ninakubali kwa sababu hajawahi kutudanganya hata siku moja ndani ya Kamati. Kwa hiyo, ninaamini Muswada huu utatoka maana watoto hawa hawawezi wakadai haki zao kupitia maandamano, hawawezi wakadai haki zao kupitia migomo, hawawezi wakadai haki zao kupitia taratibu zozote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, Mheshimiwa Waziri, kwa kweli mimi nimeku-*quote* leo, kweli kaa imara na kweli huu Muswada uwepo. Watoto wetu wanaozaliwa nje ya ndoa wanateseka, watoto wetu wanachomwa moto, wanateseka, watoto wetu hawa wanabakwa wanateseka, wana kila aina ya mateso. Namwomba Mheshimiwa Waziri, katika hili kama kweli anatosha katika Wizara hii, watoto hawa waletewe Muswada kweli ili uweze kuwalinda watoto hawa. Naomba kabisa, waletewe

Muswada watoto, wana kila aina ya taabu. Wanateswa kimaisha ya kawaida, nimekupa mfano wa kidini wanavyoteswa hawa. Naomba kabisa ushupalie pamoja na kwamba wewe ni mtunga sera, potelea mbali watungie sera lakini fuatilia mama. Tuatilia ili tuweze kuwasaidia watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, niende Mkoa wangu wa Mwanza, tuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Malya. Hiki Chuo kilikuwa kizuri, kilikuwa kizuri mama, basi ni taratibu za kawaida za Serikali kikashuka. Taratibu zake za maisha za kuendesha shughuli hii. Lakini hicho Chuo kilikuwa kina maeneo ya kazi, kina maeneo ya kawaida na kina maeneo ya malazi. Kuna mabweni Mama Margaret, Mheshimiwa Waziri, nimekatazwa kukuita hivyo. Yako mabweni mazuri mazuri kweli! Hicho Chuo kina uwezo wa kuweka watu 60, *so far* kina watu wachache tu wako kama thelathini na kuna siku nimetembelea hicho Chuo nikamkuta mwenye Jimbo Mheshimiwa Ndassa.

*(Hapa Kengele ya pili ilipigwa)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante! Tunaendelea! *(Kicheko)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Hi! Aisee!

**NAIBU SPIKA:** Sasa Margaret humuungi mkono?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Naunga mkono hoja! Hivi imegonga ya kwanza? Aaa, ungenikumbusha! *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mnajua Mawaziri wanatajwa kwa vyeo vyao, lakini kwa sababu wanafahamiana ndio akamwita Margaret. Namwita sasa Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae. Ahsante sana Madam Hewa! *(Kicheko)*

**MHE. ANNA LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia siku hii ya leo. Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo inaleta changamoto kubwa katika jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nianze kusema umuhimu wa *NGOs*. Kuna *NGO's* mbalimbali ambazo zinasaidia makundi mbalimbali ya kijamii katika nchi yetu. Tuna makundi mengi kwa mfano watoto yatima, watu waliothirika na Ukimwi, vilevile kuna akina mama wajane *NGO's* na zinaleta pesa nyingi tu kwa ajili ya walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NGO's* nyingi zina malengo mazuri tu ili kuweza kuleta zile pesa na kusaidia ile jamii iliyoathirika. Lakini NGO's hizi zinapoleta pesa zinawalengwa ambao wanapewa pesa kama NGO*'s* ambazo ziko Mikoani na Wilayani, lakini kiasi kubwa cha fedha hizi hazifiki kwa walengwa. Kuna sehemu nyingi Mikoani na Mawilayani wanakusanya akina mama wajane ili waweze kupewa misaada lakini wanapewa akina mama wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna waatoto yatima, kuna *CBO*'s ndogondogo ambazo zinakusanya watoto yatima ili waweze kusaidiwa lakini unakuta zile *CBO's* hazipati ule msaada. Wanapata *NGO's* za mijini kama Dar es Salaam kuna *NGO* kubwa ikipata pesa haishushi kwa walengwa wenyewe huko chini Mikoani na Wilayani unakuta sehemu nyingine makundi yale yanapata taabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Wizara kwa kuwa wenyewe ndio wanatoa vibali kwa *NGO's* wafuatilie hii misaada inayokuja katika haya makundi kama watoto yatima, akina mama wajane pamoja na waathirika wa ugonjwa wetu wa Ukimwi na vilevile hamasa inakuwa chache sana, kwa kuwa zile pesa hazifiki katika maeneo husika ndio maana unakuta kuna matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Serikali kama Serikali iweze kushirikiana na hizi *NGO's* ambazo zinaleta hizi pesa kwa ajili ya walengwa ili ziweze kuwafikia. Kuna kundi lingine ambalo wenzangu wengi wamezungumzia ambalo ni la watoto wa mitaani. Watoto wa mitaani wamezidi kuwa wengi mno. Inasikitisha! Nilikuwa naomba Serikali iweze kuchukua hatua ya kuwakabili hawa watoto wanaozurura barabarani maana unakuta watoto wengine wanastahili kabisa kwenda shuleni lakini wanazurura barabarani. Inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mtoto ameshikwa na mama mzima, ana nguvu zake ambaye angekaa kijijini akalima, lakini anampotezea maisha yule mtoto anaanza kufumba macho barabarani ili aweze kumsaidia kuomba hela. Hii sio haki kwa yule mtoto. Yule mtoto anatakiwa aende akasome, hii kazi yote ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto tunaomba Serikali ichukue hatua hii ili muweze kuwasaidia wale viumbe ambao baadaye watakuwa majambazi, maana sasa hivi ameshaanza kuomba, baadaye atabadilika atakuwa jambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaingia kipengele cha akina mama katika Mawilaya yetu na Mikoa yetu. Kuna maafisa wanaitwa Maafisa Maendeleo ya Jamii. Maafisa Maendeleo ya Jamii ni wachache mno, hawakidhi mahitaji yanayohitajika katika jamii hasa ya akina mama, tunawahitaji kwa ajili ya Mambo mengi. Lakini kwa kuwa sasa hivi tumekuja na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, Huyu Afisa maendeleo ya Jamii angeweza kutusaidia kuwaelimisha akina mama vijijini jinsi gani ya kulima kilimo bora, ili huyu mama aweze kulima kilimo bora ili aweze kupata mazao, aweze kujikimu katika maisha yake. Lakini hawapo! Waliopo ni wachache. Tunaomba Wizara iongeze Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kila Kata ili tuweze kusaidiana na jamii iliyoko Kijijini

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna pesa zinakwenda katika Halmashauri zetu. Mimi zile hela hata Waziri katika Hotuba yake amesema ameongeza katika Halmashauri Shilingi milioni kumi kila Halmashauri. Wale akina mama hawapati hizi fedha kabisa, hizi hazifiki kwa walengwa kabisa. Sasa mimi sijui utaratibu ambao unachukuliwa ili huyu mama wa Mpanda, Nkasi aweze kupata hizo pesa. Mimi sielewi kwa sababu sijawahi kuona mama yeyote wa Wilaya ya Mpanda au Wilaya Nkasi ananiambia

amepata hela kutoka Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, zile za Halmashauri sijawahi kusikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa zinakwenda wapi na mlengwa ni nani? Kila siku mnatuandikia katika hotuba yenu kuwa hela ziko zinakwenda kwenye Halmashauri zinafanyaje fanyaje ili hawa akina mama waweze kupata? Mbona hawapati? Kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli inasikitisha sana kwa sababu huyu mama maskini ambaye tunasema kila siku tunataka tuboreshe maisha yake, ambaye tunasema tunampelekea ili aweze kupata sijui kuna fungu la Sh. 50,000/= akirudisha sijui kuna Sh. 100,000/=, sijui kuna Sh. 200,000/= huyu mama hapati. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie hizi pesa aone zinakwenda wapi? Mbona walengwa hawapati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, au hata siku moja basi Mheshimiwa Waziri aje kutuonyesha kusema kwamba katika Wilaya ya Mpanda walipata akina mama kadhaa, Wilaya ya Nkasi walipata akina mama kadhaa, Mkoa wa Tabora walipata akina mama kadhaa, kule Urambo walipata akina mama kadhaa, katika hili fungu ambalo linapelekwa kwa ajili ya maendeleo ya akina mama kwa ajili ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, nashangaa nasikia kuna fungu la vijana. Fungu la vijana hili nalo, katika vijana kuna vijana wa kike na wa kiume, lakini mimi sijawahi kuona kundi la vijana ambalo wamepata hela kutoka Halmashauri hizo. Hela ziko wapi? Tunazisikia tu kwenye vitabu kuwa pesa zinapelekwa, lakini walengwa hawapati. Kama huo mfumo upo, basi upangwe vizuri ili walengwa wafanikiwe kupata hizi pesa mnazoziandika siku hadi siku wakati walengwa hawapati. Hili jambo lifuatiliwe kwa makini sana. Kwa hiyo, wale akina mama ni maskini, wanahitaji misaada kutoka katika Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuja katika vyuo vyetu vya maendeleo ya Jamii. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, safari hii ametukumbuka kuongeza pesa katika Chuo chetu cha Msaginya. Nampongeza sana. Vilevile umetukumbuka katika Kituo chetu cha Chala, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hivi vyuo naomba viboreshwe kwa sababu huyu mtu anayekwenda kusoma Chuo hiki hana *certificate* ambayo inaweza kumjulisha kuwa kama amesoma kama vile *VETA*. Ninaomba hivi vyuo viboreshwe viwe kama *VETA* au vishee ile *certificate* inayotoka pale iwe ya *VETA*. Kwa hiyo, tunasema hivi vyuo vinapeleka watoto wanaoishia Darasa la Saba, akitoka pale hajui chochote, tunaomba hivi vyuo viboreshwe vitaweza kuja kutusaidia ukizingatia sasa hivi tuna mambo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kundi ambalo liko kule katika maeneo yetu la watoto wadogo ambao wanachunga ng’mbe hawaendi shule. Wale watoto, hivi vyuo ndio vingewafaa. Ninaomba Serikali iende ikafanye utafiti wao, maana wale watoto

wadogo wanachunga ngo'mbe matokeo yake wanachukua zile ng'ombe wanapeleka kwenye mashamba ya mahindi halafu wale wakulima wanapata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba hivi vyuo ndio viwe madarasa ya wale watoto, kuliko tuwaache wale watoto kila siku wanachunga ng'ombe wala hatuwafikirii, wala hatuweki mikakati yao. Ninaomba Serikali kama Serikali iwatambue wale watoto wachunga ng'ombe kule Mpanda, Nkasi katika Mikoa mbalimbali Shinyanga, Mwanza maana wamekuwa ndio wachunga ng'mbe na kundi hili limekuwa kubwa mno. Ninaomba kundi hili la watoto lisaidiwe maana wanapeleka ngo'mbe wale kwenye mashamba ya mahindi matokeo yake inakuwa ugomvi kati ya mkulima na mfugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ng'ombe afuge mtu mzima mwenye akili zake anayejua kwamba ng'ombe anatakiwa apelekwe kwenye malisho, lakini yule mtoto aende shule apatiwe haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE.SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Watendaji wake kwa kutuletea hotuba hii nzuri ambayo hakika inatupa matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niseme kwamba tatizo kubwa ninaloliona kwa wanawake katika nchi yetu ni elimu. Wanawake ukiondoa wale waliosoma katika madarasa na vyuo, wale wanawake wa vijijini ambao hawakupata fursa hiyo kwa wakati huo wanataabika sana kujua haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu kama hajui haki yake hawezi pia kujitetea na hapo basi unakuta akina mama kama hao mara nyingi wao wanajua wajibu tu na sio haki. Mimi napenda kuiuliza Wizara, akina mama kama hao wanasaidiwaje? Miaka ya sasa kuna *NGO's* ambazo zimejitahidi sana kusaidia na zinatoa mafunzo katika nyanja mbalimbali .

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimanjaro kuna *NGO* zinazofundisha wanawake haki zikiwemo zile *NGO* zinashughulikia mambo ya UKIMWI kama KIWAKUKI na KINSHAI na ikiwemo *NGO* inayozungumzia mambo ya ukeketwaji kama *AFGEM*. Swali langu kwa Wizara ni kwamba *NGO* kama hizo ambazo zimejitahidi sana, Wizara inasaidiaje katika kuweka fungu kidogo ili wao wapate elimu waweze kupanua zaidi elimu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anahitimisha alitoa shukrani kwa Mataifa mbalimbali na Mashirika yaliyosaidia sana katika Wizara hii. Lakini alizungumzia yale ya Kitaifa na siyo yale ambayo yako katika Mikoa yetu. Naomba kuuliza Wizara: Je, wana taarifa na *NGO* hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nilikuwa napenda nijue katika ule ukurasa wa 49 anapozungumzia Wilaya zilizopata fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Katika Wilaya zilizoorodheshwa pale takribani Wilaya 18 siioni hata Wilaya Moja ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha, ningependa kujua ni vigezo gani vilivyotumika kutoa hela hizo na ni kwanini hakuna hata Wilaya moja katika Mikoa mingine kwa mfano Mkoa niliotaja ninaotoka mimi. Elimu ya Uchumi kwa akina mama zetu siku hizi wengi wanazungumzia sana ujasiriamali, kila mtu lugha hiyo anaifahamu, lakini utekelezaji wake ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo watu ambao wamezaliwa kwa kweli ni wajasiriamali, kwa bahati yeye akipewa shilingi kesho itakuwa shilingi tano. Lakini wapo watu ambao hawajafundishwa na hawajui, hawapo katika mfumo wowote ule. Watu hao wanatakiwa wapatiwe elimu ili sasa wajue ni jinsi gani watazalisha kwa gharama ipi atauza kwa kiasi gani na atapata faida namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wakitamka ujasiriamali wanazungumzia labda biashara ya kununua na kuuza na hapa nitatoa mfano. Utakuta kijijini kwangu ambaye hana mkungu uliokomaa atanunua ndizi kwa mwenzie, atateremsha mjini, atakwenda kushinda nao kutwa nzima akiiuza kichane au ndizi moja moja na yeye anajiita mjasiriamali. Sasa hapo kuna kupoteza muda kutwa nzima anashinda mjini na jioni labda ndizi hiyo hakumaliza kuuza, basi ataamua kutoa bure au kwa Sh. 200/= ili mradi arejee nyumbani alikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa wangetakiwa wasaidiwe kiasi kikubwa ili wajue kwamba wanaweza wakaongeza biashara au wakapanua biashara yao na kuzalisha zaidi bila kupoteza muda wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia hayo mambo ya Elimu na Uchumi ningependa nizungumzie suala la mabinti zetu. Niipongeze sana Serikali kwa kuona kwamba sasa hivi kuishia darasa la saba haitoshi, ni vyema mwanafunzi yeyote akaishia Darasa la 12, shule zimejengwa Sekondari za Kata nyingi tu, lakini bahati mbaya sana Sekondari hizi ziko mbali na nyumbani kwa vijana wetu. Kwa wale vijana wa kiume inakuwa ni rahisi kuchochea baiskeli au kukimbia mpaka shuleni lakini kwa mabinti zetu mara nyingi inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba nitumie nafasi hii kuiomba Wizara hii iwaombe wale wafadhili ambao wametutajia ili waweze kutusaidia kujenga hizo *Hostels*. Ingekuwa rahisi kusema kwamba Serikali iongeze hela ili wajenge *hostel* kama *hostel* za mabinti zetu katika maeneo hayo ya Shule za Kata. Lakini bajeti waliyopewa ni finyu mno na hapa naona niombe basi kipindi kijacho Wizara hii ifikiriwe bajeti kubwa kwasababu majukumu yake ni makubwa sana zaidi ya ambavyo tunaiona na jinsi ambavyo tunaweza kufikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo watapata bajeti, basi nawaomba wafikirie *hostel* hizo na wasaidiane na wale wadau ambao wameshaanza kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi jukumu hilo la kujenga *hostel* limekuwa ni la Wabunge wa Majimbo, Wabunge wa Viti Maalum, Madiwani na jamii yenyewe ndio inajitahidi kujenga *hostel* hizo. Natoa rai hii huko tuendako tuweze kutafuta namna ambayo tutapita Wizarani tujue tumetengewa kiasi gani cha kujenga *hostel* hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa nizungumzie hela alizotoa Mheshimiwa Rais katika mifuko ya kuendeleza akina mama. Jambo hili liko wazi katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwamba wanawake watapewa fursa zote ili waweze kujikwamua, siyo mara ya kwanza kwa Serikali yetu kufanya jambo hilo enzi za Mwalimu hela kama hizo zilitolewa na kulikuwa na kiwango mtu asichukue zaidi ya Sh. 500,000/= lakini hela hizo hazikurejea kwa sasbabu zilitolewa bila watu kupata elimu ya kutosha. Matokeo yake mzunguko ule ulikwama na sasa tumekuja kupata tena kwa mara ya pili. Lakini enzi za Mwalimu haikuishia tu kutoa hela, Mwalimu alikwenda hatua mbele zaidi akatoa mikopo ya miradi, ilikuwapo miradi ya kufuga ng'ombe na ilikuwepo miradi kufuga kuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Wizara kama itaweza ikazungumzia tena jambo hili na hasa Waziri wetu huyu katika Baraza la Mawaziri endapo itawezekana wanawake wa vijijini wakopeshwe miradi kuliko kukopeshwa hela ambazo zinapitia kwenye *SACCOS* na siyo wengi wana uwezo wa kujiunga na *SACCOS* hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba ingekuwa rahisi sana kwa wanawake hawa kupatiwa miradi na wakafikiriwa. Mwaka huu itakuwa ngumu sana kwenye kurejeshewa hela hizo kwasababu kama uko Kirimanjaro wengi walichukua hela hizo wamekwenda kulima, mwaka huu ni kiangazi hawakupata chochote katika walichokwenda kulima na hata naona taabu, watanunuaje mbegu mwakani? Sasa hiyo inakuwa ni taabu na sijui wao watasaidiwaje na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie kundi lingine ambalo ni kundi la watoto. Watoto wengi ambao wanapata mimba mashuleni inakuwa ndio mwisho wa kusoma, mabinti zetu hawa wanapata matatizo mara mbili na Taifa pia linapata tatizo mara mbili kwanza tatizo la binti aliyepata mimba hataendelea tena na shule, labda tu kama anaweza akasaidiwa vinginevyo na kama familia ina uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo kubwa zaidi wale watoto waliozaliwa katika hali hiyo, mama yule kwa vile alikuwa hakujiandaa, hamtaki mtoto. Ndio unasikia kuna watoto waliotupwa. Sasa hivi Taifa lina watoto wengi ambao wametupwa na kuokotwa; hata juzi kuna mtoto ameokotwa baada ya treni kupita eneo la Morogoro. Lakini kuna ambao wameshafikia sasa ni umri wa mika 15, naomba niulize Wizara: Je, wameshafanya tafiti *(research)* wakaona kundi hili ni kubwa kiasi gani? Je, hizo *NGO* ambazo zinalea watoto hawa zinawalea mpaka kufikia umri gani? Baada ya hapo inakuwa ni vipi*? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi kuna wale watoto wanaofiwa na wazazi wao wakati ambapo watoto hawa ni wadogo na bahati mbaya wanaweza wakafa wote baba na mama. Unakuta sasa ni kaya za watoto wadogo. Hizi kaya zinakuwa na baba, mtoto na mama, motto, lakini inakuwa kwa bahati tu *NGO* kama kule kwetu KIWAKUKI inaingia katika jukumu hilo inawajengea nyumba na inaomba viongozi wa Kata waangalie familia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Wizara inasaidiaje familia zinazolelewa na watoto? Mpaka sasa kule wamejenga nyumba 600 na 36 zikiwa ni hizo za yaani, kaya za watoto wasio na baba, mama wala ndugu, lakini hizo zilizobakia nyingine ni kwa ajili ya wajane walioachwa. Naomba Wizara ichukue hili kama tatizo ama changamoto ione kwamba siku za baadaye watasaidiwa vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi lngine linalonisumbua sana katika jamii ni kundi la wazee. Ukipita katika ziara wanakuja kwenye vikao wanauliza: “Sasa tumepatiwa hela za Mheshimiwa Rais lakini sisi hatuna nguvu ya kuzalisha hizo hela, hatuna hata watu wanaotuangalia, vijana wetu wamekufa kwa Ukimwi sisi mnatuangaliaje hapa?” Nchi yetu haijafikia bado mahali ambapo tuna vituo vya kutosha vya kulelea wazee. Eneo hili linanisumbua kiasi ambacho naona nishirikishe pia Wizara, kama huko tuendako tunaweza tukawa na vituo vya kulelea wazee ambavyo vitakuwa rasmi na vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo yalikuwa toka zamani, lakini siyo rasmi kwa wazee. Ilikuwa labda ni kwa wale waliopata ugonjwa wa ukoma au wazee ambao walikuwa omba omba njiani. Lakini sasa twende na wakati basi, tunapofikiria katika zile *program* kubwa, tuone pia hiyo ni hali ambayo tungetaka ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi waliozungumza mwanzoni, wenzangu walisema hata hii hela ya mfuko wa jamii haieleweki, niwaombe Wizara itupe mafunzo, itueleweshe ni jinsi gani ya kufikia hela hizi. Hivi juzi tulikuwa tunazungumza mahali, wengine waliona pia ni ngumu. *(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. MWINCHUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii. Vilevile naomba kuchuka nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri - Mheshimiwa Nkya, Katibu Mkuu na Wakuu wote wa Idara wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ambayo kwa hakika tunaiona pamoja na ufinyu wa fedha ambayo Wizara hii inapatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwa kuanzia kwenye Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali. Utakumbuka hivi karibuni kulikuwa na malumbano hapa kuhusu misamaha ya kodi na kwa sehemu kubwa Mashirika yasiyokuwa yamehusika katika sehemu hii, hivyo napenda kutumia fursa hii kuishauri Serikali kwa maana ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, kitengo cha uratibu wa shughuli za *NGO*, kwanza

kuhakiki Taasisi za Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ya nchi nzima kujua yapi yanayofanya kazi kwa uhakika na yapi ambayo yapo katika *briefcase*.

Naomba sana zoezi hili lifanyike kwa umuhimu sana kutaondoa sana hii mianya ya kukwepa kodi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kutumia Idara yake awahusishe uongozi wa Wilaya zote hasa Makatibu Tawala wa Wilaya ili waweze kufuatilia kwa karibu katika Wilaya zao waandikiwe rasmi wapewe muda na baadaye muwapelekee barua za *reminder* na muwape muda maalumu, wakishindwa kujithibitisha na kuonekana na Makatibu Tawala na Ofisi yako, basi ni vyema vyama hivyo vikafutwa. Naomba sana Serikali hili ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la nishati mbadala kuna mwenzetu mmoja ambaye yuko Tanga amegundua nishati mbadala ya kuzalisha umeme. Naomba sana Wizara hii kwasababu wanamfahamu vizuri mtu huyu washirikiane naye wamtangaze, washirikiane na Taasisi nyingine za Serikali ili mradi huu wa uzalishaji umeme kwa njia za nishati mbadala, naomba sana uweze kufahamika kwa Maendeleo ya Jamii na kwa Maendeleo ya Wananchi wetu wa Tanzania. Ni Nishati ambayo ina bei nafuu ukilinganisha hata wenzetu wanaozalisha kwa kutumia hizi *solarpower* naomba sana Serikali impe changamoto mwananchi wetu na kumtambulisha mbele ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa rai kuanzishwa kwa mfuko wa kusaidia vituo vya watoto yatima. Wizara hii inahusika sana kwa kweli, inasikitisha ukitembelea vituo vya mayatima utaweza kulia.

Naomba sana Serikali, tumeweza kutoa fidia kwa wafanyabiashara kwa ajili ya mtikisiko wa dunia wa sasa hivi wa fedha, sasa kwa nini tushindwe kuanzisha mfuko kama huu ambao utasaidia vijana wetu, viongozi wa baadaye wa Taifa letu katika huduma za vyakula, huduma za masomo, kwa maana ya ada au karo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara isimamie na kupeleka rai kwa Serikali Kuu ili ione itasaidiaje katika kuanzisha mfuko wa watoto yatima na kuweza kuhudumia vituo vyetu vya watoto yatima ambavyo vinatoa huduma ya dhati kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kutembelea baadhi ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii au ya wananchi tuseme. Vyuo hivi kwa kweli vinasikitisha sana na vingine vina upungufu wa wafanyakazi. Hadhi ya vituo hivi ni vibaya kabisa, havina nyenzo, vimetupwa, majengo yapo vibaya mno. Sasa naiomba Serikali, mnapouliza Wizara wanasema mgao waliopata kwa Serikali ni mdogo ili kuvipa hadhi vituo hivi ambavyo ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wetu, kwa maendeleo ya jamii ya Tanzania. Naiomba Serikali kuviangalia kwa umuhimu unaostahili kama alivyoangalia vyuo vingine ili viboreshwe viweze kufanyakazi iliyokusudiwa na iwe tija kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hotuba ya Mheshimiwa Waziri ilivyoeleza kwamba ana matatizo ya ofisi, wanakodi hawana *rest house*, kwa kweli hii ni aibu kwa Serikali. Naiomba Serikali ifanye kila njia hatimaye Wizara hii iweze kupata jengo lake na *rest house* kwa ajili ya viongozi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kwamba Wizara hii hapo nyuma ilikuwa pia na utaratibu wa kutoa udhamini wa masomo ya Elimu ya Juu kwa wanawake. Lakini kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sikuona hata sehemu moja iliyozungumzia suala hili. Sasa napenda kujua: Je, kitengo hiki kimehamishwa katika Wizara hii au suala hili limefutwa ambalo ni muhimu sana kwa maendeleo ya wanawake hasa tunapoelekea huko katika mpango wa *fifty fifty*.

Hali kadhalika, nilitaka kujua pia: Je, katika kipindi cha nyuma ni watu wangapi ambao wamefaidika na mfuko huu na pia mwamko wa wanawake wenyewe katika kutumia mfuko huu kwa maendeleo ya elimu ya wanawake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la wanawake na uongozi. Serikali imejitahidi sana kuweza kuwateua katika taasisi mbalimbali za Serikali. Lakini zaidi ya hayo, tuna wanawake wengi wenye elimu ya juu ambao kwa kweli hawako kwenye taasisi za Serikali, lakini ningependa kujua: Je, wanawake wa aina hii ambao hawawezi kutambulika kirahisi wako nje ya taasisi za Serikali, Wizara ya Maendeleo ya Jamii mnawatambua namna gani na waweze kuwasiliana vipi na Wizara ili kutambulika sifa na uwezo wao kwa Taifa letu hili?

Nawapongeza sana kwa juhudi zenu za *fifty fifty* na Serikali imeunga mkono lakini bado naomba kutoa changamoto kwa Serikali, nayo iendelee na mpango wake huu wa kuweza kuwanyanyua akina mama. Serikali imejitahidi sana. Sasa najiuliza, bado mnataka majimbo tu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la mwanafunzi na mimba za shuleni. Hili ni tatizo kwa vijana wetu wanaokumbwa na matatizo ya aina hii. Lakini tuna mfano ulio hai kabisa, mfano ambao tumeweza kuuiga na hauna athari ya aina yoyote, kwanza mimi binafsi nimesoma na watoto wa aina hii. Anasoma huku ni mjamzito, ana mume huko Zanzibar. Wanamaliza masomo yao kwa kiwango cha juu kabisa wanafaulu na hivi leo wako baadhi yao ambao nimesoma nao ni viongozi, madaktari, manesi na kadhalika. Kwa hiyo, tunawaonea vijana wetu.

Mimi naomba Serikali hili ilitazame tena kwamba vijana wetu wanapopata bahati mbaya ya kushika mimba wakiwa shuleni ni vyema tukawapata fursa kwanza waendelee na masomo wakati bado mimba yao inaweza kuwaruhusu kuendelea na masomo na baada ya kujifungua waweze kurudi tena shuleni kuendelea na elimu. Tunapoteza vipaji vyao, tunapoteza uwezo wao. *(Makofi)*

Nilikwenda siku moja kwenye *NGO* moja kule Temeke, nikamkuta mtoto mmoja alipata mimba akiwa shuleni akajifungua salama. Bahati nzuri akaweza kupata mtu wa kuweza kumsaidia akajiendeleza kielimu. Mtoto yule alilia sana. Alitoa machozi kwa sababu ya jinsi alivyokatizwa masomo yake. Lakini baada ya kujiendeleza, alifika kiwango cha juu vile vile. Sasa hii ni mifano hai. Naomba Serikali itafakari sana ili tuwawezeshe vijana wetu kuendelea na masomo na hatimaye waweze kuwa viongozi wa Taifa letu la kesho ambayo kwa kweli inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naomba kulizungumzia hapa, wenzangu wamezungumza kwa njia moja au nyingine, ni suala la kuwakomboa wanawake Waislam akina mama. Ni kwamba huu hili pendekezo la kuanzishwa Ofisi ya Kadhi kwa kweli mtawakomboa, mtawasaidia wanawake wa Tanzania wa Kiislam kuondokana na dhuluma zinazofanywa na familia baada ya waume zao kufariki.

Ndugu zangu kwenye sheria zetu za Kiislam iko bayana kabisa, iko wazi jinsi ya kugawa mali. Sasa kuna tatizo gani? Zanzibar wameweza, Kenya jirani wameweza, Uganda jirani wameweza, tunashindwa nini? Tuwasaidie kama kweli tuna uchungu wa wanawake wa Tanzania, tunasema tuwape maendeleo, basi tuanzie hapa kuonyesha kweli tunawajali. Naomba Serikali kwa nguvu zake zote kwamba hili suala ilisimamie ifumbe macho, izibe masikio, maana yake yanasemwa mengi! Zibeni masikio, hatimaye Ofisi ya Kadhi iweze kuanzishwa. Nawaombeni sana. Mwenye macho haambiwi tazama, mwenye masikio haambiwi sikia. Serikali, sikieni ndugu zangu. Naomba kwa heshima na taathima uma wa wanawake wa Tanzania wa Kiislam mtawakomboa ndipo sheria hizi au ofisi hii ikianzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo machache tu, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Kwa kuwa moja haki ya mtoto ni kupata Elimu ya Msingi, Sekondari na kisha Elimu ya Juu; je, kwa nini Wizara yako bado imefumbia macho sheria zilizopitwa na wakati kama ile inayomzuia mwanafunzi kukariri au kurudia darasa la saba?

Pamoja na majukumu mengine, kazi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ni kusaidia upangaji mipango na uandaaji wa bajeti katika Kata; je, Serikali au Wizara inawasaidia vipi kutimiza wajibu huo muhimu?

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kuwapongeza Waziri na Naibu wake kwa Hotuba nzuri. Aidha, nawapongeza Katibu Mkuu wa Wizara, pamoja na Watendaji wote, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kufanikisha shughuli zote za Wizara hii. Pamoja na kuwa, Wizara hii imekuwa ikitengewa fedha kidogo kila mwaka na kusababisha Watendaji wa Wizara hii kufanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mawazo yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua umuhimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, lakini nasikitika kuwa, Vyuo hivi vimekuwa kama yatima; majengo hali za watumishi na hata vitendea kazi, viko katika hali duni sana. Japokuwa serikali hutoa

fungu la ukarabati wa majengo na kadhalika, bado hali ni ngumu sana. Mimi nashangaa sana.

Je, Wizara itakuwa tayari kuishinikiza Serikali kuyaomba/kuyaagiza Mashirika kama NSSF na PPF kujenga/kukarabati majengo yote katika Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi? Nasema hivyo kwa sababu, Mashirika haya yamejikita kujenga majengo mijini tu; kwa nini yasisaidie na kwenye Maendeleo ya Jamii kwa kujenga majengo mazuri na nyumba za watumishi?

Jambo lingine ni lini Wizara hii itaweka msukumo wa kuleta Muswada wa Kurekebisha Sheria ya Ndoa?

Namwomba Mheshimiwa Waziri, aje atembelee Vyuo vya Maendeleo vilivyopo Mkoa wa Singida ili ajionee yaliyopo kule. Pamoja na hayo, naomba Chuo cha Msingi kiongezewe fedha za kutosha kwani kina hali mbaya.

Wizara iweke mfumo mzuri wa kusimamia NGOs zinazoshughulikia watoto yatima na kuwe na ukomo Kimkoa na Wilaya ili kudhibiti wizi wa NGOs hizo na iwe rahisi kuzi-*monitor*.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya jinsia ni mtambuka kama yalivyo masuala ya watoto, lakini masuala ya watoto bado hayajawekwa vizuri; naomba serikali iliweke vizuri zaidi. Hapa ninachosema; haijawa sawa sana kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kutunga sera na kuhamasisha tu. Hili likiendelea kukaa hivi, watoto chini ya miaka mitano wanakuwa katika hatari kimalezi. Mfano, Walemavu wa Ngozi wakipelekwa katika vituo vya kulelea watoto, kwa ajili ya mambo yalivyo; watakosa malezi wanayostahili na tutambue watakuwa hawakuzwi kwa kujali kuwa ubongo wao bado unakua. Naiomba serikali ijipange upya sasa ili Sheria ya Mtoto itungwe na kupitishwa ili mtoto apate *protection* kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze serikali kwa mapambano dhidi ya maharamia wanaouawa na wakongwe na walemavu wa ngozi (Albino). Wizara kwa maana ya Serikali, inafanya kazi kubwa tena ya ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, inajitahidi kukarabati Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi/Jamii, vinavyochochea maendeleo nchini. Naomba serikali iongeze Bajeti ya Wizara hii ili kufanikisha ukarabati wa vyuo vyote 53 nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichukue fursa hii kuiuliza serikali, ni watu wangapi wamefungwa au kuadhibiwa tangu kuwepo kwa sheria inayokataza ukeketaji ya mwaka 1998? Swali hili limetokana na kutokupungua ukeketaji hasa Mkoa wa Mara. Upungufu wa 3% ni sawa na 0% kimwonekano. Je, ni lini serikali itaweka nguvu zaidi katika suala la ukeketaji? Je, ni nyenzo zipi mpya zilizobuniwa kupambana na ukeketaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara inashughulikia maendeleo ya mtoto na makuzi; watoto nchini ni wengi, naomba eneo hili liongezewe fedha kuliko zilizotengwa mwaka huu Sh. 123,100,000, tena zikiwa fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya mipango kadhaa ya serikali, bado wanawake wengi vijijini na mijini, hawajawahi kuwezeshwa kiuchumi. Bado serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, inahitaji kuwawezesha Maafisa Maendeleo ya Jamii usafiri ili waweze kuwafikia wananchi vijijini na kuhamasisha maendeleo kwa wote ili mashirika ya kifedha yakifika kwao, wawe na mwamko wa kukopa kwa maana ya kuzitumia kwa kuzalisha na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono haja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, pamoja na Wafanyakazi wa Wizara.

Naipongeza Wizara hasa Mheshimiwa Waziri, kwa kutembelea Malya FDC.

Waziri alijionea mwenyewe fedha zilizotumwa na kufanya kazi ya ukarabati wa majengo, lakini *value for money* haionekani, naomba utume timu iende ikafanye *valuation.* Bado, mbali na ombi langu la kutumia mabweni, pamoja na msimamo wako, naomba mabweni hayo ambayo hayatumiki yatumiwe kwa ajili ya kuwalaza Wasichana wa Shule ya Sekondari ya Malya, ambayo watoto wa kike wanaoanza kidato cha kwanza, wakianza 80 wanamaliza 20. Huu ni mfano hai, nimeshakueleza wewe Waziri na Naibu wako.

Majengo hayo tungefurahi zaidi kama yangetumika kama mabweni kwa ajili ya wasichana wa Shule ya Sekondari ya Malya. Tuwasaidie wasichana hao wakati tunajiandaa katika ujenzi wa mabweni yetu wenyewe. Hili ni ombi maalumu, namwomba Mama Sitta, ombi hili lifikiriwe mara mbili mbili; Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wengine, wamesoma katika shule za *boarding.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii.

Kikubwa kwenye Wizara hii ni ukombozi wa mwanamke na motto. Naanza na Wanawake wa Vijijini, hawanufaiki na Mfuko wa (WDF). Serikali ihimize uanzishwaji wa Mfuko wa Kuweka na Kukopa na kujikwamua kimaisha.

Kwa upande wa mtoto ni kwa Serikali kuongeza juhudi ili kukamilisha Muswada wa Sheria ya Mtoto (The Law of Child Act, 2009) ili itoe mwongozo wa kumpatia mtoto haki zake.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu watoto ambao ni albino. Naiomba Wizara ifuatilie kuhusu watoto albino, wapatiwe nafasi ya kusoma kwenye shule za bweni kwa ajili ya usalama wao, kwani tatizo la mauaji bado lipo na limekuwa kubwa. Kwa kuwa Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Sheria, ndio wanaotekeleza Sera ya Mtoto na Maendeleo ya Jamii; hivyo ufuatiliaji wa utekelezaji wake ni muhimu mno.

Bajeti hii haitoshi, kuna Maafisa Maendeleo ya Jamii wanatakiwa wapatiwe mafunzo, lakini pesa haitoshi. Wanatakiwa wapatiwe usafiri ili wafike kwenye ngazi za chini na uteuzi wao uwe wa Wizara hii sio Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Naipongeza Wizara kwa kuzindua Tovuti ya Idara ya NGOs, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalamu wote wa Wizara hii muhimu sana kwa jitihada zao katika kuendeleza Wizara hii muhimu na kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kuchelewa kuletwa kwa Sheria ya Haki za Watoto, Sheria ya Mirathi na Haki za Wanawake, kunasababisha makundi haya kuendelea kukosa haki zao za msingi na kukosa mara kwa mara.

Sheria ya Watoto iliyopo haimsaidii mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa. Wanaume wengi wamekuwa wanawajaza mimba wasichana na kukwepa majukumu ya malezi, hali inayopelekea watoto kukosa huduma muhimu kama vile elimu, afya na kuishi kwa tabu kubwa.

Sheria ya Mirathi pia imekuwa inamnyima mwanamke stahili zake, hasa pale anapofiwa na mumewe. Yapo baadhi ya makabila, mwanamke akifiwa na mumewe, ananyang'anywa mali zote walizochuma na mumewe na kulazimishwa kurudi kwao. Wakati mwingine, hata watoto wananyang'anywa, ndugu wanajipanga wagawana watoto wawalee. Huu ni unyanyasaji wa hali ya juu.

Fedha zinazotengwa kwa maendeleo ya jamii bado ni ndogo, tukiangalia upana wa sekta hii, ambayo inagusa kila pahala. Ili kupata taifa la watu wenye uwezo, afya, akili, makini, wachapa kazi, wawajibikaji; ni lazima kuhakikisha Wizara hii inapata wataalamu, watumishi wa kutosha na nyenzo za kuweza kurahisisha utendaji na kuleta ufanisi.

**MHE. DKT. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ndiyo Wizara muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Ndiyo Wizara yenye wataalamu wa fani ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Kata, Kijiji na penginepo Tarafa; lakini Wizara hii ndiyo ambayo wataalamu wake hawana nyenzo za kazi, nyenzo za usafiri na kadhalika.

(a) Wizara inajua idadi kamili ya Mabibi na Mabwana Maendeleo kwa ngazi mbalimbali? Iwapo inafahamu ni wangapi kwa kila ngazi?

(b) Je kati ya hao, hasa kwenye ngazi ya Kata; wangapi wanazo nyenzo za kazi; na ni nyenzo zipi na nyenzo za usafiri mathalani pikipiki na baiskeli?

(c) Iwapo hawana nyenzo hizo, Serikali inasema nini kuhusu taarifa kuwa Wataalamu hawa wameshindwa kufanya kazi kwa kutokuwa na nyenzo za kazi na usafiri; na kuwa kwa kitendo hiki ni sawa na kuwalipa bila kufanya kazi?

Kwa kuwa Serikali ni moja na Bajeti inapitishwa kwanza ngazi ya Baraza la Mawaziri kabla ya kuwasilishwa Bungeni; na kwa kuwa mahesabu yanaonesha kuwa kasma ya takrima na viburudisho kwa pamoja zimepewa jumla ya Sh. 30,886,456,365 na Wizara muhimu na kubwa ya Maendeleo ya Jamii kutengewa tu jumla ya Sh. 14,549,281,000, ambayo wala si nusu ya Takrima na viburudisho:-

(a) Je, Waziri anakubali kuwa Wizara hii haina kipaumbele ndani ya serikali na kukosa kabisa umuhimu? Iwapo hii ni kweli; serikali kupitia Wizara hii inatoa kauli gani kuhusu hali hii?

(b) Iwapo Serikali imeitosa hivi Wizara hii muhimu, kiasi cha siyo tu kulinganishwa bali kuwa nchini ya kasma 220600 na 221400 kwa pamoja; ni kwa nini Waziri asimshauri Mheshimiwa Rais kulivunjilia mbali na Watendaji kuwekwa chini ya Wizara nyingine?

(c) Ama sivyo, kwa *trend* hii ambayo kila mwaka imeendelea kuwa hivi (pamoja na actual figures kuongezeka); ana matumaini gani kuifanya Wizara hii iwe *meaningful* kwa Watanzania na Watumishi wake waliotapakaa nchi nzima wajisikie nao wanatoa mchango wao wa maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja ya Wizara hii, labda nitakapopata majibu ya matumaini kwa Watumishi wengi wa Wizara hii ambao wamekata tamaa.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana; hivyo inatakiwa kupewa uwezo ikiwa ni pamoja na kupatiwa fedha au kuogezewa Bajeti.

Maafisa Maendeleo ya Jamii waajiriwe mara wamalizapo mafunzo Chuoni ili kuhakikisha kwamba, wanapangiwa vituo ili waweze kufika ngazi za jamii ikiwa ni ngazi za Kata na Vijiji. Kuna Maafisa Maendeleo ya Jamii, waliomaliza mafunzo kutoka vyuo vyote vya Wizara hii, lakini hawana ajira wakati wananchi wanakosa utaalamu muhimu kutoka kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Chuo cha Rungemba ni muhimu kikapewa umeme wa Grid ili kuwa na uhakika wa umeme wakati wote. Chuo hiki ni cha kihistoria, naomba historia hiyo iendelee kuenziwa na kikarabatiwe na kuwekewa uzio.

Naipongeza Wizara kwa kukamilisha mchakato wa kuanzisha Benki ya Wanawake. Naishauri Wizara ishirikiane na Idara ya Ushirika ili kuhamasisha wanawake kujiunga na SACCOS za Wanawake na hatimaye SACCOS hizi ziweze kutumika kukopa katika Benki ya Wananchi, wao waweze kutoa mikopo kwa wanawake ngazi ya chini. Kwa njia hii, wanawake wetu wa ngazi za chini wataweza kufikiwa. Wizara iharakishe mchakato ili Sheria ya Watoto iletwe Bungeni. Watoto wananyimwa haki zao za msingi kila siku, ikiwa ni pamoja na kutoshirikishwa, kubakwa na kadhalika. Huu ni wakati sasa wa kufanya vitendo kwa kuwalinda kwa kuwa na sheria moja.

Wizara ishirikiane na Wizara ya Elimu ili kuhakikisha kwamba, adhabu ya viboko mashuleni inakomeshwa na iwekwe ndani ya Sheria. Watoto wengine wamesababishiwa ulemavu wa kudumu na hata vifo.

Namshukuru Waziri, kuchukulia umuhimu unaostahili, wazo nililolitoa la uanzishwaji wa Tume/Kamisheni ya Haki za Watoto. Nomba Tume hii ianzishwe haraka iwezekanavyo. Hivyo basi, Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Tume hii uletwe mapema.

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vianze pia kutoa mafunzo ya ujasiliamali kwa wanawake na wasichana ili waweze kuendesha miradi yao kwa ufanisi.

Vituo vya Habari *(Information Resource Centre)* ni muhimu sana. Hivyo, naomba kukumbusha tena kwamba, Wizara ishirikiane na NGOs ili kuhakikisha vituo vinafunguliwa au kuanzishwa kwenye Ofisi za Wilaya na Mikoa. Vitawezesha wanawake na jamii kwa ujumla kupata taarifa.

Elimu ya UKIMWI iwafikie wanawake na wasichana. Wizara ishirikiane na NGOs za masuala ya wanawake ili kuhakikisha wanawake vijijini wanapata elimu.

Fedha za Wizara zipitie katika SACCOS za Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, kwanza kabisa, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia machache kuhusiana na Wizara hii. Wizara hii ni muhimu mno katika ustawi wa jamii zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri waandae utaratibu au sheria ya kuwalinda watoto wadogo. Kwa mfano, itungwe Sheria ya Kuzuia Watoto chini ya miaka 18 kuchunga ng'ombe ili vijana wapate haki ya kwenda shuleni badala ya kufanya kazi za uchungaji tu na kukosa elimu ambayo ni haki yao.

Pia wale vijana wadogo wanaowasaidia walemavu wasioona na kadhalika. Kazi ya kuwashikilia walemavu na kuwatembeza barabarani, inawafanya wakose haki yao ya kusoma shule. Hivyo basi, la msingi tuimarishe vituo vya kutunzia walemavu ili walemavu wanaohitaji msaada, walelewe katika vituo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuitumia fursa hii, kumpongeza Mheshimwia Waziri, kwa Hotuba yake nzuri sana. Hotuba hii imejaa ubunifu mkubwa na umakini mkubwa sana wa kiutendaji. Hotuba hii inadhihirisha uongozi bora wa ngazi za juu za Wizara hii. Uongozi huu unasababisha mshikamano mkubwa baina ya Watumishi na Wizara hii, ndani na nje ya Wizara. Aidha, Hotuba hii inaonesha wepesi wa kupokea mawazo kutoka nje ya Wizara na kufanyia kazi mapema, wakiyafanya kuwa sehemu ya mawazo ya Wizara hii.

Kwa mantiki hii, ninawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote, kwa usikivu wao mkuu. Kwa mantiki hiyo hiyo, ninawapongeza watumishi wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika uandaaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kuipongeza Wizara hii, kwa kuendelea kuifanya kuwa ya Jinsia na Watoto zaidi kuliko kuwa ya Wanawake na Watoto kama ilivyokuwa ikielekea kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuendelea kuelewa na kuwekea uzito kwa majukumu ya Wizara hii. Kuiongezea fedha ni ishara nzuri, japo fedha hii iliyoongezwa bado haijatosha.

Naipongeza Wizara hii kwa kuanza kutekeleza majukumu yake kwa vitendo; kwa kupeleka teknolojia muafaka katika vyuo vya ufundi vilivyo chini yake ni ishara nzuri kwa Wizara hii. Ni dhahiri, wahitimu wa vyuo hivyo, kokote watakakokwenda kwanza, itakuwa rahisi sana kujiajiri wenyewe au kuwa chumvi ya maendeleo miongoni mwa jamii watakamokuwa wakiishi.

Ninaomba Serikali itoe fedha iliyoombwa kwa ajili ya vyuo hivyo mapema ili mipango iliyokusudiwa, itekelezwe yote bila kukwama kwa aina yoyote.

Mheshimwia Spika, naipongeza sana Wizara kwa kufuatilia kwa karibu na hatimaye kukamilisha utaratibu wa kuanzisha Benki ya Wanawake.

Naomba Benki hiyo ianze kufanya kazi mara moja na ni vyema utaratibu ukaandaliwa vyema ili matawi yake yasichelewe kufunguliwa katika Makao Makuu ya Mikoa, Wilaya na ngazi za chini zaidi ili kuwakaribia akina mama wengi walioko vijijini, ambao kimsingi ndiyo walengwa wakuu wa kuanzishwa benki hii.

Juhudi kubwa ziendelezwe kwa kuwashawishi akina mama wengi, kununua hisa za Benki hii ili waweze kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kumiliki Benki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto ni kikundi ambacho ni vigumu kujitetea wenyewe, pamoja na kuwa haki zao zimeainishwa, lakini usimamizi wake na uratibu wake hufanywa nje ya uwezo wao. ili watoto wapatiwe haki zao, hawana njia nyingine zaidi ya kusubiri fadhila za vikundi vingine nje yao. Wizara hii ndiyo iliyopewa jukumu la kusimamia uratibu na kusimamia haki za watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imesubiri kwa muda mrefu sana, Sheria ya Haki za Mtoto. Sheria hiyo haijaja bado. Binafsi, sisikitiki sana na kucheleweshwa huko; ni vyema ichelewe ili itakapokuja ije ikiwa imeiva na isiyokuwa na utata wa kubomoa kuliko kujenga.

Maeneo yanayotakiwa kuangaliwa kwa uangalifu mkubwa ni haki za mtoto katika mirathi. Eneo hili lisipoangaliwa kwa uangalifu na kupangwa kwa makini, linaweza kusababisha maafa makubwa kwa watoto wenye stahili hiyo.

Tafsiri ya mtoto wa nje ya ndoa na haki zake hasa katika mirathi, isipoangaliwa vizuri inaweza kusababisha ongezeko la matumizi ya DNA na watoto wa mitaani.

Kuhusu eneo hili, ninaomba Wizara hii iwe makini sana na hatimaye walete sheria hiyo mapema ili kuwatendea haki watoto wa Kitanzania, ambao hata wao wenyewe hatima yao hawaifahamu. Njia ya kusonga mbele katika maisha yao itakuwa wazi kwao na itakuwa rahisi hata kuwasaidia sheria hiyo ikiwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuipongeza Wizara kwa kupeleka teknolojia.

Ninashauri Wizara iangalie shughuli mbalimbali zinazofanywa katika maeneo mbalimbali, mfano, yapo maeneo ya Wananchi ambayo ni wafanyakazi hodari katika kilimo. Tatizo lao ni kuwa, hutumia nguvu zaidi bila maarifa. Ni vyema kuwasaidia hao, wakasaidiwa kuongezewa maarifa zaidi kwa juhudi zao. Aidha ni vyema Wizara hii ikayatambua mazingira na hali ya hewa ya kila Wilaya na Mikoa ili Wizara iwasaidie wananchi katika maeneo yao, kwa kuwapatia teknolojia sahihi ili kuwaongezea tija katika shughuli zao.

Mwisho, naiomba Wizara hii iwasaidie wanaume kubadili mawazo na kuwaona wanawake kuwa ni sawa nao; hali hiyo ikikubalika mambo mengi yatakwenda vyema kwa kushirikiana na kuleta maendeleo kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa ya kwanza, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayofanya. Aidha, nimefurahishwa kuona Bajeti ya Wizara yako imeongezeka kidogo. Bado tuna kazi ya kuendelea kuitetea bajeti iongezwe na wakati huo huo tukijitahidi kubuni mbinu tofauti za utekelezaji wa majukumu ya maendeleo ya jamii.

Pamoja na kwamba, mnatambua kuwa kuna upungufu mkubwa wa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata, naomba nikuarifu katika Wilaya ya Kilindi kuna upungufu mkubwa wa Wataalamu hao; mbali kwenye Kata. Aidha, Idara hii haina gari ijapokuwa ina kazi kubwa ya kuzunguka. Pengine Halmashauri ndiyo yenye jukumu la kutafuta gari, lakini tunaomba msukumo wa Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliongelea uundaji wa Baraza la Wanawake, ambalo litahusisha wanawake wa itikadi, rangi, kabila, ilimradi kuzunguzia maslahi ya mwanamke. Je, Wizara imechukua hatua zozote katika hili?

Mporomoko wa maadili kwa kisingizio cha nyakati umebadilika; tabia, mavazi, lugha vyote vinaenda kinyume cha taratibu. Nadhani ni vyema mkaandaa mafunzo maalumu, ambapo mtakuwa mnatoa mafunzo ya TOT ambapo nashauri na akina mama watu wazima, wastaafu, wazee wa waume ili iwe ni lazima kutoa mafunzo hayo kwa jamii, hususan watoto na vijana, ambao maadili yanakiukwa na ile dhana ya Tanzania na Uafrika unapotea.

Mheshimiwa Waziri, mimba za utotoni ni tatizo ambalo linazungumzwa juu juu, naomba Wizara ilichukulie kwa umakini wake. Pengine pawe na Programu Maalum na kitengo cha kujaribu kutoa mbinu mbalimbali za kuondoa tatizo hilo, ilhali ikihakikisha kuwa wale wanaosuluhisha kimya kimya kuchukuliwa hatua na wale wanaotia hizo mimba kuchukuliwa hatua na vijana hawa kuangalia ni namna gani ya kuwaendeleza. Niko tayari kushirikiana nanyi kutekeleza hilo.

Mwisho, naomba mpatapo nafasi, muweze kuitembelea Wilaya ya Kilindi. Wananchi watafurahi kuwaona. Hongereni.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu, kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya na pia kwa hotuba yenye mwelekeo na dira kwa maendeleo ya Jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na tatizo la wanawake, wanavyonyanyasika wakati wanapokwenda kujifungua katika Hospitali ya Muhimbili. Hivi ni kwa nini mama baada ya kujifungua hapewi mtoto wake inaweza ikapita siku tatu mpaka atakapomdai mtoto wake na anapoletwa mtoto huyo anakuwa mchafu hajashughulikiwa hata kwa kupewa maji ya kunywa? Hilo linaweza kusababisha vifo vya watoto kwa uzembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto ndio taifa la baadaye, ndio tegemeo letu; je, ni lini serikali italeta Sera ya Mtoto ili tuweze kumlea na kumtunza kama stahili yake kwa manufaa ya Taifa letu?

Kwa kuwa suala la ukeketaji sasa hivi linawalenga zaidi watoto wadogo ambao hawana uwezo wa kujitetea; je, sheria ya kumlinda mtoto hadi sasa imewatia hatiani watu wangapi ambao wanawakeketa watoto? Je, hatuoni kwamba tatizo hili ni kubwa na linahitaji kufanyiwa kazi kwa umakini mkubwa? Je, kuna uchunguzi kiasi gani wa kuhakikisha kwamba watoto wadogo hawakeketwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la utumikishwaji wa watoto, bado ni kubwa na hilo ndilo linalochangia ukahaba wa watoto, kwani mtoto wa kike anapotumikishwa katika mazingira yasiyo na huruma, anaweza kukimbia na hatimaye akakumbana na wanaume wasio na imani na kumtendea vitendo viovu na pia kubeba mimba na ama kuambukizwa maradhi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Albino au walemavu wa ngozi kuuwawa Tanzania, limekuwa ni tishio. Naomba sana serikali iongeze juhudi ya kuweka mikakati madhubuti ya kuweka ulinzi katika maeneo yote ambayo wapo wenzetu, ambao wana ulemavu wa ngozi, kwani hawa nao ni binadamu; wanahitaji haki na uhuru sawa na wengine. Pia hatua kali na adhabu kali zitumike kwa watu wanaojihusisha na kadhia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima wa afya na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana Mheshimiwa Magreth Sitta (Mb) na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya (Mb) na Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Mariam J. Mwaffisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Wizara kwa kuzingatia wito wa Kilimo Kwanza, kutokana na nia nzuri ya kutekeleza mpango wa kusambaza teknolojia kupitia mafunzo yanayotolewa katika Vyuo vyake vya Maendeleo na Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni la kupigiwa mfano na la kuigwa na Wizara na Taasisi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni ushahidi tosha kuwa, Wizara hii ni Wizara muhimu ya kuleta maendeleo kwa jamii zote nchini bila kujali jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Wizara ni nzuri na haina budi kuungwa mkono kwa kupatiwa fedha walizoziomba mapema na kwa wakati ili watimize malengo yao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze serikali kwa kuiongezea fedha Wizara hii kwa kipindi hiki cha 2009/2010. Hata hivyo, bajeti hii haitoshi kulingana na umuhimu wa Wizara; kwa hiyo, naomba katika kipindi kijacho iongezewe mara mbili zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimba za utotoni zimeongezeka na hili linatokana na kuporomoka kwa maadili yetu ya malezi, pamoja na kufuata ustarabu wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani ilikuwa mtoto wa mwenzako ni mtoto wako, siku hizi hilo halipo. Unamkuta mtoto anafanya kitendo kibaya huna habari naye na unaomba litokee baya kwake ili usherehekee. Pia walimu walikuwa walezi wazuri kwa watoto, lakini tokea kuondoshwa viboko shuleni, wanafunzi hawaogopi walimu wao na hufanya mapenzi nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la mimba tutaendelea kulisema kila leo, kwa sababu bado serikali ina kigugumizi cha kuwachukulia hatua kali, kwa kuogopa kuambiwa inakwenda kimyume na haki za binadamu. Kwa hiyo, ninaiomba serikali iache kuogopa lawama, kunzia sasa ichukue hatua kali kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza Waziri na Watendaji wote wa Wizara, pamoja na Viongozi wengine alioshirikiana nao katika kuandaa hotuba nzuri, iliyosomwa mbele ya Bunge hili Tukufu. Sasa naomba kuchangia yafuatayo:-

Kwa kuwa Wizara hii ni muhimu kwa kushughulikia masuala ya udhalilishwaji wa wanawake na watoto, ingefaa iongezewe Bajeti kwani inayotolewa bado haitoshi kukidhi mahitaji.

Kwa kuwa vitendo vya ukatili kwa wanawake bado vinaendelea, hasa vya kuwapiga wanawake na kuwasababishia ulemavu wa kudumu, nashauri itungwe sheria na kuletwa Bungeni ili kuwabana wanaume wa aina hiyo, kupewa adhabu kama inavyotolewa kwa wanaume wanaobaka wanawake na watoto na kufungwa miaka si chini ya 30 ili liwe fundisho kwa wengine.

Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ifanyiwe marekebisho, kwani inaruhusu msichana wa umri wa miaka 16 kuweza kuolewa kwa ridhaa ya wazazi. Hii ni sawa kabisa na ubakaji na ukatili wa hali ya juu. Mtoto wa miaka 16, kwanza, anahitaji aendelee na elimu, wala siyo kuolewa! Kwa nini serikali inachelewa kuleta Sheria hii Bungeni?

Nashauri Sheria ya Mirathi pia ifanyiwe marekebisho, sielewi kwa nini serikali inacheleweshа kuileta Bungeni? Baadhi ya wanawake wananyang'anywa kila kitu wanapofiwa na waume zao. Wengine hupewa masharti kukubali kurithiwa na ndugu wa

mwanaume ndipo aachiwe mali. Baadhi ya wajane hukubali kurithiwa, jambo ambalo wengi wao wameambukizwa maradhi mbalimbali ukiwemo UKIMWI.

Kumekuwepo na mifumko ya uanzishwaji wa Asasi zisizo za Kiserikali, zinazoshughulikia watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi, nyingine watoto wanoishi kwenye mazingira hatarishi na nyinginezo. Nashauri uwepo ufuatiliaji, kwani misaada inayotolewa haiwafikii walengwa, bali baadhi ya viongozi hao hujinufaisha binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mola wangu, ambaye amenijalia uzima na kuchangia Hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote, kwa ushirikiano walionao, kwa kutengeneza bajeti nzuri yenye kuonesha njia na mwanga kwa akina mama na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna udhalilishaji wa wanamke katika ofisi zetu, hospitali na hata majumbani mwetu. Akina mama wengi wananyanyasika wakati wa kutafuta kazi, kuna vikwazo vingi ambavyo wanawake tunashindwa kuvimudu na kubakia majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikwazo hivyo wakati mwingine vinatuletea maradhi na watoto wa mitaani vile vile kuonekana si lolote si chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba serikali kupitia Mheshimiwa Waziri, iliangalie hili katika Maofisi, pia kuwe na pahala makusudi, akina mama tupeleke matatizo yetu ili wachukuliwe hatua kwa upesi wanaodhalilisha wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa mitaani wanaongezeka kila siku, hali ambayo inatisha na ikiachiwa hivi hivi, itailetea Taifa aibu. Kwa hiyo, ninaiomba serikali iwakamate wazee wenye watoto hao, ambao wanawatuma kuombaomba mitaani na wale ambao hawana wazee wawekewe utaratibu maalumu wa kuwatunza.

**MHE. AZZAN A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Napongeza kwa kazi nzuri. Suala la UKIMWI, Wizara ianze kutoa *literature* ya hofu, kwa maana vipeperushi vinavyoonesha shida wapatazo wagonjwa wa UKIMWI ili kuitia hofu jamii.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mfuko wa Mikopo ya Wanawake uongezewe fedha, kwani hivi sasa ni wachache wanaonufaika. Wanawake ni wakopaji na warejeshaji wazuri.

Wizara ianzishe utaratibu maalumu wa kuwawezesha wanawake wajane, ambao wanabeba mzigo mzito wa kulea watoto chini ya mazingira magumu.

Wizara ikishirikiana na taasisi husika, ianzishe utaratibu wa kufuatilia haki za wajane hasa mirathi. Wajane wengi wanatia huruma, kwani wanaonewa na kudhulumiwa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, ningependa kuchangia yafuatayo:-

Chuo cha FDC Kasulu hiki ni muhimu sana, lakini kipo hoi bin taabani, kinahitaji ukarabati haraka. Mheshimiwa Waziri atupie jicho lake Kasulu ili Chuo hiki kifanye kazi iliyokusudiwa. Aidha, tuletewe fedha za upimaji eneo ili eneo hili liwekewe mipaka yake inayofahamika. Chuo hiki kipo karibu sana na Uwanja wa Ndege na mipaka yake inakanganya.

Kwa kuwa sasa Bajeti ya Wizara imeongezeka kidogo, basi tuletewe gari jipya la Chuo hiki muhimu katika maendeleo ya Wananchi wa Kasulu. Tafadhali, tuleteeni gari jipya sasa 2009/10.

Chuo hiki kina uhaba mkubwa wa wataalamu wenye sifa. Tafadhali, angalia ikama ya watumishi wako na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu tuletewe maafisa/walimu wa FDC wenye sifa stahili. Vitendea kazi ni jambo la kuangalia pia.

Nchi yetu inakabiliwa na shida kubwa ya watoto wa mitaani *(Street Children)*, hasa katika Miji Mikuu ya Nchi yetu. Jambo hili lichunguzwe kwa kina ili kubaini chanzo, athari na namna na kurekebisha hali hiyo. Mji wa Kasulu unalo tatizo hilo. FDC Kasulu wapelekeeni fedha ili wafanye utafiti na kubaini tiba ya tatizo hili. Fanyeni *study* mapema na taarifa iletwe Bungeni. Nashauri utafiti mijini ufanyike sambamba na Wilaya za pembezoni kama Kasulu, Kibondo, Mpanda na kadhalika.

Ninaomba kufahamu katika mikakati ya Wizara hii ni shughuli gani imefanyika katika kusaidia juhudi za maendeleo ya wanawake katika Halmshauri ya Wilaya ya Kasulu?

Ni dhahiri wazalishaji wengi ni wanawake; je, ni namna gani Wizara yako itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya na Wizara ya Kilimo katika kutekeleza mkakati huu wa Kilimo Kwanza/Chakula Kwanza? Ni maeneo gani Wizara yako itaingilia *in supporting* Kilimo Kwanza *Strategy*?

Je, Maafisa Maendeleo ya Jamii *(Community Officers)* katika Halmashauri ya Wilaya wana maelekezo yoyote kimkakati kusaidia kaulimbiu hii muhimu? *What are the*

*issues?* Nafasi ya Wizara hii lazima ionekane na siyo kama ilivyo sasa, ambapo siyo rahisi kuona *role* hiyo moja kwa moja. Wizara *must take lead.*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hatua mbalimbali zinazolenga kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi, pia kufikia asilimia 50/50.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wangu hasa upo katika kuhakikisha jinsi ya gani wanawake wanapata demokrasia ya kweli katika kuingia Bungeni, kupitia Viti Maalum. Kwa kuwa utaratibu uliopo ni kila chama kuwa na utaratibu wake na idadi ya majina yao na utaratibu sio wa uwazi; ni vyema basi suala hilo liangaliwe kwa undani ili kuweka uwazi na haki kutendeka.

Suala langu la pili ni kuhusu sheria kandamizi kwa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala mengine yanahusu mambo ya imani zetu na hivyo kuleta woga wa kiroho. Masuala mengine ni ya *obvious* hasa kwa mfano, hili la matunzo ya watoto nje ya ndoa; hivi kweli shilingi 100 inatosha kumtunza mtoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Wizara hii kwa kufanikisha uanzishaji wa Benki ya Wanawake Tanzania. Hii ni juhudi kubwa, inaonesha jinsi ambavyo Serikali inaweza kuwajali wanawake

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa na bajeti ndogo, Wizara pia iangalie uwezekano wa kutoa mafunzo ya shria na haki za akina mama, watoto na masuala ya jinsia ikiwemo walemavu ili kuongeza uelewa mpana zaidi kwa jamii zetu.

Wizara pia ifuatilie kwa karibu, mgao wa vifaa kama *ultrasound* kwa zahanati au hospitali ikiwemo za misheni ili kuwasaidia akina mama, kugundua tatizo mapema na hivyo kuweza kuwahi kwenda hospitali kubwa kwa matibabu zaidi.

Mwisho, niishukuru Wizara kwa kutembelea katika kituo chetu cha kuangua na kuatamia wajarisiamali *(Ruvuma Enterprenership Incubator)*, kinachoendeshwa na Better Life Tanzania; na hivyo kuleta mwamko na kuhamasisha wanawake kujiunga pamoja katika shughuli zao za kujipatia kipato. Akina mama wameyapokea maelekezo ya Wizara, yaliyotolwa na Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Siku ya Wanawake Duniani na kuendelea kuyafanyia kazi.

Nawatakieni kila la kheri katika kutekeleza majukumu yenu na dada Mwaffisi aendelee kutusaidia akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuipongeza Wizara kwa mchakato na hatua waliyofikia kuanzisha Benki ya

Wanawake. Nashukuru pia kwa sababu mtoto wangu Damas ameajiriwa na Benki hiyo kama Chief Internal Auditor, kwa kudhihirisha uwezo wake mwenyewe.

Ushauri, wanawake ndiyo wanaochangia nguvukazi kubwa katika kazi za maendeleo kikiwemo kilimo. Nashauri Benki iangalie uwezekano wa kufungua dirisha la uwezeshaji wa wakulima (hasa wanawake), kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu kama vile mikopo ya ununuzi wa zana za kilimo kama *power tillters* na matrekta makubwa.

Nashauri pia Benki iangalie uwezekano wa kuwasaidia, kwa kuwapa mikopo ya elimu wanafunzi hasa wasichana, wanaoshindwa kujilipia gharama za vyuo na vyuo vikuu.

Wizara ipanue wigo kwa kwenda mpaka katika mikoa ya pembezoni ya Kigoma, Rukwa na kadhalika, kuwasaidia wanawake kuibua miradi ya maendeleo. Katika Mkoa wa Kigoma, anzisheni Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kihinga.

Mwisho, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa maandalizi mazuri ya Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kuandaa hotuba yenye kuonesha mwelekeo wa Wizara katika kipindi cha mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanywa kwa kutekeleza vyema Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005. Utekelezaji huu unaonekana kwa vitendo. Baada ya maelezo hayo, naomba kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuhakikisha Benki ya Wanawake itaanza wakati wowote. Tunaomba matangazo ya kuuza hisa za benki hiyo yatolewe mapema na yaenee nchi nzima ili wananchi katika maeneo mengi, wanunue hisa hizo. Wasije wakanunua wengi wa Dar es Salaam tu; ikiwezekana zigawanywe kwa mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Wanawake ni muhimu; hivyo ni vizuri Mfuko huu ukiwepo utasadia akina mama ili kupata mtaji wa kuwawezesha kuendesha kazi za biashara ndogo ndogo na kuweza kujikimu hasa akina mama waathirika na wajane.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongesza Wizara kwa kufanyia ukarabati baadhi ya vyuo na kuendelea kutoa mafunzo. Naiomba Serikali iongeze fedha ili wananchi wengi wafaidike na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wanyamakazi ni muhimu ili kuwapunguzia kazi kama vile kuchota maji, kukata kuni na kazi mbalimbali. Vile vile ni muhimu teknolojia mbalimbali zilizoelezwa kwenye bajeti hii, wanawake waelimishwe ili kuwapunguzia mzigo mkubwa walionao.

Mheshimiwa Spika, haki za watoto ni muhimu. Wananchi waelimishwe vizuri ili kuondoa ukatili kwa watoto. Hata hivyo, haki za watoto ni vizuri zitafsiriwe vizuri ili wazazi wasishindwe kuwarekebisha watoto kwa kuogopa kufikishwa mahakamani na watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia siku ya leo kuamka nikiwa mzima. Pia napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa imani yako kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake iliyojaa matumaini kwa Watanzania. Pamoja na nia ya Serikali kuwa njema, nami napendelea kutoa mchango wangu katika Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hali halisi ya Watanzania, utaona walio wengi wanaishi bila ya kuwa na uhakika katika maisha yao. Hii inatokana na umaskini uliokithiri. Ukuaji wa uchumi katika nchi yetu, haujaweza kukidhi haja ya kuwaondolea maisha duni na kuwapeleka Watanzania kule kunakoitwa Maisha Bora kwa Kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia huduma za afya nchini, utaona walio wengi wanakosa huduma hii ipasavyo hasa vijijini, vifo vya wajawazito vinaendelea siku hadi siku, kutokana na umbali wa vituo vya afya na ukosefu wa miundombinu; na pia uhaba wa madaktari nchini; na ukosefu wa elimu kwa watu wetu hasa vijijini. Kwa hili ni vizuri Wizara itoe elimu kwa watu wetu na pia kuwapa uwezo na elimu wakunga wa jadi ili waweze kunusuru vifo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia majukumu ya akina mama, duniani kote utaona mama ndiye aliyebeba begi la maisha ya familia. Kutomkuza mama unaua familia. Hivyo basi, Wizara inafaa iwawezeshe akina mama kwani kumuwezesha mama mmoja umesaidia familia nzima.

Kuhusu jinsia na watoto; naipongeza Wizara kwa jitihada yake kwa kunusuru maisha ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia nia ya Wizara, juu ya kununusu vifo vya watoto, bado Wizara ina changamoto kubwa kufanikisha azma yake njema. Hii inatokana na uhaba wa bajeti, kwa kuzingatia miundombinu ya nchi yetu. Vifo vya watoto bado ni tatizo sugu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto ana haki ya kulelewa, kukuzwa na pia kusomeshwa. Kwa kuzingatia hilo, Wizara inalazimika kuwapatia haki hii watoto wote ambao ama wametupwa na wazazi wao au wamefariki wazee wao, mzigo huu ni wazi utahudumiwa na Wizara. Hivyo basi; ni vyema Serikali iitupie jicho la rehema Wizara katika bajeti yake ili ifanikishe mema juu ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mila zenye kuleta madhara; pamoja na jitihada ya Wizara kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa sheria ili kuzuia na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake; hii ni nia njema ya Wizara ila Wizara ingewezeshwa zaidi. Wizara pekee ilibeba maendeleo ya jamii, nikiwemo mimi na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake tunaweza kuona yako mambo hutendewa kikatili na mengine hujitendea wenyewe kimila. Iko haja Wizara ishuke chini kwa baadhi ya mikoa inayoongoza katika ukeketaji ili itoe elimu kwa watu waachane na mila hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mauaji ya watoto maalbino; ni Wizara hii hii inayopaswa kuwalinda watoto wetu hawa. Ni vyema Serikali iongezee fedha Wizara hii ifanikishe malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la ajira za watoto bado limo majumbani. Je, Serikali inachukua hatua gani kuwalinda watoto hao huko majumbani? Ni vyema Wizara ianze kutoa nusura kwa watoto hao, kwani wanafanyishwa kazi ngumu na pia wanakosa elimu zao za msingi.

Baada ya maelezo yangu hayo, nawaombea maisha mema Mheshimiwa Waziri na Naibu wake.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuwambua na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na timu yake, wameweza kutekeleza kwa kiwango cha juu, moja ya majukumu ya Wizara ya kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili waweze kushiriki katika nguzo zote za utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo na kufaidika sawa katika maendeleo hayo. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii katika kuhamasisha na kuhimiza matumizi ya teknolojia sahihi ili kuwapunguzia wananchi mzigo wa kazi na kuongeza tija uzalishaji mali vijijini; kwa niaba ya vikundi 327 vya wajasiriamali na Wana-SACCOS 12 Wilayani Rorya, wametuma niwafikishie maombi yao kwa Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Wananchi wajasiriamali ambao wameunda vikundi na SACCOS wanaomba Wizara iwakumbuke katika kusambaza matrekta 23 ya kusukumwa na mkono. Mgawanyo utaandaliwa kwa kuzingatia SACCOS/Vikundi vya wakulima wa mpunga kwa mfumo wa umwagiliaji. Naomba Mheshimiwa Waziri aisaidie wilaya hii mpya.

Katika mchakato wa kuandaa Sera ya Wizara, maoni ya wananchi Wilayani, Tarafani na Vijijini, yajumuishwe kwa njia ya kongamano/semina. Kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Rorya, ambayo ni Wilaya pembezoni, naomba zoezi hili liwafikie wakati wa kuandaa sera hii.

Napenda kutoa ushauri/ombi kwa Mheshimiwa Waziri au Mwakilishi wake kuwatembelea SACCOS zifuatazo: SACCOS ya A to Z Kata ya Koryo – Kijiji cha Utegi; SACCOS ya Upendo Kata ya Bukwe – Buganjo; SACCOS ya Nyamtinga Kata ya Nyamtinga; SACCOS ya Nyathorogo Kata ya Nyathorogo; na SACCOS ya Nyamunga Kata ya Nyamunga.

SACCOS saba zifuatazo ziko katika hatua za mwisho kuundwa: SACCOS ya Kyangombe Kata ya Rabuor; SACCOS ya Rabuor Kata ya Rabuor; SACCOS ya Bukura Kata ya Bukura; SACCOS ya Nyanduga Kata ya Koryo; SACCOS ya Kisumwa Kata ya Kisumwa; na SACCOS ya Roche Kata ya Roche.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Waziri na Timu yake, kwa jinsi walivyoandaa na kuwasilisha Hotuba.

Watoto wa Mitaani wanaongezeka; ni muhimu hili suala litafutiwe ufumbuzi ama sivyo vijana hawa siku za usoni watakuwa hatari kwa jamii. Vilema pia wameongezeka, Serikali iweke mipango ya kuwasaidia.

Hosteli za wasichana mashuleni ni suala la Wizara ya Elimu, lakini pia Wizara hii iongeze chagizo ili kwa haraka hosteli za wanafunzi wa kike zijengwe ili kuepusha haraka tatizo la sasa la watoto wetu wa kike kuvamiwa na kutumiwa na mibaba mibovu kwa kuwa wanapanga mitaani.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, natoa pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, zinasaidia sana kwa wanawake, ila kiasi cha asilimia kinachotolewa kwenye Halmashauri bado ni kidogo. Nashauri Wizara iweke mpango na mikakati, kusudi asilimia iongezeke na walengwa ziwafikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutambua kuwa, Wizara hii ni pana sana. Watoto wanatakiwa wapate haki zao sawa. Bado kuna wimbi la watoto wa mitaani, hasa katika miji mikubwa hapa nchini kwetu. Watoto hawa wanapata shida sana, wanaishi kwa kuombaomba. Nashauri Wizara, iweke mikakati pamoja na kuungana na wadau wengine kusudi wimbi hili la watoto wa mitaani liishe kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kama mikakati kwa vitendo itatimizwa na kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, haipendezi kabisa kuona watoto wanakaa mitaani na kuishi kwa kuombaomba badala ya kwenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua kuwa, Wafanyakazi wa Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana hasa huko vijijini, kwani ndio wanaopaswa kusimamia maendeleo ya jamii. Nashauri Wizara iwaangalie kwa kuwapatia vitendea kazi kama baiskeli kama inawezekana, kusudi wafanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuona mwaka huu bajeti imeongezeka. Hata hivyo, bajeti bado ni ndogo, kwa hiyo, Wizara ijitahidi kwa kuomba, kusudi bajeti izidi kuongezeka, Wizara iweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mambo ni mengi yanayopaswa kuangaliwa na Wizara hii. Nashukuru kwa Benki ya Wanawake itakayoanzishwa, kwani itakuwa mkombozi kwa mwanamke ila mikakati iwepo kusudi benki hii iwanufaishe hata akina mama wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara iwatupie macho ya kuwasaidia vijana na wazee, kwa kuwaongoza na kuwaelekeza miradi/teknolojia mbalimbali kupitia kwenye Wizara hii, kwa kupitia Wafanyakazi wa Maendeleo ya Jamii tulionao huko vijijini na mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeweka mipango mizuri ya baadaye, ninachoomba kwa Waziri, Naibu Waziri na Wafanyakazi wote wa Wizara hii ni kusimamia mipango hii mizuri itimizwe kama Wizara ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kutoa hongera na pongezi kwa Waziri Mama Magaret Sitta (Mb), Naibu Waziri Dkt. Lucy Nkya na Wizara nzima, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote, kwa ushirikiano wao na kwa kutuletea hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa, mauaji ya Albino. Kwa kuwa Serikali yetu inaumia sana na suala hili la kinyama ambalo wanafanyiwa wenzetu

hawa walemavu wa ngozi, hivi haioni sasa ipo haja kuiharakisha Mahakama iweze kutoa maamuzi ya kesi hizi ili wenzetu hawa wawe na imani na matumaini ya maisha yao kwani kuchelewa kwa kesi hizi hakuleti imani nzuri kwa Watanzania walio wengi kwani adhabu zikiwa kali itakuwa ni fundisho kwa wahalifu wengine.

Ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii kusimamia kesi hizi ili ziweze kwenda kwa haraka zaidi kwani wanawake, jinsia zote na watoto, tunaamini kuwa Wizara hii inaweza kusimamia na kutetea jinsia zote na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SACCOS* na miradi ya wanawake. Wanawake wengi wanapenda kujishughulisha na miradi ya maendeleo na kujiunga na *SACCOS* lakini wanawake walio wengi hawana mitaji, mabenki yana riba kubwa na haya mamilioni ya Mheshimiwa Rais hazikuwafikia wanawake wengi kwenye SACCOS zao, ninaiomba Wizara ilione suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba Waziri kushirikiana na Waziri mwenzie wa Zanzibar, kuhakikisha michakato ya fomu za mikopo ya pesa walizotoa Marais wetu wawili, zinawafikia wananchi kwa haraka zaidi kwani mchakato huchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na kupata pesa kidogo ndani ya Wizara yao lakini wanasimamia kikamilifu Wizara hii kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri za kusimamia Wizara inayozingatia jinsia zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapa pole Wizara hii kwa kupewa fedha kidogo, ukilinganisha na kazi ngumu wanayosimamia lakini hawakati tamaa wameendelea vizuri, naishauri Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha hapa Tanzania tuna watoto wa mitaani, nakataa ni uzembe wa wazazi si wa Serikali. Nashauri Wizara ijipange vizuri kukabiliana na tatizo kubwa la lishe linaloendelea kuwa kubwa, watoto wote watunzwe na wazazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzishwa Benki ya Wanawake, benki hii itakuwa mkombozi kwa wanawake. Nashauri benki hii iweke matawi hadi Mikoani baadaye kwenye Wilaya wanawake walio wengi sana huko vijijini, wana miradi mingi hawana mahali pa kwenda kupata mikopo, ili wajiendeshe vizuri kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kutembelea Chuo chetu cha Malya, tunamshukuru sana na tunaendelea kumkaribisha tena. Viongozi wakipita kwenye vyuo vyetu, tunapata changamoto nyingi na marekebisho yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM 2005, kuhakikisha asilimia 50/50 inatimizwa kuanzia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 na nafasi zingine nyeti za utendaji na nafasi za masomo kwa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kulaani vitendo vibaya vinavyofanywa na baadhi ya makabila ya kuwakeketa watoto wa kike, wasichana wanateseka na maumivu makali, ukimwi unawapata kwa vifaa visivyo na usalama vinavyotumika katika ukeketaji na wasichana hawa wanapunguziwa sehemu nyeti za miili yao. Nashauri Wizara hii, iweke mkakati endelevu katika kukomesha vitendo hivi vya kikatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Wizara kufuatilia *NGOs* zote zinazoletewa mafungu toka kwa wafadhili toka nje kusaidia watoto, wazee na jamii kwa ujumla, ziwafikie walengwa wetu wengine wanajinufaisha wenyewe watoto yatima wanateseka fedha hazitumiki ipasavyo. Naomba sana watu wote wenye vituo vya watoto yatima waandikishwe Wizarani ili iwe rahisi kufuatilia malipo na fedha hizo zitumike ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara inavyojitahidi kuishawishi Serikali kuzingatia suala zima la haki za wanawake, yenye lengo la kuleta usawa kati ya wanawake na wanaume, katika masuala ya kisiasa. Naishauri Serikali iangalie pia suala la usawa wa jinsia kwa upande wa kiuchumi na kijamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado uko mtazamo hasi kwa wanawake ndani ya jamii (wanawake wenyewe na wanaume pia). Naishauri Serikali ikaze uzi wa mafunzo, jamii ielimishwe kuzitambua haki hizi tangu familia hadi Taifa. Aidha, fursa mbalimbali zinazoweze kuwakomboa wanawake kama mikopo, michezo, elimu yapewe nafasi ili yafungue nafasi ya kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya tatizo kubwa linalowagandamiza wanawake, ni pamoja na tatizo la kipato kuwa kidogo au kutokuwa nacho. Jamii inathamini kipato badala ya uwezo. Kimsingi wanawake wengi wana uwezo. Naendelea kuishauri Serikali iwawezeshe ili hatimaye wajiwezeshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali pia iviangalie vyama vyetu vya kisiasa. Nafasi ya mwanamke inaangaliwa sana katika nafasi ndogo ndogo. Naiomba Serikali, ivishauri vyama vya kisiasa, kujiangalia na kuona ni vema iwape pia nafasi

wanawake. Naamini wanawake wana mchango mzuri na mkubwa katika siasa za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali hasa Wizara hii kwa hatua iliyofikia katika kuanzishwa Benki ya Wanawake. Benki hii itakuwa ukombozi mkubwa wa wanawake na ni jambo la kihistoria na kujivunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ituletee Sheria za Matunzo ya Watoto wanaoitwa watoto wa nje ya ndoa. Hawa ni watoto sawa na wale wa ndani ya ndoa, maana baba mwenye ndoa ndiye baba wa wale anaowaita wa nje. Haitoshi, baba huyu akemewe kwa kuzaa watoto ambao hawatunzi. Aidha, akina mama wazidi kuelimishwa kuwa waangalifu sana katika kuingia mahusiano yoyote na akina baba hata kama ni ndoa au vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Serikali ituletee Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971. Serikali ijitahidi kuirekebisha vizuri sheria hii ikishirikisha wadau wote ili ukarabati utakaofanywa uwe wa kuwaridhisha watu walio wengi. Kasoro zinazoendelea kuachwa ndani ya sheria hiyo, zinachochea matatizo yasiyokwisha ya ndoa na watoto wengi wanateseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazotufaa sisi Watanzania ni zile ambazo zitasimamiwa na Serikali. Naitahadharisha Serikali isije hamakika au hamasika hata siku moja ikatunga sheria inayoangalia mtazamo wa dini moja. Ninavyojua, wapo wengi wanobadili dini kutoka Ukristo kwenda Uislamu au kutoko Uislamu kwenda Ukristo, hawa kama waliunga mkono kwa sababu ya dini, je, watasimama wapi? Serikali ndiyo pekee itasimamia haki za watu wote bila kujali dini, jinsia na bila kuvunja Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa mitaani wamezidi, tunaomba jitihada zifanyike kwa bidii maana hali si nzuri kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wengi wa vijijini, kazi yao kubwa ni kazi za nyumbani hususani vijana, watoto na mabinti. Watoto wa kiume wanachunga mifugo hali si nzuri kwa maendeleo ya leo pia watoto hao hawapati haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa za akina mama za Halmashauri hazipatikaniki kabisa. Ni nini haswa au ni urasimu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii wanaoishi katika maeneo hayo kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi ni wachache mno, tunaomba Maafisa wa Maendeleo ya Jamii kila kata, kwa sababu ya shughuli mbalimbali za maendeleo katika Halmashauri zetu hapa nchini.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri ya kisayansi na yenye takwimu nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Kabambe wa Kusaidia Masomo ya Watoto Yatima. Pamoja na kuwepo wahisani na Serikali Kuu kupitia Wizara ya Elimu na Maendeleo ya Ufundi, katika kusaidia watoto yatima, linapaswa kubeba na kuratibu matatizo yote ya watoto. Kwa msingi huo, kusimamia mipango yote ya kuleta na kuwatafutia misaada ya elimu watoto yatima. Ukitathmini michango ya Waheshimiwa Wabunge kwa kulipia ada, mavazi na mahitaji muhimu ya watoto yatima na wasiojiweza, utaona ukubwa wa jukumu linalostahili kimsingi kuchukuliwa na Wizara inayosimamia watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Chuo cha Maendeleo Kiwanda, napongeza kazi za ukarabati wa chuo unaoendelea. Tatizo la kukosa umeme chuoni bado linaendelea. Kwa mpango wa *MCC*, mwaka huu 2009 umeme utafika jirani na chuo maeneo ya Bombani hadi Tongwe, eneo dogo linalobaki litafikiwa katika awamu ya pili 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo jitihada za wahisani kutoka Sweden kusaidia chuo hicho kupata umeme zimezaa matunda. Wahisani wameshatoa vifaa vya uzalishaji umeme wa upepo *(wind mill)* kubwa yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa kutosha mahitaji ya chuo na eneo dogo la kijiji jirani ya chuo. Naiomba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ishirikiane na Halmashauri ya wilaya ya Muheza kugharamia ufungaji wa mtambo huo wa '*wind mill*' na *'solar panels'* na kusambaza umeme huo chuoni na katika zahanati jirani ya chuo (Zahanati ya Kiwanda).

Mheshimiwa Naibu Spika, *wind mill* na *solar panels* zimeshapelekwa eneo la Kiwanda na inatakiwa ujenzi wa eneo la kuweka mnara *(basement*) na kutengeneza minara na kuisimamisha. Nawaomba sana muwasiliane na Mkuu wa Chuo Kiwanda na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule mpango mwingine wa kutoa umeme kutoka Mto Ziggi umekwama kupata wahisani hasa baada ya chuo kushindwa kufuatilia upatikanaji wa "haki wa matumizi ya maji" *(water right)* kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji tangu mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza nyote kwa kutuletea hotuba nzuri licha ya pesa mlizopewa kuwa kidogo, hongereni sana. Nishauri mambo machache yafuatayo, Maafisa Maendeleo wa Wilaya wahimizwe kuwatembelea wananchi na kuwafundisha mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi zile "*Community Centres*" (Majumba ya maendeleo) zilienda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri wale watoto tunaowaona mitaani, tuangalie utaratibu wa kuwatunza kama hawana ndugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwe na udhibiti/uhakiki wa *NGOs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao wameanzisha vikundi vya kulelea watoto yatima, baadhi yao hawatekelezi azma hii na huwatumia watoto hawa ili kujinufahisha wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea Serikali imeshaliona suala hili, ni mkakati gani wa kuweza kuondoa hali hii ambayo ni kinyume cha maadili na sheria? Hongereni sana.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margaret S. Sitta, (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya (Mb), Katibu Mkuu, Wakurugenzi na viongozi wote wa Wizara na taasisi zake kwa hotuba nzuri sana na kwa kazi nzuri ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la faraja kubwa sana kwamba hata kwa Wilaya mpya kama Mkinga, tayari Wizara imetusaidia kupata Maafisa Maendeleo ya Jamii takribani kwa kila Kata. Hata hivyo, ipo haja ya kuwapatia Maafisa hawa vitendea kazi kama pikipiki na baiskeli ili waweze kuvifikia vikundi na wananchi sehemu mbalimbali ili waweze kuwahudumia wananchi hao kwa karibu na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna haja kubwa kuwapa Maafisa hawa madaraka na uwezo mkubwa zaidi katika kusimamia mikopo na miradi ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani vilikuwepo Vituo vya Maendeleo *(Community Centres)* ambazo zilikuwa zikijihusisha sana na maendeleo ya jamii. Hivi sasa vituo hivyo havipo. Napendekeza Serikali ifikirie kurudisha *“community centres”* angalau kwa mtazamo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Margaret Sitta (Mb) Waziri, Naibu Waziri, Dr. Nkya (Mb) Ndugu Katibu Mkuu na wataalam wote. Naunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu itolewe zaidi kwa wanawake wajane, kuhusu haki zao. Kuna kutumia vipeperushi kwa njia rahisi/lugha yenye wepesi, ili wanapopata tatizo wajane waweze kujitetea. Kwa mfano, haki za miradhi na kadhalika. Mpaka sasa wanawake wengi hutatizwa kutumia haki hizo ni kutokana na mfume dume na mila inayomkandamiza mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi, Wizara hii iangalie pia kuhamasisha wanawake kujitokeza kushika nafasi mbalimbali, hususani za kugombea uongozi. Pia Wizara hii itoe changamoto kwa Serikali kwa kufanya yafuatayo:-

- Kuhakikisha asilimia 50% ya Wabunge na Madiwani, vitongoji inapatikana;

- Sheria ya Ndoa ya mwaka 1970, ifanyiwe marekebisho haraka kwani nayo inaleta masikitiko kwa wanawake (kero);

- Benki ya Wanawake ianze mapema sana tena kwa riba nafuu, pia ifike Mikoani, kwa kutoa vipeperushi. Watumiwe Maafisa Maendeleo; na

- Maafisa Maendeleo Wilaya na Kata wapewe vitendea kazi, hasa kutokana na jiografia zilivyo hapa nchini kutokana na umbali wa kuwafikia wanawake kwa kutoa elimu kwa wakati, wakopeshwe pikipiki/baiskeli;

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu, Wizara aisimamie kuhakikisha shule zote zina mabweni ili kuwaondolea usumbufu, hofu, wanafunzi wa kike, kwani hiyo huchangia kushuka kwa elimu ya wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wote waliopata mimba shuleni ni vema warudi kusoma tena, kwani wasichaana wengi hukatisha masomo na kusababisha kuwa na asilimia ndogo katika ngazi za uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SACCOS*, Wizara isaidie kuwawezesha wanawake kujitokeza katika kujiunga na ujasiliamali, kusaidia biashara zao kuzitangaza, kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusimamia upatikanji wa mikopo kwa michango ya 10% ya Halmashauri ikilinganishwa na ile ya Wizara ili wanawake wapunguze umaskini, kwani watendaji wa maendeleo wako huko ambapo wanaweza kusimamia wakati wa utekelezaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itoe kipaumbele kwa kuangalia yafuatayo katika suala la watoto wa mitaani wanaoishi katika mazingira magumu:-

(i) Kufuatilia NGOs ambazo zinalea watoto hao kwani, wamejitokeza kusaidia lakini baadhi yao wanafanya kama miradi. Ni vema hivi sasa wasajiliwe katika Wizara hii ili kudhibiti fedha za wafadhili;

(ii) Serikali itenge fedha kila mwaka ili kuwepo na shule maalum ambayo itakuwa chini ya Wizara, kama zilivyokuwa shule za wazazi kupitia CCM, ambazo zilienea nchi nzima, kwa kulea watoto kwa maadili mema;

(iii) Kuwa na sensa ya watoto hao ili iwe rahisi kutetea wakati wa bajeti, ikiletwa hoja hiyo, kwa kujua vikundi vinavyowalea watoto hao; na

(iv) Kuwe na kitengo maalum cha kufuatilia makazi ya watoto hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalilishwaji kijinsia, niishukuru sana Wizara kwa kutoa elimu katika jamii na mpaka sasa umepungua, kwa asilimia kubwa. Hivyo basi, hivi sasa elimu hiyo iendelee kutolewa kwenye maeneo ambayo bado ya ukeketaji, upigwaji wa wanawake, nguo zisizofaa katika jamii na kero katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze NGOs ambazo zinatoa elimu kwa wanawake, lakini asilimia kubwa ziko mijini. Ni vema sasa Wizara isaidie kuomba pia zifike vijijini, huko nako kuna mzigo mkubwa wa kuonewa na kunyimwa haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo na kitengo maalumu katika Wizara, Mkoa, Wilaya ambacho kitasaidia kutoa elimu pia kuwasaidia pale ambapo kesi zipo Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai, nami nikapata fursa ya kuchangia hoja hii hapa Bungeni, ninakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliohusika kuandaa hotuba hii. Ni matumaini yangu kuwa yote yatakayojadiliwa kuboresha hoja hii, yatafanyiwa kazi wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi ya mwanamke katika jamii yoyote, ni kubwa sana lakini fursa zake ni finyu, fursa ninazozungumzia hapa ni za elimu, uchumi na maendeleo. Pamoja na nia nzuri ya Serikali kuwakwamua wanawake kwenye nafasi ya nyuma, bado changamoto ni nyingi na ninaomba nizifafanue.

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa ya elimu bora kwa vijana wetu vijijini, bado ni ndogo sana pamoja na nia nzuri ya kufikisha watoto wengi Kidato cha Nne na kuhimiza ujenzi wa Sekondari za Kata, bado mabinti wengi wanapata shida kuhudhuria darasani kutokana na umbali. Swali langu ni, je, Wizara hii kwa kushirikiana na wafadhili mbalimbali aliowashukuru mbele yetu ikiwemo WAMA, EOTF, CIDA, USAID, DANIDA, UNIFEM na UNESCO, wameshajenga *hostel* ngapi na wapi? Ninapenda kupata majibu wakati wa majumuisho. Mpango wa baadaye wa kujenga hostel hizo ukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutupatia fungu la kuanzia, lijulikanalo kama Mabilioni ya JK. Awamu ya kwanza, hela kama hizi zilitolewa na Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere na hazikuweza kuzungushwa kwani zilitokomea, hazikurejeshwa. Swali, ni kiasi gani Wizara hii imeshirikiana na wafadhili kutoa elimu ya ujasiriamali? Ni *programme* ngapi zimeendeshwa Mikoani kwa msaada wa Wizara? Jukumu hili limeachiwa wanawake na

Wabunge wao kubahatisha hapa na pale. Ni vema Waziri akatufafanulia *programme* rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo hayana mipaka wala umri, maendeleo yanatakiwa kwa watoto, vijana, watu wa rika na wazee. Maendeleo yanatakiwa kwa viongozi na wananchi wote. Katika sekta hii, ninapenda kueleweshwa; ni jinsi gani Wizara hii inawafikia wazee na watawa. Makundi haya mawili yananitatiza sana kwani huko vijijini watu hawa wamechoka kwa hali ngumu na bado wanategemewa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza sana Mheshimiwa Margaret Sitta, (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri, Mheshimiwa Nkya, Katibu Mkuu, Ndugu Mariam Mwafisi na Wakuu wa Idara wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ya kuendeleza jamii ya Tanzania, pia naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusaidia Serikali Kuu, naomba Wizara kufanya kazi ya ziada ya kuchambua/kukagua uhalali na utendaji wa Mashirika yasiyo ya KiSerikali yaliyosajiliwa na Idara ya Mashirika yasiyo ya KiSerikali ili kuelewa yapi yanafanya kazi kwa dhati na yapi ni ya ubabaishaji. Ukaguzi huu utasaidia sana katika kupunguza matumizi mabaya ya misamaha ya kodi inayotolewa kwa *NGOs* hapa nchini kwa mujibu wa sheria. Naishauri Wizara kuzifuta *NGOs* zote zitakazobinika kutokidhi usajili wao/madhumuni ya kuanzishwa *NGO* hizo na kutangazwa rasmi katika vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaelewa kuwa, mwananchi mmoja huko Tanga anatengeneza nishati mbadala, kwa kweli naiomba Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kumtambulisha/kumtangaza kwa jamii;

(ii) Kumsaidia kupata soko;

(iii) Kumsaidia kuongeza ujuzi wake;

(iv) Kumuunganisha na Wizara ya Nishati na Madini ili kumtambua rasmi;

(v) Kuisambaza teknolojia yake; na

(vi) Kumuomba kusomesha Watanzania wengine juu ya uwezo wake huo ili kutoa ajira kwa jamii.

Mheshimia Naibu Spika, naishauri Wizara hii tena kuanzisha Mfuko wa Kusaidia Vituo vya Kulea Watoto Yatima ambao utaweza kutoa ruzuku kwa vituo hivyo. Fedha za mfuko huo zisaidie kwa huduma za chakula, ada za masomo na mavazi ikiwezekana pamoja na kukarabati vituo inapobidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nililichangia suala hili hapo awali katika miaka miwili iliyopita, ni jambo jema kuishauri Serikali ifanye juhudi ya kuipatia fedha Wizara hii, kuwawezesha kujenga ofisi ya Wizara yao Dodoma na *Rest House* za viongozi wa Wizara hii. Hii ni aibu kubwa kwa Serikali, tuamue tuwakomboe kutoka kwenye shida hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Wizara hii ilikuwa na utarabibu wa kutoa udhamini wa masomo ya elimu ya juu kwa wanawake lakini hakuna taarifa zake. Je, utaratibu huu umeondolewa? Kama upo, ni wangapi wamefaidika chini ya mpango huu na maendeleo yake yakoje na kama unafahamika vyema na wanawake wa Tanzania?

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufahamu nafasi ya mtoto wa kuanzia umri wa miaka 0 hadi 5 Kisera na Kisheria. Kama Sera haisemi chochote juu ya watoto wa umri huu, je, Wizara hii inasema nini juu ya haki na wajibu wa Serikali kwa kundi hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko shule za watoto wadogo wa umri huu mitaani (Chekechea) na viko vyuo mfano Kile cha Mtumba – Dodoma, vinavyofundisha Walimu wa watoto wa kundi hili, je, Wizara ipi inahusika na ubora wa mafunzo au kiwango cha mafunzo yapaswayo kutolewa kwa watoto wenye umri huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ilitolee maelezo jambo hili maana pengine linafanyika kimakosa bila kuwepo na chombo cha Serikali kinacholisimamia.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mzima na afya kamili na kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya maendeleo ya jamii, jinsia na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukukushukuru wewe pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kuwa Mwenyezi Mungu amekujaalieni busara ya kuweza kuendesha Bunge letu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sikuwatendea haki kama sijawapongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ya kuandaa bajeti hii.

Mheshimniwa Spika, naanza kuchangia kwa kuuliza, je, ile Benki ya Wanawake, maendeleo yake yakoje? Maana siku zimeshakuwa nyingi lakini bado mpaka leo mchakato unaendelea! Pamoja na maelezo na mipango mizuri, naiomba sasa ianze kufunguliwa ili wanawake kwa asilimia kubwa wapate kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu asilimia 50%, Serikali ishughulikie na vile vile iwawezeshe wanawake kufikia jitihada hii ya Serikali, kwani wanawake wana uwezo mkubwa lakini uwezo wa kifedha hawana kwa hivyo wanarudi nyuma na kujiona kama

hawafai. Kwa hiyo, Serikali itoe elimu ya kutosha ili wanawake wajitokeze kwa wingi katika kugombea nafasi za uongozi kuanzia ngazi za chini mpaka uongozi wa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanawake kunyanyasika kwa kufanyishwa kazi nyingi kuliko wanaume kwani wanaume wanahisi kazi zote zinamhusu mwanamke, Serikali iwape elimu ili waone ni haki yao kuwasaidia wanawake kazi kwani hakuna mtu aliyezaliwa afanye kazi kuliko mwingine. Wanaume waache kucheza bao na karata pamoja na kwenda vilabuni kunywa pombe na kuwaacha wanawake wanateseka na kazi na ulezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwatesa na kuwauwa watu wenye ulemavu wa ngozi yaani ni Albino. Serikali katika kipindi kilichopita cha kama miezi mitatu, kura za maoni zilipigwa kuhusu mauaji ya Albino lakini mpaka leo hakuna ripoti yoyote inayohusu mauji hayo na kujua watu wangapi walijulikana katika sakata hilo na wamechukuliwa vipi?

Naiomba Serikali itoe taarifa kuhusu habari hizo. Kutokana na usiri huo hivi sasa yameanza tena mambo ya kuwauwa Maalbino. Naiomba Serikali itoe hukumu kali ili kuweza kuwafanya watu wanaowauwa Maalbino waweze kuogopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukeketaji, inaonekana bado baadhi ya mila hazijakubali kuacha habari hiyo. Naiomba Serikali isichoke kuwaelimisha wananchi ili waache tabia ambayo ina madhara makubwa kwa taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Margaret Sitta (Mb), Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri, Mheshimiwa Lucy Nkya (Mb), Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara, kwa utendaji wao mzuri katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake bado wanateseka sana hasa katika suala la mirathi vijijini na mijini bado wananyang’anywa mali wanazochuma na waume zao; wananyang’anywa watoto; wanafukuzwa na kukosa makazi lakini wengi wao bado hawajajua pa kukimbilia. Wizara hii ione namna ya kuwasaidia maana wanakosa haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili wa kijinsia unaendelea katika maeneo mengi vijijini kutokana na mila na desturi za baadhi ya makabila hapa nchini. Kutokana na ukandamizaji wa wanawake na kwamba mwanamke haruhusiwi kusema jambo lolote la familia, wameendelea kunyanyasika katika maeneo yao bila msaada. Uhamasishwaji wa mara kwa mara kwa Mikoa yenye unyanyasaji kwa wanawake uendelezwe kwa bidii zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni kweli Serikali kwa kushirikiana na wananchi tumeshindwa kukomesha au kupunguza watoto kuzurura mitaani wakiombaomba na

kuacha kwenda shule? Baadhi ya watoto wana wazazi na wanatumwa na wazazi wao kwenda kuomba mitaani. Serikali ifanye utafiti kwa kuwahoji watoto hao na kujua ukweli wao la sivyo tutakuwa na taifa la kesho lisiloweza kufanya kazi. Wazazi, walezi wa watoto wawajibike katika kulea watoto kabla ya au bila ya kuiachia jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii pia iwasaidie wanawake katika Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971. Pesa zinazotolewa kwa malezi ya mtoto ambaye haishi na baba yake mzazi ni kiasi kidogo mno na imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Margaret Sitta, kwa kusimamia uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania. Nashauri uhamasishaji wa kununua hisa za benki hii uendelee kwa wanawake maofisini, wanawake wafanyabiashara, wanawake wakulima kwa Mikoa na Wilaya zote Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kupata fursa hii nichangie kupitia Wizara hii kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Margaret Semwanza Sitta, (Mb), Waziri mwenye dhamana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, (Mb), Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Katibu Mkuu, Mama Mariam Mwafisi na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya bajeti ya Wizara, kwa kipindi cha mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara nyeti sana kwa maana imegusa masuala ya maendeleo ya wananchi, jamii, wanawake jinsia, watoto na *NGOs*. Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2009/2010, ni ndogo sana kwani kulingana na shughuli za Wizara, hazitoshelezi. Ninaiomba Serikali kuongeza bajeti ya Wizara hii ili iweze kutekekeza majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vile vya Singida na Msingi kilichopo Wilayani Iramba, vifanyiwe ukarabati kwenye majengo yake ili viendane na hali ya kisasa. Pia Chuo cha Msingi kiwekewe umeme ili kiweze kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itilie mkazo kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maadili ili kujenga jamii yenye tabia na mwelekeo unaoendana na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itengeneze programu za radio, TV na maagizo kupitia mikutano ya hadhara kupiga vita maambukizo ya UKIMWI hasa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata uwakilishi/uwiano, sawa sawa kwenye vyombo vya maamuzi, Wizara itumie fursa ya kuhamasisha zaidi na mafunzo yatakayoshawishi wanawake kupata hamu ya kuomba nafasi za uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)*, Wizara idhibiti uholela wa *NGOs* za mifukoni. Uratibu ufanyike kwa nchi nzima ili kubaini *NGOs* zisizo na usajili unaotambuliwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu changamoto nyingi zinazokabili Wizara hii lakini pamoja na ufinyu wa bajeti, Wizara ijielekeze zaidi katika kutekeleza kwa ufasaha majukumu yake kupitia bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET A. MKANGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri inayoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nina mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo kwa wanawake toka kwenye mifuko husika, ni kweli kazi ya ukopeshaji inaendelea lakini katika Halmashauri nyingi Maafisa Maendeleo ya Jamii hawahamasishi vikundi vya wanawake wenye ulemavu pekee yao au wachanganyike na wanawake wasio na ulemavu katika kufaidika na mikopo hiyo; ingawa wenye ulemavu ndio wana maisha magumu na maskini zaidi.

Hivyo nashauri watendaji wasichoke kuwahimiza wanawake wenye ulemavu kujiunga pamoja ili wapate mikopo na kuweza kujikwamua kiuchumi ili maendeleo yawe kwa wote. Wenye ulemavu wakiachwa nyuma basi maendeleo ya wanawake hayakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nafasi na fursa kwa wanawake, naipongeza Serikali kwa kuongeza idadi ya wanawake katika ngazi za maamuzi na utendaji Serikalini. Naamini mchakato wa dhati utaendelea kwa muda wote. Hata hivyo, nashauri wanawake wenye ulemavu ambao wamekidhi vigezo vya uteuzi na kadhalika, nao waongezwe katika sehemu hizo kwani kwa sasa wapo wanawake wenye ulemavu waliosoma vizuri tu. Hivyo, itakuwa ni mfano mzuri kwa wenye ulemavu wenyewe na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mila zenye kuleta madhara bado zinaendelezwa pamoja na jitihada zote ambazo Serikali na *NGOs* zinafanya za kujaribu kuzipiga vita mila hizo kwa njia mbalimbali. Kinachosikitisha ni kwamba ukatili huo unaendelea sasa kwa mauaji ya Albino hapa nchini. Natoa rai, elimu iendelezwe juu ya madhila ya mila hizo kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yaliyokithiri na ukatili huo licha ya sensa iliyofanyika kuwatambua wauaji na watesaji wa wanawake na wazee nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. MCHUNGAJI DR. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu wote kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, naibu Waziri na watendaji wote kwa hotuba nzuri inayokidhi haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake na maendeleo, pongezi kwa Benki ya Wanawake, kwa kurudisha Mfuko wa Elimu ya Juu kwa Wanawake, kwa utendaji wenu mzuri mpaka bajeti yenu ikaongezwa kutoka shilingi 14.6 bilioni mpaka shilingi 21.6 billion na kwa tovuti iliyozinduliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imeelemewa na majukumu mengi mno. Je, hawawezi kutoa watoto wakawapeleka afya au elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara hii waipe kipaumbele kwa sababu suala la wanawake ni pana sana linajumuisha familia, watoto, wanaume na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na kadhalika, ni pana mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maofisa Maendeleo wakae vijijini sio mijini. Kwa kufanya hivyo itasababisha ukatili kwa wanawake kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutoe msaada kwa wajane walindwe kwa sheria kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupiga mke ni ushamba. Wanaopiga wake zao wapewe adhabu kali au wafungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tuzingatie *‘exchange programs’* kwa wanawake.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba yao nzuri yenye kueleweka na maelezo yote yaliolezwa yanafahamika na yana ufanisi mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuhusu Benki ya Wanawake ianze kazi mara moja ili wanawake wapate kufaidika zaidi kwani kunasubiriwa nini tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya ushirika yatolewe vijijini hasa kwa vikundi vya kina mama ili wapate kujiunga zaidi na kujishughulisha katika shughuli za kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miswada ya Kisheria ya Haki za Wanawake na Watoto, iharakishwe kuletwa Bungeni ili wapate kutambua haki zao na waepukane na unyanyasaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo vya Wananchi, vizidi kuboreshwa kimafunzo, kinyenzo pia kupatiwa wataalamu ili vipate kutoa watendaji bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NGO*, ziwekewe mikakati kabambe ya kueleweka na kuwe na ufuatiliaji kuhusu shughuli zao na namna gani wananchi wanafaidika nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naitakia kila la kheri Wizara na kazi ya utekelezaji bora.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wa Wizara kwa kuandaa taarifa na bajeti za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za Wizara hii ni msingi wa maendeleo, malezi na makuzi ya jamii ya Tanzania kiuchumi, kijamii, *emotionally* na kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itoe elimu ya jinsia katika jamii ili kupunguza fikra finyu na potofu dhidi ya usawa wa ki-jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ihimize Sheria (au Miswada) ya mirathi iletwe Bungeni ili marekebisho yafanyike ili ihuishwe ilingane na mahitaji yetu ya leo kama jamii ya Wantanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu na mkakati wa kutokomeza ukeketaji wa watoto wa kike katika jamii. Pendekezo litolewe la jamii kutenga *Ritual/Rite* na *physical operation* kwenye Tohara ili mafunzo ya utu uzima yadumishwe, lakini *operation* itokomezwe kama utamaduni.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu sana nimetetea haki za wanawake kwani haki za binadamu ni haki za wanawake. Jambo la kushangaza, hivi ni kwa nini na ni kitu gani kinachocheleweshа kuleta Sheria ya Mirathi? Ni miaka kumi mimi nikiwa Waziri Kivuli wa Wizara hii na nilisemea sana jambo hili lakini hadi sasa Sheria hii haijaja kwa nini? Serikali yetu inathamini sana wanawake, naishauri sana ilete sheria hii ili wanawake wajane wapate haki zao za urithi ambapo wameshiriki katika kutafuta mali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imesisitiziwa kwamba ni Wizara ya Jinsia, Wanawake na Watoto. Ukisema jinsia, umemaliza kwani jinsia ni wanawake na wanaume, watoto, wazee, walemavu na kadhalika lakini imesisitizia wanawake na watoto. Kwa misingi hiyo, Wizara ihangaike zaidi kwa wanawake na watoto. Kwa misingi hiyo basi walete Sheria ya Mirathi ili tu-*solve* tatizo hili *"once and for all"* na pia watoto wataangaliwa na mama zao. Sheria isisitize watoto wote aliozaa mama aliyebaki kama mjane na watoto aliowakuta au walioletwa na baba ambao walikuwa wanaishi hapo wakati baba akifariki. Hii itasaida watoto pia kutoenda kwenye makundi ya kuvuta bangi

au madawa ya kulevya na kadhalika. Serikali au Wizara hii iwe makini katika kuangalia sheria hii ili haki ya mke na watoto iwe bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina mikakati gani katika kuelimisha wananchi (jamii) kuandika wosia? Ni muhimu!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza kuona watoto wanazagaa wakiombaomba mitaani hasa Dar es Salaam. Watoto hawa wengi wao wana wazazi wanaowatuma kwenda mitaani kuomba, ni mradi ili wawe wanalisha familia. Je, Wizara hii inaonaje hasa ukizingatia ni kioo cha jamii ya Tanzania, kama tukiachia iwe ndio mila na desturi ya Watanzania, kweli ni aibu! Akina mama na Wizara yetu iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri wafuatiliwe hawa watoto na wazazi wapatiwe adhabu, namaanisha wakipatikana washitakiwe na ikitangazwa sana, naamini, itakwisha, ila tukizembea itakuwa sheshe. Kama ujuavyo Watanzania tunavyojua kuiga, mfano mtu akiuza juisi, kila mtu ana uza juisi na hivi mtoto akitumika kiuchumi kulisha familia kwa kuomba basi kila mwanamkie mzembe atafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la 50% ya viongozi mfano Wabunge, naafiki sana ila nashauri kama tunaongeza idadi ya wanawake si kwenda au kutaka mwanamke mwingine kumtoa hasa mwanamke anayeweza. Naamini lengo la kuongeza wanawake ni kuongeza namba (namba inayoweza) sio mtu tu amezaliwa mwanamke, ni mwanamke anayeweza. Tusambae basi sio kufuata mwenzio na kubaki na namba ile ile. Naamini kabisa sisi kina mama tunaoweza, tukijipanga tunaweza kuongeza namba bila kuyumba na kushambuliana na hapo watu watatucheka, watasema “wanawake bwana” ambapo sisi tumepita hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MGANA I. MSINDAI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na watumishi wote wa Wizara hii wakiwemo Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana kwani pamoja na kupewa fedha ndogo, watumishi wachache, bado kazi yao inaonekana na kutukuka. Endeleeni hivyo kwani jamii inawategemea sana, maendeleo ya jamii ya Tanzania huwategemea sana. Endeleeni kuishawishi Serikali iwaongezee uwezo na nyenzo za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa nchi hii wanawategemea Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara hii. Watoto wengi bado hawana uhakika wa kuishi, watoto wengi bado wanaajiriwa wakiwa na umri mdogo wengi wanaachishwa shule na kuolewa, wanabakwa na baadhi ya familia watoto wakikataa matendo mabaya ya wazazi wao wanafukuzwa na kutengwa na familia. Watoto wengi bado wanakeketwa, wananyimwa haki ya kujieleza, watoto wengi wa makabila ya wachungaji, wawindaji (Wahadzabe) na kadhalika bado wanaishi maisha ya dhiki bila elimu na matibabu. Naomba mambo yote hayo yafuatiliwe kwa karibu zaidi.

Iramba Mashariki tuna watoto wengi wa aina hiyo. Naomba sasa Serikali ibadili msimamo, maeneo haya yajengwe shule za bweni ili wanafunzi hawa wapate masomo bila taabu ili waachane na mila zao za asili waingie kwenye mfumo wa maisha ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado uwakilishi wa wanawake kwenye maeneo mengi ya uongozi ni mdogo. Maeneo mengine ni kutokana na woga ambao wanawake bado wanao. Naomba elimu zaidi itolewe ili kina mama kuanzia ngazi za Vitongoji, Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya mpaka Taifa, waendelee kujitokeza kutafuta uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikumpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa semina ambazo Wizara yako iliendesha mwaka jana na mwaka huu kuhusu mambo ya jinsia na pia nimpongeze sana kwa kusimamia mpaka Kamati (kikundi) cha kusukuma mambo ya jinsia ndani ya Bunge na maeneo mengine. Nakuahidi kwamba waliochaguliwa, ni watu makini, watafanya kazi nzuri sana kwa manufaa ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri asaidie kutatua matatizo yaliyoko kwenye Chuo cha Maendeleo Msingi – Iramba Mashariki. Matatizo makubwa ni umeme, ambao unapita km.4, naomba wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo hiki kipo mbali na Wilaya na Mkoa kwa hiyo naomba sana wapatiwe usafiri wa gari.  Pia kuna tatizo la maji naomba wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizi kushauri mambo yafuatayo:
Mosi huko Wilayani wafanyakazi wa Wizara hii ni wachache kwa hiyo waajiriwe maana hawa ndio wanaokaa na kufahamu matatizo ya wanachi wetu.

Pili, narudia kuandika kwamba uendelee kuishawishi Serikali na wafadhili waongeze fedha.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi katika miji yetu limekuwa kubwa, huku Serikali bado haijalipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hili. Hivyo ushauri wangu ni kuandaa mpango mkakati wa muda mfupi na muda mrefu wa kuwatambua watoto hao na kuangalia namna bora ya kuwakusanya na kuwaweka katika eneo moja kwa Tanzania nzima na hatimaye kuwapatia elimu inayostahili kuanzia msingi, sekondari hadi chuo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika kiwango cha malipo cha wafanyakazi wa ndani katika nyumba (yaya, ni kidogo mno na hakuna utaratibu maalum wa Serikali uliowekewa wamiliki wa wafanyakazi hao kuwapatia kiinua mgogo mara tu muda/mkataba unapoisha. Wakati mwingine hufukuzwa wafanyakazi hao bila kupata hela zao na kunyanyasika. Hivyo, ushauri wangu ni kuweka utaratibu maalumu wa kuwalinda wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kuandaa mpango mkakati wa ziada utakaotoa elimu kwa wananchi wa vijijini ambao bado hadi leo wanaendelea kutumia mila na desturi na utamaduni kwa ujumla wake ambao unaleta madhara mfano tatizo la ukeketaji, mauaji ya vikongwe na Albino.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kufahamu ni watu wangapi wamefikishwa katika vyombo vya sheria waliohusika na ukatali dhidi ya wanawake pamoja na mauaji ya vikongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuelimishwa ni watu wangapi wamegundulika kufikishwa katika vyombo vya sheria baada ya kugundulika wanaeneza/kusambaza ugonjwa wa UKIMWI tangu sheria itungwe hapa Bungeni?

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Naibu Waziri pamoja na watendaji kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Chuo cha Musoma *FDC* Bweri, mbali na matatizo mengi yaliyopo chuoni, pia lipo tatizo kubwa la fidia ya ardhi katika eneo la chuo. Wizara iliagiza chuo kipeleke uthamini uliofanyika na chuo kilifanya hivyo zaidi ya miaka mitatu sasa. Napenda kufahamu ni lini gharama hizo zitalipwa ili chuo kiweze kupata eneo hilo kwa upanuzi wa maendeleo ya chuo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kukiwezesha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare kutoa Diploma. Naiomba Wizara ipeleke fedha za kutosha za kukarabati chuo, kujenga fensi na kufanya chuo kiweze kutoa elimu tarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri kwa juhudi yake ya kuinua kiwango na heshima ya Wizara hii. Naishauri Serikali iongeze fedha ya bajeti ili kusaidia Wizara hii mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, vipewe nyezo na matengenzo ya majengo ili yafanane na maendeleo yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ushiriki wa wanawake wa uwiano 50/50 upewe kipaumbele ili Bunge lijalo uwakilishi uwe 50/50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake imekuwa ni kitendawili, napendekeza ifunguliwe kabla ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Wizara nzima ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu na timu yake yote kwa kuandaa bajeti nzuri ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inagusa jamii nzima kwa ujumla hasa ukizingatia akina mama na watoto ambao ni sehemu kubwa kabisa ya jamii ya taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchangia kuhusu unyanyasaji wa akina mama katika ndoa zao hasa ukatili usio wa kawaida. Katika maisha ya mwanadamu, ukatili wa jinsia ni ukiukwaji wa haki ya mwanamke kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nichangie kuhusu akina baba wanaotelekeza watoto na kuacha kutoa huduma muhimu za mtoto. Serikali iangalie kwa macho mawili katika eneo hili ili kuleta haki ya mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchangia kuhusu kuajiri watoto wadogo kufanya kazi za ndani. Watoto wamekuwa wakinyanyasika majumbani mwa watu kwa kufanya kazi za ndani kikubwa zaidi kulipwa pesa isiyo na tija. Kwa mtoto huyo, naomba Serikali itamke kwamba ajira ya mtoto afanyaye kazi za ndani anapaswa alipwe shilingi ngapi? Kwani watu wengi sana wanamtumia mtoto kufanya kazi za ndani bila kujali anamlipa pesa itakayomsaidia. Naomba Wizara ivalie njuga jambo hili muhimu kwa mtoto Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie juu ya watoto Watanzania wanaokeketwa. Ni wazi kwamba mtoto huyu anaharibiwa maisha yake ya baadaye hasa wakati wa kujifungua, lakini kikubwa zaidi anaweza kupoteza maisha pindi anapokuwa amekeketwa. Ni kweli tatizo hili limekuwa sugu kutoka makabila yanayohusika na ukeketaji, naomba tuseme kwamba sasa umefika wakati Serikali itamke ni hatua gani zinachukuliwa ili kuhakikisha tunapunguza tatizo hili zito la ukeketaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nichangie kuhusu mikopo itolewayo kwa wanawake kutoka asasi mbalimbali. Ni kweli kwamba mikopo hii haimsaidii mwanamke kwani riba yake ni kubwa na pindi anapokwama kidogo tu mama huyu hufilisiwa kabisa wakati mwingine kubebewa vitu vyote vya ndani. Naiomba Serikali iangalie kwa upya eneo hili kwani badala ya kumsaidia mwanamke humdhalilisha mwanamke kwa kumfilisi hata alichokuwa nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchangia kuhusu Wizara hii. Inasikitisha bajeti yake ni ndogo kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nakwenda kwa watoto wenye mazingra magumu Tanzania nzima pamoja na Mkoa wa Kagera hasa kwa viongozi kutowatendea haki watoto wenye mazingira magumu. Misaada ya watoto hawa haiwafikii ipasavyo na haina usimamizi pamoja na Wizara kutembelea mara kwa mara kuhakikisha kuwa wanapewa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajane kupewa mikopo, wakiomba mikopo hawapewi. Je, hiyo si kuwanyanyapaa wajane? Pia yatima kunyang'anywa mali zao, sasa wakati umefika kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla Benki ya Wanawake kufunguliwa na wenyewe wajione tunawajali, naomba Wizara yako itoe rai viongozi waache kutumia misaada ya walengwa kusomesha watoto ambao wazazi wao wapo, sio vizuri. Nimekumbana nao wengi sana hasa Wenyeviti wa Mitaa pamoja na Mabalozi wana tabia mbaya sana na mchezo mchafu. Mikakati yote inayosemwa hapa, je, Mkoa wangu upo au haupo? Hapa kuna matatizo makubwa, naomba Wizara yako itoe rai kwenye Manispaa kuwa watoto yatima wanalipiwa pesa hizo kwa wakati sio kuwanyanyasa, wanazungushwa mpaka wanakata tamaa, ni kwa nini pesa za misaada zisitolewe kwa wakati muafaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Watoto Yatima na Shule za Walemavu Albino. Mkoa wangu viko vingi sana angalau kutembelewa mara moja kwa mwaka inakuwa rahisi kujua matatizo wanayoyapata. Mambo mengi yasingekuwa yanatokea, naomba sana ujitahidi kufika Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia bajeti njema, kila la kheri Mungu awe nanyi, utekelezaji mwema, Vyuo vya Maendeleo vyote viko taabani.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupongeza kwa hotuba yako nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yako. Pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi – Chisalu. Kwa kuwa chuo hiki hakina usafiri, gari limeharibika zaidi ya miaka mitano, Serikali iliahidi kutoa Sh. 4,000,000/= kwa ajili ya matengenezo, je, kwa nini ahadi hii haijatekelezwa hadi sasa? Je, mwaka huu wa fedha wa 2009/2010, fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya ukarabati na uendeshaji wa Chuo cha Maendeleo ya Mwananchi – Chisalu, Wilayani Mpwapwa? Je Serikali ina mpango gani wa kukipatia Chuo hiki *computer* za kutosha, simu na umeme wa grid ya Taifa? Je Serikali ina mpango gani wa kuongeza idadi ya Walimu katika chuo hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii, kwa kuwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata na Wilaya, wanafanya kazi katika mazingira magumu ya kukosa vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri magari/pikipiki na maslahi duni, je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Maofisa hao kwa

kuwapatia vitendea kazi kama vile usafiri, kuboresha maslahi yao na kuwaendeleza kitaaluma?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka zake alizonijalia na kunilinda mimi na familia yangu. Pili, ningependa nimshukuru sana mume wangu Profesa E. Nkya, watoto wangu Febu, Manka, Jonas Manka na Petro wamekuwa wananipa nguvu sana katika kazi yangu hii kwa kuniombea pamoja na kunisaidia kwa kunipa ushauri wakati ambapo nahitaji ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jakaya - Mheshimiwa Mrisho Kikwete kwa kuonyesha juhudi kubwa sana ya kuwatumikia Watanzania kama alivyoahidi kwa nguvu zake zote. Rais huyu hapumziki kama hayuko nje kututafutia fedha, yuko Mikoani anahimiza maendeleo pamoja na kutoa maelekezo kwamba wananchi ni *number one* wasikilizwe na matakwa yao yatekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, amekuwa ni kiongozi mwenye mfano wa kuigwa katika kumsaidia Rais kwa kufanya kazi bila kuchoka hasa katika kuhimiza suala la maendeleo na kutetea Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Peter Mizengo Pinda. Huyu Mheshimiwa Waziri Mkuu, anafanya kazi kama mchwa, kama tungeruhusiwa kusema hivyo. Huyu Mheshimiwa anaongoza vizuri, shughuli zote za Serikali, analiongoza hili Bunge letu Tukufu vizuri sana na inaonekana jinsi ambavyo anawatembelea wananchi kusikiliza kero zao na kuzitatua na umahiri wake wa kujibu maswali na kero za Waheshimiwa Wabunge katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wangu wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, amekuwa kama dada yangu, ananiongoza ananifundisha kazi, lakini zaidi ya yote kwa juhudi zake na umahiri wake wa kuhakikisha kwamba Wizara hii sasa inaonyesha mfano ambao ni chanya na sio hasi kama tulivyokuwa tunafikiriwa mwanzoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Bibi Mariam Mwafisi ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara yangu, anafanya kazi nzuri sana ya kuongoza watendaji wetu, ndiyo sababu inaonekana kwamba sasa hivi kazi inakwenda vizuri na ndiyo sababu hata hotuba hii imekuwa ni nzuri sana kwa sababu amekuwa anaonyesha ushirikiano mkubwa kweli. Nawapongeza na kuwashukuru watendaji wote wa Wizara

kwa sababu bila wao mimi na Mheshimiwa Waziri, tusingeweza kufanya kazi nzuri ambayo leo Waheshimiwa Wabunge wengi wametupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya pekee, mara nyingi sisi tunasahau wale wadogo ambao ndiyo wanatuwezesha kuzunguka na kufanya kazi. Naomba nimshukuru na kumpongeza dereva wangu, anaendesha gari vizuri na hajawahi kunifanya mimi niogope kusafiri. Nampongeza pia na Katibu Muhtasi wangu ambaye anafanya kazi vizuri na kuniongoza na kunishauri pale anapoona ninasita kufanya kazi. Mara nyingi tunawasahau hawa. *(Makofi)*

Pia natoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge hili Tukufu kwa kazi yake nzuri anayoifanya ya kuliongoza Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya pekee nakushukuru wewe, umekuwa ni mwanamke ambaye umependa sana kutusaidia sisi viongozi ndani ya Bunge lako tuweze kufanya kazi nzuri na tuweze kudhihirisha kwamba wanawake tunaweza. *(Makofi)*

Nawashukuru Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge wanatuongoza vizuri na wanafanya kazi nzuri na kwa umahiri mkubwa. Nashukuru sana Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii. Hii Kamati yetu imekuwa ni Kamati ambayo ni ya mfano wa kuiga. Sisi Wizara yetu haina rasilimali nyingi, lakini wanashauri wanasema fanyeni hili, fanyeni lile ili muweze kuishawishi Serikali ione umuhimu wa kuwaongezea fedha na matokeo yake yameonekana, tumeongezewa fedha kipindi hiki na kipindi kilichopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza na Mawaziri wenzangu ambao wamemaliza *speech* zao. Nawapongeza sana na kuwapa pole wale ambao mambo yalikuwa magumu, lakini niwapongeze Mawaziri wote kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye hoja. Ningependa kwanza niseme kwamba ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge wametoa hoja ambazo kweli zinajenga sana Wizara yetu. Naomba niseme kwamba kila hoja iliyotolewa hapa itakuwa na msukumo wa pekee kutuwezesha sisi tuweze kufanyakazi yetu kama tulivyoahidi na kuzungumza mbele yenu katika bajeti yetu ya leo Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia leo hoja ambayo inagusa watoto. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia sana suala la watoto wanaoishi mitaani. Ilifikia mahali mpaka hata Mbunge mmoja akasema jamani watoto hawazaliwi mitaani ingawaje sasa hivi kama hatutapunguza hili wimbi watazaliwa wengine mitaani. Wabunge ambao wamezungumzia juu ya ongezeko la idadi ya watoto wanaoishi mitaani na watoto hawa wanakosewa haki zao, wananyanyaswa, wanaishi kwenye mazingira magumu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhali, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Dr. Christina G. Ishengoma, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Eustace Katagira na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba hili ni tatizo. Naomba niseme kwamba hili tatizo linasababishwa na mambo mbalimbali ambayo nafikiri sisi wote tunayaelewa. Lakini la msingi hapa ni tatizo la umaskini. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba sisi kama Wizara tumetambua kwamba hatua muhimu ya kuweza kusaidia ni kuhakikisha kwamba hawa watoto tunawazuia wasitoke kule walipo kuja mijini kuja kuishi mitaani. Kinachotakiwa kufanyika ni kwamba tuboreshe mazingira ya maisha ya vijijini kwa kupambana na umaskini na kuhakikisha watoto wote wanakwenda shule na kuhakikisha kwamba kila kaya inakuwa na chakula cha kutosha ili watoto wasishawishike kukimbia nyumbani kwa sababu hawapati chakula. *(Makofi)*

Mikakati ya ziada ya Wizara ni kwamba Wizara yangu ikishirikiana na wadau mbalimbali, tunaendesha zoezi la kuwatambua watoto wanaoishi mitaani katika miji nane, ukiwemo Dar es Salaam, Arusha, Morogoro, Singida, Mbeya, Iringa, Dodoma na Mwanza. Nia na madhumuni ya zoezi hili ni kutambua kwamba ni watoto wangapi wako mitaani? Ni kwa nini wako mitaani? Mahitaji yao ni nini ili tuweze kutengeneza mkakati wa kuweza kuzuia hili tatizo na kuweza kuwasaidia wale ambao tayari wameshaingia mitaani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mwingine ni ule wa kutengeneza mkakati kazi ambao utatusaidia katika kutekeleza yale ambayo tumeyaona na kuyatambua katika huu utambuzi. Huo mkakati sasa hivi rasimu yake imeshakuwa tayari, tuliwahusisha wadau mbalimbali ikiwepo jamii, wakiwepo watoto wenyewe pamoja na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ambayo sasa hivi yanajishughulisha na kuwasaidia watoto wanaoishi mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwamba kama huu mkakati tukianza kuutekeleza ni kwamba hili tatizo la watoto wa mitaani litaanza kupungua kama inavyoonyeshwa kwenye ile miji ambayo tayari kuna huduma zinazotolewa kwa watoto wa mitaani. Kwa mfano, Mji wa Mwanza, Mji wa Morogoro, Mbeya pamoja na Mji wa Moshi na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa inazungumzia ukatili dhidi ya watoto na mimba za utotoni. Hoja hii inahusu akina baba wanaotelekeza watoto wao. Serikali iangalie kwa macho mawili katika eneo hili ili kuleta haki ya mtoto.

Waliozungumzia hili ni Mheshimiwa Mercy Mussa Emmanuel, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Haroub Masoud ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir pamoja Waheshimiwa Wabunge wengine. Tunalozungumzia hapa ni kwamba sasa hivi kuna rasimu ya sheria moja ya mtoto, pamoja na kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutekeleza mkakati

ambao sasa hivi ndio unajadiliwa wa kuangalia namna ambavyo watoto wanaopata mimba wanaweza wakarudishwa shuleni. Lakini la muhimu hapa tunahimiza na kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii ni malezi bora ya watoto pamoja na kushirikiana na *NGO* ambazo zinashughulikia hawa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine walilozungumzia ni hatua zinazochukuliwa na Serikali kuhakikisha tunapunguza tatizo la ukeketaji. Hili limezungumziwa. Lakini naomba kusema kwamba kweli ni tatizo, lakini limeanza kupungua sasa hivi katika maeneo mengine na sasa hivi linafikia kwenye asilimia 15. Wizara yangu ikishirikiana na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali wametengeneza sekretarieti ambayo sasa hivi inajumuisha na Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoa elimu katika ile Mikoa ambayo imeathirika sana katika tatizo hili ambayo ni Arusha, Singida, Dodoma, Kilimanjaro na Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne imekuwa ni sheria ya mtoto. Waliozungumzia hili ni Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Haroub Masoud, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Al – Shymaa J. Kwegyir, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o. Kama tulivyosema wakati tunajibu swali la msingi siku chake zilizopita ni kwamba sasa hivi rasimu iko kwenye *Cabinet Secretariat* na ninaamini kwamba muda siyo mrefu itakwenda kwenye Baraza la Mawaziri na mchakato utaendelea ili tuweze kuileta hiyo sheria katika Bunge Tukufu tuweze kuipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ni mapungufu ya sheria ya ndoa ya mwaka 1971 ambayo imezungumzwa na Wabunge kama watatu, naomba niseme kwamba sasa hivi Wizara ya Katiba na Sheria ikitushirikisha na sisi kama wadau, imeanzisha mchakato wa kupitia hizi sheria na ninafikiri muda sio mrefu italetwa katika Bunge lako Tukufu.

Jambo lingine kubwa ambalo wamezungumzia Waheshimiwa Wabunge ni ajira ya watoto. Serikali itamke kwamba ajira ya mtoto anayefanya kazi za ndani anapaswa kulipwa shilingi ngapi. Nafikiri sisi kama Serikali hatutaweza kutamka hilo kwa sababu bado tunashikilia kwamba mtoto yeyote chini ya miaka 18 hastahili kuajiriwa. Hivyo basi, hatutaweza kupata jibu la kutamka kwamba mtoto ambaye ameajiriwa nyumbani atalipwa shilingi ngapi kwa sababu anayemwajiri mtoto ni kosa la jinai.

Hoja nyingine ilikuwa ni watu wangapi tangu kupitishwa sheria ya utumikishwaji wa watoto wametiwa hatiani? Kuna sheria ya *Employment of Labour Act* Na.6 lakini mpaka sasa hivi sidhani kwamba kuna mtu ambaye ametiwa hatiani kwa sababu haya mambo yanafanyika kichini chini hata hawa watoto wenyewe ukiwaendea hawataki kuyazungumzia hayo. Lakini naomba kusema kwamba ni kosa la jinai, unaweza ukafungwa mwaka mmoja au ukapigwa faini ya shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kwamba Wizara imekuwa inatunga tu sera na kuzihamasisha haijaweza kutoa utekelezaji na kufuatilia

utekelezaji. Mwingine akaishia kusema kwamba naomba Serikali ijipange upya sasa ili mtoto aweze kupata *protection* kubwa.

Naomba kusema kwamba Wizara yangu sasa hivi inadurusu sera ya makuzi na maendeleo ya mtoto ambayo inamlinda mtoto kuanzia miaka *zero* mpaka miaka nane pamoja sasa hivi tunatengeneza hii sheria ya mtoto. Naomba kusema sisi tunatengeneza sera, tutatengeneza sheria, lakini naomba nieleze Bunge lako Tukufu kwamba mwenye jukumu la kusimamia malezi ya watoto wenye ulemavu pamoja na watoto ambao hawatendewi haki ni Ustawi wa Jamii, Idara ya Ustawi ambayo iko chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Naomba nitofautishe, sisi tunatengeneza sera kama Wizara, tunatengeneza pamoja na sheria; tunatengeneza mikakati ya utekelezaji, lakini utekelezaji na ufuatiliaji unakuwa ni chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na siyo Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba kwa kuwa Wizara inayoshughulikia maendeleo ya mtoto na makuzi, watoto nchini ni wengi, naomba hili liongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, yale ambayo sikupata nafasi ya kuyafanunua tutayafanunua na kuwaletea Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili nihitimishe hoja niliyowasilisha hapo asubuhi. Awali ya yote napenda pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi kwanza ya kutoa hoja asubuhi na hatimaye kupata nafasi ya kukamilisha jioni hii.

Pia ningependa kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia kwa namna ambavyo imetupa moyo sana sisi watendaji na viongozi wa Wizara hii. Aidha, tunashukuru sana kwa hongera mlizotupa zimetupa moyo wa kufanyakazi tunawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwanza kutaja majina ya Waheshimiwa Wabunge 71 ambao wamechangia. Wabunge 54 kwa njia ya maandishi na 17 kwa kauli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini hautahesabu muda wa kuyataja majina haya.

**NAIBU SPIKA:** Huo muda hautahesabiwa.

**WAZIRI MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Maida M. Abdallah Mbunge, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Asha Jecha, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Suzan

Lyimo, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Shally J. Raymond na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi. *(Makofi)*

Aidha, Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa njia ya maandishi ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Azzan Zungu, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Christopher Chiza.

Wengine ni Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Hemed Mohamed, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Zuilekha Y. Haji, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Florence S. Kyendesya, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Al-Shymaa J. Kwegyir, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kutoa maelezo ya jumla katika maeneo mbalimbali yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatatavyo:- Lakini nakiri tangu mwanzo kwamba kutokana na uzito wa hoja, sio rahisi kujibu zote. Kwa hiyo, natanguliza kuomba radhi kwamba iwapo muda utakwisha kabla sijamaliza kujibu hoja zote, naomba radhi na kwamba naahidi tutatoa majibu kwa maandishi kwa hoja zote zilizotolewa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Tuanzie na upungufu mkubwa wa watumishi. Hili limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge sana Mheshimiwa Dr. Ishengoma, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Charles Keenja na wengine wengi ambao kwa bahati mbaya inawezekana sikuwataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosikia katika maelezo ya Waheshimiwa Wabunge, Maafisa Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana. Kama alivyoelezea Mheshimiwa Keenja, ni kwamba wao ndio wanaotafsiri sera mbalimbali za kimaendeleo

na kuzirahisisha ili wananchi wazielewe na kwa hiyo, kuwasaidia kuzitafasiri katika mazingira yao. Aidha, kuelewa sera zilivyo na kuwasaidia kubuni miradi ndani ya mazingira yao ambayo inawasaidia katika kujiletea maendeleo yao binafsi na Taifa kwa ujumla.

Kwa hiyo, ni kweli kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwa na Maafisa Maendeleo ngazi hasa ya Kata. Tunao Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Mkoa ambao wanafanya kazi vizuri, hali kadhalika tunao ngazi ya Wilaya, lakini tunaowahitaji sana ni wale walioko katika ngazi ya Kata. Wao ndio wanaweza kusaidiana na wananchi katika maeneo yao kubuni miradi ya maendeleo.

Kwa hiyo ni kweli sasa hivi tuna upungufu wa asilimia 57 wa maafisa hao katika ngazi ya Kata. Tunao asilimia 43 tu. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii, kutoa wito kwa Halmashauri zote kwamba, waajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nirudie maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliyoyatoa tarehe 06 Desemba, 2008 tukiwa Chuo cha Tengeru kwamba, Halmashauri zote ziajiri Maafisa Maendeleo ngazi ya Kata. Tusisahau kuwa, hawa ndiyo wanaoweza kuharakisha maendeleo katika sekta zote. Ninashakuru maagizo yalipotolewa tulikuwa na Mheshimiwa Celina Kombani, ambaye naye alitilia mkazo na kutoa maagizo kwamba, Wakurugenzi na Viongozi wote wa Halmashauri, wasimamie jambo hili. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote mliopo hapa na ambao hawapo, mkahimize Halmashauri ziajiri Maafisa Maendelo ya Jamii ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, isiishie kuajiri tu, wawape nyenzo za kufanyia kazi na wawasaidie pia kujiendeleza kwa mafunzo ya juu zaidi, kwa sababu mambo yanabadilika kila siku. Zaidi ya yote, wawape fedha zao ambazo tangu mwaka jana wameanza kupewa. Katika kuzunguka tumekuta kwamba, Wakurugenzi wengine hawawapi fedha hizo. Mwaka jana, Serikali ilitoa shilingi milioni 3.6 ili kuwawezesha Maafisa Maendeleo ya Jamii wafanye kazi yao, lakini hawakuwapa. Mwaka huu nashukuru Serikali imetoa shilingi milioni 7.2 kwa kila Halmashauri, kuwawezesha hawa wafanye kazi, watembee, wahamasishe, lakini bahati mbaya sana Wakurugenzi wengine hawawapi. Kwa hiyo, ningeomba kusisitiza kwamba, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Maafisa Maendeleo ya Jamii wawape ili waweze kufanya kazi nzuri ya kuhimiza maendeleo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mikopo ambayo ni ya kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, kwa Kiingereza *Women Development Fund* (WDF), inakwenda kwa Wilaya zinazoomba. Kwa, hiyo natoa wito kwa Halmashauri kuomba, lakini kwa masharti kwamba warudishe, wakirudisha wanaongezewa nyingine. Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na mimi, tunashiriki katika Vikao vya Halmashauri, tuulizie mikopo hii imekwenda wapi. Napenda kutoa mfano mzuri niliouona; Mheshimiwa Mbunge mmoja anasema tutoe mfano wa wapi Mfuko huu umesaidia. Napenda kutoa mfano ndani ya Bunge lako Tukufu; nilikwenda Mafinga walinipokea vizuri wakasema twende ukaone jinsi Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake unavyofanya kazi. Wakanipeleka kwenye kikundi cha akina mama, ambacho wanafuga ng'ombe, nguruwe, kuku na baada ya hapo wakaniambia twende ukaone matunda, yaani

fedha zile ambazo walipata akina mama wamezitumiaje. Tukaenda kwenye nyumba ya mama mmojawapo, ambaye ni mwanachama akanionesha fanicha akasema siku niliyoleta samani hizi kabati na viti, mume wangu alinishangilia sana. Kwa hiyo, Mfuko huu una faida kutokana na jinsi nilivyoona Mafinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba zile Halmashauri ambazo hazijaomba ziombe, lakini Waheshimiwa Wabunge, tufuatilie wapi hizi fedha zinakwenda na baada ya hapo tuendelee kuongeza ili fedha ziwe nyingi zaidi kwa kukopesha akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, ningechukua mfano wa Mafinga huko huko. Nilifurahi sana kwamba, wao kwa kuthamini Maafisa Maendeleo ya Jamii, wameajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kila sekta. Yuko Afisa Maendeleo ya Jamii anayeshughulikia kilimo, mwingine afya, mwingine maji na mwingine UKIMWI. Nilifurahi sana, nikasema kumbe ziko Halmashauri ambazo zinathamini kazi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini, kuthamini kazi ya taaluma hii ya Maendeleo ya Jamii ili kusukuma maendeleo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa pia suala la ushiriki wa wanawake kwa asilimia hamsini kwa hamsini katika ngazi ya uongozi, utendaji na ngazi za maamuzi. Suala hili limechangiwa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangaro, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Fatma Mikidadi na Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy. Hatuwezi kufikia asilimia hamsini kwa hamsini kama watoto wetu wa kike wataishia shule za msingi, kutokana na tatizo tulilonalo. Ili tufikie asilimia hamsini kwa hamsini katika ngazi ya utendaji, lazima watoto wa kike wasome. Kwa hiyo, natoa wito kwa jamii nzima; ili kufikia asilimia hamsini kwa hamsini ya uwakilishi katika nyanja mbalimbali, lazima watoto wa kike wasome. (*Makofi*)

Sasa hivi tuna tatizo kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge kwamba, watoto wa kike wanapata mamba, kwa hiyo hawaendelei. Kuna takwimu ambazo zilioneshwa katika kipindi fulani, wasichana 18,000 walipata mimba. Mimi natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wote wapenda maendeleo, suala hili litakapoletwa kwa ajili ya uamuzi wa kurudisha watoto wa kike kuendelea na masomo baada ya kujifungua tuliunge mkono, kwa sababu wako wengine wamelipinga hata humu ndani Bungeni, lakini wanasahau; ukipanda ndege dakika 15 tayari umefika Zanzibar, wana sheria ambayo inaruhusu mtoto wa kike aliyezaa kurudi shuleni kuendelea na masomo. Mimi naamini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inalifanyia kazi. Ombi langu ni kwamba, muda muafaka utakapofika, liungwe mkono ili watoto wa kike waweze kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila elimu hatuwezi kufikia asilimia hamsini kwa hamsini hasa katika ngazi ya utendaji. Kwa upande wa siasa, pamoja na umuhimu wa elimu lakini tunaweza. Nachukua nafasi hii, kuwaomba akina mama wote wasiwe waoga, wajitokeze kugombea uongozi katika nafasi zote kuanzia uchaguzi utakapofanyika mwezi wa kumi katika ngazi za Serikali ya Mtaa, Vitongoji na Vijiji wajitokeze. Nawaomba akina baba muwaunge akina mama mkono kama mlivyomuunga

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, pamoja na mwenzetu kule Zanzibar, kwa kudhihirisha kwamba, akina mama wakipewa nafasi wanaweza.

Mila na desturi zinawafanya wanawake wajisikie wanyonge. Suala hili la kuhimiza watoto wa kike kusoma ni letu sisi sote, naomba tulivalie njuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ya kwamba, pengine Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, inapata fedha kidogo kwa sababu haina programu. Nataka nikuhakikishie kwamba, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ina programu ambazo nyingine tayari zimeshapata baraka za ngazi ya juu ya maamuzi, iliyobaki ni kwamba, tuendelee kufuatilia. Tlishaandaa mkakati wa kuboresha Sekta ya Maendeleo ya Jamii na tulishawasilisha kunakopaswa, jambo la muhimu nadhani ni kufuatilia ili Sekta hii hasa kwa kupitia Wizara yangu, iendelee kupewa mafungu zaidi. Tumeona mwaka huu, naamini miaka ijayo pia Serikali itazidi kuongezea fedha za bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na suala la ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Vyuo hivi ni kweli viko katika hali mbaya, lakini kuanzia mwaka jana Serikali imekuwa ikitenga fedha kama mtakavyoona kwenye vitabu vya maendeleo. Kuna zaidi ya shilingi bilioni mbili ambazo zimetengwa kwa mwaka huu. Lengo lake ni kwamba, tunachukua vyuo vichache tunafanyia ukarabati wa uhakika na ninaamini Serikali itaendelea kutoa fedha mwaka hadi mwaka ili vifanye kazi iliyokusudiwa ya kutoa ufundi na kuwezesha watu kijiajiri na kuajiriwa. Kwa hiyo, wale ambao kwa bahati mbaya wataona vyuo vyao havimo katika mpango wa mwaka huu, wavute subira mipango ijayo itazingatia mahitaji ya vyuo ambavyo bado havijafikiwa. Hoja hii ilichangiwa sana na Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Komba, Mheshimiwa Mfaki na Mheshimiwa Mntangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii, kujibu kwa kifupi sana kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Malya. Mimi nimetembelea kule, sasa hivi ukarabati unaendelea vizuri sana. Kitu kikubwa ambacho ningesisitiza hapa ni kwamba, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Wakurugenzi wa Halmashauri husika ndiyo Wenyeviti. Kwa hiyo, natoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, waangalie jinsi ya kuvisaidia hivi vyuo. Kwa mfano, nilipokwenda Malya nilikutana na Mkurugenzi, akaahidi mambo mengi ambayo yatasaidia pale. Matumizi ya eneo hili ni uamuzi wa eneo husika, kwa kushirikiana na Wizara yetu. Kwa mwaka huu wa fedha, mtaona kwenye vitabu tuna kama shilingi milioni 300 ambazo tumetenga kwa ajili ya vyuo hivi kufanyiwa utafiti ili vitoe mafunzo kulingana na mahitaji ya maeneo husika, kwa sababu vinahudumia watoto, vijana na watu wazima walioko katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la msingi lilikuwa ni kuhusu vifo vya watoto na akina mama. Suala la vifo vya watoto na akina mama, linahitaji ushirikiano wa sekta zote. Tukichukulia mfano mzuri ambao tuliuona juzi; Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, pamoja na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, walikutana wakaona kuna umuhimu wa kuunda kikundi kidogo cha Waheshimiwa

Wabunge, ambacho kitasaidia kuangalia namna gani Bajeti zinapoandaliwa zinavyotengenezwa kwa namna ambayo itasaidia rasilimali zile kuwafikia wote wanaume na wanawake. Maana yake ni kwamba, Bajeti zinazoandaliwa ziwe na mtazamo wa kusaidia au kuwafikia pia akina mama, zisilenge kufikia pengine wanaume tu au wanawake tu, lakini ziwafikie wote.

Ukichukulia hili suala la vifo vya akina mama na watoto, linataka sekta zote kushirikiana. Kwa mfano, mama anapofariki anaweza akawa amefariki pengine kutokana na bahati mbaya kule nyuma lishe haikuwa nzuri au kwa bahati mbaya hakupata kinga au chanjo mbalimbali au hakupata matunzo mazuri ndani ya familia yake. Ni mambo mengi ambayo yanasababisha vifo. Kwa hiyo, linahitaji msaada wa sekta zote kwa pamoja. Kwa mfano, Sekta ya Kilimo; Kilimo Kwanza, kilimo kikiwekewa makazo kama inavyoonekana mwaka huu wa fedha, watu watapa chakula zaidi, lishe itakuwa nzuri na akina mama watapata nguvu.  Wakati huo kwa mpango wa maendeleo ya afya, itabidi vituo vya afya vijengwe zaidi wanawake wakapate kinga zao, chanjo zao, hali kadhalika watoto. Kwa hiyo, unapozungumzia vifo vya watoto na akina mama, unagusa sekta nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo wamefanya Waheshimiwa Wabunge, ambalo nawapongeza sana siku ya leo ni kuunda Kamati yao Ndogo ambayo inaitwa Kamati ya Kutoa Chachu ya Waheshimiwa Wabunge ya kuangalia ni jinsi gani ambavyo bajeti zinavyoandaliwa zinagusa jinsia zote.  Kwa mfano, Bajeti ya Afya vipi imegusa maeneo ambayo itamsaidia mama na mtoto au kama ni Bajeti ya Kilimo vipi ambavyo pengine pembejeo zitamfikia mwanaume na mwanamke.  Cha maana ni kwamba, rasilimali ziwanufaishe wote; wanaume na wanawake.  Kwa hiyo, maeneo kama haya ya vifo vya watoto na akina mama, yatiliwe mkazo zaidi katika maandalizi ya Bajeti.

Ninaamini kuwa, kikundi kile kilichoundwa na Waheshimiwa Wabunge, kikifanya kazi yake utaona hata mtazamo wa Bajeti utabadilika. Wizara kwa mwaka huu wa fedha wa 2009/2010, tutaomba kibali maalumu cha kukaa na Makatibu Wakuu ili tuone ni jinsi gani ambavyo wanaweza kuhakikisha Bajeti zinazoandaliwa zinaenda kusaidie pia makundi maalumu wakiwemo akina mama na watoto, ilimradi rasilimali za nchi ziguse maeneo au vikundi mbalimbali vyenye mahitaji maalumu. Naamini kabisa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, atatuтуhusu ili tuwe na kikao na Makatibu Wakuu, kuona jinsi ya kuandaa bajeti zinazotilia maanani vikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto, suala hili limezungumziwa na wengi; Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Nuru Bafadhil, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya; kwamba hivi hii kampeni mwisho wake nini?  Inazaa matunda; mbona watu wanaendelea kufariki, albino wanaendelea kuuawa?  Nataka kusema, suala la kuzuia ukatili dhidi ya wanawake, watoto na maalbino na ukatili wa aina yoyote wa kijinsia, linatutegemea sisi sote Watanzania, hasa kwa kuelimishana kuachana na mila potofu, zilizopitwa na wakati, pia kuelimishana kuwaumbua au kuwatambua na kutoa taarifa juu ya wale wote wanaojihusisha na ukatili wa kijinsia na unaogusa moja kwa moja wanawake, watoto na

maalbino. Tukiwaumbua, tukiwafichua na tukitoa taarifa, mimi naamini kabisa, kampeni hii ya kukataa ukatili dhidi ya wanawake, watoto na maalbino, itafanikiwa lakini kwa nguvu zetu sisi sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumziwa sana ni umuhimu wa NGOs. Jambo la msingi ni kwamba, NGOs zinasaidia sana juhudi za Serikali za kuleta maendeleo nchini. Tunazishukuru NGOs nyingi kwa kufanya kazi vizuri. Kwa NGOs zile ambazo hazifanyi vizuri ni wajibu wetu sisi sote Watanzania kuzifichua na hasa baada ya kuzindua tovuti ambayo nimeitaja asubuhi; *www.tnnc.go.tz;* hii itatusaidia sisi wote kufungua internet na kuona NGOs tulizonazo, zipo wapi, zinafanya nini na zile ambazo mtaona hazieleweki tunaomba mtoe taarifa, kwa sababu NGOs ni nyingi mno na sasa hivi tunatoa wito ziende vijijini. Wanaoweza kutusaidia hasa zile ambazo hazifanyi kazi vizuri ni sisi Watanzania tushirikiane, hii Wizara peke yake haiwezi. Naomba ushirikiano kwa Watanzania wote. Kwa NGOs zinazofanya kazi vizuri, nazipongeza na ziendelee kufanya kazi hasa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo lilizungumziwa sana ni la uwezeshaji na uanzishaji wa Benki ya Wanawake. Hili limezungumzwa na Mheshimiwa Capt. Komba, Mheshimiwa Getrude Lwakatare, Mheshimiwa Mgeni Kadika, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Chiza, Mheshimiwa Sakila na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma. Wamezungumzia sana kuhusu umuhimu wa Benki. Wakati wowote, naamini kabla Bunge halijaisha, Benki itakuwa imeshaanza na tutatoa kauli ya Serikali humu Bungeni na nitawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, mkafungue akaunti zenu huko, kwa sababu Benki hii tunaitegemea sana hasa katika kutoa mafunzo ya ujasiliamali, unaoweza kuwasaidia akinamama wainue maisha yao, lakini pia maisha ya familia na taifa kwa ujumla.

Waheshimiwa Wabunge, walionunua hisa naomba waongezee na wale ambao bado mkanunue hisa, kwa sababu Benki hii naamini itakuwa na manufaa sana katika kuleta maendeleo nchini hasa kwa akina mama ambao wengi wako katika hali duni kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hoja nyingine ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, ambazo nitazitaja kama muda utaruhusu, lakini kama hautaruhusu basi naomba mniwie radhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hoja ambazo sikuzizungumzia katika hoja za jumla, lakini pia zimezungumzwa. Waheshimiwa Wabunge, hasa kwa kupitia Kamati ya Maendeleo ya Jamii, wamezungumzia umuhimu wa SACCOS. Sasa sisi tunasema, ushauri ni mzuri kwamba, SACCOS zifunguliwe nyingi kadiri iwezekanavyo, kwa sababu zitasaidia sana katika kuleta maendeleo ya akina mama, ambao kwa mmoja mmoja si rahisi kupata maendeleo ya kiuchumi bila kuungana na wenzake. Pia walizungumzia suala la Serikali kujitoa katika Benki ya Wanawake. Serikali itaendelea kujitoa katika Benki ya wanawake kadiri ambavyo hisa zitakavyoendelea kununuliwa. Ndiyo maana nimeomba Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla, tununue hisa

za Benki ya Wanawake ili pole pole Serikali ijitoe baada ya hisa zote kununuliwa na kumilikiwa na watu binafsi na hususan wanawake na akina baba ambao wataunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitoa shilingi bilioni 2.9 kwa lengo la kuanzisha tu, lakini baadae itajitoa. Pili, ilikuwa kwamba, Wizara iandae mkakati wa kuwezesha kuinua akina mama ili waweze kuepukana na Ugonjwa wa UKIMWI. Kwa sasa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kushirikiana na TACAIDS, inaendesha mapambano dhidi ya UKIMWI, kwa kutoa elimu ndani ya vyuo na wananchi wanaozunguka Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii, pamoja na Vyuo vya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine wamesema kwamba, Benki ifungue dirisha la uwezeshaji wanawake wakulima. Benki itafanya mambo mengi kadiri ambavyo itakuwa ikikomaa. Mwanzoni, inawezekana isiweze kukidhi mahitaji yote, lakini kadiri ambavyo itakuwa ikiendelea kupata uwezo inaweza. Ilizungumzwa pia na upande wa Kambi ya Upinzani kwamba, kwa nini imeanzia Dar es Salaam tu. Nadhani sisi sote ni mashahidi; Benki nyingi zinaanzia Dar es Salaam, baadaye jinsi zinavyokua zinafungua matawi mengine. Kama tulivyoona ile *Community Bank* ya Wakazi wa Dar es Salaam, sasa hivi imeanza kufungua matawi kwingine na sisi tunaamini Benki ya Wanawake wa Tanzania, ikishapata nguvu itafungua matawi sehemu nyingine za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo Mheshimiwa Mkanga alilizungumzia ni watendaji wasichoke kuwahimiza wanawake wenye ulemavu kujiunga pamoja ili wapate mikopo ya kujikwamua kiuchumi. Ni kweli ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri na mimi natoa wito hasa kwa tunaotegemea Maafisa Maendeleo ya Jamii na sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge, tuwashawishi wenzetu wenye ulemavu wajiunge, siyo peke yao tu pia wajiunge na watu wengine ili waweze kujikwamua kwa kupata mikopo na kujiendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ilisemwa kwamba, Wizara iweke utaratibu maalum wa kuwawezesha wanawake wajane. Suala hili ni la kwetu sisi sote kuanzia Halmashauri, Wizara na wala si suala la Wizara moja au Serikali Kuu tu, hata Halmashauri inaweza ikaweka utaratibu wa kusaidia wajane kwa kuwapa mikopo ili waweze kuishi vizuri. Pia kulikuwa na suala la Baraza la Wanawake, ambalo litahusisha wanawake wa itikadi zote. Suala hili bado linafanyiwa kazi, lakini naamini kabisa hapo baadaye itawezekana kuwa na Baraza ambalo litakuwa si la itikadi, bali litashughulikia masuala yanayohusu maendeleo ya akina mama na haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema si rahisi kujibu yote; labda nimalizie la mwisho kuhusu Sheria ya Mtoto. Sheria ya Mtoto, ilizungumziwa kwa uchungu sana na Mheshimiwa Maria Hewa. Mimi nachelea kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kusema kitu ambacho sina uhakika nacho na kama nitakuwa nimesema kitu ambacho sina uhakika, niko tayari kuja kukifuta mbele ya Bunge lako Tukufu. Nimesema katika mwaka huu wa fedha, kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, tutaletea hapo baadaye Sheria ya Mtoto, ambayo itaangalia haki za msingi za mtoto ili azipate.

Kuhusu Sheria nyingine za Ndoa na Mirathi, nadhani suala hili linashughulikiwa kwa sasa hivi na Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa sasa hivi sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, tunashughulikia suala la Muswada wa Sheria ya Mtoto, ambayo itazungumzia haki za mtoto. Mengine hayo yatakuja kwa utaratibu, lakini kwa mwaka huu wa fedha, Sheria ambayo tunatilia mkazo ni hiyo ya haki za mtoto. Kwa hiyo, naomba tuvute subira, itakapokuwa tayari italetwa. Sasa hivi iko katika ngazi nzuri tu na hatimaye italetwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kurudia niliyosema pale nilipoanzia; kwanza, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana. Yapo ambayo yametolewa na Kambi ya Upinzani, ambapo kwa asilimia kubwa tumeshayatekeleza, lakini kwa yale ambayo hatujayatekeleza tutayafanyia kazi. Kwa upande wa Kamati ya Maendeleo ya Jimii, ushauri mwingi tutauzingatia na maelekezo yote waliyotoa kwa sababu wao ndiyo wanaotushauri na hatimaye kufanya kazi tunayoifanya. Kwa Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa michango yenu, tutaizingatia na tutaleta kwa maandishi hoja moja baada ya nyingine ili muone tutakavyozijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nakupongeza wewe kwa kazi nzuri, tunajivunia kuwa na mama wa ngazi yako, kwingine hakuna. Pia nakushukuru jinsi ambavyo unafanya kazi karibu na Mheshimiwa Spika, hapo ndipo ninapokupendea. *(Kicheko*)

Hali kadhalika, nawashukuru Wenyeviti wa Bunge, ambao wanampa msaada mkubwa sana Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kupata ushauri. Naomba kutoa hoja. *(Makofi*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

Kif. 1001- *Administration and General* … … … .. …. Sh. 2,453,580,600

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM**: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, ninataka kupata ufafanuzi; baadhi ya watoto wako magerezani, wengine wakiwa wafungwa na wengine ni mahabusu. Wanakosa haki zao za msingi za elimu, lakini pia wanakosa maadili ya kiroho. Kwa kuwa suala hili ni la mtambuka; je, Wizara ina mkakati gani wa kuwapatia haki yao ya msingi hiyo? Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Haki ya kufanyaje?

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM**: Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya kupata elimu na maadili ya kiroho wakiwa magerezani.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, watoto wanapokuwa kifungoni kwa taarifa niliyonayo ni kwamba, Maafisa Ustawi wa Jamii, huwa wanawasaidia kupata elimu wakiwa huko. Kwa hiyo, wanapata haki zao.

Njia nyingine ni ile ile ya kukata rufaa ili kama mtoto ameonewa basi atoke, lakini Ustawi wa Jamii wanalishughulikia suala hili kikamilifu sana.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Wakati anahitimisha hotuba, mara nyingi nimemsikia Mheshimiwa Waziri akizungumzia kwamba, Wizara yao iko katika mikakati mikubwa sana ya kuondoa unyanyasaji dhidi ya wanawake, watoto na maalbino. Nakiri kwamba, kuna tatizo *sensitive* juu ya maalbino. Nilikuwa naomba nipate ufafanuzi wa jina la Wizara yenyewe; walemavu sasa katika hali hiyo wanakuwa wako kundi gani? Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya kama ifuatavyo:-

Suala la watoto walemavu kupata haki zao ni la msingi kama wanavyopaswa kupata watoto wengine wowote. Nataka kusema kwamba, sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, tunashughulikia haki za msingi ili wapate watoto wote. Suala la kuwahudumia watoto wenye ulemavu, liko chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mnamo mwezi Aprili, 2009, tulifanya ziara na Mheshimiwa Waziri Wilayani Tarime na tulikitembelea Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Tarime; na kwa bahati na kwa masikitiko makubwa, tulijionea namna gani Chuo kile kilivyo chakavu, yaani kiko kwenye hali mbaya sana. Sasa nilitegemea Chuo hiki kwa mwaka huu wa fedha, kingekuwepo katika utaratibu mzima wa ukarabati mkubwa, jambo ambalo silioni. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa aliahidi Chuoni pale kwamba, katika mwaka huu wa fedha chuo kile kitafanyiwa ukarabati mkubwa na kinaonekana hakitafanyiwa ukarabati mkubwa; je, anasema nini kuhusu hilo? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Kinaitwa nini?

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Kinaitwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tarime.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri maelezo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Ahsante Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kumjibu Mheshimiwa Rosemary Kirigini kama ifuatavyo:-

Ni kweli tulikwenda kwenye Chuo cha Tarime; ni kichakavu. Mimi nilitoa masikitiko yangu tukiwa naye kwamba, kuna baadhi ya vitu ambavyo hata Halmashauri ingeweza kutusaidia na tulifuatana na Mheshimiwa Charles Mwera. Yako mambo mengine, ambayo tunaomba Halmashauri zisaidie na hili tulizungumza kwamba, kwa mfano, tenki la maji. Tarime pale pana tatizo la tenki, ambalo lilikuwa linahitaji ukarabati na kwa kukisikia, inaweza kufikia hata milioni ne hivi tukaomba kwamba, pale ambapo Wizara haijasaidia, Halmashauri itusaidie kwa suala kama hilo. Hata hivyo, kama nilivyotoa maelezo wakati wa kuwasilisha hotuba yangu hapa, maelezo yangu yalikuwa kwamba, tunatengeneza hivi vyuo kwa awamu.

Unapopata shilingi bilioni mbili, ukizitawanya kwa vyuo labda 20 au 30; si rahisi kufanya matengenezo ya maana. Kwa hiyo, ili kufanya matengenezo ya maana, hatutoi chini ya shilingi milioni 200 au milioni 250 kwa chuo kimoja ili kipate matengenezo ya uhakika. Kwa msingi huo, mimi ningeomba Mheshimiwa Mbunge, tuvute subira miaka haikawii, lakini kwa yale madogo madogo, naomba sana kwa heshima na taadhima, Halmashauri zitusaidie kama vile kutengeneza tanki la maji, ambalo tuliona ndiyo lilikuwa tatizo kubwa sana kwa wakati ule. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Wakati nachangia kwa maandishi, nilitaka ufafanuzi kwamba, kwa kuwa moja ya haki ya mtoto ni kupata elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu; kwa nini Wizara inachelewa kuleta mapendekezo ya kufuta Sheria zilizopitwa na wakati kama ile inayozuia mtoto kukariri darasa la saba kwa sababu ni Sheria ambayo inamgandamiza mtoto bila sababu kwa kipindi hiki?

**MWENYEKITI:** Jamani siyo Wizara ya Elimu hiyo, ninafikiri ni suala la Wizara ya Elimu na mwenyewe kalisikia; haya kama unataka kujibu Waziri wa Elimu. Ataisoma katika hotuba yake.

**MHE. DKT. LUKA J. SIYAME:** Ahsante Mwenyekiti. Kwa muda mrefu, Wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi hususan akina mama na watoto, wamekuwa wakiwalalamikia viongozi wa ngazi za juu kwa kutokuwatembelea ili kuwahamasisha kwa shughuli za maendeleo na uchumi; na Mheshimiwa Waziri ni mtoto wa kule Mbozi Magharibi; je, anaweza kuwahakikishia Wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi ni lini atawafikia na kuwahamasisha kwa sababu sasa hivi amekuwepo kwenye uongozi kwa miaka takriban minne?

**MWENYEKITI:** Mtoto wa Tanzania huyo, Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kumjibu Mheshimiwa Dkt. Siyame kama ifuatavyo:-

Kwa kweli ukiwa Waziri, unapaswa uifahamu Tanzania nzima. Kwa hiyo; ni suala la muda tu, katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, tumetembelea sana Mkoa wa Singida karibu vyuo vyote; Mwanza tumepita sana Malya, Malampaka na sehemu nyingine; Shinyanga mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri. Tulichoongea mimi na Naibu Waziri ni kwamba, tunapangana sasa katika mwaka huu wa fedha tunaelekea sehemu nyingine. Mimi mwenyewe kwanza, nitakwenda Rukwa na huko kwingine. Halafu na Naibu Waziri naye, ana mpango wa kwenda huko. Sasa hivi tutakwenda upande huo. Ni suala la kupata muda tu, lakini napaswa kuitembea nchi nzima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wenzako wanasema lini utakuja kututembelea wewe unasema utahamasisha! Yeye mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Siyame. *(Kicheko)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo tu; mwaka 2006/2007 Serikali iliahidi kukipatia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu, shilingi milioni nne kwa ajili ya kukarabati gari ambalo liko juu ya mawe; na 2007/2008 vile vile iliahidi; hadi sasa hizo milioni nne hazijafika na hilo gari liko juu ya mawe Chuo hicho hakina gari; je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu kukisaidia Chuo cha Maendeleo Chisalu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri maelezo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwa kuokoa gari tutaangalia, kama itazidi milioni nne, pengine inaweza kutupa matatizo, lakini kama ni milioni nne, mimi naamini Wizara inaweza kutoa kwa ajili ya gari la chuo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* … … Sh. 526,737,682.00
Kif. 1003 – *Policy and Planning* … … Sh. 545,877,600.00
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* … … … Sh. 222,994,000.00
Kif.1005–*Info, Education and Communication Unit* ...... ...... ..... . ...... ...... Sh. 137,300,000.00
Kif. 1006 – *Procurement Unit* … … … Sh. 266,649,000.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Training and Folk Development*

*Colleges* … … .... ..... .... ..... ..... Sh. 5,132,848,082.00

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho, vifungu vidogo 230200 mpaka 411000. Vifungu hivi vidogo vinahusu matengenezo na havikupewa fedha. Sasa vyuo hivi vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vitatengenezwa vipi kama katika kifungu hiki hakuna pesa zilizotolewa? Matengenezo ya namna hiyo yanatumia *Recurrent Budget*, kwa hiyo, hatutarajii kwamba, zitakuwa katika *Development Budget.* Naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Umekipata kifungu chenyewe? Hebu rudia tena Mheshimiwa kwa utaratibu.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 2001.

**MWENYEKITI:** Programu 20?

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** 2001.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Vifungu vidogo 230200 mpaka 411000; vifungu vyote hivyo vinahusu *maintenance and rehabilitation* na vyote havikupewa fedha. Sasa tutatengenezaje hivi vyuo ambavyo vinahitaji kupewa fedha za *recurrent* ili viweze kufanyiwa matengenezo?

**MWENYEKITI:** Umeona Mheshimiwa Waziri? Haya tafadhali maelezo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kuhusu suala la Mheshimiwa Keenja ni kwamba, kwanza, kuna fedha kidogo ambazo zinakuja kwenye Idara. Pamoja na kwamba, Mheshimiwa anasema haziko kwenye Maendeleo, utakuta kuna matengenezo madogo madogo kama ilivyo kwenye majedwali husika, ambako tumeonesha vyuo ambavyo vitapata matengenezo makubwa na vyuo ambavyo vitapata matengenezo madogo. Kwa hiyo, kuna fedha ambazo zitawasaidia.

**MWENYEKITI:** Kwa maana hiyo ziko kwenye *Development* na siyo kwenye *Recurrent?*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Zipo kwenye *Development*.

**MWENYEKITI:** Ziko kwenye *Development* na hii ni *Recurrent?*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Ndiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Community Development* … Sh. 2,595,525,000.00
Kif. 2003 – *Community Development College – Tengeru* … .... ..... ..... ..... Sh. 721,233,276.00
Kif. 3001 – *Gender Development* … … Sh. 920,171,000.00
Kif. 3002 – *Children Development* … … Sh. 594,904,640.00
Kif. 4001 – *Non-Government Organizations* … Sh. 431,460,120.00

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

Kif. 1001 – *Administration and General* … Sh. 1,956,253,823.00
Kif. 1003 – *Policy and Planning* … … Sh. 767,396,177.00
Kif. 2001 – *Training and Folk Development Colleges* ..... .... .... .... .... .... ...... ..... Sh. 3,035,777,000.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Community Development* … … Sh. 607,480,000.00

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya, wanasema usimame. *(Kicheko)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Nilikuwa naomba katika kifungu hiki cha 2002 kifungu kidogo cha 6532 – *Self Help Projects.* Nimeona hapa kuna milioni 130 tu na nimeangalia pia kwenye Mradi wa Artisan Development Agency of Tanzania (ADAT), uliopo kwenye Ripoti yao, mwaka jana walifundisha watu 40 na mwaka huu ni 50 tu, lakini mafunzo yao ni ya muhimu sana. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami ni vyema sasa tukiangalie hiki kifungu ili kiweze kuwafikia hata wananchi ambao wako vijijini badala ya mafunzo mengi kutolewa katika maeneo ya mijini?

**MWENYEKITI:** Wewe ungesema hizi hela ni za kazi gani, maana huwezi kujua kama ni za mjini au vipi. Mheshimiwa Waziri anauliza hizi hela ni za kazi gani; je, vijijini zitahusika?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya kama ifuatavyo:-

Kifungu hiki cha 6532 hiyo milioni 130 ni ya utafiti wa teknolojia za kuleta maendeleo vijijini. Sasa ukiangalia kwa upande wa Vyuo vya Maendeleo, katika Kitabu cha Hotuba, tumeonesha kwamba, tutatafuta teknolojia rahisi zitakazosaidia kilimo kutokana na msimamo wa Serikali sasa hivi wa Kilimo Kwanza. Kwa hiyo, tunategemea hiyo milioni 130, itasaidia teknolojia kama vile kununua matrekta, kununua wanyama kazi na tutaiunganisha pamoja na 6229 na 4312.

Kwa hiyo, jumla itakuwa milioni 430 ambazo ukiangalia ndani ya hotuba, tumezitenga kwa ajili ya teknolojia ya kusaidia watu wa vijijini hasa wanawake kwa kununua matrekta yanayoendeshwa kwa mkono, yaani *power tillers* na wanyama kazi kwa ajili ya Vyuo kufundishia wakulima katika Vyuo vya Wananchi ili wajifunze kutumia teknolojia. Kwa upande wa (ADAT) anayoizungumzia, inayowasaidia akina mama wajane kwa upande wa UKIMWI, yenyewe iko kwenye suala la UKIMWI. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, unasema tumepita lakini kifungu kile 4312.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Zinachanganywa pamoja. Hizo ni fedha za msaada toka Canada, unalenga suala hilo hilo la kusaidia utafiti wa teknolojia ya kusaidia watu kujiletea maendeleo kwa urahisi hasa vijijini. Tumeamua kwamba, zitasaidia katika teknolojia inayohusiana na kilimo. Kwa hiyo, kwenye vitabu ukiona 430 katika hotuba ni kwamba, hii 300 pamoja na 130 inakuwa 430. Teknolojia rahisi ya kusaidia akina mama wapunguziwe mzigo wa kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 – *Community Development College*
– *Tengeru* ... .... .... ..... .... .... ..... ..... Sh. 400,000,000.00

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 – *Gender Development* … … Sh. 255,295,000.00

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nasikitika kwamba, *last time* nilisimama lakini hukuniona. Niko katika *Sub-Vote 4943,*

kwenye suala zima la *Women Economic Empowerment Project.* Ni wazi kwamba, tumesema wanawake wakiwezeshwa wanaweza, lakini hakuna fedha kabisa. Nilikuwa naomba kujua Mheshimiwa Waziri anatuambia nini hasa ikizingatiwa kwamba sasa hivi tunakwenda kwenye chaguzi za Serikali Mitaa na tunahitaji sana akina mama waweze kushiriki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umekiona kifungu chenyewe hicho? Haya eleza tu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Kifungu hicho kimepata sefuri. Naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba, sisi tumeiona hiyo kama Wizara na kwa msingi huo, tukawaomba wenzetu wa *European Union (EU)* na wakakubali kwamba, watatupa msaada wa fedha wa kama shilingi milioni 500 kwa ajili ya kampeni ya kukataa ukatili dhidi ya watoto na albino, yaani kuendeleza ile kampeni halafu nyingine zitakwenda kuwawezesha akina mama kiuchumi na kisiasa. Ndiyo maana ndani ya hotuba tumezungumzia kuhusu uanzishwaji wa Vituo vya Biashara kwa kuanzia na Mkoa wa Dar es Salaam na hatimaye mikoa tisa kutokana na msaada huo wa *European Union.*

Kwa hiyo ni suala ambalo Wizara ya Fedha inalijua kwamba, tutapata fedha hizo. Sasa hivi zinashughulikiwa ili zitoke tuanze kazi. Kwa hiyo, naomba nikutoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge; suala la *Women Economic* na *Political Empowerment* limefanyiwa kazi. Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 – *Children Development* … …. … Sh. 123,100,000,00

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipatia nafasi. Nadhani Wabunge wengi na wote tunatambua, jinsi ambavyo kumekuwa na *child abuse.* Vile vile tume…

**MWENYEKITI:** Tunakwenda kwa kifungu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** *Sub-Vote 4305* na ile inayofuata ya 5414 na ile ya mwisho 5415. Ukiangalia vifungu vyote hivi, havijapewa fedha kabisa. Sote tunasema kwamba, tunatetea haki za watoto na tunajua jinsi ambavyo watoto hawa wanapata matatizo na tulijua kabisa kwamba, wanapopata zile *life skills* watoto hawa baadaye kuja kuwa watu wazuri, lakini tukiangalia vifungu vyote hivi havijatengewa fedha. Kwa hiyo, nilikuwa naomba pia Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, lazima umehamishia mahali, toa maelezo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Kuhusu suala hili aliloulizia Mheshimiwa Susan Lyimo, nilikuwa nataka tu kumtoa Mheshimiwa Mbunge wasiwasi kuhusu suala la utafiti na jinsi ya kumsaidia mtoto. Tumeweka katika kile kifungu cha 5414, ndiyo itakayofanya kazi hiyo.

Pia sisi tumekwenda zaidi ya hapo, tumeomba kwa kupitia Ubalozi wa Uingereza, wenzetu wa *International Street Children Consortium* ambao tunafanya nao utafiti kuhusu watoto wa mitaani na tulikuwa nao Morogoro tarehe 29 mwezi uliopita. Kwa hiyo, yote hayo tunayafanyia kazi. Kwa sasa hivi, kwa madhumuni ya kitabu hiki, naomba isomeke suala hilo limo katika kifungu 5414.

**MWENYEKITI:** Halafu Mheshimiwa Susan ungeangalia hela hizi zote zilikuwa *foreign funded.* Kwa hiyo, suala la kwamba kulikuwa na *allocation* upande wetu halikuwepo, hii ilikuwa *foreign funded*. Tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 – *Non-Government Organizations* … Sh. 7,145,302,000.00

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi, baada ya kujadili Taarifa ya Makadirio na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha makadirio hayo bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na kuungwa mkono, wote wameafiki. Kwa hiyo, Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, yamepitishwa na Bunge hili rasmi na tunaomba yafanyiwe kazi. Ikiwezekana, miaka ijayo kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge wengi, Watumishi wa Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana hasa katika suala zima la uwajibishaji wa mambo mengi ambayo tunayafanya. Sisi tunawatakia kheri na muweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mezani kwangu sina matangazo yoyote yale. Kwa hiyo, napenda kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.17 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 10 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*